**29 OKTOBA, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

___

## MAJADILIANO YA BUNGE

___

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 29 Oktoba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

## D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninayo Taarifa ambayo imeandaliwa chini ya Kanuni ya 39(1) lakini kabla ya Taarifa hiyo, tumepata Katibu wa Bunge mpya ambaye ni Ndugu Baraka Idelphonce Leonard. Kwa hiyo, tumkaribishe sote pamoja siku ya leo. *(Makofi)*

Ahsanteni sana.

Katibu wa Bunge mpya, karibu sana Bungeni, tunakutakia kila la heri katika majukumu ambayo umeaminiwa na Mheshimiwa Rais kuja kuyatimiza hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nilete Taarifa kwenu kwamba katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada minane ya Sheria kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania wa Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania Amendment Bill, 2024)*;

(ii) Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2024 *(The Social Security Laws Amendment Bill, 2024)*;

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Zinazohusu Ulinzi wa Watoto wa Mwaka 2024 *(The Child Protection Laws Miscellaneous Amendments Bill, 2024)*;

(v) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption Amendment Bill, 2024)*;

(vi) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendment Bill, 2024)*;

(vii) Muswada wa Sheria ya Ushindani wa Mwaka 2024 *(The Fair Competition Amendment Bill, 2024);* na

(viii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 2) Bill, 2024)*.

Waheshimiwa Wabunge, kwa Taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kuwa tayari Miswada hiyo minane imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuwa sheria za nchi. *(Makofi)*

Sasa sheria hizo zitaitwa ama zinaitwa:-

(i) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shule ya Sheria Tanzania (Na. 7) ya Mwaka 2024 *(The Law School of Tanzania Amendment Act (No. 7) of 2024)*;

(ii) Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania (Na. 8) ya Mwaka 2024;

(iii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Hifadhi ya Jamii (Na. 9) ya Mwaka 2024 *(The Social Security Laws Amendments Act (No. 9) of 2024)*;

(iv) Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Watoto (Na. 10) ya Mwaka 2024 *(The Child Protection Laws Miscellaneous Amendments Act (No. 10) of 2024);*

(v) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Na. 11) ya Mwaka 2024 *(The Prevention and Combating of Corruption Amendment Act (No. 11) of 2024);*

(vi) Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 12) ya Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments Act (No. 12) of 2024)*;

(vii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ushindani (Na. 13) ya Mwaka 2024 *(The Fair Competition Amendment Act (No. 13) of 2024);* na

(viii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) Sheria (Na. 14) ya Mwaka 2024 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 2) Act (No. 14) of 2024)*.

Waheshimiwa Wabunge, sheria hizi sasa zimeshaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Tunaendelea na ratiba yetu, Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI *(PAC)*:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

**MHE. MARY F. MASANJA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA *(PIC)*:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 1

### Kurudisha Mikopo ya Asilimia 10 Kwa Makundi Maalum

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itarudisha mikopo ya asilimia 10 kwa Makundi Maalum?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ilisitishwa tarehe 13 Aprili, 2023 ili kupitia na kuboresha utaratibu wa utoaji wa mikopo hiyo kutokana na changamoto zilizobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesharekebisha sheria na imepitisha Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2019 na 2021 na kutoa Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizoanza kutekelezwa ni kutoa mafunzo kuhusu mfumo mpya wa utoaji na usimamizi wa mikopo hiyo kwa wasimamizi 862 katika ngazi za mikoa na halmashauri. Aidha, mafunzo yanaendelea kutolewa kwa Kamati za Usimamizi za Huduma za Mikopo ngazi za kata, halmashauri, wilaya pamoja na vikundi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafunzo yaliyotolewa, uchambuzi wa awali wa mikopo umeshaanza katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na mikopo hiyo inatarajiwa kuanza kutolewa kabla au ifikapo tarehe 30 Novemba, 2024, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Santiel Kirumba, swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa

Rais kwa namna ya dhati ambayo amerudisha mikopo hii ya 10% katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Serikali imejipangaje kushirikiana hasa na sisi Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum katika kutoa semina na mikopo hii ya 10%? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwa na mifuko mingi ya Serikali inayotoa mikopo sawasawa na hii ya halmashauri. Je, Serikali imejipangaje ku-*link* mifuko hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ile 18 na mifuko mingine ili kuwafikia wananchi kiurahisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge na kwa hakika shukrani na pongezi nyingi zimfikie Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kuhakikisha kwamba vikundi hivi vya makundi maalumu wanapata mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maelekezo ya Serikali yalishatolewa kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri kuhakikisha wanawashirikisha Waheshimiwa Wabunge wa majimbo, Wabunge wa Viti Maalum, Waheshimiwa Madiwani wote katika kuhamasisha wananchi kujiunga katika vikundi hivyo na kunufaika na mikopo hiyo. Kwa hiyo, suala hili litaendelea kusimamiwa, na Waheshimiwa Wabunge wote tutashiriki katika kuhamasisha wananchi kunufaika na mikopo ya 10%.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali yetu ni moja, na Wizara zote tunafanya kazi kwa pamoja. Kwa hiyo, uratibu wa mikopo ya 10% na mikopo inayotolewa na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu unafanyika kwa pamoja kwa kupitia halmashauri zetu, lakini tutahakikisha

tunaendelea kushirikiana kama Wizara ili mikopo yote hii iwafikie wananchi kama inavyotarajiwa, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtakaopata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, mwende moja kwa moja kwenye swali.

Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeongeza umri kwa vijana wanaokopa mpaka miaka 45, je, hamwoni ni wakati sahihi sasa kundi la wanaume wote na wenyewe kunufaika na mikopo hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, lengo la mikopo hii ni kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; na kwa kuwa tumeongeza umri wa vijana kutoka miaka 35 mpaka 45, tunaamini vijana wengi wamekuwa *covered* na eneo hili la mikopo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kabla hatujasimamisha kutolewa kwa hii mikopo kulikuwa na makundi ambayo yameshaomba na mengine yaliendelea kuomba na tunatumaini kila halmashauri iliendelea kutenga fedha hizi, napenda kufahamu, mikopo hii ikisharuhusiwa, fedha yote yote itatolewa kwa pamoja au tutaanza na wale ambao walikuwa wameshaanza kuomba mikopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, makundi yote ambayo yalishawasilisha maombi kwa ajili ya mikopo hii yaliendelea kufanyiwa tathmini na kuwekwa kwenye orodha ya kupata mikopo. Kwa hiyo, mara tutakapoanza kutoa mikopo hii, kwanza tuta-*consider* vikundi vilivyoomba mwanzo kama kipaumbele na vikundi ambavyo vimeomba baadaye vitapata mikopo hiyo pia, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 2

**Ujenzi Wa Dampo - Kibaha Vijijini**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kujenga madampo Kibaha Vijijini kwani kuna viwanda vingi na uzalishaji wa taka ni mkubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.
**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kibaha Vijijini kwa sasa ina viwanda 145. Kati ya hivyo, viwanda vikubwa ni 29 na vya kati na vidogo ni 116. Uwepo wa viwanda hivyo umeongeza uzalishaji wa taka katika eneo la Kibaha Vijijini hususan eneo la Kwala ambalo linatarajiwa kujengwa viwanda zaidi ya 200.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ongezeko la uzalishaji wa taka, Serikali imeanza kuchukuwa hatua za awali za ujenzi wa madampo kwa kutenga eneo la viwanja namba mbili na namba

tatu katika kitalu G eneo la Kwala vyenye jumla ya *meter* za mraba 124,901 maalumu kwa ajili ya kukabiliana na taka ngumu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mpango jumuishi katika eneo la Kwala kuwa mji wa viwanda na uwekezaji, Serikali imebainisha maeneo mengine ya ujenzi wa madampo yenye ukubwa wa hekta 142.8 ili kukidhi taka ngumu kutokana na viwanda. Maeneo hayo ni pamoja na Mizuguni hekta 39.5; Pingo hekta 32.2; Mihugwe hekta 35.6; na Madege hekta 35.5. Wakati wa utekelezaji wa mpango kabambe huo, maeneo hayo yatatwaliwa kwa ajili ya kujengwa madampo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba niulize swali moja, lakini kwa upande mwingine nitaikumbusha Serikali kazi ambayo wameifanya Kwala ya kubaini maeneo ni vyema ikafanywa na pale Mlandizi kwenye eneo la Kikongo, kwani kuna viwanda zaidi ya 300 na ni umbali wa kilometa 20 kuelekea Kwala walikopanga.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, kwa kuwa, tayari wamebaini maeneo, ni lini sasa watapeleka fedha kwa sababu, uzalishaji wa viwanda hivyo umeshaanza na taka zinazalishwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na Wakurugenzi wote kote nchini kuweka kwenye mipango yao ya kila mwaka fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madampo maeneo yote ambayo yanahitaji kupata huduma hizo. Hivyo eneo la Mlandizi ni

eneo la kipaumbele, nimsisitize Mkurugenzi kuhakikisha wanaanza kutenga fedha kwa ajili ya kujenga madampo hayo.

Mheshimiwa Spika, kiwanja namba mbili na tatu (Kitalu G) tayari Serikali imeanza kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuanza kujenga dampo hilo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, sasa hivi kutokana na maendeleo yanayopigwa na Tanzania katika maeneo mbalimbali, miji imekuwa ikichipuka katika maeneo mengi ya nchi yetu ambayo yanahitaji kuwa na suala zima la ukusanyaji na uteketezaji wa taka liwe ni suala la msingi kabisa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka sera maalum itakayoainisha sehemu hizo za dampo pamoja na namna ya kuteketeza taka ikiwemo kuzitenganisha? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali tayari ina Sera ya Uhifadhi wa Mazingira na Sera ya Afya ya Jamii ambayo inatambua umuhimu wa kujenga madampo kwa ajili ya kuteketeza taka ngumu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kutekeleza sera hizo pamoja na kuhakikisha kwamba, maeneo yote na hususan ya miji na miji ambayo inachipuka iendelee kupata huduma za madampo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, changamoto ya ongezeko la viwanda na watu liko

katika Mkoa wa Dar es Salaam, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza dampo katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu dampo kuu ni lile la Kinyamwezi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba Jiji la Dar es Salaam lina idadi kubwa ya wananchi na viwanda, kwa hiyo, uzalishaji wa taka ngumu nao umeendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali pia imeendelea kuweka mipango katika kila Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Dar es Salaam, kutenga maeneo kwa ajili ya kujenga madampo. Pia tutaendelea kufanya tathmini kuona namna ambavyo tutaongeza madampo makubwa zaidi ili kuendana na kasi ya uzalishaji wa taka katika Mkoa wa Dar es Salaam.

**SPIKA:** Hili nalo ni la kwako Mheshimiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ndio.

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 3

**Hitaji la Sehemu ya Kuchomea Taka – Hospitali ya Wilaya Ileje**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga eneo la kuchomea taka Hospitali ya Wilaya Ileje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Ileje ina kichomeataka ambacho kilijengwa muda mrefu. Kutokana na kuongezeka kwa huduma za hospitali, kichomeataka hicho kwa sasa hakikidhi mahitaji, lakini pia ni chakavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ileje itatenga shilingi milioni 70 katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya ujenzi wa kichomeataka kikubwa na cha kisasa katika Hospitali hiyo ya Wilaya ya Ileje, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza ni je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa fedha ya dharura ili kujenga kichomeataka katika Hospitali ya Wilaya ya Ileje na kunusuru maisha ya wananchi waliozunguka eneo lile ikiwa ni pamoja na wagonjwa na wahudumu wa afya kwenye hospitali ile?

Mheshimiwa Spika, swali langu namba mbili, nataka kujua, ni lini Serikali mtajenga wigo kwenye Hospitali ya Wilaya ya Ileje, ili kutenganisha maeneo ya hospitali na makazi ya watu waliozunguka hospitali ile? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali hii iko makini sana kuhakikisha maeneo ambayo yanahitaji huduma za dharura yanafanyiwa hivyo, lakini kwa sababu, Hospitali ya Halmashauri ya Ileje tayari ina kichomeataka, tunatambua ni kidogo na chakavu, lakini *at least* kinatoa huduma ambayo haihatarishi wagonjwa na wananchi. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba katika bajeti ya mwaka 2025/2026, Serikali itapeleka fedha hiyo shilingi milioni 70 na kujenga kichomeataka cha kisasa ambacho kitakidhi zaidi mahitaji ya hospitali ile.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali imeweka kipaumbele katika kuboresha miundombinu ya hospitali na baadaye kwenda kwenye ujenzi wa fensi za hospitali hizo. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi kufanya tathmini ya mahitaji ya hospitali na ikiwa fensi ni kipaumbele waanze kutenga fedha katika mapato ya ndani. Pia, walete andiko hilo Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa ajili ya kutafuta fedha za kujenga fensi hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga njia za kupitishia wagonjwa na wahudumu kwenye Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa hospitali zetu unafanywa kwa awamu na eneo la kupitishia wagonjwa ni muhimu sana. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii

kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafanya tathmini kuona kiasi gani cha fedha kinahitajika katika Hospitali ya Halmashauri ya Nyang'hwale kwa ajili ya ujenzi wa *walk ways* na ikibidi mapato ya ndani yatatumika au fedha za Serikali Kuu zitapelekwa kwa ajili ya ujenzi wa *walkways,* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, hivi ni lini Serikali itapeleka mpango wa *theatre* na *X-Ray* katika Kituo cha Afya cha *Mkwawa University*?

**SPIKA:** Kituo gani cha afya umesema? *University!*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, *Mkwawa University*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba, vituo vyetu vya afya vina uwezo wa kutoa huduma kwa upana wake, ikiwepo kufanya upasuaji pamoja na kuwa na vifaatiba vya kisasa. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka hii mitatu amenunua vifaatiba kwa wingi na kuvipeleka katika vituo vyetu karibu 900.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuwasilina na Chuo Kikuu cha Iringa na Wizara ya Elimu pamoja na Wizara yetu ya TAMISEMI kuona uwezekano wa kupata fedha, kwa ajili ya kuboresha kituo hicho cha afya, ahsante.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 4

**Hitaji la Walimu Shule za Msingi na Sekondari – Mtwara**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka Walimu wa kutosha wa Shule za Msingi na Sekondari Mkoani Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiajiri walimu wa shule za msingi na sekondari kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023, Serikali iliajiri walimu 29,879 wakiwemo walimu 16,598 wa shule za msingi na walimu 13,281 wa shule za sekondari. Mkoa wa Mtwara ulipangiwa walimu 968 wakiwemo walimu 502 wa shule za msingi na walimu 466 wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Julai, 2024 Serikali ilitangaza ajira za walimu 11,015 ambapo mchakato wa ajira ukikamilika watapangiwa vituo vya kazi. Mkoa wa Mtwara utapata walimu 502 wakijumuisha walimu 184 wa shule za msingi na 318 wa shule za sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anastazia Wambura, swali la nyongeza.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mkoa wa Mtwara una upungufu wa walimu wa shule za sekondari zaidi ya 11,300 ikiwa ni pamoja na walimu 205 ambao walihama, lakini nafasi zao bado hazijajazwa. Je, Serikali itajaza lini nafasi za walimu hawa ambao walihama kwa muda mrefu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ukiangalia idadi ya walimu wa shule za msingi na sekondari ambao tutaletewa bado haitatosha ukizingatia upungufu ambao upo na kikubwa ambacho sisi tunahitaji ni kwamba, pale walimu wanapokuwa wamehama, basi angalau Serikali ijitahidi kujaza zile nafasi kwa wakati. Swali langu ni kwamba, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inakuwa ikijaza nafasi hizi za walimu wanaohama kwa wakati? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri sana. Kuhusu swali lake la kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, katika ajira mpya zilizotangazwa za walimu Mkoa wa Mtwara atapata walimu 502.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari ilishatoa mwongozo wa utaratibu wa uhamisho wa walimu kwamba, uhamisho wa walimu unafanywa kwa kuzingatia kubadilishana, kwa hiyo, sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutaendelea kusimamia utaratibu huo ili kuondoa upungufu wa walimu kwenye eneo moja kutokana na uhamisho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutazingatia ili wale walimu wanapohama kwenye kituo kimoja, basi apatikane mwalimu

mwingine wa kuja kuziba ile nafasi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tumezingatia sana ombi na mwongozo wako na sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutazingatia utaratibu huo.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri watu waliosimama ni wengi kuashiria wana maswalli mengi hapa.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena, nenda moja kwa moja kwenye swali ukianza na maelezo ndiyo maana inabidi niite watu wawili tu kati ya nyie mliosimama. Sasa nendeni moja kwa moja ili wote mpate nafasi.

Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, hali ya miundombinu katika Shule ya Msingi Kakesio, Tarafa ya Ngorongoro ni mbaya sana, inahatarisha walimu na wanafunzi. Je, ni lini Serikali itapeleka msaada wa dharura kwa sababu wako katika hali mbaya, ukizingatia Tarafa ya Ngorongoro imesharudishiwa huduma za kijamii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, swali linahusu miundombinu, kama una majibu unaweza kumpa Mbunge, kama huna lije kama swali la msingi. Lije kama swali la msingi au unampa majibu Mheshimiwa Mbunge?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, nitampa majibu.

**SPIKA:** Lije kama swali la msingi. Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Mbogwe ina upungufu wa walimu wengi kwenye...

**SPIKA:** Nenda moja kwa moja kwenye swali la upungufu; watu wote humu ndani tunao huo upungufu, nenda maalum la kwako wewe.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatoa walimu upande wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Mbogwe kwa maana zina upungufu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali tayari ilishatangaza ajira za walimu kuwa katika mwaka huu kutakuwa na ajira za walimu 11,015. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mgao wa walimu hawa, naye katika Wilaya ya Mbogwe atapata walimu kwa ajili ya shule za msingi na sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Naibu Waziri amekiri kwamba, ili uhamisho uweze kufanyika lazima kuwe na programu ya kubadilishana, lakini *recently* katika Wilaya ya Biharamulo tumekuwa tunapokea barua za uhamisho wa watumishi kutoka TAMISEMI bila hata halmashauri kuhusika na chochote.

**SPIKA:** Mheshimiwa swali, swali, swali.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, sasa uko tayari kutoa kauli ya kusimamisha uhamisho wowote ambao

umetokea TAMISEMI moja kwa moja kuja Biharamulo bila programu ya kubadilishana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, mimi na yeye tutakaa na tutafanya ufatiliaji kuona tatizo alilolisema katika jimbo lake ili tuweze kuchukua hatua stahiki, lakini msimamo wa Serikali ndiyo huo kwamba, uhamisho unapofanyika, mwalimu anapotoka katika kituo kimoja lazima awe amepatikana mwalimu mwingine wa kuja kuziba pengo lake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza changamoto ya upungufu wa walimu katika shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Kilwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuendelea kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari Serikali imeshatangaza ajira za walimu wapya 11,015 na katika jimbo lako, Mheshimiwa Mbunge, utapata mgao wa walimu hawa wa shule za msingi na sekondari. Tunaendelea kuwasisitiza Wakurugenzi kutumia utaratibu wa kupata walimu wa kujitolea ambao watalipwa posho, pamoja na kuajiri walimu kwa mikataba ili waweze kutosheleza na waweze kuongeza nguvu kuwafundisha wanafunzi wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Je, Serikali itakuwa imewazingatia wale walimu waliojitolea kwa muda mrefu katika ajira hii mliyotoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tayari ilishatoa utaratibu na kwa sababu ajira hizi ziko katika ofisi hii walitoa utaratibu wa kwamba watu waombe, lakini watazingatiwa pia kwa uzoefu na kujitolea kwao katika maeneo ambayo wanafanya kazi kwa maana ya kwamba, kama anazungumzia suala la walimu, basi ni wale walimu ambao wanajitolea. Kwa hiyo, nadhani suala hilo linazingatiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene ule Mwongozo wa Walimu Wanaojitolea, Madaktari Wanaojitolea na Manesi Wanaojitolea, mmeshautoa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, tutautoa. Tulifika mahali tukapata changamoto hasa kwenye vigezo, lakini hata hivyo tunashirikiana na Kamati na tunadhani tujadili kwa pamoja tena tutapate mawazo zaidi kwa sababu vigezo vinatusumbua sana.

**SPIKA:** Sawa. Sasa hili mngetusaidia kama linahitaji mawazo mapana, basi mnaweza kushirikisha watu wengi zaidi, kwa nini? Ajira zimetolewa hivi karibuni na nitaenda kwenye mfano mmojawapo. Kuna madaktari ambao wako hospitali kwa mkataba huo huo wa kujitolea kwa sababu, wanalipwa nusu, hawa wanawafundisha wale wanaokuja kama *interns,* halafu wanaajiriwa *interns* hawa wanaachwa wakati wote waliomba. Sasa, hivi ni vigezo gani vinavyotumika kumwajiri huyu *intern* wakati

vinamwacha yule ambaye amemfundisha huyu *intern* akiwa amempokea pale kazini?

Kwa hiyo, myatazame haya mambo, yanawaumiza wale watoa huduma kule. *(Makofi)*

Sasa nimetoa mfano wa madaktari kwa sababu, mimi pale kwenye jimbo langu hospitali zipo nyingi. Kwa hiyo, nimetoa mfano wa madaktari, lakini ni hoja hiyo hiyo kwa walimu, ni hoja hiyo hiyo kwa wengine pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, walimu wangu wa *Salma Rashid Kikwete Secondary,* Kilolambwani pamoja na Kilangala wanakidhi vigezo. Je, ni lini watapata ajira? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tayari ilishatoa tangazo la ajira na tayari wameomba. Kwa hiyo, naomba tuache utaratibu wa kufanya mchakato nina imani kwamba, walimu au waliojitolea katika shule alizozitaja Mheshimiwa Mbunge na wenyewe watakuwa na sifa ambazo zinahitajika, kwa ajili ya kuajiriwa kwenye nafasi hizi. Nadhani basi utaratibu utafatwa ili waweze kupata ajira hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa wa walimu wa shule za sekondari na *primary* katika Mkoa wa Simiyu. Je, ni lini Serikali itatuletea walimu wa kutosha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika ajira 11,015 za walimu ambazo tayari zimetangazwa na yeye katika mkoa na katika jimbo analotokea atapata mgao wa walimu hawa wa shule za sekondari na shule za msingi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Shule za Msingi za Itema, Tumbi, Itonjanda pamoja na shule nyingine za Kata ya Kabila zina upungufu mkubwa sana katika Manispaa ya Tabora.

**SPIKA:** Mheshimiwa swali.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, lini Serikali itapeleka walimu katika shule hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu tayari Serikali imetangaza ajira za walimu. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, naye atapata mgao wa walimu hawa katika jimbo lake. Naomba niendelee kutumia fursa hii kuwasisitiza Wakurugenzi na wenyewe waweze kutumia utaratibu wa walimu wa kujitolea na pia, waweze kuajiri walimu kwa mikataba ili kuendelea kupunguza ukali wa upungufu wa walimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, kwa hakika uhaba wa walimu kwenye shule za sekondari na msingi kwa Mkoa wa Lindi ni mkubwa sana, lakini wimbi la kuhama nalo ni kubwa sana. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia uhamaji huu mkubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili la walimu kuhama (uhamisho), Ofisi ya Rais, TAMISEMI itatia mkazo zaidi ili kuhakikisha changamoto aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge inaweza kudhibitiwa ili walimu wasihame na kuleta upungufu mkubwa katika Jimbo lake. Kwa hiyo, utaratibu utazingatiwa. Pale mwalimu anapohama awe amepatikana mwalimu mwingine wa kuja kuziba pengo.

Mheshimiwa Mbunge, mwaka huu katika ajira hizi 11,015 zilizotangazwa, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge nawe utapata mgao wa walimu wa shule za msingi na shule za sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshajenga shule ya vipaji maalum ya wasichana pale jimboni kwangu, je, ni lini sasa italeta walimu ili waanze kutoa huduma ya ufundishaji ulio bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, katika walimu wanaoajiriwa mwaka huu, zile ajira za walimu 11,015, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaleta walimu katika Jimbo lake ambao wataenda kuhudumu katika shule aliyoitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, katika ajira mpya, tungependa kujua kwa Jimbo la Bunda Mjini tutapata mgao hasa katika walimu wa sayansi na hesabu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Jimbo la Bunda naye atapata mgao wa walimu wa shule za sekondari na shule za msingi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmesimama wengi kweli! Mheshimiwa Josephat Kandege swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa una upungufu mkubwa sana wa walimu, hususan Wilaya ya Kalambo. Je, katika mgao ambao utafanyika, Serikali itahakikisha inapeleka walimu wengi Kalambo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imetangaza ajira 11,015 za walimu katika mwaka huu. Naomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mgao wa walimu hawa 11,015 Mkoa wa Rukwa na wenyewe utapata walimu wa shule za msingi na shule za sekondari. Kwa hiyo, katika Jimbo lake atapata mgao wa walimu hao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba Abbas, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, shukrani sana. Naomba nimwulize Naibu Waziri, hivi Serikali inayo kanzidata inayoonyesha ni walimu wangapi na madaktari wangapi wanaojitolea katika nchi hii kwa madhumuni ya marejeo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari imeanza kutengeneza utaratibu mzuri wa kutunza kumbukumbu na rekodi za watumishi wote wanaojitolea. Pia, kwa sababu tumesema tunajipanga kwenda katika utaratibu wa kuhakikisha wale wanaojitolea wanakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuweza kuajiriwa na kuwa *considered* kupata ajira hizi, kwa hiyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari ina utaratibu wa kutunza taarifa za hawa watumishi wanaojitolea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

Na. 5

**Mfumo wa TEHAMA Ulivyoongeza Uwajibikaji wa Watumishi Nchini**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza: -

Je, kwa kiasi gani mifumo ya TEHAMA inasaidia kuongeza uwajibikaji wa Watumishi wa Umma nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga na kuimarisha mifumo na miundombinu ya TEHAMA, ikiwa ni pamoja na kutunga Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 na Kanuni zake za mwaka 2020, kwa ajili ya kusimamia matumizi ya Mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga mifumo mbalimbali ya TEHAMA ikiwemo, *e*-Watumishi, *e*-Utendaji, *e*-Mrejesho na *e-Office* ili kuimarisha uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Matumizi ya Mifumo hii yameboresha uendeshaji wa shughuli za Serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, uwajibikaji katika utendaji kazi kwa Watumishi na Taasisi za Umma ulipimwa kupitia mfumo wa *e-Utendaji* ambapo jumla ya Watumishi wa Umma 507,136 sawa na 87% na Taasisi za Umma 531 sawa na 93% zilipimwa utendaji wake ambapo zoezi hilo limesaidia kuongezeka kwa uwajibikaji, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bakar Bakar, swali la nyongeza.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na vilevile namshukutu na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu haya mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya muda mrefu ya kusomana kwa mifumo ambayo Mheshimiwa Waziri ameitaja na mifumo mingine ya Serikali. Kwa kuwa kuna ahadi na mapendekezo mbalimbali ambayo yametolewa ndani ya Bunge na nje ya Bunge ya kwamba mifumo hii inakwenda kuunganishwa, sasa

nataka kujua, katika utekelezaji huu Serikali imefikia wapi ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi kazini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Bakar Hamad kwa kufuatilia habari ya mifumo kusomana. Kwa kweli hili ni agizo la Mheshimiwa Rais katika nyakati mbalimbali kuhakikisha mifumo inasomana. Vilevile, katika kuchukua hatua, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kupitia taasisi yake ya *e-GA* ikishirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imejenga mfumo wa kuwezesha mifumo kusomana ambao unaitwa *Government Enterprises Service Bus*. Mfumo huo mpaka kufikia tarehe 30 Septemba, 2024 umesaidia taasisi zaidi ya 175 mifumo yao kusomana na kubadilishana taarifa, ikiwemo ile mifumo muhimu ya Hakijinai, Polisi, Mahakama na *PCCB*. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa vile mifumo hii pia inatumika kupima utendaji kazi wa watumishi, je, Serikali ina mpango gani kwa wale watumishi ambao wako pembezoni ambako hakuna mitandao na pia wale wenye kazi kubwa ili zile asilimia wanazowapimia kufika waweze kupanda vyeo na shughuli nyingine? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage kwa kufuatilia masuala yanayohusu watumishi. Naomba nimhakikishie kwamba, tulipoanza zoezi la kuwapima watumishi, hatukupata malalamiko ya watumishi

kushindwa kuingia kwenye mfumo wa *PEPMIS* kwa maana ya kujipima.

Mhshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kutambua kwamba maeneo mbalimbali ya nchi yanakumbana na changamoto ya mitandao, Ofisi ya Rais, Utumishi imeendelea kushirikiana na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, katika programu yao ya Tanzania ya Kidigitali, kuhakikisha minara inajengwa nchi nzima na mawasiliano yanakuwepo ili watumishi wa umma nao watakapokuwa wanatumia mifumo yao katika kujipima, wasiweze kupata changamoto, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Na. 6

**Ujenzi wa Nguzo za Umeme *REA III* - Newala Vijijini**

**MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa nguzo za kilometa 2 katika Vijiji ambavyo *REA III* Mzunguko wa Pili unatekelezwa - Newala Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Judith Kapinga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *REA,* inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa *R3R2* ambapo kwa upande wa Newala Vijijini inatekeleza katika vijiji 76 na imefanikiwa kuwasha umeme katika vijiji vyote 76 kwa umbali wa kilomita moja. Aidha, kwa nyongeza ya umbali wa kilometa mbili, *REA* kupitia mkandarasi aitwaye *Central Electrical International Limited,* anaendelea na kazi na amefanikiwa kufikisha umeme kwenye vijiji 32 kati ya vijiji 76. Vijiji vilivyosalia vinatarajiwa kukamilika hivi karibuni, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba vijiji vyote 785 vya Mkoa wa Mtwara tulipokea taarifa ya kutoka kwa Mkuu wa Mkoa kwamba vimeshapatiwa umeme. Isipokuwa, kazi hii sasa inaendelea kwenye vitongoji. Kijiji cha Mnyambe, Mitema pamoja na Kijiji cha Mapinduzi tayari wakandarasi wako huko. Tunaiomba Serikali itoe maelekezo ya kuhakikisha kazi hii inafanywa kwa spidi ili iweze kukamilika mapema.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mwingiliano wa kazi, kama utakumbuka, kulikuwa na vitongoji 15 ambavyo sisi Waheshimiwa Wabunge tulipendekeza, lakini kuna kazi ya ujazilizi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Chiwata, Mkalinga, Ngalole, Chikoweti, Maswela pamoja na Kitongoji cha Magomeni na Mjimwema…

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa Serikali iweze kufanya *review* ya ramani kwenye maeneo hayo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Cecil, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa yale maeneo ambayo miradi inaingiliana, huu wa vitongoji 15 na miradi ya ujazilizi ambayo pia imeanza, kwa niaba ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, naomba nimwelekeze Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Nishati Vijijini, waweze kufanya mapitio pamoja na wakandarasi ili kuhakikisha miradi hii haiingiliani, ila yote inatekelezwe kwa kasi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya umeme kwa haraka, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, je ni lini Serikali itaunganisha umeme katika Kitongoji cha upendo, Tupendane, Ikwambi na *Mission* katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Vitongoji hivi alivyovisema Mheshimiwa Mbunge vya Upendo, Tupendane, Ikwambi pamoja na *Mission,* vipo katika miradi ya vitongoji ambayo inaendelea. Tuna Mradi huu wa Vitongoji 15, lakini tuna mradi mwingine wa vitongoji ambao unatarajia kuwepo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, dhamira yetu ni kuhakikisha tunaendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji, na kwa vitongoji hivi ambavyo amevisema, tutahakikisha na vyenyewe vinakuwepo katika mradi na wananchi wapate umeme, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Vitongoji vya Iduya “A” na Iduya “B”, Kata ya Utengule Usangu pamoja na Kitongoji cha Ngolongolo Kata ya Ihai, ni Vitongoji vyenye watu wengi sana na mpaka leo havina. Nini mkakati wa Serikali wa kutusaidia kupeleka umeme kwenye vitongoji hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Vitongoji vya Iduya "A" na Iduya "B", pamoja na Mngolongolo, vipo katika miradi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji 15. Tumefanya mapitio ya vitongoji hivi kutoka kwenye ile *list* ya kwanza kwenda *list* ya pili. Kwa hiyo, kwa sababu kuna miradi iliyokuwa inaendelea kwenye baadhi ya vitongoji, basi vitongoji hivi vitaingia kwenye vile vitongoji ambavyo tayari vimeshapelekewa miradi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ALLY I. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, jimboni kwangu kuna vitongoji vingi sana vyenye hadhi ya kuwa Kijiji, lakini havina umeme kabisa. Je, Wizara ina mpango gani wa kuviangalia vitongoji hivi kwa jicho la huruma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama ambavyo nimeshasema, tayari Serikali tumeanza utekelezaji wa miradi kwenye vitongoji baada ya kufika karibia na mwisho kwa mradi mkubwa wa kupeleka umeme kwenye vijiji. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba dhamira yetu ni kuhakikisha tunaendelea kupeleka umeme kwenye vitongoji ikiwemo vitongoji katika Jimbo la Mheshimiwa Mchungahela.

Mheshimiwa Spika, tumeanza na vile vitongoji 15 na tuna miradi mingine ya vitongoji inakuja. Vilevile, katika Mkoa wake tuna mradi wa ujazilizi ambao pia umeanza. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, miradi ipo na wakandarasi wako *site* na tutaendelea kupeleka kwenye vitongoji kwa kadri miradi na upatikanaji wa fedha unavyoendelea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, Vitongoji vya Mipetu, Kairo na Majengo katika Jimbo la Singida Mashariki, ni vitongoji vyenye shughuli nyingi za uchumi. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji hivyo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Vitongoji vya Kairo, Mipetu na Majengo, ipo miradi ambayo inaendelea, lakini kama vitongoji hivi havipo katika miradi ambayo wakandarasi wako *site*, basi tutavichukua ili kuweza kuviweka katika miradi ya vitongoji ambayo inakuja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

Na. 07

**Ukosefu wa Uwiano Kwenye Bei ya Kuunganisha Umeme Nchini**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA K.n.y. MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu kutokuwepo uwiano katika bei ya kuunganisha umeme nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa uwiano katika bei ya kuunganisha umeme nchini hasa katika maeneo ya mijini kunatokana na umbali alipo mteja kutoka sehemu unapochukuliwa umeme na aina ya njia ya umeme iliyoombwa na mteja *(Single Phase/Three Phase),* gharama hizi anazotozwa mteja ni zile zilizoidhinishwa na *EWURA* kupitia Tangazo la Serikali Na. 1020 la Mwaka 2020. Aidha, kwa upande wa vijijini, wateja wanaunganishiwa umeme kwa gharama ya shillingi 27,000 tu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, yako maeneo ya vijiji ambayo mpaka sasa hayaunganishiwi umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 badala yake wanaunganishiwa kwa shilingi 320,000. Mfano ni eneo la Manyata Kata ya *USA River* kule Arumeru Mashariki. Je, nini kauli ya Serikali juu ya jambo hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Wilaya ya Korogwe mpaka sasa kazi ya kuunganishiwa umeme wa kilometa mbili, pamoja na ujenzi wa vile vitongoji 15 haijaanza. Ni lini kazi hii itaanza kwenye Wilaya ya Korogwe, Jimbo la Korogwe Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la kwanza la hili eneo la Manyata - *USA River*, maeneo yote ya vijiji, umeme unaunganishwa kwa shilingi 27,000 labda isipokuwa maeneo haya ni maeneo ya mamlaka ya Mji mdogo ambayo yanatambulika kama mitaa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, niendelee kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, maeneo yote ya vijijini, ada ya

kuunganisha umeme ni shilingi 27,000. Kwa hiyo, tutaangalia eneo hili la Manyata ambalo lipo *USA River*, kama wanachajiwa zaidi ya hapo na ni eneo la vijiji, basi tutachukua hatua ili kuhakikisha wanarudi kwenye shilingi 27,000; lakini kama ni eneo ambalo liko kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo, basi ndiyo maana ada yake inakuwa ni shilingi 321,000.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mkandarasi ambaye yupo Korogwe, tayari Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwa mkandarasi kutoa *commitment* ya kumaliza mradi kwa wakati kwa sababu alikuwa anasuasua. Tayari imeshafanyika hivyo na ndani ya wiki hii tutasaini na mkandarasi ili aanze kupeleka umeme katika kilometa mbili kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, Haydom ni Kijiji na Dongobesh ni Kijiji, lakini umeme wake unaingizwa kwa shilingi 320,000. Je, ni lini utatoa mwongozo katika vijiji hivyo ili walipe shilingi 27,000 kama vijiji vingine vyote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema kwenye swali la msingi, maeneo yote ya vijiji gharama ya kuingiza umeme ni shilingi 27,000. Kama maeneo haya kulingana na miongozo ya TAMISEMI ni maeneo ya vijiji, tutafuatilia kuhakikisha gharama ya kuunganisha umeme ni shilingi 27,000, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda Wizara ya Madini. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 8

**Faida Inayopatikana kwa Vijiji Vinavyozunguka Kiwanda cha Gesi – Kata ya Itagata**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza: -

Je, Vijiji vinavyozunguka Kiwanda cha Gesi ya Kiwanda kilichopo Kata ya Itagata Rungwe vinapata faida gani kutokana na kuwepo kwa kiwanda hicho?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Gesi kilichopo Kata ya Itagata Wilaya ya Rungwe Mkoa wa Mbeya ni kiwanda cha kuzalisha Gesi Ukaa *(Carbon Dioxide)* na kinamilikiwa na Kampuni ya *TOL Gases Limited*.

Mheshimiwa Spika, faida za kiwanda hiki kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2020 hadi Oktoba, 2024 ni pamoja na malipo ya kiasi cha shilingi milioni 213 kama ushuru wa huduma *(Service Levy)* kwa halmashauri; kuchangia kiasi cha shilingi milioni 159 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Isebe; vyumba viwili vya madarasa, pamoja na Ofisi ya Shule ya Sekondari Itagata; ujenzi wa uzio katika Shule ya Msingi ya Katumba na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa darasa katika Shule ya Sekondari ya Itagata; pamoja na Ofisi ya Kijiji, na kutoa ajira za kudumu 112 na ajira za muda mfupi

takribani 150 kwa wananchi wanaotoka maeneo yaliyo jirani na kiwanda kama sehemu ya uwajibikaji wao kwa jamii, kwa mujibu wa Kanuni za Uwajibikaji wa kampuni za Uchimbaji madini kwa Jamii *(corporate social responsibility - CSR)*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leseni ya madini ya mradi huu ipo katika Halmashauri mbili za Wilaya za Rungwe na Busokelo, kwa mwaka 2024 kampuni ya *TOL Gases Limited* iliwekeana mkataba na Halmashauri ya Busokelo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mabweni ya Shule ya Msingi Lupata kwa thamani ya shilingi milioni 39.7 ambapo mradi huo umekamilika.

Mheshimiwa Spika, vilevile kampuni ya *TOL Gases* inatarajia kukaa na Halmashauri zote mbili mwezi Desemba, 2024 ili kuandaa na kuweka mpango wa utekelezaji wa *CSR* kwa mwaka 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa *CSR* inatolewa kwa kampuni au uwekezaji; na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri amesema ni mwaka 2020 mpaka 2024; siyo kweli, kwa sababu wametoa mpaka 2022. Kwa miaka hii miwili hawajatoa chochote kwa vijiji husika. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wenzetu hawa wanapitisha malori makubwa sana yaliyobeba gesi na kuharibu barabara; na kijiji kilishawaomba watengenezewe barabara japo kwa changarawe lakini hawajafanya hivyo: Je, kama Waziri, anatoa tamko gani ili watu hawa waweze kufaidika na gesi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la kwanza, kama mwekezaji huyu kakoma kutoa *CSR* tangu mwaka 2022, nitumie fursa hii kumwelekeza kwamba kwa mujibu wa

uwajibikaji wa kampuni za uchimbaji madini kwa jamii, ni lazima kila mwaka atenge fungu la kuweza kusaidia miradi ya maendeleo ndani ya jamii.

Mheshimiwa Spika, uzuri ni kwamba, fungu hili huwasilishwa kwenye halmashauri na vipaumbele vinawekwa ili aweze kuendelea kutekeleza hili. Kwa hiyo, nimwagize Afisa Madini Mkazi wa Mbeya afuatilie suala la *CSR* kwa mwekezaji huyu ili ajue kwa nini tangu mwaka 2022 hajatoa, kama maelezo ya Mheshimiwa Mbunge ndiyo sahihi?

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili alisema malori hayo yanayopita kwenye hii barabara anayoisemea na kuiharibu ni sehemu ya wajibu wake kwa jamii ile, kupitia lile fungu analolitenga ambalo ni fungu la kutengeneza mahusiano yake na jamii, kuhakikisha kwamba hii barabara inakuwa sehemu ya fedha anazochangia kuitengenezea jamii waweze kupita bila bughudha kwa sababu ya malori yake kuiharibu. Kwa hiyo, pia nitumie fursa hii kumwagiza kwamba aangalie hiyo barabara aiweke katika mpango wake wa miradi ya kutekeleza kupitia mfumo wa *CSR* uliowekwa kisheria na Wizara.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Ameir Abdalla Ameir Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

Na. 9

**Tafiti za Mbegu za Mazao ya Kilimo**

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR** aliuliza: -

Je, ni tafiti ngapi za mbegu za mazao ya kilimo zimefanyika hivi karibuni na kuleta matokeo chanya ?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(TARI)* imetekeleza miradi 93 ya tafiti mbalimbali katika kilimo, ambapo imegundua teknolojia 52 za aina bora za mbegu za mazao. Aina hizi za mbegu zimesambazwa katika mikoa yote ya Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ameir Ameir, swali la nyongeza.

**MHE. AMEIR ABDALLA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, napenda kujua, ni miradi ipi ya kiutafiti wa mbegu bora mpya na zenye kuhimili mabadiliko ya tabianchi kati ya hiyo miradi 52 ambayo Mheshimiwa Waziri ameizungumzia hapo imetekelezwa kwa pamoja kati ya taasisi zetu hizi mbili za kiutafiti wa kilimo baina ya *TARI* kwa Tanzania Bara na *ZARI* kwa Tanzania Zanzibar na hatimaye imeleta matokeo chanya? Hayo matokeo chanya ni yapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, tuna miradi 93. Tuliyopata matokeo chanya ni maradi 52, na sehemu ya mradi ni kama nilivyoeleza hapo. Kwa mfano, mbegu za mahindi kuna T104 na T105 ambazo zimeonesha zina matokeo mazuri sana na zinafanya kazi kwenye takribani mikoa 14. Kwa hiyo, hizo ni miongoni mwa mbegu ambazo tumezifanya.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na ushirikiano mzuri kati *TARI* pamoja na *ZARI* katika utafiti hususan katika zao la karafuu, utafiti bado unaendelea. Nimthibitishie tu kwamba katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jambo hili limekuwa likifanyika kwa sababu

matokeo yote yanayoleta tija yamekuwa yakileta manufaa kwa wakulima wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na tafiti zinazoendelea kufanyika na pamoja na mbegu mpya ambazo zinaendelea kugundulika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuzilinda mbegu zetu za asili, nikitolea mfano wa mbegu ya mbegu ya ule mpunga wa Kilombero, ama mchele mzuri wa Kyela unaonukia ambayo imetoweka sasa hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya jukumu kubwa ambalo *TARI* wanalo, wanapofanya tafiti ni wanazifanya kupitia mbegu zetu za asili zikiwemo kulinda uasili wake. Kwa hiyo, katika sehemu kubwa ya tafiti zile ni kuhakikisha kuwa mbegu zile ambazo zilikuwa labda zinaathiriwa sana na magonjwa ama hali ya hewa, zinaongezwa tija, kwamba mbegu ni ile ile ya asili, isipokuwa tunachotaka sisi iongeze tija, hususan mavuno yaliyo bora pamoja na kukabiliana na magonjwa. Kwa hiyo, hilo ni jukumu letu, tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba, sasa hivi kule Arusha tumefungua benki ya mbegu za asili ambazo tumekuwa tukizihifadhi kwa ajili ya vizazi vijavyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Dkt. Chaya.

Na. 10

**Hitaji la Bwawa la Umwagiliaji – Itigi**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA K.n.y. MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itachimba Bwawa la Umwagiliaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi baada ya Bwawa la Itagata kutofanya kazi kwa ufanisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.
**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Bwawa la Itandamilomo lililopo ndani ya Halmashauri ya Itigi ili kupata gharama halisi za ujenzi. Bwawa hilo litatumika kwa kiasi kikubwa katika kuchochea kilimo cha umwagiliaji kupitia mbuga kubwa iliyopo katika Kata za Kitaraka, Itigi Mjini, Tambukareli, Itigi Majengo, Sanjaranda, Ipande, Aghondi na Idodyandole katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Itagata lililopo katika Halmashauri ya Itigi linafanya kazi na Serikali itaendelea kulifanyia maboresho kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Je ni lini sasa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Bwawa la Itandamilomo utakamilika katika Wilaya ya Itigi?

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni tuna ujenzi wa Bwawa la Mbwasa ambalo tenda yake ilishatangazwa, je, ni lini sasa mkandarasi ataanza ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Mbwasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba upembuzi huu utakamilika katika mwaka huu wa fedha 2024/2025. Kuhusu Bwawa la Mbwasa, tumeshamkabidhi *site* mkandarasi anayeitwa Kagwa. Juzi ameshalipwa *advance payment,* na hivi sasa ninavyozungumza yuko *site*. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona mmesimama wengi, lakini kwa kuwa huwa mnauliza maswali marefu kidogo, kwa hiyo kidogo mnanipa changamoto hapa mbele.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 11

**Hitaji la Mahakama – Muleba**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga jengo la Kisasa la Mahakama ya Wilaya ya Muleba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mapya na kukarabati yaliyochakaa. Kutokana na uhaba uliopo wa majengo ya Mahakama, majengo hayo yanajengwa na kukarabatiwa kwa awamu kwa kuzingatia mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, jengo la kisasa la Mahakama ya Wilaya ya Muleba limepangwa kujengwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na *commitment* ya Serikali kwamba jengo la Muleba litawekwa kwenye bajeti ya mwaka 2025/2026. Wilaya ya Muleba ina majengo mengi ya Mahakama za Mwanzo ambayo yamechakaa. Je, Serikali ina mpango wowote wa kuyakarabati?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Kuna wadau walitupatia majengo kwa ajili kuyaendeleza kidogo na kuyafanyia ukarabati ili yatumike kama Mahakama za Mwanzo. Je, Serikali ililipokea hili jambo; na imepangia pesa kwa ajili ya kulikarabati ambalo liko Kata ya Ijumbi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mahakama nyingi kama nilivyosema kwenye jibu la msingi hazina hali nzuri. Ni kwa msingi huo ndiyo maana Idara ya Mahakama imeweka Mpango wa Miaka Mitano wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo haya. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango huo unatekelezwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, pia kwa taarifa, kwa ujumla Mahakama za Mwanzo ambazo zimejengwa na kukarabatiwa ni 185, Mahakama za Wilaya ni 66, Mahakama za Ngazi ya Mkoa ni saba na Mahakama Jumuishi ni zaidi ya 12. Kwa hiyo, mpango huu unatekelezwa kila mwaka. Itakapofikiwa Wilaya ya Muleba, pia itanufaika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kwamba majengo tuliyapata kutoka kwa mdau; namwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawasiliana na Idara ya Mahakama wafanye *assessment* ya utoshelevu au kufaa kwa hilo jengo kuwa Mahakama ili ikiridhiwa, basi ukarabati ufanyike ili liweze kutumika kama Mahakama kwenye Kata ya Ijumbi, aliyoitaja. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Morogoro Vijijini haina kabisa jengo la Mahakama. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo la kisasa la Mahakama katika Halmashauri hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi, ni kwamba Wilaya zinaendelea kujengewa Mahakama kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa mpango wa Mahakama hivi sasa, Morogoro ina Wilaya tatu zilizopata ujenzi wa Mahakama. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kulingana na mahitaji, Wilaya ya Morogoro Mjini pia itafikiwa, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Jengo la Mahakama ya Mwanzo Wilayani Urambo lina hali mbaya sana. Je, ni lini Serikali itatujengea jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba ni kweli nimeiona Mahakama ya Mwanzo Urambo, hadi picha nililetewa na tumethibitisha kwamba ni mbaya sana. Mahakama imeuweka ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo Urambo katika bajeti ya mwaka 2025/2026, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate Mbunge wa Kyerwa, sasa aulize swali lake.

Na. 12

**Utekelezaji wa Mradi Mkubwa wa Maji – Kyerwa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Je, lini utekelezaji wa mradi mkubwa wa Maji wa Kyerwa, Nyaruzumbura, Nyakatuntu hadi Kamali utaanza?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa Mradi mkubwa wa Maji wa Kyerwa, Nyaruzumbura, Nyakatuntu hadi

Kamali katika mwaka wa fedha wa 2025/2026. Vijiji vitakavyonufaika na mradi huo ni pamoja na Kyerwa, Nshunga, Milambi, Nyaruzumbura, Omukiyonza, Nyakatuntu, Rukiri, Kishanda A, Kishanda B, Kyerere, Kasoni, Kamuli, Rwabigaga na Ruhita.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha hali ya huduma ya maji Kyerwa, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa mitano ya Runyinya – Chanya, Kikukuru, Kimuli – Rwanyango – Chakalisa, Kaisho – Isingiro na Mabira. Jumla ya vijiji 30 vinatarajiwa kufikishiwa huduma ya majisafi na salama pale ambapo miradi hiyo itakapomalizika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Serikali ya kukatisha tamaa, Mheshimiwa Naibu Waziri ameelezea kuhusu miradi inayoendelea Wilayani Kyerwa. Miradi hii ambayo inaendelea, wakandarasi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilakwate, Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu hapa swali, naye ameleta majibu kwa mujibu wa swali lako. Sasa umeanza na maelezo kwamba yanakatisha tamaa. Ni kwamba majibu hayana uhalisia, ama majibu yana uhalisia lakini wewe kama Mbunge umekata tamaa? Maana kanuni zetu zinataka ajibu maswali kwa ukamilifu.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, majibu yamekuwa ni hayo hayo kwa zaidi ya miaka mitano, kwamba mradi unatengewa fedha, unatengewa fedha. Kwa hiyo, ndiyo maana ninasema ni majibu ya kukatisha tamaa.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani umeelewa hoja yake. Haya, maswali.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, miradi aliyoeleza inayoendelea Wilayani Kyerwa, wakandarasi wanadai zaidi ya shilingi bilioni sita. Je, ni lini wakandarasi hawa watalipwa ili miradi hii iweze kukamilika na kuwapa wananchi majisafi na salama?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mradi wa Kirera – Isingiro unajengwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza imeshakamilika. Je, ni lini Serikali itatoa kibali ili mradi huu uanze ili wananchi wapate huduma ya majisafi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, nikianza na swali la kwanza ambapo wakandarasi wanadai shilingi bilioni sita, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kupitia Wizara ya Fedha, tayari Wizara ya Fedha imetupatia *exchequer* ya shilingi bilioni 140. Pia kwenye miradi ile *EP4R* tayari wafadhili wameshaleta shilingi bilioni 150 na hivyo tayari Katibu Mkuu, leo nimeongea naye, ameshaanza kukusanya madai ya wakandarasi ili waweze kuwasilisha Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo ya wakandarasi wanaodai.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kabisa na ninatambua kwamba Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiupigania sana. Mradi huu una zaidi ya shilingi bilioni hamsini na kitu. Tunapotoa kibali, lazima tuwe tumejiridhisha kwamba tuna fedha za kwenda kumlipa *advance payment* mkandarasi huyu ili aweze kuingia *site*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali iko kwenye utafutaji wa fedha, na itakapopatikana, kibali kitatolewa kwa ajili ya kutangaza tenda na mkandarasi atapatikana kwa ajili ya kwenda kutekeleza mradi huu ndani ya jimbo la Mheshimiwa Bilakwate,ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kufahamu, je, ni lini mradi wa kutoa maji katika Mto Momba na kuyasambaza katika Miji ya Tunduma, Vwawa pamoja na Mji wa Mlowo utaanza kutekelezwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa kutoa maji kutoka Mto Momba tayari Serikali imeshaanza kuufanyia kazi. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana nasi ili tukamilishe hatua ambazo tuko nazo na baada ya hapo tutakwenda kuukamilisha mradi huo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali kuhusu Mradi wa Maji wa Tukuyu Mjini ambapo hili swali ninauliza ni mara ya tano sasa. Je, ni lini Serikali itakamilisha tenki la maji la Tukuyu Mjini ukizingatia wananchi wa Tukuyu Mjini wanasumbuka sana na maji hasa wanawake? Naomba majibu hayo ambayo ni ya kuridhisha kwa leo ili wananchi wa Tukuyu waweze kusikia na kuelewa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nafahamu changamoto ya mradi huu kuchelewa kukamilika. Namwomba Mheshimiwa Mbunge tukitoka hapa tuonane ili tuweze kupitia changamoto ambazo zimesababisha kuchelewa kwa mradi huo na hatua ambazo Serikali tunaweza kuzichukua ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaosubiri kwa hamu sana maji haya kutokana na tenki

hilo litakapokamilika waweze kupata maji yaliyo safi na salama, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu, sasa aulize swali lake.

Na. 13

**Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria wa Igaga, Mwamashele hadi Lagana**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza: -

Je, lini Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria wa Igaga, Mwamashele na Lagana wenye thamani ya shilingi bilioni 6.6 utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria wa Igaga, Mwamashele na Lagana kwa mujibu wa mkataba umekamilika. Kazi zilizofanyika katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa bomba kuu kwa umbali wa kilometa 33.65, ujenzi wa tenki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 100,000 katika Kijiji cha Lagana, Ujenzi wa vituo sita vya kuchotea maji katika Kijiji cha Lagana na ulazaji wa bomba la usambazaji maji umbali wa kilomita 7.86 katika Kijiji cha Lagana ikijumuisha matoleo ya maji *(offtake)* sita katika Vijiji vya Igaga, Isagala, Mwamashele, Busongo/Mwamanota, Bubinza na Mwamadulu. Katika Vijiji vya Mwamashele na Mwamadulu, Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria wa Igaga, Mwamashele na Lagana unatoa huduma kwa wananchi wapatao 3,040 wa Kijiji cha Lagana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nampongeza Naibu Waziri kwa ziara yake aliyoifanya miezi mitatu katika Jimbo la Kishapu. Wakati huo huo naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kishapu kata zaidi ya 20 zilikuwa na changamoto kubwa sana ya maji, lakini kata nne zina taabu sana. Usanifu ulishafanyika katika Kata za Seke-Bugoro, Mundo na Nyasamba ambapo takribani shilingi bilioni 15 zinahitajika. *Old Shinyanga*, Busangwa, Nyamtengela, Seke-Bugoro, shilingi bilioni nane; Iselamagazi, Mwanhili na Itongoitale shilingi bilioni tatu; na Mwamashele, Ngofila hadi Kiloleli shilingi bilioni 5.9. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Butondo kwa kushirikiana na Serikali vizuri sana na kukamilisha ule mradi wa bomba kutoka Ziwa Victoria. Amefanya kazi nzuri sana na tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mradi ambao katika vijiji ambavyo amevitaja na kata hizi, kwa gharama za jumla utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 33.5. Ni mradi ambao tunatarajia katika mwaka wa fedha 2025/2026 ndiyo tutakaouingiza ili kuutafutia fedha kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana na kuhakikisha kwamba tunaandaa mazingira rafiki ya kwamba mradi huu unaenda kuwezekana kufanyika ndani ya Jimbo lake la Kishapu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama, nimewaona, lakini sasa muda wetu umetutupa mkono na pia mnauliza maswali marefu, mnarejea tena. Mngekuwa mnauliza maswal mafupi

tungeuliza mengi. Sasa unataka uanze na historia, pongezi, halafu ufuate swali wakati hiki ni kipindi cha maswali na majibu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Changamoto ya Ugonjwa Sugu wa Kisukari Nchini**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya Ugonjwa Sugu wa Kisukari nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mkakati wa tano wa Sekta ya Afya, imetoa kipaumbele kwa kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari kama ifuatavyo:-

(1) Kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma juu ya kujikinga na ugonjwa wa kisukari kama vile kuzingatia ulaji unaofaa, kushughulisha mwili, mazoezi ya viungo pamoja na kuepuka matumizi ya pombe na tumbaku;

(2) Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vitendanishi na mashine za kupimia sukari katika maeneo yote ya kutolea huduma za afya; na

(3) Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya kibingwa kwa wataalamu wa afya juu ya matibabu ya ugonjwa wa kisukari.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa hapo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Je, kuzingatia ulaji unaofaa ni kupi?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: Pamoja na nia njema ya Serikali kutoa elimu ya kutotumia pombe na tumbaku, kwa nini Serikali isiamue kuhamasisha matumizi ya pombe na tumbaku nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika,…

**SPIKA:** Ngoja kwanza, Mheshimiwa Mwantumu, ulikusudia kusema wahamasishe matumizi ya tumbaku na pombe ama ulikusudia wakataze?

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, wasitishe.

**SPIKA:** Wasitishe?

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, wasitishe kuhamasisha matumizi ya pombe na tumbaku nchini.

**SPIKA:** Aah, sawa. Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani umesikia. Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Mbunge, mama yangu, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji kwa sababu amekuwa akifuatilia masuala ya afya, hata kule Muhimbili amekuwa akifuatilia wagonjwa mbalimbali ambao wanapata matatizo kama haya na kuhakikisha kwamba wanapata huduma, ahsante sana. Hata hivyo, nimwambie tu, amesema tufanye ulaji upi?

Mheshimiwa Spika, ili kuokoa muda, namwomba aende aka-*google* ahakikishe kwamba anasoma vizuri na kuzingatia maelezo ya mzee wangu Prof. Janabi. Kwa hiyo, ukienda pale, hayo yote anayoyasema Prof. Janabi tukiyazingatia tutaondokana na matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwenye suala la kusitisha pombe na sigara, kwa kweli mchakato umeanza, lakini utaona kwenye sigara na kwenye mambo mengine imehamasisha kwamba ina madhara kiafya. Sasa suala la kusitisha isitumike kabisa, ninachofikiri siyo kusitisha kabisa, nafikiri kila mtu atambue kwamba ukifanya jambo hili unapata madhara haya na ukiacha jambo hili unapata faida, na kila mtu azingatie hayo ambayo yanaelezwa na wataalamu wetu wa afya. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali lake la nyongeza la kwanza ameuliza hivi, "Ni ulaji upi unaofaa?" Sasa umemtuma Mbunge aende aka-*google* na akamfuatilie Prof. Janabi ambapo tuna maswali kwa kweli kwa yale anayohamasisha...

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika,…

**SPIKA:** Sasa kuna namna mbili; moja, labda useme utampatia Mheshimiwa Mbunge majibu ya ulaji unaofaa ni upi? Ama sivyo,

nadhani lengo la Mbunge kuuliza hapa alikusudia Watanzania wapate picha ya ulaji unaofaa ni upi? *(Makofi)*

Sasa ninakupa nafasi wewe nenda ka-*google*, ukishaupata ule ulaji unaofaa utakuja hapa utupe hayo majibu kwa sababu mama wa watu yule hawezi kwenda ku-*google*. Kwa hiyo, nakupa nafasi Mheshimiwa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama utanipa nafasi mimi niliona tu kwamba nikianza kutumia muda kufafanua itachukua muda mrefu. Niseme kwamba kuna mambo rahisi, kwanza, kuhakikisha una uzito ule unaotakikana kulingana na urefu wako; uzito unaokubalika kwa maana ya kwamba ulaji wako unaweza ukala kila kitu, lakini kila jambo kwa kiwango, kupunguza wanga na vyakula vile vingine vinavyoongeza uzito, lakini kuhakikisha uzito wako uko kwenye kiwango na mafuta yaliyoko mwilini mwako yako kwenye kiwango ambacho hakina shida.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nasema pia sisi binadamu tumezaliwa kwa *natural* kwenye *genome* yetu sisi kwa asili ni *hunters and gatherers.* Kwa maana hiyo, hakikisha vyakula ambavyo unakula vingi ni vile ambavyo vimetayarishwa, siyo *fried foods.* Ni vile vyakula vya asili kama mbogamboga. Ukila protini ziwe ni protini ambazo siyo *fried.* Kwa namna hiyo, tunaweza kuhakikisha kwamba afya yetu inakuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni *topic* ndefu, ndiyo maana niliona nikianza kugagatua hapa itachukua muda mrefu sana. Kikubwa tuzingatie maelekezo ya wataalamu wetu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, bado uhitaji wetu wa ulaji unaofaa ni upi, uko pale pale. Hapa umetaja *hunters and gatherers. Gatherers* ni wa matunda na *hunters* ni wanyama. Kwa hiyo, tule nyama ama tusile, kama anavyotuambia huyo unayesema anatuelekeza?

Kwa hiyo, katutafutie tu hayo maelezo Mheshimiwa, halafu utaturahisishia. Pia Mheshimiwa Mbunge anaweza akapata majibu, lakini nadhani nia yake ilikuwa Watanzania wasikie ulaji unaofaa ni upi? *(Makofi)*

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo hivyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Haya, basi Mheshimiwa Naibu Waziri nakupa nafasi usiwe na wasiwasi, hayo majibu yakiwa tayari tutakupa nafasi ya kuwaambia Watanzania ulaji unaofaa ni upi?

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, sasa aulize swali lake.

Na. 15

**Kuondoa Manunuzi Chini ya Shilingi Milioni 100 kwenye Mfumo wa NeST**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuondoa miradi chini ya shilingi milioni 100 katika Mfumo wa *NeST* ili kupunguza ucheleweshaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante, Mfumo wa *NeST* unawezesha matumizi ya njia ya ununuzi wa thamani ndogo usiotumia fedha

taslimu *(Minor Value Procurement Method)* kwa kazi za ujenzi hadi zenye thamani ya shilingi milioni 100. Kwa njia hii, taasisi nunuzi inaweza kununua moja kwa moja kutoka kwa muuzaji wa bidhaa, mkandarasi au mtoa huduma bila kuhitaji kuwashindanisha wazabuni zaidi ya mmoja. Kwa kupitia mfumo wa *NeST,* taasisi nunuzi itatumia siku zisizozidi tatu kukamilisha mchakato wote hasa kwa ununuzi wa miradi yenye thamani chini ya shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Spika, hivyo taasisi nunuzi zinashauriwa kutumia mfumo wa *NeST* na kuchagua njia ya ununuzi inayoendana na thamani ya mradi ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hasa hasa yenye thamani chini ya shilingi milioni 100, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Antipas Mngungusi, swali la nyongeza.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakandarasi wengi wale ambao wana sifa za kuendana na mfumo kwenye miradi midogo hawapatikani vijijini, mara nyingi wanatoka mijini. Muda wao wa kuji-*mobilize* kufika *site* kutoa huduma unakuwa mwingi na kazi huwa zinachelewa. Je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha kwamba inawapa upekee *local* fundi au wakandarasi wadogo kutotumia mfumo au kujengewa uwezo ili waweze kutosheleza vigezo vyao kusudi kazi ziweze kufanyika kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Antipas, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baadhi ya wakandarasi wale wadogo wadogo bado iko changamoto ya uelewa juu matumizi ya mfumo huu, lakini Serikali itaendelea kutoa elimu kwa *local* fundi na wale wote wenye mahitaji ya matumizi ya mfumo huu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Wafanyabiashara Wanaokwepa Kulipa Kodi Nchini**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza: -

Je, nini mkakati wa Serikali kumaliza tatizo la wafanyabiashara kukwepa kulipa kodi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, *TRA* imekuwa ikijikita kwenye matumizi ya teknolojia za kisasa ili kuboresha ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha ulipaji kodi unafanyika kwa uwazi na usahihi. Matumizi ya TEHAMA yameleta mabadiliko makubwa katika mfumo wa kodi nchini hasa kupitia zana kama vile *Electronic Fiscal Devices* na mifumo mingine ya kidijiti kama *vile E-filing, EFDMS, ITAX* na *TANCIS*. Matumizi ya TEHAMA katika mifumo ya kodi yameimarisha uwajibikaji, uwazi na kuongeza ufanisi wa *TRA* katika ukusanyaji wa mapato. Hii imepunguza ukwepaji kodi, kuimarisha nidhamu ya walipa kodi na kurahisisha shughuli za biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendesha kampeni za uelimishaji ili kuwawezesha wafanyabiashara kuelewa umuhimu wa kulipa kodi na mchango wake katika maendeleo ya Taifa letu. Elimu hii hutolewa kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina, redio, televisheni, elimu ya mlango kwa mlango, mikutano ya wadau, pamoja na matumizi ya mitandao ya kijamii kama vile *facebook*, *instagram*, *twitter (X)* na *whatsapp*. Lengo ni kuhakikisha wafanyabiashara na

wananchi kwa ujumla wanapata uelewa wa kutosha kuhusu haki na wajibu wao wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, vilevile sheria za kodi zimeimarishwa ili kuhakikisha kuwa hatua kali zinachukuliwa dhidi ya wale wanaokwepa kodi. Adhabu hizi ni pamoja na faini kubwa, kufungwa kwa biashara au kufunguliwa mashtaka ya jinai kwa wafanyabiashara watakaobainika kukwepa kodi. Ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa sheria za kodi, *TRA* pia inafuatilia kwa karibu utendaji wa Maafisa wake ili kuondoa uwezekano wa rushwa au upendeleo unaoweza kusababisha ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Serikali pia imeboresha mfumo wa kodi ili kuhakikisha viwango vya kodi vinawiana na hali halisi ya biashara, hivyo kuwaondolea wafanyabiashara mzigo wa kodi usio wa lazima na kuwatia moyo kulipa kodi kwa hiari bila kujihisi wanaonewa. Uboreshaji huu unalenga kuunda mazingira rafiki ya kufanya biashara bila kuathiri juhudi za Serikali kuongeza mapato, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maida Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza na ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miongoni mwa makusanyo ya kodi ni pamoja na utoaji na upokeaji risiti pale tunaponunua bidhaa dukani, na kwa kuwa wapo baadhi ya wafanyabiashara bado hawajaelewa suala la umuhimu wa kutoa risiti pale wanapouza bidhaa kwa visingizio kwamba kumekuwa na utitiri wa kodi kwa wafanyabiashara bila kuangalia mtaji wa mfanyabiashara huyo tangu bidhaa inatoka bandarini hadi kufika dukani, je, Serikali inalichukuliaje suala hili?

Swali la pili, kwa kuwa…

**SPIKA:** Mheshimiwa uliza kwa kifupi.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni tulipitisha sheria ya adhabu kwa wafanyabiashara wote wanaokwepa kodi, je, kutokana na malalamiko haya kwa wafanyabiashara, Serikali inasema nini au inalifanyia kazi kwa kiasi gani? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa ridhaa yako nijibu maswali yote mawili ya Mheshimiwa Maida, Mbunge wa Viti Maalum kwa pamoja. Kwanza, naomba nimpongeze sana kwa ufuatiliaji mkubwa wa jambo hili. Niseme tu kwamba ni kosa kisheria kwa mfanyabiashara kutotoa kodi na hata mnunuzi (mteja) kutodai risiti, tuwajibike. Tuna programu inaitwa Tuwajibike, inatakiwa mfanyabiashara lazima atoe risiti, ni wajibu wake na mteja wajibu wake ni kudai risiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuseme kwamba yule ambaye anafanya biashara, lakini hatoi risiti kwa bidhaa ambayo ametoa au kutoa risiti ambayo haiendani na uhalisia wa biashara ni kosa kwa mujibu wa sheria, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang’ata, Mbunge wa Viti Maaloum, sasa aulize swali lake.

Na. 17

**Ujenzi wa Vituo vya Polisi – Rukwa**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa Vituo vya Polisi vilivyoanza kujengwa Mkoani Rukwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa una Vituo vya Polisi vya Kata vinavyojengwa kwa kutumia nguvu za wananchi, ambavyo ni Kate, Kambo, Milepa, Ilemba na Kirando. Tathmini kwa ajili ya kumalizia ujenzi imefanyika na kiasi cha fedha shilingi 311,000,000/= kinahitajika.

Mheshimiwa Spika, ili kuunga mkono jitihada za wananchi, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imeviingiza vituo hivyo kwenye mpango wa kumaliza ujenzi wa maboma 77 ya Vituo vya Polisi vya Kata kuanzia mwaka wa fedha wa Bajeti ya Serikali 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia maboma hayo yaliyojengwa na wananchi, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Sumbawanga Mjini Kituo cha Polisi ni cha tangu enzi za mkoloni, ni kidogo na hakina hewa kabisa, wala hadhi ya mkoa. Ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Sumbawanga Mjini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Wilaya ya Kalambo haina Kituo cha Polisi kabisa na inaazima majengo kutoka CCM na shahidi wangu ni Mbunge mwenye Jimbo, kaka yangu Mheshimiwa Kandege, amekuwa akilalamika siku nyingi hapa kuwa hana Kituo cha Polisi Wilaya ya Kalambo. Ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Kalambo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Bupe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli Kituo cha Polisi cha Sumbawanga pale mjini ni cha zamani kama alivyosema na kimechakaa na Serikali tumeshafanya tathmini. Kinahitajika ni kiasi cha fedha shilingi 1,200,000,000. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 tumetenga shilingi milioni 400 tayari kwa kuanza ujenzi wa Kituo cha Daraja A pale Sumbawanga Mjini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kwa ukosefu wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Kalambo, hilo nimelichukua na tutaliingiza kwenye mpango kwa ajili ya kukijenga katika mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa.

Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa Serikali wa kujenga Kituo kidogo cha Polisi katika eneo la Kizota - Mbuyuni ambako kumekuwa kuna matukio ya uhalifu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani tayari ina mpango wa kujenga Vituo vya Polisi kwa awamu. Awamu ya kwanza ambayo inaanza kwa mwaka wa fedha 2024/2025 vituo 12, na kumaliza mabomba 76 kama alivyosema. Pia, ipo awamu ya pili ambayo itajenga Vituo vya Polisi mbalimbali ikiwemo na kata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitaangalia kwenye mpango wetu wa 2024/2025 kama Kituo cha Kizota kipo, kama hakipo nitakiweka kwenye mpango kwa ajili ya mwaka wa fedha unaokuja wa 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

Na. 18

**Kukamilisha Ujenzi wa Soko la Samaki – Nyakarilo Buchosa**

**MHE. ERICK J. SHIGONGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Soko la Samaki la Nyakarilo – Buchosa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa soko hilo la samaki, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara inaendelea na jitihada za kujenga, kuboresha na kukamilisha masoko mbalimbali ya samaki hapa nchini likiwemo soko la Samaki la Nyakarilo kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, ninaielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa kuweka ujenzi wa masoko ya samaki kwenye miradi yake ya kimkakati kwa kutenga fedha kupitia mapato yake ya ndani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERICK J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu la Serikali, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, zilitumika shilingi milioni 300 kujenga soko hili kwenye eneo ambalo sasa linajaa maji; na kwa kuwa, tayari Mkurugenzi wa Halmashauri ya Buchosa, Benson Mihayo, ameshatoa shilingi milioni 19: Je, Serikali iko tayari kuiunga mkono halmashauri kwa kutoa angalau shilingi milioni 100 ili tuweze kukamilisha ujenzi wa soko hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tumepokea taarifa kwamba eneo hilo ambalo tumejenga soko pale Nyakarilo limejaa maji na tumeshatuma wataalamu kwenda kufanya tathmini juu ya kiasi gani kinatakiwa kwa ajili ya kukarabati soko hilo. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kukarabati soko hilo na halmashauri nao waweke nguvu yao, na Wizara itaweka nguvu yake ili kuweza kukamilisha soko hilo liweze kukamilika vizuri, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Fidia kwa Waliowekewa Alama ya X Barabara ya Masasi – Liwale**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza: -

Je, lini wananchi waliowekewa alama ya X kwenye barabara ya Masasi mpaka Liwale watalipwa fidia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi wote ambao wamewekewa alama ya X kwenye barabara ya Masasi mpaka Liwale. Serikali itahakikisha inalipa fidia kwa mujibu wa sheria kabla ya ujenzi wa barabara hiyo kuanza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA AHMAD PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ni kulingana na sheria. Sasa nauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sheria inataka watu waliofanyiwa tathmini wawe wameshalipwa ndani ya miezi sita, lakini sasa ni zaidi ya miaka nane. Je, haoni kwamba hawatendei haki wananchi hao ili kuweza kufanya maendeleo?

Mheshimiwa Sika, swali la pili, kwa kuwa, umepita muda mrefu sasa, je, Serikali itafanya tathmini upya ili ipate gharama za miaka hii au itafanyaje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tathmini ilifanyika muda mrefu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria hiyo hiyo inatuelekeza kwamba kama hatutakuwa tumelipa ndani ya miezi sita lazima tufanye mapitio ya tathmini ili gharama ambayo inatolewa iende sambamba na gharama ya sasa ya watu ambao watapisha kama ni ardhi au majengo, tutafanya upya tathmini.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli tumechelewa, lakini lengo la Serikali ni kuijenga hiyo barabara tukiwa tayari tuna usanifu ili wananchi wasiweze kuendeleza maeneo ambayo wanajua barabara itajengwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tutakapokuwa tayari kuanza kuijenga, wananchi hao watalipwa kwa gharama ya kipindi hicho ambacho tutaanza kuijenga barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, barabara ya Mianzini Serikali ilishatoa nusu fidia, je, ni lini sasa Serikali itamalizia fidia iliyobaki kwa wananchi wa barabara hiyo ya Mianzini mpaka Ngaramtoni? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama anavyosema Mheshimiwa Mollel, Wizara tumeshalipa nusu na tulishaomba gharama hiyo ambayo imebaki kufidia Wizara ya Fedha na ninaamini wanalifanyia kazi na fedha itakapokuwa tayari wananchi hawa ambao wamepisha barabara watalipwa fidia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa twende Wizara ya Uchukuzi, nimejulishwa hapa, Serikali imeomba swali hilo lisiulizwe leo ili ilete majibu yanayofanana na swali. Kwa hiyo, swali Na. 20 halitaulizwa siku ya leo, tutalipangia siku nyingine.

Sasa kabla hatujaendelea, nawaletea matangazo tuliyonayo; Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo hapa. Tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu upande wa Serikali.

Jambo moja ninakumbushwa hapa mbele kuwa Waheshimiwa Naibu Mawaziri huwa mnakumbuka kuwapongeza baadhi ya Wabunge na wengine mnawasahau. Ukiamua kupongeza, pongeza wote mwanzo mpaka mwisho kwa sababu wote ni Waheshimiwa Wabunge, wanauliza maswali hapa kwa niaba ya wananchi. *(Makofi)*

Nilishawahi kutoa ushauri kwamba pengine iwe vinginevyo, lakini naona bado linajirejea. Kama umeamua wewe kuwa wa kupongeza, pongeza Waheshimiwa Wabunge wote ili asiwepo Mheshimiwa Mbunge anayejisikia kwamba pengine yeye hajauliza maswali yale ambayo yanawakilisha wananchi. Kwa hiyo, hilo tulizingatie. Nimeshalisema mara nyingi sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wako Bungeni asubuhi hii na tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika, hawa ni wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Yupo Ndugu Joseline Kamuhanda ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Masoko - *CRDB Bank* na Ndugu Ruby Mbwilo ambaye ni Meneja wa *Jembe Group*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard kutoka Jijini Dar es Salaam, hawa ni Ndugu Juliana Mwingira ambaye ni mke wake, karibu sana. Pia ameongozana na Ndugu Heri Ildephonce Leonard, ambaye ni kaka yake; Ndugu Laban Ildephonce Leonard, mdogo wake na Ndugu Sophia Asheli Ndahani ambaye ni shemeji yake, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu ambao ni Maafisa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Yupo Ndugu Elibariki Lyatuu ambaye ni Msaidizi Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kanda ya Kati, ameongozana na Ndugu Dickson Bisile ambaye ni Mkaguzi wa Ufanisi katika Kitengo cha Mahusiano ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Bunge. Ahsante sana na karibuni sana Bungeni wageni wetu. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mnaozungumza, bado nimesimama.

Tunao wageni wawili ambao ni watumishi kutoka Bunge la Malawi, ambao ni Ndugu Stella Banda ambaye ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu na Ndugu Julian Chamasova ambaye ni Karani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali; kwanza, mgeni wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini, huyu ni Mkurugenzi Mtendaji wa *Jembe Group* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Huyu ni yule niliyemtambulisha au ni mwingine? Haya, naambiwa huyu ni Mkurugenzi Mtendaji. Yeye amekaa upande upi? Haya, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Maimuna Pathan ambao ni dada zake kutoka Nachingwea, Mkoa wa Lindi pamoja na watoto wake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Abubakar Asenga ambaye ni Daktari wa Viungo kutoka Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Halima Mdee ambaye ni mdogo wake Kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tutaanza na wageni watano ambao ni Mhandisi Mgeni Kisinzah kutoka Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* na familia yake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 22 ambao ni Umoja wa Walimu Wakuu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 37 na walimu wanne wa Shule ya Sekondari Senge kutoka Mkoani Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 90 na walimu 10 wa Shule ya Sekondari Ihumwa kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa tunakaribia kuanza Mashindano ya 14 ya Mabunge ya Afrika Mashariki yatakayofanyika Desemba 2024.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo, tunaombwa kujiandaa vyema kwa ajili ya mashindano hayo. Kwa hiyo, tuhudhurie mazoezi, kwani hicho ni kigezo cha muhimu sana cha kujihakikishia nafasi kwenye safari hii.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, mnatangaziwa kuwa *IPU* kwa kushirikiana na *UNESCO* tumeanzisha kozi kwa njia ya mtandao kuhusu *Freedom of Expression for Parliaments and Their Members*. Kozi hii itatolewa bure na itaanza rasmi tarehe 28 Oktoba, 2024. Kwa hiyo, imeanza jana na itaendelea kwa wiki tano. Kozi hii itatolewa kwa lugha ya Kiingereza, Kifaransa, Kihispania na Kireno. Aidha, wahitimu watatunukiwa vyeti mwishoni mwa kozi hii.

Waheshimiwa Wabunge wote watakaopenda kujiunga na kozi hii wanataarifiwa kuwa usajili umefunguliwa tangu jana. Kwa hiyo, njia ya kuingia kwenye huo usajili mmeshatumiwa Waheshimiwa Wabunge wote.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanaohitaji kujisajili wafanye hivyo na wale wanaopata changamoto, maafisa walioko hapa Bungeni wanaweza kuwasaidia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023;**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na 11 Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023; na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hoja za Kamati. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC),* kwa niaba yake Mheshimiwa Kakunda.

Sasa, Mheshimiwa Kakunda kwa sababu nilishasema tutakupa muda, hapa katikati huruhusiwi kupita kwa sababu Siwa ipo. Kwa hiyo, rudi kule kazunguke hivi ili uje usome, huwezi kukatiza hapa mbele kwenye Siwa.

Mheshimiwa Kakunda, sasa hebu rejea. Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii itasomwa na Mjumbe wa Kamati hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI *(PAC)*:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali

kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu Zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 kama zilivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* na kuliomba Bunge liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya taarifa hii ni kulijulisha Bunge lako Tukufu, iwapo matumizi ya fedha za umma yamefanyika kwa namna iliyokusudiwa na Bunge na kwamba matumizi hayo yamezingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu za msingi. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla; sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa Ripoti za *CAG* na sehemu ya tatu, inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imeandaliwa kwa kuzingatia Kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kinachoainisha majukumu ya Kamati kama yanavyoonekana kwenye aya 1.3 ya taarifa kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilichambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mafungu 19 ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma 20, taasisi zinazojitegemea 27 na mifuko maalumu minne.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matokeo ya uchambuzi; uchambuzi wa Kamati umegawanyika katika maeneo makuu sita ambayo ni uchambuzi wa usimamizi wa mapato ya Serikali, uchambuzi kuhusu utawala bora, mifumo ya udhibiti wa ndani na usimamizi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, subiri kidogo. Haya endelea.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI *(PAC)*:** Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni uchambuzi wa ukaguzi maalumu, eneo la nne ni uchambuzi wa hoja za ukaguzi zinazohusu usimamizi wa mikataba; eneo la tano, uchambuzi wa hoja za ukaguzi zinazotokana na dosari katika usimamizi wa matumizi na mwisho ni uchambuzi wa hoja za jumla za ukaguzi katika uzingatiaji wa kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali, ukusanyaji wa mapato ya Serikali ni msingi mkuu katika kuchochea maendeleo ya uchumi wa nchi. Uchambuzi katika eneo hili ni kama ifuatavyo: -

(i) Nakisi ya shilingi trilioni 1.069. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya jumla ya shilingi trilioni 22.583, chini ya lengo lililowekwa la shilingi trilioni 23.652, ikionesha upungufu wa shilingi trilioni 1.069, sawa na 4.5% ya malengo ya mapato yote katika Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizosababisha kutofikia kwa lengo la makusanyo ni pamoja na:-

(a) Uwepo wa kodi zinazoshikiliwa zenye thamani ya shilingi trilioni 10.489 kutokana na kucheleweshwa kwa maamuzi ya mashauri ya rufaa za kodi;

(b) Dosari katika mfumo wa ving'amuzi vya kielektroniki wakati wa kuthibitisha bidhaa zinazopita nchini kwenda nchi jirani;

(c) Uwepo wa bakaa ya lita za mafuta 1,105,466.01 zilizoingizwa nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi jirani zenye

makadirio ya kodi ya shilingi milioni 929.6, ambayo hayakusafirishwa kwenda nje ya nchi; na

(d) Uwepo wa walipakodi 17,575, sawa na 49%, ambao hawakuwasilisha *return* za kodi ya ongezeko la thamani.

(ii) Upotevu mkubwa wa maji *(non revenue water),* katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira, Tanga wa 34% ambao unachangia kupunguza mapato ya mamlaka kwa wastani wa shilingi bilioni 5.28. Pia, uwepo wa deni la Taasisi za Umma la shilingi bilioni 2.3 ambazo Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga *(Tanga – UWASA)* inazidai taasisi za Serikali, limekuwa likikwamisha utekelezaji wa majukumu ya mamlaka kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini uwepo wa deni ambalo halijakusanywa na *DUWASA* la kiasi cha shilingi bilioni 5.1. Kati ya hizo, taasisi za Serikali ambazo ni pamoja na Polisi, Jeshi la Wananchi Tanzania, Hospitali ya Mkoa, Hospitali ya Mirembe, na Magereza zinadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 1.2. Madeni hasa ya taasisi za Serikali kama haya, na upotevu wa maji, yamekuwa yakipunguza uwezo wa *DUWASA*, Tanga *UWASA* na mamlaka nyingine katika kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuchelewa kurejesha mikopo katika Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma kiasi cha shilingi bilioni 5.72. Ukaguzi katika Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma ulibainisha uwepo wa mikopo ya muda mrefu ambayo haijarejeshwa kiasi cha shilingi bilioni 7.82. Kati ya hizo, shilingi bilioni 5.72 ni mikopo ambayo awali makato yalianzishwa baadaye yakasimamishwa na shilingi bilioni 2.09 ni madeni ambayo makato yake hayajaanza.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni uchambuzi wa hoja za ukaguzi kuhusu, utawala bora, mifumo ya udhibiti wa ndani na

usimamizi wa vihatarishi. Matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwa hoja zinazohusu masuala hayo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, tathmini ya ufanisi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Fungu 19 katika usimamizi wa fedha za umma. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kuimarisha uwezo wa Serikali katika kuratibu, kusimamia, kushauri na kuendesha mashauri yote ya madai na mashauri ya usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya vikwazo vilivyobainishwa kama changamoto kwa ofisi hii kiutendaji ni pamoja na upungufu wa watumishi, upungufu wa bajeti na mfumo uliopo wa uingiaji na usimamizi wa mikataba hali ambayo inaisababishia Serikali hasara inapotokea kuna shauri linafunguliwa na Serikali kushindwa.

Mheshimiwa Spika, pili, changamoto zilizopo katika umiliki na uendeshaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Dawa cha Keko. Uchambuzi wa Kamati umebaini dosari kadhaa kama ifuatavyo: -

(a) Kutokuwepo kwa Katiba ya Kampuni iliyoidhinishwa *(MEMART)* kinyume na matakwa ya kifungu 9(1) cha Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002;

(b) Kutothibitishwa uwepo wa deni la kiasi cha shilingi bilioni 21.4 ambalo *KPI* inadaiwa;

(c) Kutotangaza *KPI* katika Gazeti la Serikali kama Shirika la Umma;

(d) Kuwepo kwa mbia mwenza (binafsi) ambaye amekuwa akilipwa kiasi cha shilingi 15,000,000 kila mwezi kama ada ya ushauri, ushauri ambao Bodi na Menejimenti ya Kiwanda cha Madawa Keko hawajathibitisha faida yake;

(e) *KPI* kutekeleza majukumu yake bila ya kuwa na Cheti cha Ithibati *(Goods Manufacturing Practices, GMP)* kinachotolewa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba *(TMDA)*; na mwisho

(f) Kihatarishi cha *KPI* kuendelea na biashara kwa siku zijazo *(Going concern)* kwani Kampuni ina mtaji hasi *(Adverse working capital)* ambao umeongezeka kutoka shilingi bilioni 5.23 mwaka 2009 hadi shilingi bilioni 12.17 mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, tatu, utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya kiasi cha shilingi bilioni 32.7 katika Chuo cha Uhasibu Arusha bila kuwa na Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na gharama kubwa za miradi iliyokuwa inatekelezwa, kulikuwa na hoja zifuatazo: -

(a) Miradi husika ilikuwa inatekelezwa kwa kutumia *Force Account*;

(b) Miradi husika haikuwa imesajiliwa na Bodi za Kitaaluma na Kiufundi kama vile Bodi ya Usajili wa Wakandarasi *(CRB)*; na

(c) Miradi yote ilitekelezwa bila ya kuwa na ithibati ya Mamlaka ya Usalama Mahali pa Kazi *(OSHA)*.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne. Katika eneo hili ni kutokuunganishwa kielektroniki Mfumo wa Usimamizi wa Matukio *(EMS)* na Njia ya Malipo ya Serikali ya Kielektroniki *(GePG)* katika Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* na kutokuwepo baadhi ya kanuni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini dosari katika Mfumo wa Usimamizi wa Matukio *(EMS)* na Njia ya Malipo ya Serikali ya Kielektroniki *(GePG)* katika Bodi ya Utalii Tanzania. Mfano Kitengo cha Fedha hakikutengeneza ankara za malipo kutoka kwenye Mfumo wa Uratibu wa Maonesho na nambari za udhibiti kutoka kwa

*GePG*. Utoaji wa utoaji wa ankara za malipo nje ya Mfumo wa *GePG* ni kihatarishi cha upotevu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano katika eneo hili ni upungufu wa udhibiti wa ndani katika manunuzi ya gesi yanayofanywa na *TANESCO* kwa baadhi ya maeneo. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, *TANESCO* ilinunua gesi yenye thamani ya shilingi bilioni 543.1 ambayo ilitumika kuzalisha umeme kilowati 5,579,000 katika mitambo nane. Upungufu ufuatao ulibainika: -

(a) Hapakuwa na ushahidi wa baadhi ya mita za gesi kufanyiwa marekebisho *(calibration)* kama inavyotakiwa na Kanuni za Wakala wa Vipimo;

(b) Utofauti wa usomaji wa mita kati ya muuzaji na mita ya ukaguzi hivyo kusababisha hatari ya kutozwa na wazabuni gharama za ziada; na

(c) Kutoweka mita ya ukaguzi katika Kituo cha Ubungo,

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu la uchambuzi ni kuhusu uchambuzi wa Taarifa za Ukaguzi Maalumu. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya Kaguzi mbili Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi maalumu kuhusu ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo wa wanafunzi wa elimu ya juu inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kipindi cha 2015/2016 hadi 2023/2024 ulibaini yafuatayo: -

(a) Fedha za mikopo zilitolewa kwa wastani wa 91.6% ya bajeti kati ya mwaka 2015/2016 hadi 2021/2022;

(b) Changamoto katika kupima uhitaji wa mikopo na uwezo wa kugharamia mahitaji ya mikopo;

(c) Upungufu katika kanzidata ya Mfumo wa Mikopo unaofahamika kama *Integrated Loan Management System (ILMS);* na

(d) Bodi haikuweza kukusanya kiasi chochote kutoka kwa wanufaika 168,183 wanaodaiwa jumla ya kiasi cha shilingi trilioni 2.2.

Mheshimiwa Spika, aidha, uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi maalumu kuhusu ugavi na usambazaji wa vifaatiba kwa ajili ya huduma za mama na mtoto ulibaini hoja zifuatazo ambazo utekelezaji wake haujakamilika: -

(a) Baadhi ya vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 3.3 vilikuwa havijanunuliwa ili kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma;

(b) Baadhi ya vifaa vilipelekwa katika vituo ambapo havikuwa vimepangwa hapo awali;

(c) Baadhi ya vifaa vilipelekwa katika maeneo ambayo vilikuwa havitumiki;

(d) Vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 417 viliwasilishwa kwa idadi ya juu zaidi ya mahitaji; na

(e) Upungufu kadhaa katika uandaaji wa nyaraka mbalimbali za mradi katika awamu zake za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni uchambuzi wa hoja za ukaguzi zinazotokana na usimamizi wa mikataba. Katika eneo hili, upungufu uliobainika katika Mkataba wa Makubaliano *(Memorandum of Understanding)* kati ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* na *London School of Hygiene*

*and Tropical Medicine* ambao umesababisha athari katika uendeshji wa shughuli za *Mwanza Intervention Trials Unit (MITU)* ni kama ifuatavyo: -

(a) Kuikosesha Serikali mapato kutokana na kwamba *MITU* imekuwa ikiendeshwa kama Kampuni binafsi na kutumia mali za Taasisi ya *NIMR*;

(b) Kutokufikiwa kwa malengo ya uanzishwaji wake ikiwa ni pamoja na kuboresha zaidi tafiti za afya zinazofanyika nchini Tanzania; na

(c) Kumekuwepo na ushindani kati ya *NIMR* na *MITU* katika kutafuta fedha za ufadhili wa Miradi ya Utafiti kinyume na makubaliano.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine katika eneo hili ni ongezeko la deni ambapo *TPDC* inaidai *TANESCO* kutokana na kutolipwa ankara za mauzo ya gesi kiasi cha shilingi bilioni 713.5 kutoka kiasi cha shilingi bilioni 579 zilizoripotiwa mwaka 2021/2022. Hili ni ongezeko la 23%.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano la uchambuzi ni hoja za ukaguzi zinazotokana na dosari katika usimamizi wa matumizi. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu hoja zinazotokana na usimamizi wa matumizi katika baadhi ya taasisi za umma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, kutokuwepo mfumo thabiti wa udhibiti wa matumizi ya mafuta ya magari katika Shirika la *TANESCO*. Kamati ilibaini gharama za juu za matumizi ya mafuta zinazotokana na kutokuwepo kwa mfumo thabiti wa kufuatilia matumizi ya mafuta na umbali ambao magari yanatembea badala yake *TANESCO* inategemea vitabu vya kumbukumbu *(log books)* kama nyenzo ya kudhibiti matumizi ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili katika eneo hili, ni hasara ya shilingi bilioni 3.266 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa kutokana na kukataliwa madai ya *NHIF*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini uwepo wa hasara ya shilingi bilioni 3.266 inayotokana na kukataliwa kwa madai ya Hospitali ya Benjamin Mkapa kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)*. Sababu zilizofanya kukataliwa kwa madai hayo ni pamoja na hospitali kushindwa kutimiza matakwa ya Sheria ya *NHIF* kuhusu mwongozo wa viwango vya matibabu na utofauti wa bei za matibabu kati ya Hospitali ya Benjamin Mkapa na bei zilizoainishwa na *NHIF* kulingana na mwongozo wa matibabu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, matumizi ya shilingi 257,334,800 kukarabati Mgodi wa Kiwira bila kuanza uzalishaji. Mnamo mwaka 2022, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* lilifanya ukarabati mkubwa wa Mgodi wa Kiwira kwa kutumia shilingi milioni 257.3. Hata hivyo, pamoja na ukarabati huo, wakaguzi walipotembelea mgodi huo tarehe 28 Agosti, 2023 walikuta shughuli za mgodi zilikuwa hazijaanza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, eneo la sita la uchambuzi ni hoja za ukaguzi za ujumla zinazohusu uzingatiaji wa sheria, taratibu na kanuni *(Compliance)*. Baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kutozingatia Mwongozo wa Wizara ya Fedha katika utunzaji wa mali za Serikali kwenye Mfumo wa Kielektroniki *(GAMIS)*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kupitia Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2021/2022 ilitoa Mwongozo Kuhusu Usimamizi wa Mali za Serikali kwa Kutumia Mfumo wa Kielekroniki *(GAMIS)*. Hata hivyo, Taasisi nyingi za Serikali hazizingatii mwongozo huo kama jedwali Na. 2.6 lilivyoainisha.

Mheshimiwa Spika, pili, changamoto ya kutokuzingatia miongozo ya *IPSAS* katika kuandaa hesabu za baadhi ya Sekretarieti

za Mikoa. Kamati ilibaini baadhi ya Sekretarieti za Mikoa zina changamoto ya kutozingatia Miongozo ya Kimataifa ya Uhasibu katika sekta ya umma wanavyofunga hesabu zao. Hoja hii ilibainika katika hesabu za Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza na Tabora, ambapo vitabu vya hesabu *(financial statements)* vilisainiwa bila ya kuwa na viambatisho muhimu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, kuhusu kutofikiwa lengo la ukusanyaji wa mapato ya *TRA* kwa kiasi cha shilingi trilioni 1.069, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Mamlaka ya Mapato Tanzania ikamilishe maboresho ya ujenzi na usimikaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kuondokana na changamoto kwenye taarifa zinazopatikana kwenye mifumo iliyokuwa inatumika hapo awali. Aidha, *TRA* iendelee na kukamilisha zoezi la kusafisha taarifa za kwenye mifumo *(Data clean up exercise)* ili kuondoa changamoto ya uwepo wa taarifa zisizo sahihi za walipakodi;

(b) *TRA* ikamilishe zoezi la kutambua na kusajili idadi halisi ya walipakodi waliopo hapa nchini ili kuwezesha kutambua kila aina ya kodi na kiasi kinachotakiwa au kinaweza kukusanywa kutoka kwa walipakodi husika. Aidha, *TRA* ihuishe kanzidata ya walipakodi *(Taxbase)* ili kupata uhalisia wa mwenendo wa ukusanyaji wa kodi na kupanua wigo wa kodi; na mwisho

(c) *TRA* ianze kuandaa hesabu zake za kila mwaka kwa kutumia mfumo wa *Revenue Statements and Financial Statements* ili kuondoa uwezekano mkubwa wa kuwa na makosa ambayo huathiri taswira halisi *(fair view)* ya vitabu vya hesabu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu deni ambalo *TANESCO* inadaiwa na Kampuni ya *TPDC*. Bunge linaazimia kwamba: -

(a) *TANESCO* iandae na kutekeleza kikamilifu mkakati na mpango wa malipo *(payment schedule)* ili kuhakikisha malipo ya deni la *TPDC* yanafanyika kwa wakati, hali itakayoepusha ukuaji wa deni; na

(b) *TANESCO* ishirikiane kikamilifu na *TPDC* katika kusuluhisha ankara zinazobishaniwa na kuhakikisha ankara zote ambazo hazijalipwa zinazohusiana na *TPDC* zinatatuliwa ipasavyo na kwa makubaliano.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu Ukaguzi Maalumu wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Baada ya kukamilika mapitio ya uendeshaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu yanayoendelea, Serikali iangalie uwezekano wa kuifanya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuwa Mfuko ili kuipa uwezo wa kupata vyanzo vya ziada vya fedha ikiwemo kuwekeza kwa faida na kujenga uwezo stahimilivu kukopesha wanafunzi wengi wenye uhitaji ambao mahitaji yanaongezeka mwaka hadi mwaka;

(b) Serikali na Bodi iweke utaratibu ambao utahakikisha wanafunzi wote wanaoomba mikopo ya Elimu ya Juu na waliopo vyuoni ambao hawana Namba ya Kitambulisho cha Taifa *(NIDA)* wapatiwe ili kurahisisha taratibu za uombaji na wepesi wa utambuzi wakati wa urejeshaji wa mikopo;

(c) Serikali iendelee kutilia mkazo kuunganishwa kwa mifumo ya kieletroniki kwa taasisi zote za umma ili kurahisisha zoezi la kuwabaini wanufaika wote wa Mikopo ya Elimu ya Juu na kuongeza ufanisi kwenye urejeshwaji wa mikopo; na

(d) Kwa kuzingatia hali ya makusanyo ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliyoiva kutoka kwa wanufaika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inashauriwa kutoa maagizo kwa wadau wote kusaidia shughuli za urejeshaji wa mikopo kwa kuweka kigezo cha hali ya mkopo wa mwombaji wa nyaraka kibali cha utoaji huduma kama sharti la awali kabla ya kutoa nyaraka za kisheria.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu kuiimarisha na kuijengea uwezo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe wigo wa Bajeti wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali unaongezeka ili kuboresha mazingira ya kazi na ubora wa huduma zitolewazo na Ofisi hiyo;

(b) Serikali iwajengee uwezo Mawakili kwa kuwapatia mafunzo katika maeneo maalumu ya kimkakati;

(c) Serikali iweke utaratibu ambao utawezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kushiriki kikamilifu katika hatua za awali za uingiaji na utekelezaji wa mikataba inayoingiwa na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ili kuikinga Serikali na hasara zinazotokana na Serikali kushitakiwa kwenye kesi za madai; na

(d) Serikali ihakikishe masuala ya uwekezaji yanasimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria na mikataba inayokuwa imeingiwa ili kuepusha madai makubwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo la tano kuhusu Mkataba wa Makubaliano kati ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* na *London School of Hygiene and Tropical Medicine*, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ifanye mapitio ya mkataba wa makubaliano husika ili kuhakikisha yanazingatia sheria mama ya *NIMR* na kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa; na

(b) *NIMR* ihakikishe hesabu za kila robo mwaka na za mwaka za Kituo cha *Mwanza Intervention Trials Unit (MITU)* zinaandaliwa na kupitiwa kwa pamoja kisha ziwasilishwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, eneo la sita kuhusu kukataliwa madai ya hospitali yanayopelekwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF),* Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kushirikiana na hospitali waboreshe utaratibu uliopo wa uandaaji wa nyaraka sahihi na utaratibu mzuri wa malipo ili kuhakikisha kwamba madai ni sahihi, ikijumuisha uhakiki wa nambari za malipo, kutoa maelezo ya awali ya huduma zitolewazo na kutunza rekodi sahihi za wagonjwa;

(b) *NHIF* iendelee kutoa mafunzo na elimu ya mara kwa mara kwa watumishi wa kada ya afya kuhusu Kanuni na Miongozo ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na utaratibu wa malipo ili kusaidia kupunguza makosa na kuboresha taarifa;

(c) *NHIF* ianze mchakato wa mapitio ili kubaini madai yaliyo sahihi na madai yasiyo sahihi. Hii inatakiwa kujumuisha mawasiliano thabiti na watoa huduma husika ili kuthibitisha uhalali wa madai hayo kabla hayajawasilishwa *NHIF* au kukataliwa; na

(d) Kuanzishwe mfumo utakaowezesha hospitali kupata mrejesho wa madai yaliyokataliwa na Mfuko kwa wakati ili kuweza kufanya marekebisho kwa wakati na kuyapeleka kwa muda unaoruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, eneo la saba, kuhusu umiliki na uendeshaji wa Kiwanda cha Utengenezaji Madawa cha Keko *(KPI)*, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Madeni yote ya Kiwanda cha Madawa Keko yafanyiwe uhakiki wa kina ili kubaini usahihi na uhalali wake;

(b) Serikali ikamilishe mchakato wa uhamishaji wa hisa na kutiwa saini kwa nyaraka muhimu mapema iwezekanavyo;

(c) Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina iangalie uwezekano wa kuikabidhi *KPI* kiwe chini ya uendeshaji wa *MSD* kama kampuni tanzu; na

(d) Serikali iangalie uwezekano wa kutoa mtaji kwa ajili ya kiwanda kununua mitambo mipya ya uzalishaji wa dawa kutokana na mitambo inayotumika hivi sasa kuwa ya muda mrefu na chakavu. Hatua hii itasaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kununua dawa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, eneo la nane kuhusu madeni ambayo Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zinadai Taasisi za Umma, Bunge linaazimia kwamba kabla ya kukamilika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji ziandae na kutekeleza mkakati wa uwajibikaji ambao utawezesha ufuatiliaji wa malipo ya Taasisi za Umma kwa Mamlaka za Maji. Mkakati huu utasaidia kupata suluhisho la kudumu litakalohakikisha kuwa huduma za maji zinaendelea kutolewa bila kutatizwa na madeni ya Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo la tisa kuhusu mita za kupima kiasi cha gesi inayonunuliwa na *TANESCO* kuzalisha umeme kwa baadhi ya vituo, Bunge linaazimia kwamba ndani ya kipindi cha miezi sita, *TANESCO* ikamilishe ufungaji na upimaji wa mita za kudhibiti manunuzi ya gesi katika maeneo ambapo mita zilibainika kuwa na

changamoto ya kutofanyiwa vipimo kwa mujibu wa Kanuni za Wakala wa Vipimo. Hatua hii itasaidia kutambua kiasi halisi cha gesi inayonunuliwa na kutumika, hivyo malipo yataendana na ankara halisi kwa matumizi halisi.

Mheshimiwa Spika, eneo la kumi, kuhusu Uzingatiaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Serikali *(GAMIS)*, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Ifikapo tarehe 30 Juni, 2025 Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali ziwe zimetekeleza kikamilifu Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2021/2022 kuhusu Usimamizi wa Mali za Serikali, kwa kuhakikisha mali zote za Serikali zimeingizwa katika Mfumo wa Kielektroniki *(GAMIS)* unaoratibiwa na Wizara ya Fedha; na

(b) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 Mlipaji Mkuu wa Serikali achukue hatua stahiki kwa Maafisa Masuuli wote watakaoshindwa kutekeleza masharti ya Waraka huo baada ya muda uliowekwa kukamilika.

Mheshimiwa Spika, eneo la kumi na moja, kuhusu kuziwezesha Sekretarieti za Mikoa kuandaa hesabu kwa kuzingatia Miongozo na Viwango vya Kimataifa *(IPSAS)*, Bunge linaazimia kwamba Wizara ya Fedha kupitia Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iandae mkakati maalumu wa kuzijengea uwezo Idara za Fedha katika Sekretarieti za Mikoa hapa nchini ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hatua hii itasaidia kuimarisha usimamizi wa fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, eneo la kumi na mbili kuhusu Ukaguzi Maalumu wa Ugavi na Usambazaji wa Vifaatiba kwa Ajili ya Huduma za Mama na Mtoto, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TAMISEMI, wahakikishe wanakamilisha ununuzi wa vifaa ambavyo bado havijanunuliwa na

kuvipeleka katika vituo vilivyokusudiwa ili kuweza kutoa huduma iliyokusudiwa;

(b) Wizara ya Afya ihakikishe kwamba inafuatilia ukamilishaji wa mradi kama ulivyokuwa umepangwa ili thamani ya fedha iweze kupatikana na wananchi waweze kupata huduma kwa wakati; na

(c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye uhakiki wa kina wa majibu ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mradi huu katika ukaguzi unaoendelea hivi sasa. Baada ya uhakiki wa majibu ya utekelezaji wa mradi, Bunge lijulishwe ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la kumi na tatu kuhusu Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* kutengeneza ankara za malipo nje ya mfumo na kutokamilika Kanuni za Sheria ya *TTB* Sura 364, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Kabla ya kukamilika mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao wakamilishe maboresho ya mfumo ili uweze kusomana na Mfumo wa Malipo wa Serikali *(GePG)*;

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB),* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao, wakamilishe maboresho ya mfumo ili uweze kusomana na Mfumo wa Malipo wa Serikali (GePG); na

(b) Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utalii atekeleze masharti ya Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura 364, inayompa mamlaka ya kutengeneza kanuni ili kusaidia utekelezaji wa Sheria ipasavyo. Kanuni hizo, mathalani Kanuni za Mabalozi wa Hiari wa Utalii ni muhimu ili kusaidia katika kuongeza makusanyo ya fedha za umma kupitia Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa miongozo yako kwa kamati. Aidha, namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kusaidia kuliongoza Bunge letu. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka I. Leonard kwa uongozi wake wa Sekretarieti ya Bunge ambayo imeratibu na kufanikisha shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(NAOT)*. Aidha, naishukuru Wizara ya Fedha na Maafisa wao wote kwa ushirikiano walioutoa katika kuratibu shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na Wajumbe wa Kamati wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

## TAARIFA YA KAMATI KUHUSU RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 kama zilivyokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kuliomba Bunge liipokee na kuijadili. Madhumuni ya Taarifa hii ni kulijulisha Bunge lako Tukufu, iwapo matumizi ya Fedha za Umma yamefanyika kwa namna

iliyokusudiwa na Bunge na kwamba matumizi hayo yamezingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kurahisisha ufuatiliaji wa taarifa hii, naomba kubainisha sehemu kuu tatu za msingi. Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo muundo wa Taarifa, majukumu ya Kamati, msingi wa kazi za Kamati na muhtasari wa matokeo ya Uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lengo la Sehemu hii ni kubainisha muktadha wa Taarifa ili kuwezesha ufuatiliaji utakaosaidia kufanya uamuzi.

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma.Katika Sehemu hii, Taarifa inafafanua mambo ya msingi kuhusu uchambuzi na kubainisha matokeo ya uchambuzi huo. Lengo la sehemu hii ni kuonesha dosari zilizobainika katika matumizi ya Fedha za Umma na kuweka msingi wa mtazamo wa Kamati kuhusu Matumizi ya Fedha za Umma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023. Sehemu hii inajenga msingi wa Sehemu ya Tatu inayohusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati.

### 1.3 Majukumu ya Kamati

**Mheshimwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 13 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ina majukumu yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**1.4 Njia Zilizotumika Katika Utekelezaji wa Kazi za Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Bunge Toleo la Februari, 2023 zimeweka masharti kwamba Taarifa yoyote ya Kamati inayoingia Bungeni, inatakiwa kubainisha njia zilizotumiwa na Kamati kufanya kazi inayotolewa Taarifa. Kwa msingi huo naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii. Njia hizo ni zifuatazo: -

a) Mapitio ya jumla ya Ripoti za CAG ili kubaini maeneo ya kuwekea mkazo na kukidhi masharti ya Ripoti hiyo ulikuwa msingi wa kazi za Kamati zilizopangwa kwenye Ratiba;

b) Kupokea Vidokezo ("briefs") vya Ripoti za CAG kwa hoja za ukaguzi za mafungu yaliyopangwa kujadiliwa na Kamati kabla ya Kukutana na Afisa Masuuli anayehusika. Mbinu hii iliiwezesha Kamati kuzielewa hoja na wigo wa mahojiano na Afisa Masuuli kwa lengo la kupata undani wa tatizo la matumizi mabaya ya fedha za umma;

c) Mahojiano na maafisa masuuli kuhusu hoja za ukaguzi ili kupata undani wa matatizo ya matumizi ya fedha za umma na kubaini chimbuko la tatizo, wigo wa dosari na uwezekano wa kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za Wakaguzi wa hesabu za Fungu linalohusika kwa pamoja na majibu ya Menejimenti za Taasisi, Wizara au Shirika lililokaguliwa. Lengo ni kuelewa kwa kina muktadha wa hoja na matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma; na

e) Tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma. Lengo la njia hii ni kuona na kuutumia uzoefu wa jumla unaopatikana kwa tafiti hizo ili kutathmini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kama yalivyoainishwa na CAG.

**Mheshimiwa Spika,** njia na mbinu hizo ziliiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa kina kwa nia ya kulishauri Bunge kuhusu hatua za kuchukua. Mbinu hizo ziliendana na matumizi na marejeo ya miongozo ifuatayo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoonesha dhamana ambayo Serikali imepewa na wajibu wa Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwemo eneo la matumizi ya fedha za umma.

b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 inayofafanua masharti muhimu kwa ajili ya kuwezesha ukaguzi, uandaaji wa Ripoti za CAG, uwasilishaji wake na hatimaye kujadiliwa na Kamati;

c) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 inayoweka miongozo ya matumizi ya fedha za umma na kusaidia kuamua iwapo kuna matumizi mabaya ya fedha za umma;

d) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, inayohusika na usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma kwa kuweka taratibu za utekelezaji wa bajeti na usimamizi wake;

e) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 inayogusa usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma katika mashirika ya umma;

f) Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410, inayoweka taratibu za kufuatwa wakati wa ununuzi wa bidhaa, huduma na kuingia mikataba kwa gharama ambazo zinahusisha matumizi ya fedha za umma;

g) Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286, inayosimamia weledi wa wahasibu na wakaguzi ili kuwezesha kumbukumbu za kutumainiwa za fedha na usimamizi bora wa matumizi ya Fedha za Umma;

h) Sheria ya Kinga Madaraka na Haki za Bunge, Sura 296 inayoliwezesha Bunge, Wabunge na Kamati za Bunge kupata stahili kutokana na madaraka yake na kupata ushahidi bila vikwazo wakati wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma; na

i) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 zinazobainisha utaratibu wa Ripoti za CAG kuhusu matumizi ya fedha za umma kuwasilishwa Bungeni, kushughulikiwa na Kamati na hatimaye Kamati kutoa Taarifa hii.

### 1.5 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha mwezi Agosti 2024 hadi Novemba 2024, shughuli za Kamati zilijielekeza katika kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika wizara na mashirika ya umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Aidha,

shughuli hizo zilikusudia vilevile kufuatilia utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa nyakati tofauti kwa kipindi chote cha mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2023, kwa upande wa Serikali Kuu, CAG alikagua na kutoa Hati za ukaguzi kwa Wizara na Idara za Serikali **64**, Balozi **43**, Sekretarieti za Mikoa **26**, Wakala **30** na Mifuko Maalumu **19.** Aidha, katika kundi hilo la Serikali Kuu, Kaguzi za Vyama vya Siasa **19**, Hospitali za Rufaa na Maalumu **34** na Taasisi nyinginezo **266** zilifanyika na kukamilika. Hali kadhalika, ukaguzi ulijumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa (consolidated accounts) na ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaafu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/23, katika mafungu ya Serikali Kuu, CAG alitoa jumla ya Hati **475** kwa Taasisi ambazo ziliwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi. Kati ya hizo, Hati **471** zilikuwa zinaridhisha, Hati **1** ilikua Hati yenye shaka, Hati **1** ilikuwa mbaya, na CAG alishindwa kutoa maoni kwa Taasisi **2**.


**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mashirika ya Umma, jumla ya kaguzi **215** zilifanyika, ambapo katika kaguzi hizo Hati zilitolewa kwa Mashirika **215** ambapo kati ya hizo, Hati **211** zilikuwa Hati zinazoridhisha, **4** ni Hati zenye shaka. Kwa mwaka huu tunaoutolea Taarifa hapakutolewa Hati mbaya katika Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mafungu 19 ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma 20, Taasisi zinazojitegemea 27 na Mifuko Maalumu 4.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa Taasisi zilizofika mbele ya

Kamati kwa mahojiano umebainishwa katika Chati Na. 1.1 hapa chini: -

**Chati Na. 1.1: Mchanganuo wa Taasisi Zilizofika Mbele ya Kamati Kati ya Agosti - Novemba, 2024**




**Chati.Na. 1.1: Mchanganuo wa mafungu yaliyofika mbele ya Kamati kati ya Agosti – Novemba, 2024.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kina wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati kwa kila fungu unapatikana katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

**1.6 Ufuatiliaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 13(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa maoni, ushauri, mapendekezo na maazimio ya Kamati na Bunge kwa nyakati tofauti tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** jambo hili hufanyika kwa CAG kufanya uhakiki wa maoni na mapendekezo yanayokuwa yametolewa na Kamati kwa fungu husika. Aidha, kila fungu linapofika mbele ya Kamati, CAG huipitisha Kamati kwenye taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati kwa fungu husika kabla ya kuanza kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu za fungu hilo.

### 1.7 Vigezo vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, uaandaji wa vigezo vya kuzingatiwa ni jambo muhimu katika uhakiki na tathmini yoyote. Suala la matumizi mabaya ya fedha za umma linaweza kubainika kutokana na vigezo vya matumizi ya fedha za umma. Aidha, uamuzi wa kuwahoji Maafisa Masuuli kutokana na Ripoti za CAG ni jambo lililohitaji kuwekewa vigezo. Kwa sababu hiyo, baada ya kupokea Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ilitengeneza vigezo muhimu vya kuzingatia katika kutimiza majukumu yake ya Kikanuni. Vigezo hivyo vilitoa mwongozo wa uchaguzi wa mafungu ambayo yalipewa kipaumbele katika uchambuzi na mahojiano na Maafisa Masuuli.

**Mheshimiwa Spika**, vigezo vilivyozingatiwa wakati wa kuchagua vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za Kamati vilikuwa kama ifuatavyo: -

a) Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na CAG;
b) Maslahi ya Umma kuhusu hoja za fungu linalohusika;
c) Hali ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa fungu linalohusika;
d) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;
e) Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa fungu linalohusika;

f) Kuleta uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa fungu husika kwa siku za nyuma;
g) Kutoa kipaumbele kwa Sekta na Mashirika Mkakati (Strategic sectors and parastatals) kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya sasa ya Serikali;
h) Kaguzi maalum (Special audit) zilizofanyika hivi karibuni; na
i) Uzingatiaji wa kaguzi za ufanisi kwa mwaka husika.

**Mheshimiwa Spika,** vigezo hivyo viliisaidia Kamati kuendelea na mchakato wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Ripoti za CAG.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ulibainisha mambo yafuatayo kuhusu matumizi na usimamizi wa fedha za umma: -

### 2.1 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

**Mheshimiwa Spika,** ukusanyaji wa mapato ya Serikali ni msingi katika kuchochea maendeleo ya uchumi wa nchi. Uchambuzi wa Kamati katika eneo hili umelenga kuangazia mifumo iliyopo, changamoto, ufanisi na kutoa mapendekezo ya kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia ukaguzi uliofanywa na CAG kwa baadhi ya Taasisi za Umma zinazokusanya mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** umuhimu wa kuchambua hali ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali unatokana na msingi wa faida za mapato hayo. Faida hizo ni pamoja na kuwezesha kuboresha huduma za afya, elimu na miundombinu. Aidha mapato hayo

hutumika kukuza uchumi na utekelezaji wa miradi ya Serikali katika miradi ya maendeleo ili kupunguza umasikini.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uchambuzi wa hali ya usimamizi wa makusanyo ya mapato ya Serikali kwa Taasisi zilizofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Nakisi ya Sh. Trilioni 1.069 Katika Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023. Lengo kubwa la uchambuzi wa taarifa hiyo ilikuwa ni kufanya tathmini ya hali halisi ya ukusanyaji wa mapato chini ya Mamlaka hiyo ukilinganisha na lengo lililokusudiwa. Hali kadhalika, Kamati ilijielekeza kupitia na kuchambua matumizi ya fedha yanayofanywa na TRA katika shughuli za ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya jumla ya **Sh. Trilioni 22.583**, chini ya lengo lililowekwa la **Sh. Trilioni 23.652**, ikionesha upungufu wa Sh. **Trilioni 1.069**, sawa na **4.5%** ya malengo ya mapato yote katika Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Tanzania Bara ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 2.1 hapa chini: -

**Jedwali Na. 2.1: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato Tanzania Bara.**

| Idara | Makisio (Sh. Bilioni) | Makusanyo halisi (Sh. Bilioni) | Makusanyo ziada/punguf u (Sh. Bilioni) | Asilimia ya ziada/ pungufu |
|---|---|---|---|---|
| Kodi za ndani | 5,024.15 | 5,287.19 | 263.04 | 5.2 |
| Walipa kodi wakubwa | 9,801.057 | 9,032.31 | (769.26) | (7.8) |
| Ushuru na forodha | 9,432.27 | 9,325.51 | (106.77) | (1.1) |
| **Jumla ya makusanyo** | **24,257.99** | **23,645.01** | **(612.99)** | **(2.5)** |
| Punguza: marejesho ya kodi na hamisho kwenda ZRB | 657.83 | 1,079.05 | 421.21 | 64 |
| **Jumla baada ya marejesho ya kodi na hamisho** | **23,600.16** | **22,565.96** | **(1,034.20)** | **(4.4)** |
| Ongeza: vocha za hazina (TVC) | 52.60 | 17.58 | (35.02) | (66.6) |
| **Jumla** | **23,652.76** | **22,583.54** | **(1,069.22)** | **(4.5)** |

**Chanzo: Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa TRA kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.**

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.1 hapo juu, Kamati imebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/23, utendaji wa Idara za Walipakodi Wakubwa na Ushuru na Forodha


katika ukusanyaji wa mapato ulikuwa chini ya malengo yaliyokusudiwa, wakati Idara ya Kodi za Ndani ukusanyaji ulikuwa juu ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi umebaini kwamba, kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato kulitokana na kutofikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa ushuru wa bidhaa (excise duty), kodi ya zuio (withholding tax), ushuru wa mafuta (fuel levy), kodi yaongezeko la thamani (VAT), na kodi ya faida (corporate tax).

**Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuchambua hali ya ukusanyaji wa mapato, Kamati iliweza kubaini kwamba, kulikuwa na ufanisi katika marejesho ya kodi (tax refund), kutokana na ongezeko la kasi ya kuhakiki madai yaliyowasilishwa. Hali hii ilisababisha ongezeko la kiasi kilichorudishwa kwa walipakodi ikilinganishwa na kiasi kilichokadiriwa. Jambo hili ni muhimu kwa kuwa linapunguza malalamiko ya siku za nyuma ya walipa kodi kucheleweshewa marejesho ya kodi kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya pia ulinganifu wa kila idara katika ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka ya Mapato (Tanzania Bara). Katika ulinganifu huo, ilibainika kuwa, Idara ya Ushuru na Forodha ilichangia asilimia 39.4 ikifuatiwa na Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa asilimia 38.2, na Idara ya Kodi za Ndani kwa 22.4%. Mchanganuo wa ukusanyaji wa mapato kiidara katika Tanzania Bara umechambuliwa katika Chati Na. 2.2 hapa chini.

**Chati Na.2:1: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato Kiidara, Tanzania Bara.**




**Chanzo: Uchambuzi wa Kamati Katika Taarifa ya Hesabu za TRA, kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar, ilikusanya jumla ya **Sh. Bilioni 456.19**, ikiwa ni zaidi ya lengo lililowekwa la **Sh. Bilioni 454.06**, hivyo kusababisha ukusanyaji wa ziada wa **Sh. Bilioni 2.14**, sawa na 0.5%. Mchanganuo wa makusanyo kiidara kwa Zanzibar umefafanuliwa katika Jedwali Na. 2.2 hapa chini.


**Jedwali Na. 2.2: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato Kiidara Zanzibar.**

| Idara | Makisio Bilioni) (Sh. | Makusanyo (Sh. Bilioni) halisi | Makusanyo ziada/punguf u (Sh. Bilioni) | Asilimia ya ziada/ pungufu |
|---|---|---|---|---|
| Kodi za ndani | 226.02 | 231.85 | 5.83 | 2.6 |
| Ushuru na forodha | 228.04 | 224.35 | (3.6.9) | (1.6) |
| **Jumla ya makusanyo** | **454.06** | **456.19** | **2.14** | **0.5** |

**Chanzo: Taarifa Hesabu zilizokaguliwa TRA kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Zanzibar, kama Jedwali Na. 2.2 hapo juu linavyobainisha, ukusanyaji wa mapato ulionesha kuwa Idara ya Kodi za Ndani ilichangia 50.8% ikifuatiwa na Idara ya Ushuru na Forodha kwa 49.2%. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato Zanzibar umeainishwa katika Chati Na. 2.3 hapa chini: -

**Chati Na. 2.2: Mchanganuo wa Makusanyo ya Mapato Kiidara (Zanzibar)**




**Chanzo: Uchambuzi wa Kamati Katika Taarifa ya Hesabu za TRA, kwa Mwaka wa Fedha, 2022/2023.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada kubwa za Serikali kupitia TRA katika ukusanyaji wa mapato kama mwenendo wa ukusanyaji mapato ulivyobainishwa hapo awali. Hata hivyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kuna changamoto kadhaa ambazo taarifa za ukaguzi zilibainisha ambazo zilichangia kutofikiwa malengo ya ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto zilizobainishwa na Kamati ni kama ifuatavyo: -

a) Uwepo wa kodi zinazoshikiliwa zenye thamani ya **Sh. trilioni 10.489**. Uchambuzi wa Kamati ulibaini uwepo wa mashauri 967 ya kikodi katika mahakama za rufaa za kodi kwa muda mrefu yanayofikia **Sh. Trilioni 10.489** (inahusisha dola za Marekani

19,261,725 zilizobadilishwa kwa Sh. 2,339.10/dola ya Marekani) kwa Tanzania Bara (Rejea Kiambatisho Na. 1 cha Taarifa hii). Hoja inayosababisha ucheleweshaji wa maamuzi ya mashauri ya rufaa ni pamoja na kutofanya uteuzi wa wajumbe wa bodi kwa mikoa isiyo na wajumbe, na kutoteua kwa wakati wajumbe, wenyeviti, na makamu wenyeviti, na uhaba wa bajeti za mahakama za rufaa za kodi;

b) Dosari katika mfumo wa ving'amuzi vya kielektroniki wakati wa kuthibitisha bidhaa zinazopita nchini kwenda nchi jirani. Katika hoja hii CAG alibaini miamala 238, ikijumuisha miamala 95 katika mpaka wa Mutukula, miamala 22 katika mpaka wa Rusumo, na miamala 121 katika mpaka wa Tunduma iliyokuwa na tatizo kwenye ving'amuzi vya ki- elekitroni (E-seal). Hali hii inaweza kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali;

c) CAG alibaini pia uwepo wa bakaa ya lita za mafuta 1,105,466.01 zilizoingizwa nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi jirani zenye makadirio ya kodi ya **Sh. Milioni 929.6**, ambayo hayakusafirishwa kwenda nchi husika kwa muda wa zaidi ya siku 30 lakini ushuru wa forodha haukukusanywa; na

d) Ukaguzi wa mfumo wa kieletroniki wa kuwasilisha ritani za kodi ya ongezeko la thamani kwa mwaka wa fedha 2022/23 ulibaini kuwa, Mikoa 9 ya kikodi ilikuwa na jumla ya walipa kodi 35,642 waliosajiliwa na kodi ya ongezeko la thamani. Kati ya hawa, walipakodi 18,067, sawa na asilimia 51, walifanikiwa kuwasilisha ritani za kodi ya ongezeko la thamani. Hata hivyo, walipakodi 17,575, sawa na 49%, hawakuwasilisha ritani za kodi ya ongezeko la thamani. Kutojaza ritani za kodi ya ongezeko la thamani kunaweza kuwa na athari kwenye malengo ya mapato, hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 19 Agosti, 2024, Kamati ilifanya mahojiano ya kina na Wakaguzi kwa pamoja na Bodi na

Menejimenti ya TRA ili kuchambua changamoto za ukusanyaji wa mapato na jitihada za kuondokana na changamoto hizo. Changamoto kubwa ya kwanza iliyotolewa ufafanuzi na Wakaguzi ilihusu mapungufu katika mfumo wa ving'amuzi vya kutambua mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi na kisha kurudishiwa kutumika hapa nchini bila ya kulipiwa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kunukuu sehemu ya maelezo[1] ya Ndugu Isaya Jeremiah ambaye ni Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, aliyotoa mbele ya Kamati kuhusu hoja ya ving'amuzi vya mizigo na kunukuliwa kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

***"Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema ni kweli, suala la mizigo inayoenda nje ya nchi linahitaji umakini mkubwa kwa maana huu ni mwanya ambapo Serikali ina uwezo wa kupoteza kodi. Mzigo unaweza kuonekana kwamba ni mzigo wa kwenda nje lakini mwisho unakuwa consumed hapa nchini bila kulipa kodi. Kwa mfano hapa tumeona ving'amuzi vilikuwa na changamoto, King'amuzi kinaweza kikaonyesha kwamba mzigo bado upo njiani lakini kiuhalisia mzigo umeshafika mpakani lakini king'amuzi bado kinasoma mzigo upo somewhere labda Makambako…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kama maelezo ya wakaguzi hapo juu yalivyonukuliwa, bado kulikuwa kuna changamoto kubwa ya mifumo ya ving'amuzi kutofanya kazi ipasavyo. Katika kujibu hoja hii, Bodi na Menejimenti ya TRA waliifahamisha Kamati kuwa, ni sahihi kwa siku za nyuma mfumo wa kufuatilia mizigo haukuwa

[1]Rejea Ukurasa wa 4 wa Mahojiano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 11, Tarehe 19 Agosti, 2024.

thabiti, hivyo kuna maboresho yamefanyika ili uweze kufanya kazi ipasavyo. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo[2] ya Ndugu Juma. B. Hassan, Kamishina wa Forodha, TRA kuhusu hoja hii kama yalivyonukuliwa hapa chini: -

**Nukuu: -**

***"…. Mheshimiwa Mwenyekiti, E-seals ni mfumo unaojitegemea, isipokuwa unatakiwa uwe linked na TANCIS. Sasa maboresho tunayokwenda nayo ni kwamba sasa hivi kwenye enhancement E-seals ni module ndani ya TANCIS. Kwa hiyo ile clearance na monitoring ya transit goods itakuwa iko ndani ya mfumo mmoja."***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya ziada yalitolewa na Bodi na Menejementi ya TRA katika hoja hii kwamba, wanakiri katika watoa huduma tisa (9) wa ving'amuzi waliokuwepo, baadhi walikuwa na changamoto. Hivyo, baada ya kupata taarifa ya ukaguzi wamewabadilisha ili kupata wenye uwezo. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Juma B. Hassan, Kamishina wa Forodha, TRA aliyoyatoa mbele ya Kamati katika kujibu hoja hii kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

***"…. Mheshimiwa Mwenyekiti, ilionekana katika ripoti ya Mkaguzi kwamba baadhi ya mifumo yao, zile selas zao haziwezi kufanya kazi sawasawa.***
***Kwa hiyo tumebadilisha, tumeitisha tenda mpya, tume invite afresh, kwa hiyo tumewapa watu***

[2] Rejea Ukurasa wa 61 wa Mahojiano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 11, Tarehe 19 Agosti, 2024.

***wapya na ambao sasa tutahakikisha kwamba ving'amuzi wanavyotumia vinakizi yale mahitaji yetu..."***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Bodi na Menejimenti ya TRA iliifahamisha Kamati hatua zinazochukuliwa katika kutatua changamoto ya mlundikano wa mashauri ya kikodi. Naomba kunukuu maelezo mahsusi ya Bodi ya TRA[3] kuhusu hoja hii kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, yale ya stratetic naomba niyajibu, kwa mfano mhe Anatropia amezungumzia issue ya delay of objection na kasema tunafanya nini kuzipunguza. Kwanza kwa mujibu wa Sheria objection inapaswa kuwa admitted na kuwa settled within six month, na hii imewekwa kutenda haki kwa watu ambao wana dispute waweze kusikilizwa na kutatuliwa mapema. Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunafanya nini kufikia hilo? Kwanza huu mfumo tunaoutengeneza, utakuwa na module ya objection, kwahiyo tracking ya disputes itakuwa rahisi sana, kwa hiyo itatusaidia sana. Pili tunaishukuru Serikali kupitia Waheshimiwa Wabunge, tumeongezewa staff, kwahiyo manpower tuliyonayo, tukiiendeleza tutaongeza watu ambao watakuwa wanasettle, zitakuwa zinakuwa settled kwa haraka…'***

**Mwisho wa Nukuu.**

[3] Rejea Ukurasa wa 59 wa Mahojiano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha 11, Tarehe 19 Agosti, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kulikuwa na hoja inayohusu wafanyabiashara kutowasilisha ritani za kodi kwa wakati hivyo kukwamisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Katika kujibu hoja hii, Kamishina Mkuu wa TRA Ndugu Yusuph J. Mwenda alitoa maelezo yafuatayo kwa Kamati: -

**Nukuu: -**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe, kulingana na sample aliyoichukua CAG na alivyofanya ni kweli asilimia 49 walionekana hawajafanya return. Hili tumelifanyia kazi tumegundua mambo mawili, moja, wapo kweli ambao hawaja file lakini pili, kuna shida ya system kuonesha kwamba haja file wakati ame file. Kwa hiyo tulichokifanya wenzangu wameshaonyesha katika 17,575 ni wangapi wamefile na kulingana na data amabazo bado haja verify CAG hawazidi asilimia 15 sasa hiyo ndiyo kazi ya kwanza ambayo tumeifanya, pili wakati anaverify sisi tunaendelea kuwafuatilia ambao hawajafile na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu hoja ya maboresho mfumo wa ukusanyaji kodi, Bodi na Menejimenti ya TRA waliifahamisha Kamati kuwa wamewekeza katika kujenga na kusimika mifumo thabiti ya kodi ambayo ikikamilika itaondoa changamoto zilizobainika. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu. Uledi A. Mussa Mwenyekiti wa Bodi ya TRA aliyotoa mbele ya Kamati kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

**"…Mheshimiwa Mwenyekiti, na sasa tunaresolve**

**hivyo lakini tax payers ni wengi, ndio maana Serikali imeinvest hela nyingi, huu mfumo ambao tunaujenga ambao utakamilika umecost karibu 52 million US Dollars, ni hela nyingi na ukishakamilika huu hizi changamoto zote za availability ya network, za mifumo kutosamana, zitakuwa zimekwisha na zikiisha hata usumbufu kwa walipa kodi utakuwa umeondoka…"**

**Mwisho wa Nukuu.**

### 2.1.2 Upotevu wa Maji kwa Asilimia 34 (Wastani wa Sh. Bilioni 5.28) na Deni la Taasisi za Umma Sh. Bilioni 2.3 kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga – UWASA)

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga (Tanga - UWASA) inaendesha na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, uchambuzi wa taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za TANGA – UWASA ulibaini hoja kadhaa ambazo zinapunguza makusanyo ya fedha za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya kwanza inahusu uwepo wa kiasi kikubwa cha maji yanayopotea (non revenue water, NRW) ya kiasi cha **Sh. Bilioni 5.28** kwa mwaka sawa na asilimia 34 ya maji yote yanayozalishwa. Naomba kunukuu maelezo ya hoja ya CAG katika eneo hili kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

***"… Review of production reports of the Authority found during the year under review the Authority reported to produce a quantity of water 12,427,090 m3. Further, our review of monthly billing statistic summary reports generated from billing system (Majis) found during the year***

***under review the Authority billed a total quantity of water 8,259,250.09 m3 equivalent to 66% of total production of water during the year. This imply that unbilled produced water (non-revenue water) was 34% (equivalent to TZS 5.28 billion) during the year 2022/23 which is higher high compared to the tolerable rate of 20% set by EWURA…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** mapungufu yaliyobainishwa hapo juu yamechangia kwa kiasi kikubwa hasara na upotevu wa mapato stahiki ya Serikali. Kama hoja inavyojieleza, kiwango cha upotevu wa maji kinachoruhusiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) ni asilimia 20 ya maji yanayozalishwa. Hivyo upotevu, wa maji wa asilimia 34 kwa TANGA – UWASA ni kiwango ambacho hakikubaliki kwa viwango vya mdhibiti wa Sekta.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ya pili kwa TANGA – UWASA inahusu uwepo wa deni kubwa ambalo Mamlaka inadai kutoka Taasisi za Serikali la kiasi cha **Sh. 2,316,817,346.75.** Deni hili linakwamisha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka kwa ufanisi na pia kupunguza mchango wa Mamlaka unaotakiwa kuchangiwa Serikalini kwa shughuli za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa deni ambalo TANGA – UWASA inadai kwa Taasisi mbalimbali za Serikali umechanganuliwa katika Jedwali Na.  2.3 hapa chini: -

**Jedwali Na. 2.3: Mchanganuo wa Madeni ambayo Tanga UWASA inadai kwa Taasisi za Umma.**

| Na. | Jina la Taasisi | Deni la Taasisi |
|---|---|---|
| 1. | JWTZ | 468,334,850.87 |
| 2. | Jeshi la Polisi | 55,922,007.33 |
| 3. | Jeshi la Magereza | 608,055,314.97 |
| 4. | Utafiti Mifugo | 20,760,480.15 |
| 5. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa | 8,250,817.31 |
| 6. | Ofisi ya Mkuu wa Wilaya | 9,181,928.20 |
| 7. | Hospitali ya Mkoa | 14,580,645.23 |
| 8. | Jeshi la Zimamoto | 2,507,274.50 |
| 9. | Madeni mengine | 829,224,028.19 |
| **JUMLA** | | **2,316,817,346.75** |

**Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za TANGA - UWASA, 2022/2023.**

**Mheshimiwa Spika,** deni hili ni kubwa na uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa ni deni la muda mrefu. Uwepo wa deni hili unaikwamisha Mamlaka kufanya ukarabati wa miundombinu muhimu ili kuzuia upotevu wa maji na hivyo kuendelea kuongeza upotevu wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 13 Agosti, 2024, Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya TANGA – UWASA ili kupata maelezo ya hatua zinazochukuliwa katika kujibu hoja za ukaguzi katika maeneo mawili ambayo Kamati iliyapa kipaumbele.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya Menejimenti ya TANGA – UWASA kwa Kamati kuhusu hoja ya kuwa na kiwango kikubwa cha upotevu wa maji yalifafanua kwamba, kwa zaidi ya miaka sita, Mamlaka

haikuwa imerekebisha bei zake za maji. Kwa kutofanya marekebisho ya bei za maji, kulisababaisha changamoto ya fedha za matengenezo ya miundombinu.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya ziada kuhusu hoja ya upotevu wa maji yalitolewa yakifafanua kuwa, mtandao wa maji katika Jiji la Tanga ni wa muda mrefu na unahitaji uwekezaji mkubwa ili kuufanyia ukarabati. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Agnes Lukindo, Mkurugenzi wa Fedha na Uhasibu TANGA – UWASA aliyoyatoa mbele ya Kamati: -

**Nukuu: -**

***"… Mheshimiwa Mwenyekiti labda niseme tu kwa ujumla, Mamlaka ya Maji Tanga mtandao wa maji safi ambao upo ni wa muda mrefu mabomba yale yamelazwa tangu mwaka 1973. Kwa hiyo utakuta eneo karibia tuna kilomita 110 za mtandao mabomba yake ni chakavu na kutokana na uwezo wa Mamlaka siyo rahisi kuyabadilisha kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo kila mwaka tumekuwa tukitenga bajeti kidogo kutokana na uwezo wa Mamlaka kuyarekebisha. Sasa mwaka huu tumetenga milioni 100…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja ya deni kubwa ambalo Taasisi za Serikali zinadaiwa na Mamlaka, maelezo yaliyotolewa ni kwamba Wizara ya Maji iliahidi kulishughulikia kwa ujumla kwa Mamlaka zote za maji hapa nchini. Ufafanuzi uliotolewa ni kwamba Wizara ingewasiliana na Wizara ya Fedha ili Taasisi za Serikali ziwe zinalipa fedha hizo moja kwa moja kwa Mamlaka husika.

### 2.1.3 Kuchelewa Kurejesha Mikopo Katika Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma Kiasi cha Sh. Bilioni 5.72

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 7.4 cha Waraka Namba 3 wa Mwaka 2011 uliotolewa tarehe 30 Juni, 2011 (kama ulivyorekebishwa tarehe 22 Machi, 2012) kuhusu mikopo ya fedha kwa Watumishi wa Umma kwa ajili ya ununuzi wa magari, pikipiki, samani pamoja matengenezo ya magari na pikipiki, kinawataka Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba marejesho ya mikopo ya Watumishi waliokopeshwa yanakatwa kwenye mishahara yao kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu 2.8 cha Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Mikopo ya Maendeleo wa Mwaka 2021, na mapitio ya Disemba,2022 kinaelezea wajibu wa wakopaji ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwa Mfuko kuwa makato ya mkopo kwenye mshahara wake yameanza au yamesimamishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, katika Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma ulibainisha uwepo wa mikopo ya muda mrefu ambayo haijarejeshwa kiasi cha **Sh. Bilioni 7. 82.**Katika fedha hizo kiasi cha **Sh. Bilioni 5.72** ni mikopo ambayo awali makato yalianzishwa na baadae yakasimamishwa, na kiasi cha **Sh. Bilioni 2.09** ni madeni ambayo makato yake bado hayajaanza.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 06 Agosti, 2024, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli wa Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma. Afisa Masuuli wa Mfuko alitoa maelezo mbele ya Kamati kwamba, kwa mikopo ambayo makato yalianza baadae yakasimamishwa sababu zilizopelekea kusimamishwa kwa makato zilikuwa ni pamoja na vifo, kuachishwa kazi, kuacha kazi (kujiuzuru), kuunganishwa kwa vitengo na ushirikiano wa wanufaika na maafisa rasilimali watu (Hrs) kufanya udanganyifu na kusitisha makato kutokana na sababu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mikopo ambayo makato yake hayajaanza sababu kubwa iliyoelezwa ni kuwa mikopo ilitolewa na maafisa mikopo kwa Watumishi wasio na uwezo wa kulipa yaani kiasi cha mishahara wanacho pata hakizidi theluthi moja (1/3) ya mshahara, kwa maana nyingine walikuwa na mikopo mingine waliyo chukua kwenye Taasisi nyingine za kifedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifahamishwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024, kiasi cha **Sh. Bilioni 1.87** kilikuwa kimekusanywa ambapo kati ya hizo **Sh. Milioni 180.33** ni kwa mikopo ambayo makato hayajaanzishwa na **Sh. Bilioni 1.69** kwa mikopo ambayo makato yalisimama.

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa Menejimenti ya Mfuko iliwaandikia Maafisa Masuuli wote Barua yenye Kumb. Na. EG.158/327/03/168 ya tarehe 18 Aprili, 2024 ikiwakumbusha wajibu wao katika kushughulikia marejesho ya mikopo iliyo simama na ile ambayo makato hayajaanzishwa katika mafungu yao husika. Aidha Menejimenti ya Mfuko wa Mikopo inaendelea kuimarisha udhibiti ili kuondoa changamoto ya makato ambayo hayajaanzishwa na yale yaliyosimama. Hii inajumuisha kuanzishwa kwa makato ya mkopo moja kwa moja kupitia mfumo wa ALS.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini sababu zinazosababisha ulipaji wa mikopo hii kuwa na changamoto ni pamoja na kutokuwepo kwa majukumu ya kina ya wawakilishi wa mikopo kwenye Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfuko, waajiri kutotimiza wajibu wa kuujulisha mfuko kuwa makato ya mkopo kwenye mshahara hayajaanza au yamesimama na kutoa mikopo kwa Watumishi wasio na sifa yaani mishahara yao haizidi theluthi moja.

### 2.1.4 Deni Lisilokusanywa Kiasi cha Sh. Bilioni 5.1 Katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) na kubaini changamoto ya uwepo wa deni ambalo halijakusanywa la kiasi cha **Sh.5,172,320,640.33**. Mchanganuo wa deni hilo ni kama unavyonekana katika Jedwali Na. 2.4 hapa chini: -

**Jedwali Na. 2.4: Mchanganuo wa Madeni Ambayo DUWASA Inadai.**

| Na. | Aina ya Wadaiwa | Kiasi cha Deni |
|---|---|---|
| 1. | Wafanyabiashara | 240,132,124.10 |
| 2. | Matumizi ya Nyumbani | 2,389,882,887.01 |
| 3. | Taasisi | 2,510,231,340.00 |
| 4. | Kiosk | 15,022,002.02 |
| 5. | Viwandani | 7,031,723.20 |
| 6. | Wengineo | 10,020,564.00 |
| **JUMLA** | | **5,172,320,640.33** |

**Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za DUWASA, 2022/2023.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika mchanganuo wa deni linaloonekana katika Jedwali Na. 2.4 hapo juu, ulibaini kuwa Taasisi za Serikali zinadaiwa na DUWASA kiasi cha **Sh.1,293,613,166.7.** Taasisi hizo ni pamoja na Polisi, JWTZ, Hospitali ya Mkoa, Hospitali ya Mirembe na Magereza. Kwa ujumla madeni haya yanapunguza uwezo wa DUWASA kutoa huduma kwa Wananchi na kuchangia mapato muhimu ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijielekeza kupata ufafanuzi wa Bodi na Menejimenti ya DUWASA kuhusu hatua zinazochukuliwa kukusanya

madeni husika. Hivyo, Kamati ilifanya mahojiano na Bodi na Menejimenti ya DUWASA siku ya tarehe 09 Oktoba, 2024 Ofisi ya Bunge Dodoma. Uongozi wa DUWASA ulikiri uwepo wa madeni hayo ambapo jitihada zinafanyika kuyakusanya. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuwafikisha wadaiwa sugu Mahakamani ambapo hadi sasa wadaiwa watatu (3) wamefikishwa Mahakamani.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo jitihada zinazochukuliwa bado hazijatoa fursa ya ukusanyaji wa madeni kwa kiasi kikubwa. Madeni haya na hususan yale ya Taasisi ni changamoto kubwa kwa DUWASA.Mathalani, Kamati ilifahamishwa kwamba DUWASA inatumia zaidi ya **Sh. Milioni 700** kwa mwezi kama gharama za umeme wanazolipia TANESCO. Ni kwa msingi huo, bila ya ukusanyaji wa madeni ya maji, uwezo wa DUWASA kutoa huduma unapungua ukizingatia kasi ya ukuaji wa Jiji la Dodoma na ongezeko kubwa la watu. Kwa hivi sasa uwezo wa DUWASA kuwahudumia Wakazi wa Dodoma ni wastani wa asilimia 50 ya mahitaji.

### 2.2 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi Kuhusu, Utawala Bora, Mifumo ya Udhibiti wa Ndani na Usimamizi wa Vihatarishi

**Mheshimiwa Spika,** kupitia uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023, Kamati ilipitia taarifa za fedha za Taasisi za Umma zinazohusiana na hoja za utawala bora, mifumo ya udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi.

**Mheshimiwa Spika,** Utawala Bora unajengwa katika Kanuni na taratibu zinazohakikisha Taasisi zinatekeleza shughuli zake kwa uwazi, uwajibikaji na uadilifu. Aidha,mifumo ya udhibiti wa ndani inahusisha taratibu na sera zilizowekwa ndani ya Taasisi ili kuhakikisha kuwa malengo ya ufanisi, ufanisi wa kiutendaji, na utekelezaji wa sheria yanatimizwa.Kwa upande wa usimamizi wa vihatarishi, Kamati ilichambua mchakato wa kutambua, kutathmini,

na kudhibiti hatari zinazoweza kuathiri malengo ya Taasisi kwa masuala yanahosu matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** hoja zote katika masuala niliyobainisha hapo awali kwa namna moja au nyingine zinachangia katika upotevu wa fedha za umma kama hayatasimamiwa ipasavyo.Matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwa hoja zinahosu masuala hayo ni kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Tathmini ya Ufanisi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) – Fungu – 19 Katika Usimamizi wa Fedha za Umma

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) ilianzishwa kupitia Hati Idhini (Instrument) ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyotolewa kwa mujibu wa Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kutangazwa tarehe 13 Februari, 2018 katika Gazeti la Serikali Na. 50 la Mwaka 2018.

**Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la kuanzishwa kwa OWMS ni kuimarisha uwezo wa Serikali katika kuratibu, kusimamia, kushauri na kuendesha mashauri yote ya madai na mashauri ya usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kuchambua hesabu zilizokaguliwa za OWMS Fungu 19 siku ya tarehe 09 Agosti, 2024 Dodoma. Kimsingi, Kamati inatambua kazi kubwa inayotekelezwa na OWMS. Mathalani, uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi wa hesabu zilizokaguliwa za OWMS kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 umebainisha kwamba hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023, OWMS ilikuwa imeendesha jumla ya mashauri ya madai 8,367 ambapo katika mashauri hayo, Serikali ilishinda mashauri 762 na kuokoa fedha kiasi cha **Sh.**

**406,407,875,176.62**. Aidha katika mashauri 14 Serikali ilishindwa na kupoteza jumla ya **Sh. 1,259,249.021**.

**Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, OWMS hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023 iliendesha jumla ya mashauri ya usuluhishi 177 na kuweza kushinda mashauri 04 na hivyo kuokoa kiasi cha **Sh. 7,286,402,818.21** na **Dola za Marekani 11,698,826.76**. Aidha, Serikali ilishindwa jumla ya mashauri ya usuluhishi 04 na hivyo kupoteza jumla ya **Sh. 1,052,201,327.20** na **Dola za Marekani 110,000,000.00**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia uchambuzi wa takwimu hapo juu, ni dhahiri kuwa OWMS ni chombo muhimu katika kusaidia usimamizi wa matumizi ya fedha za umma hapa nchini. Hata hivyo, Kamati ilibaini changamoto kadhaa zinazoikabili ofisi hii hivyo kupunguza ufanisi katika kuikinga Serikali na matumizi mabaya ya fedha za umma kama ilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya vikwazo vilivyobainishwa kuwa ni changamoto kwa ofisi hii kiutendaji ni pamoja na upungufu wa watumishi, upungufu wa bajeti na mfumo uliopo wa uingiaji na usimamizi wa mikataba hali ambayo inaisababishia Serikali hasara inapotokea kuna shauri linafunguliwa na Serikali kushindwa.

**Mheshimiwa Spika,** mathalani kwa upande wa changamoto za bajeti, uchambuzi wa Kamati ulibaini gharama kubwa zilizopo katika uendeshaji na usimamizi wa mashauri ya usuluhishi. Wastani wa gharama za kuendesha shauri moja la usuluhishi nje ya nchi ni kiasi cha **Dola za Marekani 450,000** kama ada ya usuluhishi na gharama za Wasuluhishi. Aidha, kunatakiwa gharama zisizopungua **Sh. 2,000,000,000** kwa ajili ya maandalizi na gharama za safari za Mawakili wa Serikali na mashahidi kwenda kushiriki usikilizwaji wa shauri. Kwa upande wa mashauri ambayo Mawakili wa nje wanaiwakilisha Serikali hutoza wastani wa **Dola za Marekani 2,000,000** hadi **3,000,000** kwa shauri moja.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu changamoto ya uingiaji na usimamizi wa mikataba, naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Afisa Masuuli, Fungu 19 Ndugu Alice E. Mtulo – Naibu Wakili Mkuu wa Serikali[3] aliyoyatoa mbele ya Kamati kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

***"… Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nini kinasababisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kushindwa mashauri? Mashauri mengi ambayo yanaonekana kwenye mitandao na vyombo vya habari na gharama yake ni kubwa ambayo Serikali inaingia ni mashauri ya usuluhishi ambayo ni Arbritration. Mheshimiwa Mwenyekiti sasa kinachotokea kwenye mashuri ya namna hii, A husika, wizara wanaingia kwenye mikataba ambapo wakiingia kwenye mikataba Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali siyo part ya ile mikataba. Ofisi inaletewa mashauri ambayo tayari yamekwsihaharibika…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli OWMS aliendelea kufafanua kwamba, wanaoingia mikataba ni ofisi husika pamoja na kuwa mikataba husika hupelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi. Afisa Masuuli alifahamisha Kamati kuwa, changamoto nyingine ambayo inasababisha Serikali kupata hasara ni baadhi ya Taasisi kuingia na kuvunja mikataba bila kufuata kanuni na taratibu husika pamoja na usimamizi usioridhisha wa mikataba iliyoingiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa changamoto ya watumishi taarifa ya CAG, ilibainisha suala la upungufu wa watumishi katika OWMS pamoja na hoja ya kuwajengea uwezo ili waweze

---

[3] Rejea Uk. 20-21 wa Majadiliano ya Kamati Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Kikao cha Tatu Tarehe 09 Agosti, 2024

kushindana kwa ufanisi katika kutetea maslahi ya umma. Katika eneo hili naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (AAG)
Ndugu Onesphory Nestory[4] mbele ya Kamati kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

***"…Nilikuwa naomba kusisitiza hapa Waheshimiwa Wabunge ni eneo ambalo mnaweza mkatilia mkazo tunatakiwa tupate mawakili ni bobevu yaani Serikali itenge mazingira ya kuwapata Mawakili ambao ni bobevu either kwa kuwatrain ili tuweze na sisi tuwe tunashinda hizo kesi…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia uchambuzi uliofanyika hapo juu hasa takwimu za fedha ambazo OWMS inaweza kuokoa na kwa kuzingatia umuhimu wa OWMS katika kuimarisha usimamizi wa fedha za umma kama ambavyo CAG ameifahamisha Kamati, Kamati imetoa mapendekezo na ushauri wa maeneo ya maboresho katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

### 2.2.2 Changamoto Zilizopo Katika Umiliki na Uendeshaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Dawa cha Keko

**Mheshimwa Spika**, Kiwanda cha Madawa Keko (Keko Phermaceutical Limited, KPI) kilikuwa kinamilikiwa na Serikali tangu Mwaka 1968 kama Idara katika Wizara ya Afya, ambayo ilikua na kazi ya kusambaza dawa katika maduka ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda hiki kilijengwa kwa msaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya watu wa China kwa ajili ya kutengeneza na

[4] Rejea Uk. 3 wa Majadiliano ya Kamati Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Kikao cha Tatu Tarehe 09 Agosti, 2024.

kusambaza dawa hapa nchini. Mnamo mwaka 1992 kiwanda hiki kilisajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni na Mwaka 1995 kilibinafsishwa kwa mbia binafsi aliyejulikana kama Diocare Ltd akimiliki hisa kwa asilimia 60 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia kwa msajili wa Hazina akimiliki hisa asilimia 40.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo Mwaka 2019, Serikali iliingia makubaliano na Kiwanda cha Madawa Keko (1997) Limited, KPI[5] kwa ajili ya mapitio ya umiliki na uendeshaji kupitia kwa Msajili wa Hazina na Kampuni ya Diocare Limited.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya CAG, sehemu ya makubaliano hayo ni kama inavyonukuliwa hapa chini: -

**Nukuu: -**

***"…The agreement states that the GoT and Diocare Limited have agreed to restructure shareholding and to streamline the management of KPI for the betterment of the delivery of services of said companies to the public due to the challenges facing operations and management of KPI and taking into consideration of irregularities committed in the process of acquisition of 60% stake in KPI whereby the earlier agreed contract price which based on the value of the company was later reduced basing on number of shares, uncertainties surrounding claims by Diocare Limited to the Company (KPI), the disputed payment of Tanzania Shillings 1,002,000,000 by KPI to Diocare Limited as interest, disputed claim by Diocare Limited of interest amounting to about Tanzania Shillings 7,000,000,000 to the Company, unsatisfying performance of KPI…"***

[5] Keko Pharmaceuticals Industry (KPI).

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na masuala mengine, makubaliano hayo yaliweka msisitizo kwa mambo yafuatayo: -

a) Umiliki wa kiwanda utakuwa kwa mgawanyo wa hisa ambapo Serikali itakuwa na umiliki wa 70% na Kampuni ya Diocare Limited hisa 30%. Katika hilo, 40% ya **Sh. 1,000,000,000** (**Sh. 400,000,000**) ambayo Serikali ililipa Kampuni ya Diocare Limited itatumika kama malipo ya utwaaji wa hisa 70%. Vilvile hisa 16,047 sawa na 20% hazikulipiwa na Diocare Limited, hivyo zitarudishwa chini ya umiliki wa Serikali;

b) Kwamba, deni la **Sh. 1,001,200,000** na riba ya **Sh. 7,428,518,578** haitajumuishwa katika vitabu vya KPI;

c) Ndani ya siku 30 tangu tarehe husika, Diocare Limited atahamisha umiliki wa hisa 40,117 kwenda kwa Serikali. Hivyo Diocare atakuwa na hisa 40,117 na Serikali hisa 93,608;

d) Madeni yote yatakayo hakikiwa na kukubaliwa ya KPI yatashughulikiwa tangu siku ya kusainiwa makubaliano husika kwa kuzingatia mgawanyo wa wanahisa; na

e) Kwa madhumuni ya Kifungu cha 8 cha makubaliano hayo, wanahisa watahakiki madeni yote ya KPI. Madeni yote ambayo hayahusiani moja kwa moja na KPI yatachukuliwa na mwanahisa anayehusika.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo mapitio ya taarifa ya ukaguzi ya KPI kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 kumebainika dosari katika utekelezaji wa makubaliano hayo na shughuli za uendeshaji. Dosari hizo ni kama ifuatavyo: -

a) Kutokuwepo kwa Katiba ya Kampuni iliyoidhinishwa (MEMART[6]). Suala hili ni kinyume na matakwa ya Kifungu 9(1) cha Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002. Hivyo hadi sasa hakuna nyaraka yeyote ya kisheria inayosimamia uendeshaji wa KPI baada ya makubaliano mapya ya umiliki;

b) Kutothibitishwa uwepo wa deni la kiasi cha **Sh.21,486,593,677**. Mapitio ya hesabu za KPI kwa miaka minne ya fedha yamebaini kuwa wanahisa hawajahakiki uwepo wa deni hilo kinyume na Kifungu Na. 8 cha makubaliano ambacho kilitaka deni lihakikiwe kabla au ifikapo tarehe 31 Disemba, 2022;

c) Kutotangaza KPI katika gazeti la Serikali kama Shirika la Umma. Kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992, katika Taasisi ambayo Serikali ina hisa zaidi ya 51%, inatakiwa Taasisi husika itangazwe katika gazeti la Serikali kama Shirika la Umma

d) Kuwepo kwa mbia mwenza (binafsi) ambaye amekuwa akilipwa kiasi cha **Sh. 15,000,000** kila mwezi kama ada ya ushauri, ushauri ambao Bodi na Menejimenti ya Kiwanda cha Madawa Keko hawajathibitisha ushauri ambao mbia mwenza amekuwa akiutoa kwa maendeleo ya kiwanda;

e) Kuchelewa kufanyika maamuzi yanayohusu maendeleo ya kiwanda ambako kunaletwa na mbia binafsi kutokuhudhuria baadhi ya vikao muhimu vya bodi ya wakurugenzi;

f) Hoja nyingine ni ufanisi duni wa mashine za KPI kutokana na kutumia teknolojia iliyopitwa na wakati. Mathalani ukaguzi ulibaini mashine 22 kati ya 39 zilikuwa mbovu hali inayoongeza gharama za uzalishaji;

[6] Memorundum and Articles of Association.

g) KPI kutekeleza majukumu yake bila ya kuwa na Cheti cha Ithibati (Goods Manufacturing Practices, GMP) kinachotolewa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA). Hii inakiuka matakwa ya Sheria na Kanuni za Madawa na Vifaa Tiba[7]; na

h) Kihatarishi cha KPI kuendelea na biashara kwa siku zijazo (Going concern). Hali hii inatokana na Kampuni kuwa na mtaji hasi (Adverse working capital). Mtaji hasi umeongezeka kutoka **Sh. Bilioni 5.23** (2009) hadi **Sh. Bilioni 12.17** (2022).

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 07 Oktoba, 2024, Ofisi ya Bunge Dodoma, Kamati ilipata fursa ya kufanya mahojiano na Bodi, Menejimenti ya KPI na Msajili wa Hazina. Lengo la kikao hicho lilikuwa kujadili kwa kina hoja zilizojitokeza kwa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** kimsingi kilichobainika kupitia majadiliano ni kwamba, kutohitimishwa kwa mchakato wa makubaliano ya wanahisa ndio msingi wa KPI kutokuwa na ufanisi hadi sasa. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Kayobyo Majogoro amabaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya KPI aliyoyatoa mbele ya Kamati kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

***"…Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Bodi tuliyonayo imeundawa na mimi kama Mwenyekiti pia ninasimamia kipindi hicho cha mpito kwa kuwa utaratibu wa kumpata mwenyekiti kama ambavyo taratibu zipo zitafanyika baada ya kuwa taratibu hizo za kutwaa zile share na kuzimiliki kisheria zitakuwa zimekamilika…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

---

[7] Rejea Kifungu 51(c) cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba ikisomwa kwa pamoja na Kanuni 7(1) & (2) ya Kanuni za Chakula, Dawa na Vipodozi (Good Manufacturing Practice Enforcement).

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kutokamilika kwa uhamishaji wa hisa, kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kupata hasara katika kiwanda hiki kutokana na maamuzi yaliyofanyika hapo awali. Hali kadhalika, Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa riba zinazotozwa katika mikopo iliyochukuliwa hapo awali na iliyokuwa Menejimenti ya KPI, na hadi sasa uhakiki wa mikopo hiyo haujafanyika ili kubaini uhalali wake.

### 2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi ya Kiasi cha Sh. 32,756,592,701 Katika Chuo cha Uhasibu Arusha Bila ya Kuwa na Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 37 cha Sheria ya Usajili wa Wabunifu wa Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya Mwaka 2010 inaelekeza umuhimu wa kuwa na usimamizi wa kutosha kwa miradi ya ujenzi. Kifungu hicho kinataka utekelezaji wa miradi ya ujenzi isimamiwe na wataalamu waliosajiliwa kama Wabunifu wa Majengo na Wakadiriaji Majenzi.
Naomba kunukuu masharti ya kifungu hicho kama ifuatavyo:-
**Nukuu:-**

***"… For the purpose of regulating the standard and monitoring activities undertaken by registered person, the board shall ensure that every person, client, developer, financier or firm which undertakes building or construction works engaged the services of an architectural or quantity firm…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika na CAG ulibaini kuwa pamoja na gharama kubwa za miradi iliyokuwa inatekelezwa, kulikuwa na hoja zifuatazo:-

a) Miradi husika ilikuwa inatekelezwa kwa kutumia force account;

b) Miradi husika haikuwa imesajiliwa na Bodi za Kitaaluma na Kiufundi kama AQRB[8], ERB[9] na CRB[11];

c) Miradi yote ilikuwa inatekelezwa bila ya kutumia Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi;na

d) Miradi yote ilitekelezwa bila ya kuwa na ithibati ya OSHA.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 09 Oktoba, 2024, Kamati ilikutana na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo na Menejimenti ya Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) ili kupata ufafanuzi wa kina kuhusu hoja za ukaguzi zilizokuwa zimejitokeza, hasa kwenye eneo la ujenzi wa gharama kubwa bila ya kusajili miradi husika kwenye Bodi za Kitaalam (AQRB,ERB na CRB).

**Mheshimiwa Spika,** maelezo yaliyotolewa na uongozi wa IAA kwa Kamati ni kwamba, baada ya kubaini changamoto za ujenzi kwa kutumia njia ya "force account" waliomba Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi Serikalini (PPRA) kuwafanyia ukaguzi wa eneo la manunuzi. Ukaguzi huo ulifanyika na kubainisha maeneo ambayo yanahitaji maboresho ili kukamilisha miradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Menejimenti ya IAA iliifahamisha Kamati kuwa maeneo yaliyoboreshwa ni pamoja na kuajiri wahandisi wataalam waliosajiriwa wa usimamizi wa ujenzi katika miradi husika. Aidha, uongozi wa IAA uliifahamisha Kamati kuwa, sababu nyingine ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa njia ya " force account" ni sababu ya upatikanaji wa fedha usiotosheleza.

[8] Archtects and Quantity Surveyors Registration Board.

[9] Engineers Registration Board.

### 2.2.4 Kutokuunganishwa Kielektroniki Mfumo wa Usimamizi wa Matukio (EMS) na Njia ya Malipo ya Serikali ya Kielektroniki (GePG) Katika Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Kutokuwepo Kanuni

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa hesabu za TTB na kubaini dosari katika Mfumo wa Usimamizi wa Matukio (EMS)[10] na Njia ya Malipo ya Serikali ya Kielektroniki (GePG)[11].Katika hoja hii, taarifa ya CAG ilibainisha kuwa Kitengo cha Fedha hakikutengeneza ankara za malipo kutoka kwa Mfumo wa Uratibu wa Maonesho na nambari za udhibiti kutoka kwa GePG.

**Mheshimiwa Spika,** utoaji wa ankara za malipo nje ya Mfumo wa GePG ni kihatarishi cha upotevu wa mapato ya Serikali.Kamati ilitaka kupata maelezo ya Uongozi wa TTB wa sababu ya kukusanya mapato ya Serikali nje ya Mfumo, ambapo waliifahamisha Kamati kuwa, watashirikiana na timu husika za TEHAMA ili kuanzisha Mfumo salama wa makusanyo ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** hoja nyingine kwa TTB inayohusiana na masuala ya Utawala Bora inahusu kutokuwepo kwa Kanuni za Sheria iliyoanzisha TTB ya Mwaka 2002.Kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura, 364 imempa Waziri mwenye dhamana ya utalii mamlaka ya kutengeneza kanuni za kusaidia utekelezaji wa Sheria kadri atakavyoona inafaa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokuwepo kwa Kanuni za kusaidia utekelezaji wa Sheria kunaweza kuchangia kupunguza ufanisi wa TTB. Uongozi wa TTB uliifahamisha Kamati kuwa, Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa Rasimu ya Kanuni ya Mabalozi wa Hiari wa Utalii na

[10] Event Management System (EMS).

[11] Government e – Payment Gateway (GePG).

kuziwasilisha kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa hatua za kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali[12].

### 2.2.5 Mapungufu ya Udhibiti wa Ndani Katika Manunuzi ya Gesi Yanayofanywa na TANESCO kwa Baadhi ya Maeneo

**Mheshimiwa Spika,** TANESCO hutumia kiasi kikubwa cha fedha kufanya manunuzi ya gesi kwa ajili ya kuzalisha umeme katika mitambo yake.Kampuni kubwa tatu (3) zinazoiuzia TANESCO gesi ni TPDC, M&P Exploration Production Tanzania Limited na Pan-African Energy Tanzania Limited. Kampuni hizi hupeleka gesi kwenye mitambo ya TANESCO na kisha hutoa ankara za kila mwezi kwa kuzingatia matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/23, TANESCO ilinunua gesi yenye thamani ya **Sh.543,128,780,238.31** ambayo ilitumika kuzalisha umeme kWh 5,579,430,528 katika mitambo nane (8). Mapitio ya udhibiti kuhusu upimaji wa mita za gesi inayotumiwa na ufanisi wa mitambo yalibaini changamoto zifutazo:-

a) Hapakuwa na ushahidi wa baadhi ya mita za gesi kufanyiwa marekebisho (calibration) kama inavyotakiwa na Kanuni za Wakala wa Vipimo (WMA[13]). TANESCO ina mitambo nane (8) inayozalisha umeme kwa kutumia gesi inayosambazwa na Wazabuni na inayopimwa kila mwezi kwa mita iliyowekwa kwenye kila mtambo. Ili kuimarisha ufuatiliaji wa usahihi wa kiasi kinachosambazwa, TANESCO katika mwaka wa fedha 2022/23 iliweka mita za gesi kwenye mitambo sita (6). Hata hivyo, Taarifa ya CAG inabainisha kuwa hapakuwa na nyaraka iliyotolewa kuthibitisha iwapo mita husika ilifanyiwa

[12] Rejea Nakala ya Barua yenye Kumb. Na. CAB.13/340/02 ya tarehe 23 Septemba, 2024 ya Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii kwenda kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali.

[13] Weight And Measure Agency (WMA).

marekebisho baada ya vipimo.Hatua hii ilikuwa kinyume na matakwa yaliyotajwa ya Kanuni ya 22 na 25 ya Kanuni za Wakala wa Vipimo (WMA);

b) Utofauti katika usomaji wa mita kati ya muuzaji na mita ya ukaguzi. Mapitio ya uwiano wa usomaji wa kila mwezi wa gesi kati ya mita za ukaguzi wa TANESCO na wasambazaji ulibaini kuwa, kuna tofauti kati ya kiasi cha gesi inayotumika ambayo husababisha hatari ya kutozwa na Wazabuni gharama za ziada; na

c) Kutoweka mita ya ukaguzi katika Kituo cha Ubungo III. Ankara ya kila mwezi ya gesi inayotolewa hukokotolewa kwa kuzingatia usomaji wa kwenye mita za msambazaji. Hivyo ili kuweka udhibiti, TANESCO ilitakiwa kuweka mita za ukaguzi kwa ajili ya kuhakikisha usahihi wa gharama za kila mwezi ili kuepuka kutozwa isivyo stahili. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa mita ya ukaguzi iliyowekwa katika Kituo cha Ubungo III ili kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa gharama za gesi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya TANESCO ili kupata ufafanuzi wa hoja hii inayohusu mfumo wa udhibiti wa gharama za ununuzi wa gesi. TANESCO waliifahamisha Kamati kuwa Wakala wa Vipimo (WMA) walifanya ukaguzi wa mita za TPDC Mwezi Disemba, 2023 na PAET Mwezi Machi,2024 na kuhakiki ubora wake.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, wakaguzi waliifahamisha Kamati hoja hii utekelezaji wake ulikuwa haujakamilika ipasavyo. Ni kwa msingi huo, Kamati imeendelea kusisitiza kufanyiwa kazi kwa hoja hii ili kuhakikisha gharama ambazo TANESCO inaingia kununua gesi ni halisi kwa kuzingatia kiasi halisi cha gesi walichotumia katika kuzalisha umeme.

## 2.3 Uchambuzi wa Taarifa za Kaguzi Maalum

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/2023, Kamati imefanikiwa kupitia na kuchambua jumla ya Taarifa za Kaguzi Maalumu mbili (2). Kaguzi hizo zinahusu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Wizara ya Afya Fungu 52. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya Kaguzi hizo Maalum kama ifuatavyo: -

### 2.3.1 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalum Kuhusu Ugharamiaji, Upangaji, Utoaji na Urejeshaji wa Mikopo wa Wanafunzi wa Elimu ya Juu Inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa Kipindi cha 2015/2016 Hadi 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi huu ulifanyika kufuatia maazimio ya Kikao cha Tano cha Mkutano wa Tisa wa Bunge la Tanzania cha tarehe 5 Novemba 2022. Maazimio hayo yalitokana na kujadiliwa kwa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hoja nyingine zilizojadiliwa katika kikao hicho, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliomba maelezo ya Serikali, kuhusu hali halisi ya ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na baadhi ya wanafunzi kukosa mikopo licha ya kustahili na wengine kupatiwa mikopo licha ya kutostahili. Aidha kulijitokeza hoja kuwa, baadhi ya wanafunzi wanapewa kiasi cha mikopo zaidi ya walichopangiwa na wengine kupewa kiasi cha mikopo pungufu ya walichopangiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mjadala huo, Bunge liliazimia kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya Ukaguzi wa Kina (Comprehensive Audit) kuhusu ugharamiaji,

upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia maazimio hayo na kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma[14], mnamo tarehe 16 Mei 2023, CAG alianzisha Ukaguzi Maalumu katika Bodi hiyo ambao ulilenga kuhakiki mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa miaka 7 kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2021/22 na marejesho ya mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi huu ulihakiki ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ili kubaini iwapo mikopo ilitolewa kikamilifu na kwa kuzingatia taratibu zilizopo. Vilevile, Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za mikopo ambayo haijarejeshwa na takwimu za urejeshaji wake.
Ukaguzi huu uliongozwa na Hadidu ya Rejea moja ambayo ni: -

"*Kukagua ugharamiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu hapa Nchini*"

**Mheshimiwa Spika,** CAG alikamilisha ukaguzi huu na kuwasilisha taarifa yake mbele ya Kamati mapema mwezi Agosti, 2024. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu masuala muhimu yaliyobainika katika ukaguzi huo:-

### 2.3.1.1 Fedha za Mikopo Zilitolewa Kwa Wastani wa Asilimia 91.6 ya Bajeti Kati ya Mwaka 2015/2016 Hadi 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** ukaguzi maalumu ulibaini kuwa kati ya Bajeti zilizoidhinishwa kwa ajili ya HELSB na kiasi cha fedha kilichotolewa kwa miaka minne kuanzia 2017/18 hadi 2019/20 kiasi cha zaidi ya

[14] Rejea Masharti ya Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura ya 418.

asilimia 99 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi kilipatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na marejesho ya mikopo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya 2015/16, 2016/17 na 2020/21 kiasi chini ya asilimia 90 ya Bajeti ndiyo kilipatikana. Hivyo, kwa wastani katika kipindi chote (2015/16 hadi 2021/22) kiasi cha asilimia 91.6 ndicho kilipatikana, kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 2.5 hapa chini.

**Jedwali Na. 2.5: Bajeti na Mapato ya Kiasi Kilichokopeshwa kwa Wanafunzi**

| Mwaka | Bajetilliyoidhinishwa A (Sh.) | Kiasi Kilichopokelewa | | Jumla ya Kiasi Kilichopokelewa D = (B+C) (Sh.) | Kilichopokelewa / Bajeti (%) E = D/A |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mfuko Mkuu wa Serikali B (Sh.) | Marejesho ya Mikopo kutoka kwa Wanufaika C (Sh.) | | |
| 2015/16 | 473,021,323,500 | 369,848,142,097 | 28,210,367,282 | 398,058,509,379 | 84 |
| 2016/17 | 472,749,751,400 | 214,828,445,123 | 116,814,626,463 | 331,643,071,586 | 70 |
| 2017/18 | 418,009,415,343 | 235,143,806,103 | 182,865,609,240 | 418,009,415,343 | 100 |
| 2018/19 | 418,905,519,995 | 243,912,244,530 | 177,721,671,055 | 421,633,915,585 | 101 |
| 2019/20 | 450,000,000,000 | 255,624,053,064 | 190,720,402,720 | 446,344,455,784 | 99 |
| 2020/21 | 464,000,000,000 | 233,965,305,510 | 181,047,860,350 | 415,013,165,860 | 89 |
| 2021/22 | 570,000,000,000 | 381,866,729,277 | 180,724,164,107 | 562,590,893,384 | 99 |
| **Jumla** | **3,266,686,010,238** | **1,935,188,725,704** | **1,058,104,701,217** | **2,993,293,426,921** | **91.6** |

**Chanzo: Uchambuzi wa Kamati Katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum wa HESLB, 2024**

### 2.3.1.2 Changamoto Katika Kupima Uhitaji wa Mikopo na Uwezo wa Kugharamia Mahitaji ya Mikopo

**Mheshimiwa Spika,** katika eneo hili taarifa ya ukaguzi maalumu imebainisha masuala kadhaa kuhusiana na utambuzi wa wahitaji

wa mikopo na uwezo wa Serikali kugharamia mahitaji ya mikopo husika.

Masuala yaliyobainika ni kama ifuatavyo: -

a) Kwa mujibu wa taarifa za kupima uwezo za kipindi husika, jumla ya waombaji wa mikopo 364,824 kati ya 442,225 waliostahili (sawa na asilimia 82.5) ndiyo walipewa mikopo na Bodi. Hivyo, jumla ya wanafunzi 77,401 (442,225 – 364,824) waliokidhi vigezo hawakupata mikopo katika kipindi hicho. Wanafunzi hao 442,225 walihitaji mikopo ya jumla ya **Sh. 1,377,521,786,709** katika kipindi hicho cha miaka 7 kuanzia 2015/16 hadi 2021/22. Hata hivyo, Bodi ilipanga mikopo ya jumla ya **Sh. 1,155,973,259,064** kwa waombaji 364,824 pekee, na waombaji 77,401 waliohitaji mikopo ya jumla ya **Sh. 198,918,962,259.75** (sawa na asilimia 17.5 ya kiasi kilichohitajika) kutopangiwa mikopo hiyo licha ya kustahili kutokana na ufinyu wa Bajeti;

b) Ukaguzi ulibaini mapungufu katika kanzidata ya mfumo wa mikopo unaofahamika kama intergrated Loan Management System (iLMS) ambapo kwa kipindi cha 2015/16 hadi 2018/19 kanzidata ilikuwa haijaainisha special/ordinary framework, kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22 kanzidata inaonesha kati ya wanafunzi 96,700 waliokopeshwa zaidi ya uhitaji wanafunzi 3,111 ndiyo wametumia special framework na kati ya wanafunzi 164,593 waliokopeshwa pungufu ya uhitaji wanafunzi 8,670 ndiyo wametumia special framework. Dosari hii ya kimfumo ilisababisha baadhi ya wanafunzi kupewa mikopo chini au juu ya kiwango cha uhitaji.

### 2.3.1.3 Mapungufu Katika Urejeshaji wa Mikopo Iliyotolewa na Bodi

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi Maalumu umebainisha hoja za msingi katika eneo la urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kama ifuatavyo: -

a) Kwa mujibu wa kanzidata ya Mfumo wa iLMS (Integrated Loan Management System), katika kipindi hicho cha miaka saba, wanufaika 256,632 walipaswa kurejesha kiasi cha jumla ya **Sh. 2,660,316,913,933.46**. Aidha, jumla ya wanufaika 88,449 kati ya 256,632 (sawa na asilimia 34.47) ndiyo waliofanya marejesho ya mikopo yao kwa kiasi cha jumla ya **Sh. 405,945,155,212.03** ikilinganishwa na kiasi cha **Sh. 1,033,741,741,417** kilichopaswa kurejeshwa;

b) Vilevile ukaguzi umebaini kuwa, Bodi haijaweza kukusanya kiasi chochote kutoka kwa wanufaika 168,183 wanaodaiwa jumla ya kiasi cha **Sh. 1,626,575,172,516.80**. Licha ya kufanya marejesho kutoka kwa wanufaika 88,449, kutorejeshwa kwa kiasi cha **Sh.627,796,586,204** (**1,033,741,741,417** - **405,945,155,212**) (sawa na asilimia 60.73). Hivyo kunapelekea kuwa jumla ya **Sh. 2,254,371,758,720** (**627,796,586,204** + **1,626,575,172,516.80**) kutokukusanywa hadi sasa; na

c) Kupitia Taarifa za Mikopo Chechefu (Defaulters List) ya kanzidata ya Mfumo wa ILMS ya Bodi ya Mikopo, hadi kufikia mwezi Juni 2023 jumla ya kiasi cha **Sh. 3,415,459,422,774** kinachopaswa kurejeshwa kutoka kwa wanafunzi 455,298 hakijaanza kurejeshwa kutoka kwa wanufaika hao wa mikopo. Kiasi cha **Sh. 1,934,693,673,807** kati ya kiasi hicho, ni mikopo ya wanufaika 240,521 iliyoiva (matured loans) lakini haijaanza kurejeshwa (loan defaulters). Aidha, kiasi cha **Sh. 1,480,765,748,966** cha wanufaika 214,777 pia hakikuwa kimeiva (not matured) mnamo mwezi Juni 2023, hivyo kutoanza kurejeshwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupokea taarifa ya ukaguzi maalumu, ilikutana na Bodi na Menejimenti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ili kujadili hatua zilizochukuliwa kutokana na ukaguzi huo. Kikao husika kilifanyika tarehe 20 Agosti, 2024 Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja inayohusu ugharimiaji wa mikopo ya Elimu ya Juu, Uongozi wa Bodi ya Mikopo walitoa shukurani kubwa kwa Serikali na hususan kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Daktari Samia Suluhu Hassan, ambavyo imekuwa ikijitahidi kutoa fedha na kuongeza bajeti ya Bodi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ogezeko la bajeti ya Bodi kila mwaka, uwezo wa Bodi kutoa mikopo kwa sasa ni wastani wa asilimia 70 ya wahitaji, hivyo kuwepo na upungufu wa ugharamiaji (Financing gap).Uongozi wa Bodi ulifafanua kwamba, kwa makadirio yaliyofanyika na ongezeko la wahitaji wa mikopo, kwa miaka kumi ijayo Bodi itaweza kuwahudumia wahitaji kwa wastani wa asilimia 32.Kutokana na changamoto ya rasilimamli fedha, Bodi imeendelea kufanya uchunguzi ili kuboresha kikokotoo kinachotumika kuwapata wanufaika na kiasi cha mkopo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja inayohusu urejeshaji wa mikopo, Uongozi wa Bodi uliifahamisha Kamati kuwa, wamefanya usuluhisho wa kanzi data ya wanufaika wa mikopo ambayo imefanyika kwa asilimia 98. Baada ya juhudi hizo wameongeza ufuatiliaji. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo[15] ya Ndugu. Dkt. Peter Mmmari, Mkurugenzi Upangaji na Utoaji wa Mikopo wa Bodi ya Mikopo aliyotoa mbele ya Kamati kama ifuatavyo: -

**Nukuu:-**

***"… Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeongeza ufuatiliaji na utoaji wa bili kwa ajili ya wale wadaiwa yaani tracing and billing, kwa sababu kama mmeona tumekuwa na kampeni mbalimbali. Kuna kampeni ya sifurisha, tulikuja na mapeni ya fichua sasa hivi. Hivyo kwenye forma employment coverage is almost 98 percent…"*Mwisho wa Nukuu**

[15] Rejea Uk. 28 wa Majadiliano ya Kamati Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Kikao cha Kumi na Mbili Tarehe 20 Agosti, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata muda wa kujadili matokeo ya ukaguzi huu na Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kupata maelezo ya Serikali kwa hoja zilizokuwa zimejitokeza. Katibu Mkuu aliifahamisha Kamati kuwa kuna mchakato wa mapitio makubwa ya uendeshaji wa Bodi yanaendelea kwa sasa ili kuboresha shughuli za ugharamiaji wa elimu ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kunukuu sehemu ya maelezo[18] ya Ndugu. Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Kamati kama ifuatavyo:-

**Nukuu: -**

***"… Mheshimiwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati hii, kupitia Mradi wetu wa HEET (Higher Education For Evaluation Transformation), Bodi ya Mikopo inafanyiwa mapitio na uendeshaji wake wote ili tuweze kuona ni maeneo gani tunahitaji kuboresha ili mfuko uweze kuwa endelevu…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya majadiliano hayo ya kina Kamati imetoa ushauri na mapendekezo ya maboresho ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalum Kuhusu Ugavi na Usambazaji wa Vifaa Tiba Kwa ajili ya Huduma za Mama na Mtoto (CEmONC)

**Mheshimiwa Spika,** mnamo Mwaka 2015, Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo kupitia Mradi wa Mfuko wa Afya (**Basket Fund)** ilianzisha Afua kwa ajili ya hukakikisha upatikanaji wa huduma bora ili kupunguza vifo vya Mama na Mtoto katika Jamii.

**Mheshemiwa Spika,** kupitia Makubaliano ya Mwaka 2015-2020 na 2021-2026, Serikali ilikubaliana na Wadau wa Maendeleo kupitia Mfuko wa Afya ili kusaidia kufikia matokeo chini ya Mpango wa Kimkakati wa Sekta ya Afya Awamu ya IV na V (**Health Sector Strategic PlanHSSP IV&V**) ili ifikapo mwisho wa kipindi cha Awamu ya IV, Asilimia 50 ya vituo vya afya na Asilimia 100 ya hospitali ziwe zinatoa huduma za Mama na Mtoto (**Comprehensive Emergency Obstetric and Neonatal Care- CEmONC**).

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Afua hii ulilenga kufikia Vituo 217 kwa awamu nne ambapo awamu ya kwanza ilihusisha vituo vya afya 44, awamu ya pili vituo vya afya 100, awamu ya tatu vituo vya afya 66, na awamu ya nne vituo vya afya 7 (Vituo vilivyokuwa kwenye kambi za Wakimbizi). Thamani ya Ugavi na Usambazaji wa vifaa hivi ilikuwa ni **Sh. 65,641,544,204**.

**Mheshimiwa Spika,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliombwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya kupitia barua yenye Kumb. Na. CA.125/244/02/52 ya tarehe 20 Desemba 2022 kufanya Ukaguzi Maalum juu ya Ugavi na usambazaji wa Vifaa Tiba vya CEmONC.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la ukaguzi huu maalum ilikuwa ni kuthibitisha iwapo kuna thamani ya fedha kwa vifaa vilivyonunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya afya, kubaini sababu za ucheleweshaji wa ununuzi na usambazaji wa vifaa, kubaini iwapo Sheria, Kanuni na Miongozo ya manunuzi ilizingatiwa, kufuatilia na kuthibitisha fedha zilizotolewa na Wafadhili na kutoa mapendekezo kwa ajili ya maboresho ili kuharakisha kufikia malengo yaliyokusudiwa. Ukaguzi huu ulihusisha kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2017 hadi 30 Machi, 2023.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua taarifa ya ukaguzi huu maalum na kubaini kuwa kulikuwa na jumla

ya hoja za ukaguzi ishirini na moja (21) ambazo zilitolewa. Baada ya uhakiki wa kina kufanyika na CAG, hoja ambazo utekelezaji wake ulikuwa haujakamilika hadi kufikia tarehe 16 Agosti, 2024, ni hoja nane (8).

**Mheshimiwa Spika,** hoja hizo nane (8) ambazo utekelezaji wake unaendelea zitafanyiwa uhakiki na CAG katika kipindi kijacho cha ukaguzi wa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2024. Hoja ambazo utekelezaji wake haujakamilika kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:-

a) Baadhi ya vifaa vyenye thamani ya **Sh. 3,370,408,157.96** vilikuwa havijanunuliwa ili kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma;

b) Baadhi ya vifaa vilipelekwa katika vituo ambapo havikuwa vimepangwa hapo awali;

c) Baadhi ya vifaa vilipelekwa katika maeneo ambapo vilikuwa havitumiki;

d) Vifaa vyenye thamani ya **Sh. 417,992, 400** viliwasilishwa kwa idadi ya juu zaidi ya mahitaji; na

e) Mapungufu kadhaa katika uandaaji wa nyaraka mbalimbali za mradi katika awamu zake za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana siku ya tarehe 16 Agosti, 2024 na Afisa Masuuli Fungu 52, Wizara ya Afya ili kujadiliana kuhusu hoja ambazo zilikuwa katika hatua ya utekelezaji.Kimsingi Afisa Masuuli alifafanua kuwa, hoja nyingi kwa sasa zimefanyiwa kazi na wanasubiri CAG aweze kufanya uhakiki wa majibu husika na nyaraka za ushahidi.

Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Grace P. Trofumo – Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiifahamisha Kamati kuhusu uhakiki wa hoja zilizobaki kama ifuatavyo[16]:-

**Nukuu:-**

***" …Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea majibu ya Afisa Masuuli ambayo tuliletewa tarehe 13 Agosti, 2024 kuonesha vituo ambavyo vimeshapelekewa hivyo vifaa. Kwa hiyo, kutokana na muda hatukuwa tumeweza kufanya uhakiki, tumesema tutafanya uhakiki wakati ambapo tunafanya ukaguzi…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** mathalani, kwa hoja ya ukaguzi iliyohusu baadhi ya vifaa kutonunuliwa, Afisa Masuuli aliwasilisha ushahidi wa nyaraka ya makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na Wafadhili ili kuhakikisha mradi unakamilika kama ilivyopangwa katika eneo la manunuzi ya vifaa. Vilevile MSD iliwasilisha maelezo na nyaraka za mawasiliano kati yake na TAMISEMI kubadili vifaa tiba vilivyosalia vya **Sh. 13,370, 406,159.96** ili vinunuliwe kwa kuzingatia fedha iliyokuwa imebaki kwenye akaunti.Hivyo, kwa sasa vifaa mbadala vimeshanunuliwa na kusambazwa. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Mavere Tukai, Mkurugenzi Mkuu wa MSD, akifafanua kuhusu hoja hii mbele ya Kamati kama ifuatavyo[17]:-

**Nukuu:-**

***"…Mheshimiwa mwenyekiti, mwaka huu mwezi wa sita, wa tano na wa saba kwa kushirikiana na TAMISEMI tulifanya ziara kwenye kanda nyingi. Tulifanya kwenye Mikoa 23. Tulikuwa***

---

[16] Rejea Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha Tisa Tarehe 16, Agosti, 2024.

[17] Rejea Majadiliano ya Kamati, Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Uk. 94, Kikao cha Tisa, Tarehe 16 Agosti, 2024.

***tunashirikiana na kurugenzi ya afya na lishe TAMISEMI mojawapo ya ajenda ilikuwa ni kuangalia ambacho hakijawa installed, ni kwa nini hakijawa installed, na nini kifanyike kuharakisha…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi uleule, utekelezaji wa majibu ya hoja hii pia itahakikiwa na CAG katika ukaguzi unaoendelea. Aidha, Afisa Masuuli alifafanua kwamba, TAMISEMI inashirikiana na MSD kuhakikisha vifaa vinapelekwa katika maeneo husika na endapo kunatokea vituo vinajirudia au kuhitajika mabadiliko ya mgao, MSD inaomba ridhaa kutoka kwa mamlaka husika[18].Kuhusu hoja ya baadhi ya vifaa kutotumika, Afisa Masuuli alifahamisha Kamati kuwa wameongeza watumishi katika kada zenye wataalamu wachache (rare cadres) kama vile radiolojia.Aidha, mafunzo yamefanyika kwa watumishi 35 ya matumizi ya X ray ya kisasa aina ya GXR – C52.

## 2.4 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi Zinazotokana na Usimamizi wa Mikataba

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi wa mikataba (contract management) ni mchakato wa kusimamia utekelezaji wa mikataba ili kuhakikisha kuwa kila upande unafuata masharti yaliyowekwa katika mkataba.

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi wa mikataba unahusisha hatua kadhaa muhimu kama vile, hatua ya kwanza ya uandaaji wa mikataba, uthibitishaji wa mikataba, kusimamia utekelezaji wa mikataba, kuhifadhi nyaraka za mikataba, kufanya marekebisho katika mkataba, kutatua migogoro na kufunga mikataba.

---

[18] Rejea barua ya MSD kwenda TAMISEMI ya tarehe 06 Novemba, 2023 yenye Kumb. Na. AH.227/359/01 ya mabadiliko ya vituo 67 wanufaika wa mashine ya mionzi.

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi mzuri wa mikataba ni muhimu ili kuhakikisha kuwa kuna uwazi, uwajibikaji, na ufanisi katika utekelezaji wa makubaliano kati ya pande zinazohusika. Kutokana na hoja kuwa, fedha nyingi za Serikali zinatumika kwenye mikataba, Kamati ilichambua hoja za ukaguzi zinazohusu mikataba kwa baadhi ya Taasisi za Umma kama ifuatavyo: -

**2.4.1 Mapungufu Katika Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Understanding) Kati ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na London School of Hygiene and Tropical** Medicine (LSHTM)

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) iliingia Mkataba wa Makubaliano (Memorandom of Understanding) na London School of Hygiene and Tropical Medicine (LSHTM) Mwaka 2006 kwa lengo la kusaidia utafiti katika kupambana na VVU/UKIMWI, magonjwa ya ngono (STI) na masuala mengine muhimu yanayohusu afya ya jamii. Makubaliano hayo yamekuwa yakihuishwa kila baada ya miaka mitatu (03) ambapo kwa mara ya mwisho makubaliano kati ya NIMR na LSHTM yalihuishwa tarehe 26 Julai, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia makubaliano hayo London School of Hygiene and Tropical Medicine (LSHTM) imekuwa ikitekeleza shughuli zake za miradi ya utafiti hapa nchini kupitia kitengo chake cha Mwanza Intervention Trials Unit (MITU) ambacho kipo kituo cha NIMR Mwanza. Aidha, katika kipindi chote cha mkataba MITU imekuwa ikiendesha shughuli zake zote za kitaalam na kiutawala chini ya LSHTM.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa hesabu zilizo kaguliwa za NIMR kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ilionyesha kuwa masuala ya fedha ya MITU hayakujumuishwa kwenye Taarifa ya hesabu ya NIMR, kinyume na aya ya 5.7 ya Mkataba wa Makubaliano (MOU)

wa tarehe 26 Julai, 2022 inayowataka MITU kuandaa taarifa za fedha za kila robo mwaka na za mwaka mzima ambazo zitapitiwa na MITU na NIMR kituo cha Mwanza kabla ya kuzitoa kwa wahusika.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, Kamati ilibaini kuwa Mkataba wa Makubaliano (MOU) unakinzana na Sheria mama iliyoanzisha NIMR. Kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) cha Sheria ya NIMRI, Baraza la NIMRI linawajibika kusimamia utekelezaji wa majukumu na usimamizi wa masuala yote yanayohusu NIMRI. Aidha, kifungu cha 4.1 cha Mkataba wa makubaliano (MOU) Serikali imetoa mamlaka ya uendeshaji wa MITU kwa Bodi ya Usimamizi ya MITU, ambayo itaendesha shughuli zake chini ya usimamizi wa Baraza la NIMR.

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya usimamizi wa MITU inaundwa na maafisa waandamizi watatu (03) kutoka NIMRI, muwakilishi mmoja kutoka Wizara ya Afya na Wajumbe watano (5) kutoka London School of Hygiene and Tropical medicine (LSHTM) ambapo Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi huchaguliwa miongoni mwa Wajumbe kutoka LSHTM.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Wajumbe wa NIMR wanaoingia kwenye Bodi ya usimamizi ya MITU ndio wanaotakiwa kusimamia utendaji wa MITU hivyo inapelekea mgongano wa maslahi kati ya MITU na NIMR. Naomba kunukuu sehemu ya maelezo ya Ndugu Said S. Aboud Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadam (NIMR)[19] mbele ya Kamati kama ifuatavyo: -

**Nukuu: -**

***"…Niseme ambacho nilicho-observe, kwanini tumefika hapa kwenye MITU sababu kubwa tatu, MOU iliyosainiwa nasema ni MOU mbovu na***

[19] Rejea Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), Kikao cha Tarehe 07 Agosti, 2024.

***inakinzana na Sheria mama iliyoanzisha NIMR kwa sababu DG hawezi kukaa kwenye Bodi ile ni project wale wanatakiwa kuwajibika kwa Accounting Officer. Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, hawa washirika wetu wa maendeleo (London school) wamekuwa na non-compliance. Kuna vitu viko wazi lakini hawataki kuvifuata na labda kwa maslahi yao binafsi kwa hiyo non-compliance hiyo tumeiona.***

***Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sababu ya tatu; vile vile lazima tukubali ukweli sisi NIMR hatukuwa tukifuatilia kwa karibu utekelezaji wa ile MOU tuliyosaini. Kwahiyo, nadhani tuliiachia kwa kipindi cha miaka 17 iendelee basi mambo yanaendelea lakini Sheria, taratibu, Kanuni na miongozo ya Serikali of course ilikuwa imevunjwa. Kwahiyo baada ya kuligundua hilo tukaanza kuchukua hatua mbali mbali kwa sababu mfano; hatujui nini kinachoendelea na wana-operate kama Taasisi inayojitegemea. Kwahiyo, tuliwaandikia wa-submit financial statements zao ilikuwa ni barua ya tatu, nina ushahidi wa barua tatu hapa tumewaandikia lakini wamekuwa non-compliant. Hata hivyo nimewaandikia tena kuwakumbusha bado mpaka saa hizi. Jana wameniletea barua ya kuomba extension ya ku-submit financial statement kwahiyo ndio hiyo niliyokuwa nasema non-compliant, hawa-comply na kile ambacho tumekubaliana ingawa of course vile vile na MOU yenyewe ina changamoto nyingi inakinzana na Sheria mama.***

**Mwisho wa nukuu**.

**Mheshimiwa Spika,** dosari zilizopo katika MOU hiyo kama ilivyo bainishwa hapo awali imesababisha athari zitokanazo na uendeshaji wa shughuli za MITU kama ifuatavyo: -

a) Kuikosesha Serikali mapato kutokana na kwamba MITU imekuwa ikiendeshwa kama Kampuni binafsi na kutumia mali za Taasisi ya NIMR bila kulipa gharama zinazostahili mfano magari yanayokodishwa na kulipa tozo (mileage fees) na pango la jengo;

b) Kutokufikiwa kwa malengo ya uanzishwaji wake ikiwa ni pamoja na kuboresha zaidi tafiti za afya zinazo fanyika nchini Tanzania kwa kutoa programu za mafunzo katika majaribio ya kitabibu na nyanja zinazohusiana na afya ya jamii pamoja na kuifanya MITU kama sehemu ya kituo cha NIMR Mwanza na Kituo cha Umahiri katika utafiti wa magonjwa ya VVU/UKIMWI, magonjwa ya ngono (STI) na afya ya jamii kwa ujumla; na

c) Kumekuwepo na ushindani kati ya NIMR na MITU katika kutafuta fedha za ufadhili wa Miradi ya Utafiti, hii ni kinyume na makubaliano ambapo moja ya malengo ya uanzishwaji wa MITU ilikuwa ni kuisaidia NIMR na kuijengea uwezo iweze kupata miradi kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia hoja ambazo Kamati imebaini, ni dhahiri kwamba Mkataba wa Makubaliano (MOU) uliosainiwa una mapungufu hivyo kupelekea utekelezaji wake kuwa na changamoto ambazo zimepelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kutokana na dosari za MOU hiyo, Kamati imetoa mapendekezo ya maboresho katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

### 2.4.2 Ongezeko la Deni Ambalo TPDC Anaidai TANESCO Kiasi cha Sh. Bilioni 713

**Mheshimiwa Spika,** eneo lingine ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi ni ongezeko la deni ambalo TPDC anaidai TANESCO kutokana na kutolipwa ankara za mauzo ya gesi kiasi cha **Sh.713,582,336,783.3** kutoka kiasi cha **Sh.579,055,076,254.6** zilizoripotiwa mwaka 2021/22, ikiwa ni ongezeko la 23%.

**Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo uchambuzi wa Kamati ulivyobainisha hapo juu, ongezeko hili la deni linaharibu taswira ya vitabu vya hesabu vya TANESCO. Hivyo, kunatakiwa jitihada madhubuti za Serikali ili kusaidia ulipaji wa madeni haya.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuthibitisha hoja ya kuwa deni hili ni changamoto kubwa kwa TANESCO, CAG aliifahamisha Kamati kuwa kwa kuzingatia mapato ya mauzo ya umeme ya TANESCO kwa mwaka ambayo yanafikia wastani wa **Sh. Trilioni 1.93**, ingewalazimu TANESCO kutumia asilimia 37 ya mapato yake ya mwaka kulipa deni la TPDC, hivyo shughuli nyingine za TANESCO zingeathirika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hoja hii, Kamati ilikutana na Bodi na Menejimenti ya TANESCO tarehe 08 Oktoba Dodoma ili kupata maelezo ya hoja ya deni la TPDC. Uongozi wa TANESCO uliifahamisha Kamati kuwa kwa sasa umeanza kuilipa TPDC kiasi cha **Sh. Bilioni 54** kwa mwezi ili kupunguza deni hilo. Aidha, ufafanuzi wa ziada ulitolewa kuwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu (3) kuna uwezekano wa kumaliza deni hilo.

### 2.5 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi Zinazotokana na Dosari Katika Usimamizi wa Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi wa matumizi unahusu jinsi rasilimali, hasa fedha, zinavyotumika kwa ufanisi, uwajibikaji, na uwazi katika

Taasisi za Umma. Katika Sekta ya Umma, usimamizi wa matumizi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kulingana na mipango iliyowekwa na malengo ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** maeneo ya msingi ambayo Kamati ilijielekeza katika hoja za usimamizi wa matumizi ni pamoja na uzingatiaji wa bajeti, uwajibikaji, ukaguzi wa ndani, uwazi na tathmini ya matokeo ya matumizi husika. Kufuatia maelezo hayo, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu hoja zinazotokana na usimamizi wa matumizi kwa baadhi ya Taasisi za Umma kama ifuatavyo: -

### 2.5.1 Kutokuwepo Mfumo Thabiti wa Udhibiti wa Matumizi ya Mafuta ya Magari Katika Shirika la TANESCO

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya fedha ya TANESCO kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 iliripoti matumizi ya kiasi cha **Sh.32,092,836,575.80** ikiwa ni gharama ya mafuta ya magari. Gharama hizi zilitumika kuhudumia jumla ya magari 1,774 yanayomilikiwa na TANESCO kwa shughuli za kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia uchambuzi wa taarifa ya CAG, ilibainika uwepo wa gharama za juu za matumizi ya mafuta zinatokana na kutokuwepo mfumo thabiti unaotumika kufuatilia matumizi ya mafuta na umbali ambao magari yanatembea badala yake TANESCO inategemea vitabu vya kumbukumbu (log books) kama nyenzo ya kudhibiti matumizi ya mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia uchunguzi uliofanywa kwenye Kitengo cha Usafiri na ripoti ya mafuta ya kila gari kwa mwaka ilibainika kutokuwepo mfumo mmoja wa ufuatiliaji matumizi ya mafuta na umbali wa gari ili kuwezesha ufuatiliaji na utendaji wa magari. Hali hii ilichangiwa na matumizi ya vitabu vya kumbukumbu (log book) ambayo sio nyenzo madhubuti ya kudhibiti matumizi ya mafuta kwa kuwa inaweza kuandikwa kwa utashi na matakwa binafsi ya mhusika.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile taarifa ya ukaguzi ilifafanua kuwa Menejimenti ya TANESCO ilifanya jitihada za kupata mzabuni wa kusimika mfumo wa usimamizi wa magari (car tracking system) ambao ulijumuisha moduli ya mafuta. Hata hivyo, ilibainika baadaye kuwa mzabuni alishindwa kutimiza matarajio na wajibu kwa mujibu wa mkataba ambapo mfumo huo haukufanya kazi ipasavyo. Hivyo,kwa sasa Menejimenti ya TANESCO imeamua kuanzisha taratibu za kusitisha mkataba na kununua mfumo mpya wa kudhibiti matumizi ya mafuta.

### 2.5.2 Hasara ya Shilingi Bilioni 3.266 Katika Hospitali ya Benjamin Mkapa Kutokana na Kukataliwa Madai ya NHIF

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Mojawapo ya masuala yaliyojitokeza lilikuwa ni suala la hasara ya **Sh. Bilioni 3.266** iliyotokana na kukataliwa kwa madai ya Hospitali kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

**Mheshimiwa Spika**, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilibainisha sababu zilizopelekea kukataliwa kwa madai hayo kuwa ni kama ifuatavyo: -

a) Kushindwa kutimiza matakwa ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mwongozo wa viwango vya matibabu; na

b) Utofauti wa bei za matibabu kati ya Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) na bei zilizo ainishwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kulingana na mwongozo wa matibabu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kufanya mahojiano na Afisa Masuuli wa Hospitali ya Benjamin Mkapa tarehe 17 Oktoba, 2024 ili kupata ufafanuzi wa hoja hii. Afisa Masuuli aliieleza Kamati

kuwa sababu zilizopelekea kukataliwa kwa madai hayo ilikuwa ni pamoja na mapungufu katika uandaaji wa nyaraka za malipo na kutokuwa na uelewa sahihi kwa baadhi ya watumishi waliokuwa wanashughulikia nyaraka za malipo yaliyopelekwa kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile ufafanuzi ulitolewa kuwa, utofauti wa bei kwa baadhi ya huduma zilizotolewa na ile ya kwenye mwongozo wa matibabu na mapungufu katika kutunza kumbukumbu za wateja waliohudumiwa ambayo yalipelekea baadhi ya madai kukosa viambatisho vinavyo hitajika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maelezo yaliyotolewa, Kamati imeendelea na hoja hii ili kuweza kuitolea mapendekezo. Msingi wa hoja ya Kamati unatokana na uwepo wa madai mengi kwa hospitali nyingi hapa nchini kukataliwa na NHIF kwa mazingira kama ya Hospitali ya Benjamin Mkapa. Hivyo, kuna umuhimu wa eneo hili kufanyiwa kazi kwa kina.

### 2.5.3 Matumizi ya Sh. 257,334,800 Kukarabati Mgodi wa Kiwira Bila Kuanza Uzalishaji

**Mheshimiwa Spika,** eneo lingine ambalo Kamati ilifanya uchambuzi katika suala la usimamizi wa matumizi linahusu ukarabati wa Mgodi wa Kiwira. Mnamo Mwaka 2022, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) lilifanya ukarabati mkubwa wa Mgodi wa Kiwira kwa kutumia **Sh.257,334,800.**

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, wakaguzi walitembelea mgodi huo 28 Agosti, 2023 na kukuta shughuli za mgodi zilikuwa hazijaanza kufanyika. Aidha, hadi wakati ukaguzi huu unakamilika, shughuli za ukarabati zilikuwa zimekamilika kwa asilimia 90.

**Mheshimiwa Spika,** ufafanuzi uliotolewa na STAMICO ni kuwa, walikuwa hawajaanza shughuli za uzalishaji kwa sababu za kibajeti

hivyo kuwa na changamoto ya mitambo ya uchorongaji (hydraulic props). Hivyo, ni maoni ya CAG kuwa kuendelea shughuli za uchorongaji kutofanyika kunaweza kusababisha uharibifu zaidi wa mgodi na hivyo kutopata thamani ya fedha za umma zilizotumika katika ukarabati.

### 2.6 Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi za Ujumla Zinazohusu Uzingatiaji wa Sheria, Taratibu na Kanuni (Compliance Audit Issues)

**Mheshimiwa Spika,** eneo la mwisho la uchambuzi wa Kamati katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulijikita katika masuala ya ujumla yanayohusu uzingatiaji wa Sheria, Taratibu na Kanuni.
Katika eneo hili, Kamati ilibaini hoja za ukaguzi katika maeneo yafuatayo: -

#### 2.6.1 Baadhi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali Kutozingatia Mwongozo wa Wizara ya Fedha Katika Utunzaji wa Mali za Serikali kwenye Mfumo wa Kielektroniki (GAMIS)

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha Kupitia Waraka wa Hazina Na.2 wa Mwaka 2021/2022 ilitoa mwongozo kuhusu usimamizi wa mali za Serikali kwa kutumia Mfumo wa Kielekroniki (Government Asset Management Information System-GAMIS).

**Mheshimiwa Spika,** dhumuni la mwongozo huo ilikuwa kuwafahamisha Maafisa Masuuli wote kuhusu utumiaji wa Mfumo wa GAMIS na kushughulikia suala la uhuishaji wa muda wa uhai wa mali uliobaki (estimated remaining economic life -EREL) kama ilivyoelekezwa kwenye Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019 (PAMG).

**Mheshimiwa Spika,** hatua hii ya Serikali ililenga kuhakikisha taarifa za mali za Serikali zinakuwa sahihi muda wote na zinatunzwa kwenye

Mfumo wa GAMIS na mali hizo zinatumika kufungia hesabu za Taasisi zote za Umma. Katika kutekeleza maelekezo haya Maafisa Masuuli walipaswa kuhakikisha masuala yafuatayo: -

a) Mali za fungu husika zinahesabiwa kila mwisho wa mwaka na taarifa kuhakikiwa na Msimamizi wa Mali za Serikali;
b) Taarifa ya uhuishaji wa muda wa uhai wa mali uliobaki, inaandaliwa kwa kutumia fomati inayoonekana kwenye jedwali lililoambatishwa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na uwepo wa Waraka huo, Kamati imebaini changamoto ya utunzaji wa kumbukumbu za mali za Serikali, kukosekana kwa taarifa sahihi za mali za Serikali na kuwepo kwa upungufu wa taarifa za mali zinazotumika katika uandaaji na ufungaji wa hesabu za Serikali kwa kuzingatia viwango.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambazo zilifunga hesabu kwa kutumia thamani tofauti na iliyopo katika Mfumo wa GAMIS. Mchanganuo wa Taasisi hizo, jumla ya mali, thamani ya mali na tofauti iliyopo katika Mfumo wa GAMIS umechambuliwa katika Jedwali Na. 2.6 hapa chini.

**Jedwali Na. 2.6: Mchanganuo wa Taasisi na Uzingatiaji Wake Katika Mfumo wa GAMIS.**

| Na. | Jina la Taasisi | Jumla ya mali zenye thamani | Thamani inayoonekana kwenye GAMIS mpaka Juni,2023 (TZS) | Thamani ya mali (PPE) Iliyotumika kufuangia hesabu mpaka Juni,2023 (TZS) | Tofauti (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 192 | 3,694,861,287.38 | 360,227,562,869.00 | 356,532,701,581.62 |
| 2. | Shirika la Reli Tanzania (TRC) | 22,313 | 845,071,977,394.29 | 9,253,679,974,000.00 | (8,408,607,996,605.71) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) | 12,037 | 295,284,942,747.00 | - | (295,284,942,747.00) |
| 4. | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) | 473 | 39,758,268,857.11 | 57,946,577,979.00 | (18,188,309,121.89) |
| 5. | Wakala wa Mabasi yaendayo haraka (DART) | 1024 | 136,686,703,160.72 | 183,523,746,542.00 | (46,837,043,381.28) |
| 6. | Wizara Ya Elimu, Sayansi na Teknolojia-fungu 46 | 24,327 | 595,608,126,358 | 543,461,556,000 | (52,146,570,358) |
| 7. | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) | 3573 | 93,585,246,051.93 | 50,756,805,987.00 | 42,828,440,064.93 |
| 8. | Bonde la Mto Rufiji | 63 | 1,290,124,143.07 | 14,776,053,596.53 | (13,485,929,452.46) |
| 9. | Jeshi la Uhamiaji Tanzania-fungu 93 | 857 | 30,062,876,629.05 | 197,063,301,431.61 | (167,000,424,802.56) |
| 10. | Wizara ya Mambo Ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Masharikifungu 34 | 4307 | 80,159,650,464.54 | 413,632,542,464.00 | (333,472,891,999.46) |
| 11. | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | 1 | 400,000,000 | 11,061,439,00O | (10,661,439,000) |
| 12 | Msajili wa Hazina (TR)-fungu 07 | 1,847 | 36,647,799,625.37 | 54,421,915,945.82 | (17,774,116,320.45) |
| 13. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DUWASA) | 1,646 | 176,976,630,498.88 | 220,441,342,000 | (43,464,711,501.12) |
| 14. | Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezofungu 96 | 3,486 | 39,380,663,069.70 | 133,339,229,191.00 | (93,958,566,121.30) |
| 15. | Hospitali ya Rufaa ya | 6,632 | 24,716,483,868,.09 | 160,254,589,125.11 | (135,538,105,257.02 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Benjamini Mkapa | | | | |
| 16. | Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) | 1,485 | 142,602,336,394.86 | 193,228,000,000.00 | (144,679,937,014.93) |
| 17. | Bodi ya Bonde Mto Rufiji | 63 | 1,290,124,143.07 | 14,776,053,596.53 | (13,485,929,452.46 |
| 18. | Benki ya Biashara Tanzania (TCB) | 19,825 | 81,300,036,126.77 | 70,413,262,00.00 | 10,886,774,126.77 |

**Chanzo: Uchambuzi wa Kamati Kwenye Taarifa za Hesabu za Mafungu Mbalimbali, Oktoba, 2024.**

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyonekana katika Jedwali Na. 2.6 hapo juu, Wizara, Idara na Taasisi zote zilizoainishwa zilifunga hesabu kwa kutumia thamani tofauti na iliyopo kwenye Mfumo wa Gamis. Jambo hili lilifanyika kwa kutumia thamani ya juu au ya chini. Kwa msingi huo, taarifa zilizotumika kuandaa hesabu zinakuwa na dosari hasa katika eneo la la mali za kudumu (PPE). Vilevile suala hili linaenda kinyume na matakwa ya uandaaji wa hesabu kwa Viwango vya Kimataifa vya IPSAS na IFRS.

### 2.6.2 Changamoto ya Uzingatiaji wa Miongozo ya IPSAS Katika Kuandaa Hesabu za Baadhi ya Sekretarieti za Mikoa

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za baadhi ya Sekretarieti za Mikoa, ulibaini changamoto ya uzingatiaji wa masharti ya ufungaji wa hesabu bila ya kuzingatia Miongozo ya Kimataifa ya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS)[20].

**Mheshimiwa Spika,** hoja hii ilibainika katika hesabu za Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza, ambapo vitabu vya hesabu. (financial statements) vilisainiwa bila ya kuwa na viambatisho muhimu.

[20] International Public Sector Accounting Standards (IPSAS).

Viambatisho hivyo ambavyo havikuwepo ni pamoja na maelezo ya ufafanuzi wa hesabu (notes to financial statements).

**Mheshimiwa Spika,** kutowasilishwa kwa ufafanuzi wa ziada wa taarifa za hesabu kunaenda kinyume na matakwa ya IPSAS 1 inayotaka taasisi za umma kuandaa hesabu timilifu.Naomba kunukuu sehemu ya mwongozo wa IPSAS 1 kama ifuatavyo:-

**Nukuu:-**

***"…A complete set of financial statements comprises: Statement of financial position Statement of financial performance Statement of changes in net assets/equity Cash flow statement When the entity makes it approved budget publicly available, a comparison of budget and accrual amounts Notes, comprising a summary of significant accounting policies and other explanatory notes…"***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika,** Sekretarieti nyingine ya Mkoa iliyobainika kuwa na changamoto ya uzingatiaji wa Kanuni za IPSAS katika uandaaji wa hesabu ni Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora. Ukaguzi ulibaini kuwa taarifa ya ulinganisho wa Bajeti na kiasi halisi (statement of comparison of original budget and actual amount) vilionesha kutokuwepo na uhalisia kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano katika ujenzi wa nyumba ya mapumziko kwa viongozi Nzega (Nzega rest House),bajeti ya mradi ilikuwa ni **Sh. milioni 700** ambapo gharama ya mradi huu ni **Sh. bilioni 1.134,** fedha zilizotumika hadi sasa ni kiasi cha **Sh. milioni 113.449** sawa na asilimia 10 na hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni ndogo. Kwa msingi huo, taswira halisi ya vitabu vya hesabu havikuzingatia

ipasavyo miongozo na viwango vya Kimataifa katika Sekta ya Umma.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati yamezingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni ya ujumla yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni ya jumla kuwa bado kuna changamoto kwa Taasisi za Serikali zinazohusika na jukumu la ukusanyaji wa mapato ya Serikali hivyo kusababisha kutofikiwa malengo ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali.Hali hii imeendelea kuongezeka kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira hapa nchini. Hali kadhalika, Kamati ina maoni kwamba, masuala ya utawala bora, mifumo ya udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi ni maeneo ambayo yanachangia upotevu wa mapato ya Serikali, hivyo yanatakiwa kufanyiwa kazi ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati ina maoni kwamba baadhi ya Taasisi za Umma zimekuwa hazizingatii Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo muhimu inayohusu usimamizi wa fedha za umma hali inayochangia matumizi yenye dosari katika matumizi ya fedha za

umma. Ni maoni ya Kamati kuwa Sekretarieti za Mikoa zina changamoto katika uzingatiaji wa Miongozo ya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS), hivyo ni muhimu mamlaka husika zikatatua changamoto hii.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika, matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika. Mapendekezo ya Kamati yanapatikana pia katika **Randama ya 1** iliyoambatishwa na taarifa hii. Mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo: -

#### 3.3.1 Kuhusu Kutofikiwa Lengo la Ukusanyaji wa Mapato Kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Kwa Kiasi cha Sh. Trilioni 1.069

**KWA KUWA,** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imebainisha nakisi ya kiasi cha **Sh. Trilioni 1.069** cha mapato ambayo hayakukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutokana na mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na changamoto za mifumo ya kodi, mizigo inayotakiwa kusafirishwa kwenda nje ya nchi na badala yake inatumika hapa nchini bila kulipiwa kodi, kutowasilishwa kwa wakati ritani za kodi kwa wakati na dosari katika ushughulikiaji wa mashauri ya kikodi;

**NA KWA KUWA,** Kutofikiwa lengo la ukusanyaji wa mapato kunaikosesha Serikali mapato stahiki na hivyo kupunguza uwezo wa Serikali kuwa na rasilimali za kutosha kutimiza majukumu yake;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Mamlaka ya Mapato Tanzania ikamilishe maboresho ya ujenzi na usimikaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili

kuondokana na changamoto kwenye taarifa zinazopatikana kwenye mifumo iliyokuwa inatumika hapo awali. Aidha, TRA iendelee na kukamilisha zoezi la kusafisha taarifa za kwenye mifumo (Data clean up exercise) ili kuondoa changamoto ya uwepo wa taarifa zisizo sahihi za walipa kodi;

b) TRA ikamilishe zoezi la kutambua na kusajili idadi halisi ya walipa kodi waliopo hapa nchini ili kuwezesha kutambua kila aina ya kodi na kiasi kinachotakiwa au kinaweza kukusanywa kutoka kwa walipakodi husika. Aidha, TRA ihuishe kanzi data ya walipakodi (Tax base) ili kupata uhalisia wa mwenendo wa ukusanyaji wa kodi na kupanua wigo wa kodi; na

c) TRA ianze kuandaa hesabu zake za kila mwaka kwa kutumia mfumo (Revenue statements and financial statements) ili kuondoa uwezekano mkubwa wa kuwa na makosa ambayo huathiri taswira halisi (Fair view) ya vitabu vya hesabu.

### 3.3.2 Kuhusu Deni Ambalo TANESCO inadaiwa na Kampuni ya TPDC

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa deni la kiasi cha **Sh. Bilioni 713** ambalo TANESCO inadaiwa na Kampuni ya TPDC;

**NA KWA KUWA,** Deni hilo lina matokeo hasi katika matumizi ya fedha za umma kama ifuatavyo: -

a) Ongezeko la malipo ya riba kubwa kwa kuchelewa kulipa deni kwa wakati hali inayoongeza changamoto ya madeni kwa TANESCO; na

b) Kuathiri hali ya kifedha na ukwasi ya TPDC hivyo kupunguza ufanisi wa kiutendaji kazi wa TPDC.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) TANESCO iandae na kutekeleza kikamilifu mkakati na mpango wa malipo (payment schedule) ili kuhakikisha malipo ya deni la TPDC yanafanyika kwa wakati, hali itakayoepusha ukuaji wa deni; na

b) TANESCO ishirikiane kikamilifu na TPDC katika kusuluhisha ankara zinazobishaniwa, na kuhakikisha ankara zote ambazo hazijalipwa zinazohusiana na TPDC zinatatuliwa ipasavyo kwa mujibu wa makubaliano.

**3.3.3 Kuhusu Ukaguzi Maalum wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**KWA KUWA,** Ukaguzi Maalum wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu umekamilika na kubaini changamoto kadhaa katika mchakato mzima wa ugharimiaji, upangaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu hapa nchini inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB);

**NA KWA KUWA,** Matokeo ya Ukaguzi Maalum yameainisha hoja mbalimbali kuhusu matumizi ya fedha za umma katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na;

a) Bodi kutokidhi mahitaji ya kifedha kwa wahitaji wa mikopo kwa kiasi cha **Sh. Bilioni 198.9** kwa kipindi chote ambacho mawanda ya ukaguzi yalizingatia;

b) Baadhi ya wanafunzi kupewa mikopo isivyostahili; ambapo baadhi walipewa kiwango kikubwa au chini ya mahitaji waliyoomba; na

c) Kutokusanywa kwa mikopo ya **Sh. Trilioni 2.2** ambayo imekwishatolewa hadi sasa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Baada ya kukamilika mapitio ya uendeshaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu yanayoendelea, Serikali iangalie uwezekano wa kuifanya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuwa Mfuko ili kuipa uwezo wa kupata vyanzo vya ziada vya fedha ikiwemo kuweza kuwekeza kwa faida na kujenga uwezo stahimilivu kukopesha wanafunzi wengi wenye uhitaji ambao mahitaji yanaongezeka mwaka hadi mwaka;

b) Serikali na Bodi iweke utaratibu ambao utahakikisha wanafuzi wote wanaoomba mikopo ya Elimu ya Juu na waliopo vyuoni ambao hawana Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) wapatiwe, ili kurahisisha taratibu za uombaji na wepesi wa utambuzi wakati wa urejeshaji wa mikopo;

c) Serikali iendelee kutilia mkazo kuunganishwa kwa mifumo ya kieletroniki kwa Taasisi zote za Umma ili kurahisisha zoezi la kuwabaini wanufaika wote wa Mikopo ya Elimu ya Juu na kuongeza ufanisi kwenye urejeshaji wa mikopo; na

d) Kwa kuzingatia hali ya makusanyo ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliyoiva kutoka kwa wanufaika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inashauriwa kutoa maagizo kwa wadau wote kusaidia shughuli za urejeshaji wa mikopo ya HESLB kwa kuweka kigezo cha hali ya mkopo wa muombaji wa nyaraka/kibali cha utoaji huduma kama sharti la awali kabla ya kutoa nyaraka za kisheria.

### 3.3.4 Kuhusu Kuiimarisha na Kuijengea Uwezo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS)

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imefafanua kwamba Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikipata changamoto katika utekelezaji

wa majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na bajeti isiyotosheleza, gharama kubwa za uendeshaji na usimamizi wa mashauri ya usuluhishi na baadhi ya Taasisi za Serikali kutozingatia masharti ya uvunjaji wa mikataba waliyoingia;

**NA KWA KUWA,** Changamoto hizo zimekuwa na athari ya kifedha kwa Serikali hasa Serikali inaposhindwa katika mashauri husika na kutakiwa kulipa kiasi kikubwa cha fedha;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ihakikishe wigo wa Bajeti wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) unaongezeka ili kuboresha mazingira ya kazi na ubora wa huduma zitolewazo na Ofisi hiyo;

b) Serikali iwajengee uwezo Mawakili kwa kuwapatia mafunzo katika maeneo maalum ya kimkakati;

c) Serikali iweke utaratibu ambao utawezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kushirki kikamilifu katika hatua za awali za uingiaji na utekelezaji wa mikataba inayoingiwa na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ili kuikinga Serikali na hasara zinazotokana na Serikali kushtakiwa kwenye kesi za madai; na

d) Serikali ihakikishe masuala ya uwekezaji yanasimamiwa ipasavyo kwa mujibu wa Sheria na Mikataba inayokuwa imeingiwa ili kuepusha madai makubwa kwenye maeneo hayo.

### 3.3.5 Kuhusu Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Understanding) Kati ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na London School of Hygiene and Tropical Medicine (LSHTM)

**KWA KUWA,** uchambuzi wa Kamati umebainisha dosari katika utekelezaji wa Mkataba wa Makubaliano (Memorundum of

Understanding) ulioingiwa kati ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na London School of Hygiene and Tropical Medicine (LSHTM);

**NA KWA KUWA,** Dosari katika utekelezaji wa Mkataba wa Makubaliano zimekuwa na matokeo yafuatayo: -

a) Kutofikiwa kwa lengo la awali la makubaliano husika; na

b) Ukiukwaji wa utekelezaji wa makubaliano hivyo kuwepo uwezekano wa mapato ya Serikali kupotea.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ifanye mapitio ya Mkataba wa Makubaliano husika ili kuhakikisha yanazingatia Sheria mama ya NIMR na kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa; na

b) NIMR ihakikishe hesabu za kila robo mwaka na za mwaka za kituo cha Mwanza Intervention Trials Unit (MITU – Mwanza) zinaandaliwa na kupitiwa kwa pamoja kisha ziwasilishwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi.

### 3.3.6 Kuhusu Kukataliwa Madai ya Hospitali Yanayopelekwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG umebaini changamoto ya kukataliwa baadhi ya madai yanayopelekwa na hospitali hususan Hospitali ya Benjamin Mkapa, kwenda Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Madai haya hukataliwa kutokana na sababu mbalimbali kama upungufu wa nyaraka, kughushi nyaraka na makosa ya kiuandishi;

**NA KWA KUWA,** Athari zitokanazo na kukataliwa kwa madai hayo ni pamoja na kupunguza uwezo wa hospitali kutoa huduma kwa

kukosa fedha za kununua vifaa tiba na dawa, kulipa stahiki za watumishi na kulipia huduma za msingi kama umeme na maji;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kushirikiana na hospitali waboreshe utaratibu uliopo wa uaandaaji wa nyaraka sahihi na utaratibu mzuri wa malipo ili kuhakikisha kwamba madai ni sahihi, ikijumuisha uhakiki wa nambari za malipo, kutoa maelezo ya wazi ya huduma zitolewazo na kutunza rekodi sahihi za wagonjwa;

b) NHIF iendelee kutoa mafunzo na elimu ya mara kwa mara kwa watumishi wa kada ya afya kuhusu Kanuni na Miongozo ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na utaratibu wa malipo ili kusaidia kupunguza makosa na kuboresha taarifa;

c) NHIF ianze mchakato wa mapitio (review) ili kubaini madai yaliyo sahihi na madai yasiyo sahihi. Hii inatakiwa kujumuisha mawasiliano thabiti na watoa huduma husika ili kuthibitisha uhalali wa madai hayo kabla hayajawasilishwa NHIF na kukataliwa; na;

d) Kuanzishwe mfumo utakaowezesha hospitali kupata mrejesho wa madai yaliyokataliwa na Mfuko kwa wakati ili kuweza kufanya marekebisho kwa wakati na kuyapeleka kwa muda unaoruhusiwa kisheria.

### 3.3.7 Kuhusu Umiliki na Uendeshaji wa Kiwanda cha Utengenezaji Madawa cha Keko (KPI)

**KWA KUWA,** Taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Kiwanda cha Madawa Keko umebani mapungufu katika ufanisi wa shughuli za kiwanda;

**NA KWA KUWA,** Kukosekana ufanisi katika shughuli za Kiwanda cha Madawa Keko kumesababisha athari kadhaa kwa Serikali ikiwa ni pamoja na masuala yafuatayo: -

a) Kutokamilika kwa uhamisho wa miliki ya hisa za kiwanda;

b) Serikali kutopata faida ya kifedha kutokana na shughuli za kiwanda; na

c) Kutofikiwa malengo ya uanzishwaji wa kiwanda.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Madeni yote ya Kiwanda cha Madawa Keko yafanyiwe uhakiki wa kina ili kubaini usahihi na uhalali wake;

b) Serikali ikamilishe mchakato wa uhamishaji wa hisa na kutiwa saini kwa nyaraka muhimu mapema iwezekanavyo;

c) Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina iangalie uwezekano wa kuikabidhi KPI kiwe chini ya uendeshaji wa MSD kama kampuni tanzu; na

d) Serikali iangalie uwezekano wa kutoa mtaji kwa ajili ya kiwanda kununua mitambo mipya ya uzalishaji wa dawa kutokana na mitambo inayotumika hivi sasa kuwa ya muda mrefu na chakavu. Hatua hii itasaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kununua dawa nje ya nchi.

### 3.3.8 Kuhusu Madeni Ambayo Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Zinadai Kwa Taasisi za Umma

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika hesabu za Mamlaka mbalimbali za Maji na Usafi wa Mazingira umebaini uwepo wa

madeni ya ankara za maji kwa Taasisi mbalimbali za Umma. Kwa mfano DUWASA na Tanga – UWASA zinadai kiasi cha **Sh. Bilioni 1.2** na **Sh. Bilioni 2.3** mtawalia toka kwa Taasisi mbalimbali za Umma;

**NA KWA KUWA,** Kutokulipwa kwa madeni hayo kunaathiri shughuli za Mamlaka za Maji katika maeneo yafuatayo: -

a) Kukosa fedha za uendeshaji kama vile matengenezo, ununuzi wa kemikali za kutibu maji, na kulipa mishahara ya wafanyakazi;

b) Kukwamisha miradi ya maji kama vile upanuzi wa miradi ya maji, kuboresha huduma au hata kufanya ukarabati unaohitajika; na

c) Kushuka kwa ubora wa huduma kwa wananchi, ikiwemo kupunguza upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya kila siku.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: - Kabla ya Kukamilika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji ziandae na kutekeleza mkakati wa uwajibikaji ambao utawezesha ufuatiliaji wa malipo ya Taasisi za Umma kwa Mamlaka za Maji. Mkakati huu utasaidia kupata suluhisho la kudumu litalakohakisha kuwa huduma za maji zinaendelea kutolewa bila kutatizwa na madeni ya Taasisi za
Serikali.

### 3.3.9 Kuhusu Mita za Kupima Kiasi cha Gesi Inayonunuliwa na TANESCO Kuzalisha Umeme Kwa Baadhi ya Vituo

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika hesabu za TANESCO umebainisha kuwa kuna changamoto katika matumizi ya mita za kupima na kudhibiti kiasi cha gesi kinachonunuliwa kwa ajili ya kuzalisha umeme katika baadhi ya mitambo;

**NA KWA KUWA,** Kutotumika ipasavyo kwa mita hizo kunaweza kusababisha TANESCO kulipa kiasi kikubwa cha ankara za matumizi ya gesi kuliko kiasi halisi kilichotumika;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: - Ndani ya kipindi cha miezi sita (6), TANESCO wakamilishe ufungaji na upimaji wa mita za kudhibiti manunuzi ya gesi katika maeneo ambapo mita zilibainika kuwa na changamoto ya kutofanyiwa vipimo kwa mujibu wa Kanuni za WMA. Hatua hii itasaidia kutambua kiasi halisi cha gesi inayonunuliwa na kutumika, hivyo malipo yataendana na ankara halisi kwa matumizi halisi.

### 3.3.10 Kuhusu Uzingatiaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS)

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika hesabu zilizokaguliwa za baadhi ya Taasisi za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma umebaini uwepo wa tofauti katika ufungaji wa kumbukumbu za mali za Serikali kulingana na mali zilizopo kwenye Mfumo wa GAMIS;

**NA KWA KUWA,** Kutofautiana kwa thamani kwa mali za Serikali zinazoonekana kwenye Mfumo wa GAMIS kunaweza kuathiri mambo yafuatayo:-

a) Kutoshughulikiwa ipasavyo suala ya uhuishaji wa muda wa uhai wa mali uliobaki (Estimated remaining economic life); na

b) Kutokuwepo kwa uhakika wa usimamizi bora wa mali hizo na hivyo kusababisha matumizi yasiyo na tija na upotevu wa mali za Serikali katika Taasisi husika.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Ifikapo tarehe 30 Juni,2025, Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali ziwe zimetekeleza kikamilifu Waraka wa Hazina Na.2 wa

Mwaka 2021/2022 kuhusu usimamizi wa mali za Serikali, kwa kuhakikisha mali zote za Serikali zimeingizwa katika Mfumo wa Kielektroniki (GAMIS) unaoratibiwa na Wizara ya Fedha; na

b) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 Mlipaji Mkuu wa Serikali achukue hatua stahiki kwa Maafisa Masuuli wote watakaoshindwa kutekeleza masharti ya Waraka huo baada ya muda uliowekwa kukamilika.

### 3.3.11 Kuhusu Kuziwezesha Sekretarieti za Mikoa Kuweza Kuandaa Hesabu Kwa Kuzingatia Miongozo na Viwango vya Kimataifa (IPSAS)

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kutokuzingatiwa ipasavyo kwa Miongozo na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS) katika uandaaji wa hesabu kwa baadhi ya Sekretarieti za Mikoa zilizofika mbele ya Kamati Hususan, Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza na Sektretarieti ya Mkoa wa Tabora;

**NA KWA KUWA,** Kutokuzingatiwa ipasavyo kwa Viwango vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS) katika kuandaa hesabu kunafanya taarifa ya Hesabu kushindwa kutoa taswira halisi ya Taasisi na hivyo kuweza kusababisha mianya ya upotevu wa fedha za Umma;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Wizara ya Fedha kupitia Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen) iandae mkakati maalum wa kuzijengea uwezo Idara za Fedha katika Sekretarieti za Mikoa hapa nchini ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hatua hii itasaidia kuimarisha usimamizi wa fedha za Umma.

### 3.3.12 Kuhusu Ukaguzi Maalum wa Ugavi na Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa ajili ya Huduma za Mama na Mtoto (CEmONC)

**KWA KUWA**, Taarifa ya Ukaguzi Maalum wa CAG imebainisha kuwa baadhi ya vifaa vilichelewa kununuliwa na baadhi vilikuwa vimepelekwa katika vituo ambavyo havikuwa kwenye mpango wa utekelezaji wa mradi na baadhi vilikuwa vimepelekwa kwenye vituo vilivyo kusudiwa na vilikuwa havitumiki hadi wakati ukaguzi unakamilika. Aidha, Taarifa ya CAG ilifafanuwa kuwa kuna maeneo ambayo bado hajakamilisha uhakiki baada ya kupokea majibu ya Serikali;

**NA KWA KUWA**, Kupelekwa kwa vifaa kwenye vituo amabavyo havikuwa kwenye mpango wa utekelezaji na vingine kutokutumika kwa muda mrefu kunasababisha kuchakaa kwa vifaa pamoja na Wananchi kutokupata huduma iliyo kusudiwa na hivyo kushindwa kupatikana kwa thamani ya fedha iliyotumika;

**KWA HIYO BASI**, Bunge liaazimia kwamba: -

a) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TAMISEMI, kuhakikisha wanakamilisha ununuzi wa vifaa ambavyo bado havijanunuliwa na kuvipeleka katika vituo vilivyo kusudiwa ili kuweza kutoa huduma iliyo kusudiwa;

b) Wizara ya Afya ihakikishe inafuatilia ukamilishaji wa mradi kama ulivyokuwa umepangwa ili thamani ya fedha iweze kupatikana na Wananchi waweze kupata huduma kwa wakati; na

c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, afanye uhakiki wa kina wa majibu ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mradi huu katika ukaguzi unaoendelea hivi sasa. Baada ya uhakiki wa majibu ya utekelezaji wa mradi, Bunge lijulishwe ipasavyo.

### 3.3.13 Kuhusu Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) Kutengeneza Ankara za Malipo Nje ya Mfumo na Kutokamilika Kanuni za Sheria ya TTB, Sura, 364

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ulibaini dosari katika utoaji wa Ankara za malipo kutoka kwenye Mfumo wa Uratibu wa Maonesho na nambari za udhibiti kutoka kwa GePG. Aidha, Kamati ilibaini kutokuwepo kwa Kanuni za Sheria ya TTB ya Mwaka 2002.

**NA KWA KUWA,** Masuala hayo mawili yana athari kadhaa kama ifuatavyo: -

a) Dosari katika Mfumo unaweza kuathiri ukusanyaji wa mapato ya Serikali; na

b) Ukosefu wa Kanuni unapunguza ufanisi wa TTB kutekeleza majukumu yake.

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Kabla ya kukamilika mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (E – Government) wakamilishe maboresho ya mfumo ili uweze kusomana na Mfumo wa Malipo wa Serikali (GePG); na

b) Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utalii atekeleze masharti ya Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura,364 inayompa mamlaka ya kutengeneza Kanuni ili kusaidia utekelezaji wa Sheria ipasavyo. Kanuni hizo, mathalani Kanuni za Mabalozi wa Hiari wa Utalii ni muhimu ili kusaidia katika kuongeza makusanyo ya fedha za umma kupitia Sekta ya Utalii.

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb – **Mwenyekiti**
2) Mhe.Japheti Ngailonga Hasunga, Mb - **M/ Mwenyekiti**
3) Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele, Mb
4) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
5) Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato, Mb
6) Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
7) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
8) Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
9) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
10) Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
11) Mhe.Jacqueline Ngonyani Msongozi Mb
12) Mhe.Janeth Maurice Masaburi, Mb
13) Mhe.Esther Nicholas Matiko, Mb
14) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
15) Mhe.Condester Michael Sichalwe, Mb
16) Mhe.Nancy Hassan Nyalusi, Mb
17) Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
18) Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb
19) Mhe. Bakar Hamad Bakar, Mb
20) Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka I. Leonard kwa uongozi wake wa Sekretarieti ya Bunge ambayo imeratibu na kufanikisha shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho japo sio kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), na kwa namna ya pekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere. Aidha naishukuru Wizara ya Fedha kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG), Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen, Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM), Ofisi ya Msajili wa Hazina (TRO) na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu majibu ya hoja za ukaguzi na mahojiano ya Kamati na Maafisa Masuuli.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU**
**YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)**

28 Oktoba, 2024

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Hii ni hoja yetu, ni hoja ya Bunge.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)*, Mheshimiwa Halima James Mdee, aje awasilishe taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)*:** Mheshimiwa Spika, nikiwa nimempoteza Mama tarehe 30 Julai, 2024 naomba nitoe shukrani kwa Wabunge wote wakiongozwa na wewe kwa kunishika mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati Kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu Zilizokaguliwa za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, Maelezo ya Jumla. Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati Kuhusu Hesabu za Serikali, kwa Hesabu Zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023 na kuliomba Bunge lako lipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, Muhtasari wa Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati. Katika kuhakikisha Bunge linafuatilia nidhamu ya mapato na matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwamba, kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha za Umma, Kamati iliweza kujadili na kuchambua Taarifa za Hesabu za Serikali Zilizokaguliwa na kufanya mahojiano na Wakurugenzi wa Halmashauri 55 ambazo ni sawa na 29.89% ya Halmashauri zote 84.

Mheshimiwa Spika, Kamati iligundua yafuatayo: Kukosekana kwa Mikakati Madhubuti ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani**.** Kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilipeleka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ruzuku ya jumla ya shilingi trilioni 7.60 ambapo kati ya fedha hizo shilingi trilioni 2.4 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi trilioni 5.21 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara. Aidha, Halmashauri 184 ziliweza kukusanya shilingi milioni 912.1.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri 55 zilizofika mbele ya Kamati kwa ajili ya mahojiano katika kipindi cha mwezi Agosti na Oktoba, 2024, kwa ajili ya hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilipeleka jumla ya shilingi bilioni 639.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, shilingi trilioni 1.4 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 79.2 kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Halmashauri hizo. Aidha, kwa upande wa makusanyo ya ndani, Halmashauri hizo 55 ziliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 404. Mchanganuo wa upokeaji wa ruzuku ukilinganishwa na ukusanyaji wa mapato ya ndani uko kwenye kiambatisho Na. 2 cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi zimekosa ubunifu wa vyanzo vya mapato, pamoja na mkakati madhubuti wa ukusanyaji wa mapato, hali inayosababisha kutokufikia malengo ya ukusanyaji. Ifuatayo katika jedwali Na. 1 ni orodha ya halmashauri ambazo zilifanya vibaya zaidi katika kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, Biharamulo *DC*, bajeti ambayo iliidhinishwa ilikuwa shilingi bilioni 3.5, makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 2.2, pungufu ilikuwa shilingi bilioni 1.2, ikiwa ni pungufu ya bajeti kwa 35%. Tandahimba *DC*, bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa shilingi bilioni 5.5, makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 3.8, pungufu ilikuwa shilingi bilioni 1.7, asilimia ya upungufu ni 31. Mtwara Mikindani *MC*, bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa shilingi bilioni 5.4, makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 3.8, pungufu ilikuwa shilingi bilioni 1.5 ambayo ni sawa na 29% ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati imekuwa ikizielekeza halmashauri zote zinazofika kwa ajili ya mahojiano kufanya tathmini ya kina ya vyanzo vyote vya mapato vilivyomo katika halmashauri zao ili kubaini ufanisi wa vyanzo hivyo na kuangalia fursa mbalimbali za kiuchumi (kibiashara) zilizoko pamoja na kuandaa mikakati inayotekelezeka kwa kutumia fursa

hizo, ili kuongeza mapato kwa kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Mapato Yasiyokusanywa Kutoka Katika Vyanzo Muhimu shilingi bilioni 61.15. Halmashauri zote zimekuwa zikipitisha sheria ndogo ambazo zimekuwa zikiainisha vyanzo mbalimbali vya mapato vitakavyokusanywa katika maeneo yao ya usimamizi. Kinyume na Agizo Na. 7 (d) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, baadhi ya hamashauri hazikukusanya jumla ya shilingi bilioni 61.15 kama inavyoonekana katika Jedwali Na.2.

Mheshimiwa Spika, orodha ya vyanzo vya mapato visivyokusanywa ni kama ifuatavyo: mauzo ya viwanja inaongoza katika idadi ya halmashauri 23 ikiwa na jumla ya shilingi biioni 42.5. Kodi ya pango, halmashauri 43 ikiwa na jumla shilingi bilioni 7.4. Mapato mengineyo, halmashauri 22 ikiwa na thamani ya shilingi bilioni 6.3. Rejea nyingine mtazikuta kwenye taarifa kwa sababu, hapa tunasoma kwa ufupi, haya ni maeneo matatu ambayo ni sugu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ndiyo sugu kuliko wote, imeshindwa kukusanya mapato yanayotokana na ushuru jumla ya shilingi bilioni 6.03 kutoka katika Kampuni ya Yapi Merkez iliyokuwa inajenga Reli ya Kisasa ya *SGR* ambapo deni hilo ni la tangu mwaka 2021. Kutokukusanywa kwa ushuru huo kwa wakati kunapunguza mapato ya halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa ufanisi katika ukadiriaji na ukusanyaji wa ushuru wa huduma shilingi bilioni 4.18. Kinyume na matakwa ya vifungu vya 6(1) (u) na 7(1) (y) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kama ilivyorekebishwa na Kifungu cha 44 na 45 cha Sheria ya Fedha, Sura ya 348, Kamati imebaini uwepo wa halmashauri 37 ambazo zilishindwa kukusanya jumla ya shilingi

bilioni 4.18 zinazotokana na ushuru wa huduma kutoka kwa wafanyabiashara ambao wapo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, halmashauri kukusanya ushuru wa huduma bila ya ripoti za mauzo ghafi ni shilingi bilioni 8.15. Wakurugenzi waliofika mbele ya Kamati wameeleza kuwa, wamekuwa wakipatiwa taarifa ya kiasi cha ushuru wa huduma kinachotakiwa kulipwa na wafanyabiashara kutoka katika Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Hata hivyo, kiasi hicho kinachokusanywa hakiendani na ukubwa wa biashara zinazofanyika katika maeneo hayo. Changamoto hii kwa kiasi kikubwa imebainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Spika, Mawakala wa kukusanya mapato kutowasilisha benki shilingi bilioni 5.65. Halmashauri 12 ziliingia jumla ya mikataba 53 ya ukusanyaji wa mapato ambapo, kwa mujibu wa mikataba hiyo, jumla ya shilingi bilioni 14.43 zilitakiwa kukusanywa na mawakala husika. Kinyume na matakwa ya Kifungu cha 26 (a) na (b) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kiasi cha shilingi bilioni 8.89 pekee ndicho kilichopokelewa na Halmashauri husika na kubakiwa na deni la shilingi bilioni 5.65 ambayo ni sawa na 39%, kiasi ambacho hakijawasilishwa kwa mujibu wa mikataba husika. Kamati inaweka msisitizo kwa Serikali kuchukua hatua stahiki kwa mawakala ambao hawajakidhi matakwa ya mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, kutokusuluhishwa kwa madai katika Mfumo wa *LGRCIS* yanayoweza kusababisha hasara ya shilingi bilioni 45.02. Serikali imekuwa ikifanya maboresho ya mifumo mbalimbali ya kielektroniki ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lengo likiwa ni kudhibiti upotevu wa fedha za umma, Halmashauri zote zilitakiwa kusitisha shughuli katika mfumo wa zamani wa *LGRCIS* na kuanza kutumia mfumo wa TAUSI ifikapo Tarehe 31 Machi, 2023.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutakiwa kufuta ama kumaliza kwa kutumia *LGRCIS* toka mwaka 2023 bado kuna halmashauri 125 ambazo *CAG* amebaini kushindwa kukusanya na kutofanya usuluhishi wa jumla ya shilingi bilioni 45.02. Vigogo kwenye halmashauri hiyo kuna Msalala *DC* bilioni 2.6, kuna Bukoba *Municipal Council* shilingi bilioni 1.528. Hizi ni fedha ambazo ni halali za watu wanaotakiwa kulipa kodi, lakini hawajalipa. Kwa mfano, Bukoba *Municipal Council* makusanyo yao ya mwaka ni shilingi bilioni 2.5 halafu unakuta manispaa ambayo inakusanya kidogo kiwango hicho haijaweza kusuluhisha shilingi bilioni 1.5, huku ni kukosa uwajibikaji kwa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Spika, kutokufanyika kwa usuluhishi kunaweza kusababisha hasara na upotevu wa mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

Mheshimiwa Spika, mapato yaliyokusanywa kwa kutumia *POS* kutowasilishwa benki, shilingi bilioni 6.17. Bunge lako Tukufu limeshaazimia juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa wakusanya mapato wanaohusika na kukusanya mapato ya Halmashauri bila ya kuziwasilisha fedha hizo benki ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi bilioni 11.07 zilikusanywa bila ya kuwasilishwa benki.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imejirudia mwaka huu tunaoujadili ambapo waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri wamekusanya jumla ya shilingi bilioni 6.17 pasipo kuziwasilisha katika akaunti za benki za Halmashauri. Halmashauri zenye hoja hii zimekuwa zikiieleza Kamati kuwa, hatua zilizochukuliwa kwa wakusanya mapato ambao hawajawasilisha fedha hizo benki ni kuwapeleka TAKUKURU, sababu ambayo Kamati imekuwa ikiikataa kwa sababu, unapokusanya fedha na kuthibitisha fedha umekusanya, hujapeleka benki, huo ni wizi. Huwezi kupeleka kesi ya wizi kwa TAKUKURU ambao wanahusika na kuzuia na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, mfano wa halmashauri ambazo kwa kiasi kikubwa mapato yake hayakuwasilishwa benki na wakusanya mapato ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya Momba, shilingi milioni 470, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, kwa kaka wa Taifa, shilingi milioni 282 na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, shilingi milioni 113.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine mtazikuta kwa mawanda yake ni usimamizi usioridhisha kwenye fedha za umma pamoja na Akaunti ya Amana, sitasema hapa kwa sababu ya muda, inayohusu malipo yasiyofanywa na stakabadhi za kieletroniki shilingi bilioni 743, imefanywa na halmashauri. Malipo yaliyofanyika kutoka Akaunti ya Amana kwa shughuli zisizokusudiwa, shilingi bilioni 5.16.

Mheshimiwa Spika, madeni ya halmashauri kutolipwa kwa wakati, shilingi bilioni 87.32. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi uliofanyika katika halmashauri 87 ulibaini kuwa, madeni ya wazabuni na watumishi yalifika shilingi milioni 87.32. Katika madeni hayo kwa halmashauri 37, madeni ya wazabuni yalikuwa ni shilingi bilioni 38.2 na madeni ya watumishi yalikuwa shilingi bilioni 49.09.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa madeni hayo ambapo Halmashauri ina madeni yake ambayo inatakiwa kuyalipa kwa watumishi na wazabuni kwa kuzielekeza na kuweka kipaumbele kwa ulipaji wa madeni kulingana na umri wa madeni na kukubaliana na halmashauri husika muda wa kuyalipa ili kuepukana na kufunguliwa kesi za madai au kutozwa riba inayotokana na ucheleweshaji wa malipo.

Mheshimiwa Spika, Madeni ya Watumishi. Katika madeni ya watumishi kuna madeni ambayo yanapaswa kulipwa na Serikali Kuu. Kamati imefanya uchambuzi wa taarifa kwa halmashauri 55 zilizofika kwa ajili ya majadiliano na kubaini jumla ya shilingi bilioni 38.8 ambazo hazijalipwa kwa watumishi. Madeni ya watumishi

yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu, Halmashauri vigogo zinazodaiwa ni Dar es Salaam *City Council* shilingi bilioni 4.2, Temeke *Municipal Council* shilingi bilioni 2.5 na Chemba *DC* shilingi bilioni 2.14. Ni aibu kwa Halmashauri za Dar es Salaam zinazokusanya fedha nyingi sana kuwa na madeni ya namna hii ya watumishi. Ni vyema Serikali ikaendelea kulipa stahiki hizo za watumishi ili kuongeza ufanisi na morali ya utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Spika, halmashauri nyingi nchini zinadaiwa na watumishi wake stahiki mbalimbali. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kulikuwa na madeni ya watumishi yenye jumla ya shilingi bilioni 17.1. Yale niliyotaja mwanzo ni yanayodaiwa na Serikali Kuu, hii shilingi bilioni 17.1 ni madeni ambayo Halmashauri yenyewe inatakiwa ilipe kutokana na vyanzo vyake vya ndani.

Mheshimiwa Spika, madeni ya watumishi wanaopaswa kulipwa na halmashauri, halmashauri sugu ambazo zinadaiwa kwa mapato yake ya ndani ni zifuatazo; Chato *DC* shilingi bilioni 2.98, Mpwapwa *DC* shilingi bilioni 1.062 na Dar es Salaam *City Council* shilingi milioni 957.6.

Mheshimiwa Spika, madeni ya wazabuni pia ni jambo ambalo ni sugu. Tumekuwa tukizungumza hapa, lakini Serikali haichukui hatua stahiki kuonesha kwamba inakerwa na hili jambo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kwa halmashauri 55 zilizohojiwa umebaini kuwa, Serikali Kuu inadaiwa na wakandarasi na wazabuni jumla ya shilingi bilioni 14.2. Madeni ya wakandarasi na wazabuni yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu ni kama ifuatavyo: Halmashauri ya Ubungo *Municipal Council* shilingi bilioni 8.5, Dar es Salaam *City Council* shilingi bilioni 1.5 na Chato *DC* shilingi bilioni 1.258. Haya ni madeni yanayotakiwa kulipwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, madeni ambayo wazabuni wametoa huduma mbalimbali kwenye halmashauri zetu. Kamati imebaini

katika Halmashauri 55 ambazo tumekutananazo na ni muhimu mkaelewa kwamba nchi hii ina Halmashauri 184. Hapa tunazungumzia Halmashauri 55 tu ambazo tumekutananazo zinadaiwa na wazabuni shilingi bilioni 29.9. Halmashauri hizi tumekutananazo uso kwa uso, wametoa hoja zao na zimekuwa *verified* na *CAG* shilingi bilioni 29.9.

Mheshimiwa Spika, Kamati imezielekeza halmashauri kulipa madeni hayo kwa kukubaliana muda ambao madeni yote yanapaswa kulipwa. Imebidi Kamati yako tufanye kazi ambayo kimsingi ilitakiwa kufanywa na Serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutorejeshwa kwa mikopo ya programu ya kupanga, kupima na kurasimisha, shilingi bilioni 21.85. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango wakati huo na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi zilitoa mkopo wa shilingi bilioni 42.28 kwa halmashauri 58. Mkopo huo ulitokana na Programu ya Kupanga, Kupima na Kurasimisha Viwanja (KKK).

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kiasi cha mikopo kilichorejeshwa ni shilingi bilioni 20.42 tu na kubakiwa na deni la bilioni 21.83, ambapo Halmashauri 47 ndizo zilizolipa deni huku Halmashauri 58 zikishindwa kulipa madeni yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati kwa mfano, Halmashauri ambazo bado hazijaresha kiasi chote cha fedha ni Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze shilingi bilioni 1.7, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala shilingi bilioni 1.1 na Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga shilingi bilioni 774.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya rasilimaliwatu na mishahara tulibaini yafuatayo: Makato ya kisheria kutowasilishwa katika Taasisi zinazostahili kupata makato husika, shilingi milioni 36.09, na hili ni jambo ambalo Kamati yako ilishasema, Bunge lilishaazimia lakini Serikali haitekelezi kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, mchanganuo wa makato ya watumishi ambayo hayakuwasilishwa katika taasisi husika ni pamoja na *PSSSF* shilingi bilioni 3.5, kodi ya mapato shilingi milioni 51, *NHIF* shilingi milioni 40, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii shilingi milioni 54, Mfuko wa fidia wa wafanyakazi shilingi milioni 204 na taasisi nyinginezo ni shilingi milioni 68 na kufanya jumla ya makato yote kuwasilishwa kuwa shilingi bilioni 4.01. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri 46 zilizokaguliwa na *CAG* na nataka Serikali inisikilize hapa kwa makini. Katika Halmashauri 46, zilizokaguliwa na *CAG* faini ama adhabu inayotokana na ucheleweshaji wa malipo ni shilingi bilioni 32.04. Yaani unashindwa kulipa shilingi bilioni 4.01 unaenda kutozwa faini ya shilingi bilioni 32.04! Huku ni kutokuwajibika kwa kiwango kikubwa sana, matokeo yake deni ambalo lilikuwa la shilingi bilioni nne limekuwa shilingi bilioni 36.09. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tukija kwenye Halmashauri moja; Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga iliijulisha Kamati kwamba wao wenyewe, Halmashauri ilipata adhabu ya kutakiwa kuilipa *PSSSF* shilingi bilioni 45.7 kutokana na kushindwa kupeleka michango ya watumishi ya shilingi milioni 238, licha ya kuwa Halmashauri imeshailipa jumla ya shilingi milioni 119 na kubakiwa na hiki kiasi. Tumewaomba ama tumewaelekeza Halmashauri ikakutane na *PSSSF* na tunaomba Serikali mwasaidie ili kutumia ile *room* ambayo mabadiliko ya sheria yamefanyika ya ku-*negotiate* hizi adhabu, basi ifanyike ili adhabu tuweze kuzipunguza ama kuzifuta na kilipwe kile kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kufanya ununuzi wa shilingi bilioni 28.13 nje ya mfumo wa kieletroniki. Serikali ilitoa tangazo la ununuzi wa umma kufanyika kwa njia ya mfumo wa kieletroniki, hata hivyo, kuna baadhi ya Halmashauri zilifanya ununuzi nje ya mfumo wa kietroniki. Halmashauri sugu ni kama zifuatazo: Ndugu yangu wa Msalala naona uko kila sehemu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala shilingi milioni 531, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga shilingi milioni 279, Halmashauri ya Wilaya ya Geita shilingi bilioni 9.4, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo shilingi bilioni 2.7 na Halmashauri ya Wilaya ya Siha shilingi bilioni 1.6. Ununuzi nje ya mfumo mara nyingi ni kiashiria cha kutokuwa na uaminifu, wizi na rushwa. Kwa hiyo, tunataka wajisome na wajielewe na Serikali ichukue hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa shilingi bilioni 4.79 hazikuidhinishwa na Bodi za Zabuni, hii mtaikuta kwa kina kwenye taarifa kwa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kufanya ununuzi wa shilingi bilioni 28.7 nje ya mpango wa ununuzi, kunaongeza uwezekano wa kufanya matumizi yasiyo na tija katika Halmashauri kwa kufanya ununuzi ambao haukupangwa na kukwamisha shughuli zilizopangwa katika mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa mfano wa hoja hii, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ilifanya ununuzi nje ya mpango kwa shilingi bilioni 4.6; Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa bilioni 2.6 na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala shilingi milioni 440 nje ya mpango wa ununuzi.

Mheshimiwa Spika, upungufu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, yafuatayo yalibainika. Kamati imebaini uwepo wa miradi kutokukamilika kwa wakati ambapo katika mwaka 2022/2023 miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 206 ilikuwa haijakamilika. Miradi ambayo ilikamilika na kutokuanza kutumika ilikuwa shilingi bilioni 11.2. Kwa mapana mtapa katika ripoti kubwa.

Mheshimiwa Spika, fedha za mapato ya ndani kutokupelekwa katika miradi ya maendeleo shilingi bilioni 17.6. Halmashauri ambazo hazikupeleka kiasi chote cha fedha, Maafisa Masuuli wamekiri kutumia fedha ambazo zilitakiwa zipelekwe kwenye matumizi ya

maendeleo na kupeleka kwenye matumizi ya kawaida. Maafisa Masuuli hao kwa kukiri kosa wameahidi mbele ya Kamati yako kuzirejesha fedha hizo kutoka katika makusanyo ya mapato yao ya ndani na kutoka kwenye matumizi yao ya kawaida ili ziweze kukamilisha miradi ya maendeleo ambayo haijakamilika. *(Makofi)*

Mheshmiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo yaani kuanzia 2020/2021 mpaka 2022/2023, Halmashauri 55 ambazo zimefika mbele ya Kamati yako hazikutenga jumla ya shilingi bilioni 38.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mfano wa halmashauri ambazo ni sugu ambazo kwa miaka mitatu mfululizo hazikupeleka pesa ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa miaka mitatu mfululizo haikupeleka shilingi bilioni 21.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Singida *Municipal Council* kwa miaka mitatu mfululizo, tena hawa wenzetu mapato yao kwa hiyo miaka mitatu ni shilingi bilioni 4.7, wanatakiwa wapeleke shilingi bilioni 4.7 ukitoa *sixty percent,* ukitoa mapato lindwa kiasi ambacho hakikupelekwa ni shilingi bilioni 2.3 *almost* nusu. Kigamboni *Municipal Council* wanatakiwa kupeleka shilingi bilioni 15 lakini hawakupeleka shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako imewataka Wakurugenzi wote kuhakikisha fedha za miradi ya maendeleo zinapelekwa kwa wakati na fedha ambazo zilitumika kwa matumizi mengineyo zinarejeshwa na *CAG* ataenda kufanya uhakiki wa kuhakikisha fedha hizo zimerudi na kufanya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ambavyo ilitarajiwa kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Mwaka 2018 Bunge lilifanya marekebisho ya Sheria za Serikali za Mitaa na kuongeza Kifungu cha 37A ambacho kiliweka masharti ya kutenga 10% kwa ajili ya vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu. Katika hesabu za Mamlaka za Serikali za Mtaa ambazo tunazijadili, thamani ya mfuko toka mwaka 2018

tulivyotunga sheria mpaka sasa, yaani fedha ambazo zimetoka zimeenda kwa wananchi ni shilingi bilioni 245. Kamati tulipokea na kufanya uchambuzi wa mwenendo wa mfuko huo na Kamati tulipata nafasi ya kusikiliza Wakurugenzi kuhusu uendeshaji wa mfuko husika.

Mheshimiwa Spika, mambo kadhaa tuliyagundua, kwanza shilingi bilioni 7.27 za mapato ya ndani hazikupelekwa katika mfuko husika, mtaenda kwenye taarifa, mtapata uchambuzi wa kina na halmashauri ambazo hazikuchangia kikamilifu ni Kigoma Ujiji ilienda pungufu shilingi milioni 349; Chato *DC* ilienda pungufu, shilingi milioni 275, Chalinze *DC* ilienda pungufu shilingi milioni 183. Kwenye taarifa pana vilevile tumefanya uchambuzi juu ya shilingi bilioni 38.81 za mikopo ambayo ilitolewa bila kuzingitia uwiano wa 4:4:2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ambayo ni muhimu na ningependa Serikali isikilize kwa umakini ni mikopo iliyotolewa kwa vikundi yenye thamani ya shilingi bilioni 79.76 kutokurejeshwa. Kutokana na ufuatiliaji mdogo wa ukusanyaji wa mikopo hiyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 halmashauri zilishindwa kuzirejesha shilingi bilioni 79.76. Halmashauri ambazo ni sugu kwa kutokurejesha mikopo husika ni kama ifuatavyo: Kinondoni *Municipal Council* shilingi bilioni 6.1, Temeke shilingi bilioni 5.3, na Ubungo shilingi bilioni 4.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri 55 zilizofika mbele ya Kamati, fedha za mikopo jumla ya shilingi bilioni 36.6 zilikuwa hazijakusanywa kutoka vikundi mbalimbali. Hii shilingi bilioni 79 tunayoizungumza ni ile mikopo chechefu ambayo muda wake wa kimkataba umeisha, haijakusanywa na hakuna mkakati madhubuti wa kukusanywa. Hatuzungumzii fedha ambazo ziko ndani ya mkataba. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto mbalimbali zilizobainika katika uendeshaji wa mfuko huo mwezi Aprili, 2023 Serikali ilisitisha shughuli zote za mfuko huo ili kufanya maboresho.

Tarehe 16 Aprili, 2024 wakati wakiwasilisha bajeti yake Waziri wa TAMISEMI alisema kuanzia mwezi Julai, 2024 walitakiwa ama walikuwa wanatarajia kuanza kutoa mikopo ambayo thamani yake kiujumla itakuwa shilingi milioni 227.90.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba fedha hizo ambazo Mheshimiwa Waziri alizitaja hapa Bungeni bado hazijaanza kutolewa kwenye vikundi, kutokana na maboresho ambayo yanafanyika. Hata hivyo, katika kujiridhisha juu ya hatua zinazochukuliwa na Serikali katika maboresho ya mfuko huo Kamati tatu za *LAAC,* TAMISEMI na Bajeti, tuliomba kupitishwa katika utaratibu mpya unaoandaliwa wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina na kupitishwa kuhusu mfumo mpya wa utoaji mikopo wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, Kamati zote tatu ziliona bado kuna changamoto ambazo zinahitaji kuondolewa ili upungufu uliopo sasa hivi usiweze kujirudia. Serikali inatakiwa ikafanyie kazi changamoto hizo ili kuboresha zaidi utoaji wa mikopo hiyo na wananchi wengi na wenye sifa waweze kunufaika na mikopo hiyo kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizobainika ni kama ifuatavyo:

(i) Kuruhusu fedha za kundi moja kukopeshwa na kundi lingine;

(ii) Kutowekwa wazi utaratibu wa utolewaji wa mikopo kwa kutumia mifumo ya benki;

(iii) Uwepo wa sharti la lazima na kitambulisho cha Taifa licha ya changamoto ambazo wote tunazijua za upatikanaji wa vitambulisho hivyo;

(iv) Kutozingatia upatikanaji wa mitandao katika maeneo ya vijijini; na

(v) Kiasi kikubwa cha fedha za ufuatiliaji wa mikopo hiyo kinachopunguza uwezo wa halmashauri kukopesha pamoja na uwepo wa adhabu kutolewa kwa wakopeshaji pekee bila adhabu kutolewa kwa watoaji pia. Kwa sababu kwa vikao vyetu ambavyo tumefanya tumegundua kuna uzembe mkubwa kwa watoaji mikopo pia, sasa kwa nini adhabu iwe kwa upande mmoja na siyo pande zote mbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizobainika, Kamati inaishauri Serikali kuondoa changamoto zilizobainishwa na wajumbe pamoja na kuanza na halmashauri chache zenye mfano. Tufanye *pilot study,* hatuwezi kuwa tumeshindwa kukusanya pesa nyingi, tukaingiza mabilioni ya fedha kwa kukurupuka. Tuanze na *pilot,* tuangalie tutakosea wapi? tutajifunza wapi ili tukifungua dirisha zima, basi liende kwa ufanisi ambao tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa yetu vilevile imezungumzia juu ya Tathmini ya Uwekezaji wa Halmashauri katika Mkoa wa Dar es Salaam ya Benki ya *DCB.* Mwaka 2001 Mkoa wa Dar es Salaam Halmashauri zote tano zilikubaliana kuunda Benki ya *DCB* ambayo ni Halmashauri ya Dar es Salaam, Ilala, Kinondoni, Temeke na Halmashauri ya Kigamboni na sasa hivi tuna Halmashauri ya Ubungo, ambapo jumla tumewekeza shilingi bilioni 26.8 na tuna hisa shilingi milioni 31.9.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa umiliki katika hisa za Dar es Salaam kuna makundi 11, mtaona katika taarifa yetu makundi ambayo wana hisa, lakini kulingana na jedwali ambalo tumeainisha kwenye taarifa yetu, Halmashauri za Dar es Salaam kwa pamoja zina 33% ya mtaji wote lakini vilevile ukichanganya na mashirika

mengine na Serikali pia ina umiliki wa jumla ya hisa 63% za mtaji wote.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ambayo tumeeleza ambayo mtayasoma kwa kina, *DCB* inamilikiwa na Serikali kupitia halmashauri 33% lakini pia *UTT* na *NHIF*. Hata hivyo, benki hii hapo awali ilianzishwa kama benki binafsi iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni. Kwa hiyo, hakuna Sheria ya Bunge ya kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, benki hii haimo kwenye orodha ya Mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina na hivyo haijawahi kuwasilisha taarifa zake za fedha kwa *CAG* kwa ajili ya ukaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kukutana na uongozi wa *DCB* pamoja na Wakurugenzi wote wa Halmashauri ili kufahamu juu ya nafasi ya Serikali katika uendeshaji wa benki hiyo. Hata hivyo, uongozi wa benki uliieleza Kamati kuwa Serikali haina umiliki mkubwa wa hisa kwa kuwa hisa za *UTT* zinatokana na uwekezaji wa mwananchi mmoja mmoja, hivyo siyo mali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sisi tunaona hii hoja haina mashiko kwa sababu *UTT* ipo chini ya Msajili wa Hazina na hesabu zake zinakaguliwa na *CAG*. Kwa muktadha huo, hata benki ya *DCB* inapaswa kuwa chini ya Msajili wa Hazina kwa sababu kwa huu ujumla hisa zote ni 63% pamoja na za Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa uwekezaji ambao umefanywa na Halmashauri husika kwa sasa unazidi kuwa hauna tija kwani thamani ya hisa za *DCB* zimeendelea kushuka kwa shilingi 50/= kutoka shilingi 190/= hadi shilingi 140/=. Wakati benki inaanzishwa hisa moja ilikuwa shilingi 1,000/=, zimeishaporoka

hakuna uangalizi, watendaji kule wanajifanyia mambo wanavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendelea kupungua kwa thamani ya hisa hizi kunasababisha halmashauri kuendelea kupata hasara, ambapo hadi tarehe 30 Juni, 2023 Halmashauri ya Temeke ilipata hasara ya shilingi bilioni 2.9; Halmashauri ya Kinondoni ilipata hasara ya shilingi bilioni 3.4, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilipata hasara ya shilingi bilioni 6.2, Halmashauri ya Kigamboni ilipata hasara ya shilingi bilioni 1.9, Halmashauri ya Ubungo ilipata hasara ya shilingi bilioni 2.1.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ya *LAAC* imesema itafanya kazi kwa weledi mkubwa lakini vilevile tutawataja mpaka wanyooke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati, kuhusu kukosekana kwa mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ihakikishe kuwa mapato ya shilingi bilioni 61.15 yanayotokana na vyanzo muhimu yanakusanywa na Halmashauri husika;

(b) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinahuisha kanzidata za walipakodi ili kupata taarifa sahihi na idadi kamili ya wafanyabiashara wanaostahili kulipa ushuru wa huduma na kuwasilisha *CAG* kabla ya tarehe 30 Machi, 2025;

(c) Serikali ihakikishe *TRA* inakuwa na takwimu sahihi za mauzo ghafi ili Halmashauri ziweze kukusanya kiwango sahihi cha ushuru wa huduma;

(d) Serikali ihakikishe kuwa Halmashauri zinakusanya kiasi cha shilingi bilioni 5.65 kutoka kwa mawakala wa ukusanyaji mapato;

(e) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinafanya usuluhishi wa madai yote katika Mfumo wa *LGRCIS* yenye jumla ya shilingi bilioni 45.02 ili kujua wadaiwa halali wa halmashauri na wadaiwa wasio halali ili waweze kuondolewa katika mfumo kabla ya tarehe 30 Machi, 2025;

(f) Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi za *RAS* katika mikoa yote, zifuatilie na kubainisha mashauri yote yaliyopo TAKUKURU yanayohusishwa na fedha zilizokusanywa kwa kutumia mashine za *POS* ambazo hazikuwasilishwa benki na kuhakikisha kiasi cha shilingi bilioni 6.17 kilichokusanywa kwa *POS* kinawasilishwa benki kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi usioridhisha katika matumizi ya fedha za umma pamoja na akaunti ya amana. Bunge linaazimia kwamba:

(a) Serikali ihakikishe halmashauri zote hazifanyi malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroniki kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438;

(b) Serikali ihakikishe halmashauri ambazo zilitumia jumla ya shilingi bilioni 5.16 katika shughuli ambazo hazikukusudiwa zirejeshe fedha hizo katika akaunti ya amana kabla ya tarehe 30 Juni, 2025;

(c) Serikali ihakikishe halmashauri ambazo zilitumia shilingi bilioni 1.95 zaidi ya kiasi kilichowekwa katika akaunti za amana kurejesha kiasi hicho cha fedha kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya halmashauri kutolipwa kwa wakati Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali (Wizara ya Fedha) ilipe madeni yote ya watumishi na wazabuni yaliyohojiwa na *CAG* kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2023;

(b) Serikali ihakikishe halmashauri 47 ambazo zinadaiwa kiasi cha shilingi milioni 21.85 kinachotokana na mikopo ya KKK zinarejesha fedha hizo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili na halmashauri nyingine ziweze kupata fursa husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya rasilimali watu na mishahara, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ilipe malimbikizo ya mishahara ya watumishi yenye jumla ya shilingi bilioni 11.4; na

(b) Serikali iwasilishe katika mfuko ama Taasisi za *PSSSF, NHIF,* Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na taasisi nyingine, jumla ya deni la shilingi bilioni 4.013. Vile vile, Serikali iangalie upya utaratibu unaotumiwa na mfuko katika kutoza adhabu za ucheleweshaji ili kuweza ku-*clear* hii hoja ya adhabu ya shilingi bilioni 32.07.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, ninatambua tumefanya marekebisho ya sheria inayohusiana na huu mfuko, basi tukafanye kazi hii ili kuweza kutoa hizi fedha ambazo ni adhabu kubwa kupunguza ama kuzimaliza kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410 na upungufu katika usimamizi wa mikataba, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali ihakikishe halmashauri zote nchini zinazingatia kikamilifu matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 pamoja na kanuzi zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo Bunge, linaazimia kwamba:-

(b) Serikali ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha ili miradi ambayo haijakamilika yenye thamani ya shilingi bilioni 206.89 inakamilika ili thamani ya fedha ya miradi hiyo iweze kupatikana;

(c) Serikali iondoe dosari zote zilizoainishwa na CAG kwa miradi ambayo imekamilika lakini haijaanza kutumika ili miradi hiyo ianze kutumika; *(Makofi)*

(d) Serikali itoe mwongozo utakaoweka sharti la lazima kuhusu upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo kutoka katika mapato ya ndani pamoja na namna fedha hizo zinavyopaswa kutumika, kufanya ufuatiliaji na kuchukua hatua za kinidhamu pale ambapo miongozo husika inakiukwa. Aidha, fedha zote kutoka mapato ya ndani ambazo hazijapelekwa katika miradi ya maendeleo zipelekwe kabla ya tarahe 30 Juni, 2026.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto za uendeshaji wa mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe Halmashauri zote ambazo hazikuchangia 10% ya mapato ya ndani katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, wanachangia kabla ya kufikia mwezi Juni, 2026;

(b) Kufikia tarehe 30 Juni, 2026, Serikali ihakikishe mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambayo haijarejeshwa yenye thamani ya shilingi milioni 79.76 iwe imekusanywa;

(c) Serikali iendelee kufanya maboresho ya kanuni mpya za utoaji, na hizi mpya ziboreshwe ili wakati ikianza kutoa mikopo vile vile ianze na halmashauri chache.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto katika usimamizi wa mifumo ya kielektroniki Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe Halmashauri zote nchini zinakuwa na wataalamu wa *ICT* wa kutosha na wenye weledi, kuhakikisha mifumo yote inayotumika katika ngazi ya Halmashauri inasomana na kunakuwa na maboresho ya mara kwa mara ya mifumo ili kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma;

(b) Serikali ihakikishe halmashauri zinatenga bajeti ya kutosha ili vituo vyote vya kutolea huduma za afya vifungwe mfumo wa *GOT-HOMIS; (Makofi)*

(c) Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI itenge bajeti ya kutosha ya usimamizi wa mifumo ya kielektroniki inayotumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya uwekezaji wa halmashauri katika Benki ya *DCB* Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ihakikishe mabadiliko ya sheria yanafanyika ili Benki ya Jamii ya Dar es Salaam iondoke kutoka kuwa benki binafsi na iweze kuwa katika orodha ya mashirika

yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina kwa kuwa Serikali kupitia taasisi zake ina umiliki wa hisa kwa 63%;

(b) Serikali ihakikishe taarifa za Benki ya Jamii *(DCB)* ziwe zinawasilishwa kwa *CAG* kwa ajili ya ukaguzi kwa kuwa Serikali ni mwanahisa mkubwa katika benki hiyo;

(c) Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya ufanisi na utendaji wa benki husika na kuona iwapo kuna tija ya taasisi zake kuendelea kuwekeza katika benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyotolewa na taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa. Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa na *CAG* katika taarifa ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa niaba ya Kamati, tunapenda sana kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri ambapo umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ueledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati. Wajumbe hawa majina yao yote yameainishwa, ninaomba yaingie kwenye *Hansard*. Ninaomba niwashukuru kwa niaba yako kwa kufanya kazi kwa bidii, kwa kujitolea hadi saa sita usiku kwa ajili ya kulitumikia Taifa hili. Ahsanteni sana Wajumbe wa Kamati kwa uwajibikaji wenu lakini kubwa zaidi kwa weledi wenu na kuweza kukimbizana na vishawishi vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka Leonard kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na wasaidizi wake wote, Makatibu wetu wa Kamati ambao kwa kweli

wanafanya kazi kubwa katika mazingira magumu, lakini bila kulalamika na kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, tunatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa tunaopata kwa Ofisi ya *CAG* na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndg. Charles Kichere, tunakushukuru sana na timu yako. Zaidi pia tunapenda kuishukuru Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha, kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitupatia kwenye Kamati na kwenye vikao vyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninawashukuru Wabunge wote na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

***(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (16) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)***

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 na kuliomba Bunge liipokee na kuijadili. Madhumuni ya Taarifa hii ni kulijulisha Bunge lako tukufu, iwapo matumizi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yamezingatia Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya nchi na kuleta manufaa na tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya fedha za umma, Taarifa hii inafafanua Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2023 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Uchambuzi umejikita katika kubainisha dosari zilizopo katika matumizi ya fedha za umma ikijumuisha ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayopaswa kufuatwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, sharti la muundo wa Taarifa ya Kamati inayowasilishwa Bungeni limewekwa katika Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 ambapo, Taarifa inatakiwa kuwa na sehemu kuu tatu zikihitimishwa na sehemu ya nne yenye shukrani na utoaji wa hoja. Kwa muktadha wa ufuatilijia wa Taarifa hii, sehemu ya kwanza ni maelezo ya jumla ikijumuisha muundo wa Taarifa, majukumu ya Kamati, msingi wa kazi za Kamati, muhtasari wa matokeo ya uchambuzi wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa na matokeo ya uchambuzi huo unaoonesha matumizi mabaya ya fedha za umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 umefanunuliwa katika sehemu ya Pili ya Taarifa hii ambayo inajenga msingi wa sehemu ya Tatu inayohusu Maoni na Mapendekezo

### 1.3 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 kinafafanua majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za

Mitaa. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, majukumu ya Kamati ni yafuatayo: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba, tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Umma linapungua.

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 1.4 Njia zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 inaitaka sehemu ya utangulizi kuonesha mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na njia au mbinu zilizotumika na Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Ili kukidhi matakwa ya Kanuni hii, naomba kutaja njia na mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati na kukamilisha Taarifa hii kama ifuatavyo: -

a) Mapitio ya jumla ya Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Lengo lilikuwa ni kubaini maeneo yenye

matatizo katika mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha husika na iwapo kama kuna ukiukwaji wa Sheria na Kanuni;

b) Kupokea Taarifa fupi za CAG (*Briefs*) ambazo zinaonesha utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati, Hoja za ukaguzi na Mapendekezo ya CAG kuhusu Hesabu za Halmashauri husika. Taarifa hizi huwaweka Wajumbe katika nafasi nzuri ya kuzielewa hoja kwa undani wake na kubaini maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma ili kuweza kuishauri na kuisimamia Serikali ipasavyo;

c) Mahojiano na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhusu hoja zilizobainishwa katika Ripoti ya CAG ili kubaini chimbuko la dosari pamoja na athari iliyotokana na matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma; na

d) Uchambuzi wa kina wa Taarifa za wakaguzi, majibu ya Wakurugenzi wa Halmashauri iliyokaguliwa pamoja na mashauriano na Wadau wengine kuhusu hoja za Ukaguzi zilizojitokeza. Lengo ni kuelewa kwa kina msingi wa hoja na namna ya kupunguza matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia njia na mbinu hizo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kufanya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri kwa lengo la kulishauri Bunge hatua za kuchukua ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma. Katika kukamilisha kazi hiyo, Kamati ilifanya rejea ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali kama ifuatavyo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;

b) Sheria ya Ukaguzi wa Umma (Sura ya 418) na Kanuni zake za Mwaka 2009;

c) Sheria ya Fedha za Halmashauri (Sura ya 290) na Mwongozo wa Matumizi ya fedha katika Serikali za Mitaa (*the Local Government Financial Memoranda*);

d) Sheria ya Ununuzi wa Umma (Sura ya 410) na Kanuni zake, (kama zilivyo boreshwa mwaka 2016);

e) Sheria ya Bajeti (Sura ya 439) na Kanuni zake, 2015;

f) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki ya Bunge, Sura 296;

g) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023; na

h) Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.

**1.5 Muhtasari wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa ajili ya kukidhi matakwa ya Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, tarehe 15 Aprili, 2024 Serikali iliweka mezani Ripoti mbalimbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Miongoni mwa Ripoti hizo ilikuwa ni Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Takwa hilo la Kikatiba limetimizwa baada ya CAG kukamilisha majukumu yake yaliyoainishwa katika Ibara ya 143 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambapo, kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi na kutoa ripoti katika jumla ya Mamlaka 184 za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Ripoti ya CAG kuwasilishwa Bungeni, Ripoti hiyo hujadiliwa na kuwasilishwa Bungeni na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa niaba ya Bunge kama ilivyoainishwa katika Kanuni ya 43 (1) & (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

Katika kuhakikisha Bunge linafuatilia nidhamu ya mapato na matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwamba, kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha za Umma, Kamati iliweza kujadili na kuchambua Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa na kufanya mahojiano na Wakurugenzi wa **Halmashauri 55** ambazo ni sawa na **Asilimia 29.89** ya Halmashauri zote 184 ambazo Hesabu zake zimekaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa kina wa hoja zilizochambuliwa na Kamati umefafanuliwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

### 1.6 Ufuatiliaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha shughuli za kila siku za Halmashauri zote nchini zinakuwa ni zenye ufanisi na kunakuwa na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya Serikali, Kamati imekuwa ikitoa ushauri na mapendekezo kwa kila Afisa Masuuli anayefika katika Kamati kwa ajili ya mahojiano. Aidha, Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa kila Halmashauri baada ya kuhakikiwa na CAG kupitia '*briefs*' za CAG ikiwa ni matakwa ya Kifungu cha 14 (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA RIPOTI KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### 2.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lako Tukufu kwa niaba ya wananchi, limepewa madaraka ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kama ilivyotamkwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kamati ya LAAC kwa niaba ya Bunge lako, inatekeleza madaraka hayo ya kikatiba ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika eneo la matumizi ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ili kuhakikisha kunakuwa na mnyororo thabiti wa uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma, Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imempa CAG ambaye ndiye jicho la Bunge mamlaka ya kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika Katiba na baadae kuwasilisha ripoti yake Bungeni ili iweze kufanyiwa kazi na kupata Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kujiridhisha iwapo rasilimali za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetumika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Nchi na mapendekezo yaliyotolewa na CAG yanashughulikiwa kikamilifu, Kamati ilichambua Ripoti Kuu ya Mwaka ya CAG kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Baada ya uchambuzi huo na kwa kutumia Kanuni ya 109 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 ukaelekeza Taarifa hii ipangwe kwenye Orodha ya Shughuli za leo.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu uchambuzi wa Ripoti ya CAG ambao ndio msingi wa mapendekezo ya Kamati yanayowasilishwa kwa njia ya Hoja kama ilivyoelekezwa na Kanuni ya 61 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

## 2.2 Vigezo vya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ripoti ya CAG inajumuisha hoja na mapendekezo ya Halmashauri zote zilizokaguliwa katika mwaka husika. Ili Kamati iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi katika kubaini matumizi mabaya ya rasilimali za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, vigezo muhimu hutumika katika kufanya uchambuzi wa Ripoti ya CAG.

Vigezo vilivyowekwa na Kamati vilitumika katika kutoa mwongozo wa Halmashauri ambazo zilipewa kipaumbele katika uchambuzi wa Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa (*individual financial statements*) na Maafisa Masuuli (Wakurugenzi) wa Halmashauri hizo walifika mbele ya Kamati kwa ajili ya mahojiano.

**Mheshimiwa Spika**, ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Kamati, vigezo vilivyozingatiwa wakati wa uchambuzi wa Ripoti ya CAG ni kama ifuatavyo: -

a. Uzito wa hoja ya ukaguzi kama ilivyoibuliwa na CAG;

b. Maslahi ya Umma kuhusu hoja za Halmashauri husika;

c. Hali ya hati ya ukaguzi iliyotolewa kwa Halmashauri husika;

d. Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika katika Halmashauri au Mradi wa Maendeleo uliokaguliwa;

e. Kiwango cha fedha kinachohusika katika hoja za ukaguzi wa Halmashauri husika; na

f. Kuleta uendelevu wa ufuatiliaji wa ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwa Halmashauri husika kwa siku za nyuma.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa kutumia vigezo hivyo kuliiwezesha Kamati kufikia malengo yake ya kubainisha maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Umma na hatimaye kutoa mapendekezo stahiki.

**2.3 Matokeo ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, CAG alifanya ukaguzi katika Jumla ya Halmashauri 184 ambapo katika kaguzi hizo, hati **184** zilitolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya hizo, Halmashauri **181** sawa na **98.37%** zilipata Hati zinazoridhisha za ukaguzi na Halmashauri **3** sawa na **1.63%** zilipata Hati zenye Shaka za ukaguzi. Katika mwaka huu wa fedha uliokaguliwa, hapakuwa na Halmashauri iliyopata Hati Mbaya ya ukaguzi. Orodha ya Hati hizo ni **kiambatisho namba 1** cha Taarifa hii.

Kwa muktadha wa ufuatiliaji, Kamati ilifanya uchambuzi wa jumla wa Ripoti ya CAG na kubaini kuwa, idadi ya Halmashauri zilizopata Hati zinazoridhisha imeongezeka kutoka Halmashauri **170** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi kufikia Halmashauri **181** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Aidha, Kwa upande wa Hati zenye shaka, idadi ya Halmashauri imepungua kutoka Halmashauri **13** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi kufikia Halmashauri **3** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati katika Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka

wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023, maeneo kadhaa yenye matumizi mabaya ya fedha za umma yalibainika ambayo ni pamoja na kukosekana kwa mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410, matumizi yasiyo sahihi ya Akaunti ya Amana, usimamizi usioridhisha wa mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kukosekana kwa usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na mikakati isiyoridhisha ya ulipaji wa madeni ya Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo ya utangulizi ya sehemu hii ya pili, mambo yafuatayo kuhusu matumizi na usimamizi wa fedha za umma katika Halmashauri yalibainika: -

### 2.3.1 Kukosekana kwa Mikakati Madhubuti ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikifanya uchambuzi wa kina juu ya uwezo wa Halmashauri kukusanya mapato ya ndani ili kuweza kupunguza mzigo wa Serikali wa kuzihudumia Halmashauri zote. Serikali imekuwa ikipeleka katika Halmashauri zote fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, mishahara pamoja na fedha za matumizi mengineyo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Halmashauri za kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilipeleka OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ruzuku ya jumla ya **Shilingi 7,606,495,440,872.00** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,400,603,575,489** zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na **Shilingi 5,205,891,865,383.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara. Aidha, Halmashauri 184 ziliweza kukusanya jumla ya **Shilingi 912,123,865,087.00** zaidi ya makadirio yaliyowekwa ya **Shilingi 911,863,338,485,00**.
Licha ya takwimu za jumla za makusanyo ya mapato ya ndani kuzidi makadirio yaliyowekwa, utafiti wa Kamati umebaini kuwa, iwapo

juhudi za makusudi zitachukuliwa katika kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na Serikali kuziruhusu Halmashauri zenye uwezo mkubwa kuongeza bajeti ya makadirio ya makusanyo, ukusanyaji wa mapato utaongezeka na kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri 55 zilizofika mbele ya Kamati kwa ajili ya mahojiano katika kipindi cha Mwezi Agosti na Oktoba, 2024, kwa ajili ya Hesabu zilizokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali ilipeleka jumla ya **Shilingi 639,419,162,047.46** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, **Shilingi 1,401,381,488,777.44** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 79,273,684,838.75** Kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Halmashauri hizo. Aidha, kwa upande wa makusanyo ya ndani, Halmashauri hizo 55 ziliweza kukusanya jumla ya **Shilingi 404,416,415,198.66.** Mchanganuo wa upokeaji wa ruzuku ya Serikali ikilinganishwana na ukusanyaji wa mapato ya ndani ni **kiambatisho namba 2** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kiasi kikubwa cha fedha kupelekwa katika Halmashauri hizo, baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kuwa na ubunifu wa vyanzo vya uhakika wa mapato pamoja na kukosekana kwa mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kushindwa kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kutoka katika vyanzo vilivyopo.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine iliyopelekea Halmashauri nyingi kutofikia malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani ni kukosekana kwa taarifa sahihi za mauzo ghafi ya wafanyabiashara wakubwa waliopo katika Halmashauri hizo hivyo kupelekea kukusanywa kwa kiasi kidogo cha mapato ikilinganishwa na ukubwa wa biashara zinazofanyika katika maeneo yao.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri zilizoshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa zaidi ya **Asilimia Kumi** ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 1.

**Jedwali Na. 1** Orodha ya Halmashauri ambazo hazijafikia malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani

| Jina la Halmashauri | Bajeti iliyoidhinishwa | Makusanyo Halisi | Pungufu | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Biharamulo DC | 3,511,584,000.00 | 2,267,211,793.00 | 1,244,372,207.00 | 35 |
| Tandahimba DC | 5,558,727,900.00 | 3,850,286,328.00 | 1,708,441,572.00 | 31 |
| Mtwara Mikindani MC | 5,445,000,000.00 | 3,864,829,378.00 | 1,580,170,622.00 | 29 |
| Nanyamba TC | 2,225,881,100.00 | 1,697,773,094.00 | 558,108,006.00 | 25 |
| Handeni DC | 2,562,133,980.00 | 2,057,819,165.00 | 504,314,815.00 | 20 |
| Newala TC | 2,675,619,000.00 | 2,201,985,483.00 | 473,633,517.00 | 18 |
| Kigoma/Ujiji MC | 3,300,000,000.00 | 2,812,960,519.00 | 487,039,481.00 | 15 |
| Lushoto DC | 2,789,733,000.00 | 2,375,667,024.00 | 404,065,976.00 | 15 |
| Longido DC | 2,949,771,009.00 | 2,591,266,968.00 | 358,504,041.00 | 14 |
| Kilolo DC | 4,750,338,415.00 | 4,183,436,710.00 | 566,901,705.00 | 12 |

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na kwamba Halmashauri zote zinakuwa na uwezo wa kujiendesha bila ya kutegemea kiasi kikubwa cha fedha kutoka Serikali kuu, Kamati imekuwa ikizielekeza Halmashauri zote zinazofika kwa ajili ya mahojiano kufanya tathmini ya kina ya vyanzo vyote vya mapato vilivyopo katika Halmashauri zao. Lengo likiwa ni kubaini ufanisi wa vyanzo hivyo, kuangalia fursa mbalimbali za biashara zilizopo katika Halmashauri ili kufahamu vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuandaa mkakati unaotekelezeka wa ukusanyaji wa mapato wa muda mfupi, wa kati na mrefu.

Changamoto nyingine zilizobainika wakati wa uchambuzi wa hoja ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ni kama ifuatavyo: -

### 2.3.1.1 Mapato yasiyokusanywa kutoka katika vyanzo muhimu Shilingi Bilioni 61.15

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zote zimekua zikipitisha Sheria ndogo ambazo zimekuwa zikiainisha vyanzo mbalimbali vya mapato vitakavyokusanywa katika maeneo yao ya usimamizi. Vyanzo hivyo vya mapato ni pamoja na uuzaji wa viwanja, leseni za biashara, kodi za kukodisha maduka yaliyo katika stendi za mabasi na masoko ya Halmashauri, leseni za vileo, ukodishaji wa vibanda na vizimba vya soko, kodi za nyumba, ada za uzoaji taka, kodi za upangishaji wa maeneo ya wazi yaliyokodishwa, na ada za maegesho na vyanzo vingine vya mapato kwa kutaja baadhi.

**Mheshimiwa Spika**, kila Mkurugenzi wa Halmashauri anapaswa kuwajibika kwa usimamizi wa ujumla wa mapato, matumizi, mali pamoja na madeni ya Halmashauri anayoiongoza. Kinyume na Agizo Na. 7 (d) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009, baadhi ya Hamashauri hazikukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 61.15** kama inavyoonekana katika Jedwali namba 2.

**Jedwali Na. 2** Orodha ya vyanzo vya mapato visivyokusanywa

| s/n | Chanzo cha Mapato | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mauzo ya Viwanja | 23 | 42,536,221,960.00 |
| 2. | Kodi ya pango | 43 | 7,482,506,132.00 |
| 3. | Mapato mengine | 22 | 6,317,825,455.00 |
| 4. | Maeneo ya wazi | 4 | 1,529,690,473.00 |
| 5. | Ada ya maegesho | 9 | 1,036,929,558.00 |
| 6. | Leseni za biashara | 14 | 855,806,998.00 |
| 7. | Ada za ukusanyaji taka | 5 | 803,106,330.00 |
| 8. | Leseni za vileo | 3 | 346,768,998.00 |
| 9. | Ada za uchimbaji madini | 7 | 242,976,855.00 |
| **Jumla** | | **130** | **61,151,832,760.00** |

*Chanzo: Uk: 58 wa Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2022-23*

**Mheshimiwa Spika**, kushindwa kukusanywa kwa kiasi hicho cha fedha, kunakwamisha juhudi za Serikali za kuimarisha ustawi wa wananchi. Halmashauri zote nchini zinatakiwa kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Serikali kwa kuhakikisha mifumo ya udhibiti wa ndani inaimarika na fedha yote iliyopaswa kukusanywa kwa mujibu wa Sheria inakusanywa ndani ya muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikiangalia uwezo wa kila Halmashauri wa kukusanya fedha zake kutoka kwa wadaiwa mbalimbali na kubaini baadhi ya Halmashauri kutokusanya fedha zake kwa zaidi ya mwaka mmoja. Kukosekana kwa fedha hizo kunapunguza ukwasi wa Halmashauri hizo ambapo, fedha hizo zingeweza kutumika katika shughuli mbalimbali. Baadhi ya Halmashauri ambazo hazikuweza kukusanya madai yake ni Jedwali namba 3.

**Jedwali Namba. 3** Halmashauri ambazo hazikukusanya madai yake (Receivables)

| Jina la Halmashauri | Chanzo cha mapato | Kiasi ambacho hakijakusanywa |
|---|---|---|
| Msalala DC | Ushuru wa vyanzo mbalimbali vya mapato | 3,651,891,754.00 |
| Bariadi TC | Madai kutokana na mauzo ya viwanja ambayo hayajakusanywa | 1,369,728,997.00 |
| Sumbawanga DC | Wadaiwa mbalimbali | 901,776,000.00 |
| Mtwara DC | Mauzo ya viwanja ambayo hayajakusanywa na madeni ya Vyama vya Msingi | 806,827,748.00 |
| Itilima Dc | Madeni ya Pamba | 544,529,720.00 |
| Chalinze DC | Ushuru wa huduma (Service Levy) na mauzo ya viwanja | 525,966,140.60 |
| Handeni DC | Madai mbalimbali (ada, faini na adhabu) | 513,890,958.00 |

| | | |
|---|---|---|
| Shinyanga DC | Tozo mbalimbali na faini | 486,787,703.00 |
| Kilolo DC | Ushuru wa mazao ya misitu kutoka Kampuni ya New Forest | 386,450,684.00 |
| Mpwapwa DC | Tozo (wakala wa ukusanyaji mapato) | 263,408,471.00 |
| Mkuranga DC | Ushuru wa Huduma | 174,782,861.00 |

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe imeshindwa kukusanywa mapato yanayotokana na ushuru Jumla ya **Shilingi 6,027,653,000** kutoka katika Kampuni ya Yapi Merkez iliyokuwa inajenga reli ya Kisasa ya SGR ambapo deni hilo ni la tangu mwaka 2021. Kutokukusanywa kwa ushuru huo kwa wakati kunapunguza mapato ya Halmashauri husika.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kukutana na Halmashauri za Mkoa wa pwani, changamoto kubwa iliyobainishwa na Wakurugenzi wa Halmashauri hizo ni suala la viwanda vinavyofanya uwekezaji katika Mkoa wa Pwani kutoa Ushuru wa huduma (service levy) katika Mkoa wa Dar es salaam hali inayopunguza mapato ya Halmashauri za Mkoa wa Pwani. Ni vema wawekezaji na wafanyabiashara wawe wanalipa ushuru wa huduma katika Halmashauri ambazo biashara zao zinatekelezwa.

### 2.3.1.2 Kukosekana kwa ufanisi katika ukadiriaji na ukusanyaji wa Ushuru wa Huduma Shilingi Bilioni 4.18

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi na Makampuni mbalimbali yamekuwa yakifanya uwekezaji pamoja na kufanya biashara katika maeneo mbalimbali nchini. Maeneo ambayo biashara hizo zimekuwa zikifanyika yapo katika usimamizi wa Halmashauri mbalimbali. Kwa taasisi, kampuni au mtu ambaye mauzo yake ghafi kwa mwaka yanazidi **Shilingi Milioni Nne**, Halmashauri inatakiwa kutoza kiwango kisichozidi **Asilimia 0.3** ya mauzo ghafi baada ya kupunguza kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa.

Kinyume na matakwa ya Vifungu vya 6(1) (u) na 7(1) (y) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kama ilivyorekebishwa na Kifungu cha 44 na 45 cha Sheria ya Fedha, Sura ya 348, Kamati imebaini uwepo wa Halmashauri 37 ambazo zilishindwa kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 4.18** zinazotokana na ushuru wa huduma kutoka kwa wafanyabiashara ambao wapo katika maeneo yao kutokana na kukosekana kwa kanzi data iliyohuishwa hivyo kuzikosesha fedha Halmashauri hizo

**Mheshimiwa Spika**, ili kuondoa changamoto iliyoainishwa hapo juu, Kamati imekuwa ikizitaka Halmashauri zote nchini, kuhuisha kanzi data ya walipa kodi ili kupata taarifa sahihi na idadi kamili ya wafanyabiashara wanaostahili kulipa ushuru wa huduma. Kwa kufanya hivyo, kutaziwezesha Halmashauri kukusanya fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kila siku za Halmashauri pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mfano wa Halmashauri zilizobainika kukutwa na changamoto hiyo ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

#### 2.3.1.3 Halmashauri kukusanya Ushuru wa huduma bila ya ripoti za mauzo ghafi Shilingi Bilioni 8.15

**Mheshimiwa Spika**, taratibu za ukusanyaji wa ushuru wa huduma kama zilivyoelezewa katika Aya ya 6.6.1(iii & iv) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 zinamtaka mtoza kodi kutoa fomu ya kukiri jumla ya mauzo ghafi ambayo hujazwa na mlipakodi. Lengo la sharti hili ni kujiridhisha juu ya usahihi wa mauzo ghafi na kiwango cha kodi kitakachotozwa ili Halmashauri ziweze kukusanya stahiki zao kwa mujibu wa Sheria.

Kutokana na kutokuzingatiwa kwa aya hiyo, baadhi ya Halmashauri zimekusanya ushuru wa huduma bila ya uthibitisho wa mauzo halisi ya wafanyabiashara. Kutokuwepo kwa uthibitisho wa mauzo ghafi, kunaziweka Halmashauri katika hatari ya kupoteza mapato kwa

kukusanya kiasi kidogo cha fedha kutoka katika ushuru wa huduma ikilinganishwa na kiwango cha mauzo halisi.

**Mheshimiwa Spika**, Wakurugenzi waliofika mbele ya Kamati wameeleza kuwa, wamekuwa wakipatiwa taarifa ya kiasi cha ushuru wa huduma kinachotakiwa kulipwa na wafanyabiashara kutoka katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Hata hivyo, kiasi hicho kinachokusanywa hakiendani na ukubwa wa biashara zinazofanyika katika maeneo hayo. Changamoto hii kwa kiasi kikubwa imebainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

### 2.3.1.4 Mawakala wa Ukusanyaji Mapato kutowasilisha Shilingi Bilioni 5.65

**Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato, Halmashauri zimekuwa zikiingia mkataba na Mawakala wa ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri 12 ziliingia jumla ya mikataba 53 ya ukusanyaji wa mapato ambapo, kwa mujibu wa mikataba hiyo, jumla ya **Shilingi Bilioni 14.43** zilitakiwa kukusanywa na mawakala hao na kulipwa kwa Halmashauri husika.

Kinyume na matakwa ya kifungu cha 26 (a) na (b) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kiasi cha **Shilingi Bilioni 8.89** pekee ndicho kichopokelewa na Halmashauri husika na kubakiwa na deni la **Shilingi Bilioni 5.65** ambayo ni sawa na **Asilimia 39** ambacho hakijawasilishwa kwa mujibu wa mikataba husika.

**Mheshimiwa Spika**, kutochukuliwa kwa hatua stahiki kwa mawakala waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri kunapunguza uwezo wa Halmashauri hizo kujiendesha ikiwa ni pamoja na kushindwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kamati inaweka msisitizo kwa Serikali kuchukua hatua stahiki kwa mawakala ambao hawajakidhi matakwa ya mikataba yao.

### 2.3.1.5 Kutokusuluhishwa kwa madai katika Mfumo wa LGRCIS yanayoweza kusababisha hasara ya Shilingi Bilioni 45.02

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikifanya maboresho ya mifumo mbalimbali ya kielektroniki ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika juhudi za kudhibiti upotevu wa fedha za umma, Halmashauri zote zilitakiwa kusitisha shughuli zote za ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa LGRCIS na kuanza kutumia mfumo wa TAUSI ifikapo tarehe 31 Machi 2023.

Katika mchakato wa mabadiliko hayo ya mifumo, OR – TAMISEMI ilizielekeza Halmashauri zote nchini kufanya usuluhishi wa madai (receivables) ili kupata taarifa zilizo sahihi za makusanyao. Wajibu wa kila Halmashauri ni kuainisha wadaiwa (defaulters) halali ili fedha za Halmashauri ziweze kukusanywa. Aidha, kwa upande wa wadaiwa (defaulters) wasio halali, Halmashauri inatakiwa kufuata taratibu za kisheria na kuomba kibali OR – TAMISEMI waweze kufunguliwa na kufanya marekebisho katika mfumo.

Pamoja na hatua zinazotakiwa kufuatwa kujulikana na Halmashauri zote, bado kuna **Halmashauri 125** ambazo katika ukaguzi wa Mfumo wa LGRCIS, CAG amebaini Halmashauri hizo kushindwa kukusanya na kutofanya usuluhishi wa jumla ya **Shilingi Bilioni 45.02**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa, Taarifa zilizopo katika mfumo wa awali wa LGRCIS zimekuwa haziwezi kuhamishika kwenda katika mfumo mpya wa TAUSI hali inayoashiria upotevu wa mapato ya Halmashauri. Halmashauri ambazo zimefika mbele ya Kamati na zimebainika kutofanya usuluhishi wa mfumo wa LGRCIS zimeainishwa katika Jedwali namba 4.

**Jedwali Na. 4** Halmashauri ambazo hazikufanya usuluhishi katika Mfumo wa LGRCIS

| s/n | Jina la Halmashauri | Kiasi ambacho hakijasuluhishwa |
|---|---|---|
| 1. | Msalala DC | 2,622,365,529.00 |
| 2. | Bukoba MC | 1,528,219,586.00 |
| 3. | Biharamulo DC | 304,326,504.00 |
| 4. | Iringa DC | 117,928,091.00 |

**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa taarifa sahihi za makusanyo ya mapato kunakotokana na kutofanyika kwa usuluhishi, kunaweza kusababisha hasara na upotevu wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa husika. Kamati inawasisitiza Wakurugenzi wote wa Halmashauri kuhakikisha wanafanya usuluhishi wa madai yote ili kujua wadaiwa halali wa Halmashauri pamoja na ufuatiliaji wa karibu ili madai yote yakusanywe haraka iwezekanavyo pamoja na kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya mfumo wa TAUSI.

#### 2.3.1.6 Mapato yaliyokusanywa kwa kutumia POS kutowasilishwa benki Shilingi Bilioni 6.17

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako Tukufu limekwisha azimia juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa wakusanya mapato wanaohusika na kukusanya mapato ya Halmashauri bila ya kuziwasilisha fedha hizo benki ambapo, katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya **Shilingi Bilioni 11.07** zilikusanywa bila ya kuwasilishwa benki.

Pamoja na juhudi zilizochukuliwa na Serikali za kuhakikisha fedha zote zilizokusanywa zinawasilishwa benki na kwamba, hoja hiyo haijirudii, bado kuwa baadhi ya Halmashauri ambazo, waliopewa dhamana ya kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri wamekusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 6.17** pasipo kuziwasilisha katika Akaunti za benki za Halmashauri husika.

Halmashauri zenye hoja hii zimekuwa zikiieleza Kamati kuwa, hatua zilizochukuliwa kwa wakusanya mapato ambao hawajawasilisha fedha hizo benki ni kuwapeleka TAKUKURU sababu ambayo Kamati imekuwa ikiikataa kwakuwa, kukusanya fedha za Halmashauri na kutoziwasilisha benki hakuhusiani na shughuli za Rushwa. Kwakuwa ushahidi wa wahusika kukusanya fedha hizo upo wakiwemo watumishi wa Halmashauri husika, Kamati inashauri Halmashauri kufata taratibu za kisheria ili fedha hizo ziweze kurejeshwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa Halmashauri ambazo kwa kiasi kikubwa mapato yake hayakuwasilishwa benki na wakusanya mapato ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya Momba **Shilingi 470,790,962**, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/ujiji **Shilingi 282,904,421** na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala **Shilingi 113,595,189**.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa kiasi cha hoja ya kutowasilishwa kwa fedha zilizokusanywa kutopelekwa benki kupungua kutoka **Bilioni 11.07** mwaka 2021/22 hadi **Bilioni 6.17** mwaka 2022/23, kila Mkurugenzi ana wajibu wa kuhakikisha kuwa hakuna upotevu wa mapato katika Halmashauri yake. Kuendelea kuwepo kwa hoja hiyo ni kiashiria cha kukosekana kwa usimamizi na ufuatiliaji wa mapato ya Halmashauri.

### 2.3.1.7 Usimamizi Usioridhisha katika Matumizi ya Fedha za Umma pamoja na Akaunti ya Amana

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 14 (a) imeipa Kamati jukumu la kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ili kutekeleza kikamilifu jukumu hilo, Kamati imejikita katika kuangalia ufanisi katika matumizi na utendaji wa Halmashauri ili kuhakikisha kunakuwa na nidhamu ya matumizi ya Fedha za Serikali za Mitaa

kwa ujumla wake. Vile vile, Kamati imekuwa ikiangalia ufanisi katika usimamizi wa Akaunti ya Amana.

**Mheshimiwa Spika**, Akaunti ya Amana ni akaunti inayomilikiwa na Halmashauri zote nchini ambapo, kazi ya msingi ya akaunti ya amana ni kutunza fedha za walioweka amana ili zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Kwa muktadha huo, matumizi ya fedha zilizopo katika akaunti hiyo yanapaswa kuendana na lengo kuu la amana hizo kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001.

Changamoto zilizobainika na Kamati katika matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa pamoja na usimamizi wa Akaunti za Amana ni kama ifuatavyo: -

### 2.3.1.8 Malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroniki Shilingi Bilioni 7.42

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikiendelea kufanya uwekezaji katika mifumo ya kielektroniki ili kudhibiti upotevu wa fedha za Umma katika ukusanyaji wa mapato na utumiaji wa fedha hizo. Pamoja na juhudi zilizochukuliwa, bado kuna Halmashauri ambazo zimefanya malipo kwa wazabuni na watoa huduma mbalimbali bila ya kudai stakabadhi/risiti za kielektroniki kinyume na Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438 [iliyorekebishwa mwaka 2019] kinachomtaka mtu ambaye anasambaza bidhaa, anatoa huduma au anayepokea malipo kuhusiana na usambazaji wa bidhaa au huduma aliyotoa, kutoa stakabadhi au ankara kwa kutumia mashine za kielekitroniki. Halmashauri kushindwa kudai risiti za kielektroniki kunazuia ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuhamasisha ukwepaji wa kodi kwa watoa huduma.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2023, jumla ya Halmashauri 64 zilifanya malipo bila ya kudai stakabadhi za kielektroniki zenye jumla ya **Shilingi Bilioni 7.42**. Katika Halmashauri

ambazo zilikiri mbele ya Kamati kufanya malipo bila ya kudai risi za kielektroniki ni pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji **Shilingi 123,543,942.49**. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Singida ilipokea stakabadhi bandia za kielektroniki zenye thamani ya **Shilingi Milioni 147.29** kinyume na Kifungu tajwa hapo juu.

### 2.3.1.9 Malipo yaliyofanyika kwa fedha taslimu Shilingi Bilioni 1.44

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikisisitiza Halmashauri zote nchini juu ya matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ili kuzuia matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kuhakikisha malipo yote yanafanyika kwa kutumia mifumo badala ya kutumia fedha taslimu. Pamoja na juhudi za kuhamasisha uzingatiaji wa Aya ya 6.7.3 ya Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2019, baadhi ya Halmashauri zimeendelea kukiuka utekelezaji wa takwa la Mwongozo huo kwa kufanya malipo kwa fedha taslimu hali inayoshawishi wazabuni kutolipa kodi stahiki pamoja na matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Baada ya kufanya mahojiano na baadhi ya Maafisa Masuuli wa Halmashauri mbalimbali, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilibainika kufanya malipo kwa fedha taslimu kwa kiasi cha **Shilingi 108,101,700**.

### 2.3.1.10 Malipo yaliyofanyika kutoka katika Akaunti ya Amana kwa shughuli zisizokusudiwa Shilingi Bilioni 5.16

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa matumizi ya Akaunti ya Amana kwa lengo la kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha zinazowekwa katika Akaunti hizo ambazo zinamilikiwa na Halmashauri zote nchini. Licha ya kuwa, Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 kuweka sharti la matumizi sahihi ya Fedha za Akaunti ya Amana, kuna Halmashauri ambazo zilitumia **Shilingi Bilioni 5.16** kwa shughuli ambazo hazikukusudiwa.

Pamoja na kiasi hicho cha fedha kupungua kutoka **Shilingi Bilioni 7.7** kilichoripotiwa katika Hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2022, Kamati inaendelea kuzitaka Halmashauri zote kukidhi matakwa ya sheria kwa kufanya matumizi sahihi ya fedha za amana kwa kuzingatia lengo la uwekwaji wa fedha hizo kwakuwa, matumizi ya fedha hizo kinyume na lengo kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri kutumia fedha za Akaunti ya Amana kinyume na lengo kumesababisha baadhi ya Halmashauri kuwa na salio pungufu la benki kufidia madai ya waweka Amana yenye jumla ya **Shilingi Milioni 745.23**. Hali hii isipodhibitiwa itaziweka Halmashauri katika hatari ya kufunguliwa kesi za madai. Changamoto hiyo ilibainika kwa baadhi ya Halmashauri ambapo, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilitumia jumla **Shilingi Milioni 400** kutoka Akaunti ya Amana kinyume na lengo la Amana iliyowekwa.

### 2.3.1.11 Malipo zaidi ya kiasi kilichowekwa kwenye akaunti ya Amana Shilingi Bilioni 1.95

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyofafanuliwa hapo awali kuhusu matumizi sahihi ya fedha za Akaunti ya Amana, kiasi kitakachotumika hakitakiwi kuzidi kiasi cha fedha kilichokatiwa risiti wakati wa uwekaji wa fedha hizo. Pamoja na utaratibu huo kufahamika, Halmashauri 17 zilifanya malipo zaidi ya kiasi kilichowekwa kwa **Shilingi Bilioni 1.95**. Tafsiri ya matumizi ya fedha hizo zaidi ya kiasi kilichowekwa ni kwamba, kuna shughuli ambazo hazitatekelezwa kwa wakati uliopangwa kutokana na kukosekana kwa fedha.

Pamoja na changamoto hiyo, Kamati pia imebaini uwepo wa Halmashauri 15 kufanya malipo ya **Shilingi Milioni 935** bila ya uthibitisho wa fedha kupokelewa katika akaunti ya Amana. Kuendelea kutumia fedha za akaunti za amana kwa utekelezaji wa shughuli ambazo fedha zake hazikupokelewa kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma, kuongezeka kwa mzigo

wa madai ya waweka amana kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuchafua taswira ya Halmashauri hizo. Mfano Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilitumia zaidi kwenye vifungu vya mfuko wa Amana **Shilingi 52,288,714.00**.

### 2.3.1.12 Madeni (Payables) ya Halmashauri kutolipwa kwa wakati Shilingi Bilioni 87.32

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri nyingi nchini zimekuwa na madeni mengi ya watumishi ikijumuisha likizo, kukaimu, kujikimu, safari, madeni ya wastaafu, uhamisho, posho za kisheria pamoja madeni ya wazabuni waliotoa huduma katika Halmashauri zao. Madeni hayo kutolipwa kwa wakati kunapunguza morali ya utoaji wa huduma kwa jamii.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi uliofanyika katika Halmashauri 37 ulibaini kuwa, madeni ya wazabuni na watumishi yalifikia **Shilingi Bilioni 87.32**. katika madeni hayo kwa Halmashauri 37, madeni ya wazabuni yalikuwa ni **Shilingi 38,233,201,828.00** na madeni ya watumishi yalikuwa ni **Shilingi 49,091,896,967.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa madeni ambayo Halmashauri inatakiwa kuyalipa kwa watumishi na wazabuni kwa kuzielekeza kuweka kipaumbele cha ulipaji wa madeni kulingana na umri wa madeni na kukubaliana muda wa kuyalipa ili kuepukana na kufunguliwa kesi za madai au kutozwa riba inayotokana na ucheleweshaji wa malipo. Uchambuzi wa madeni hayo ni kama ifuatavyo: -

### 2.3.1.13 Madeni ya Watumishi

**Mheshimiwa Spika**, madeni haya yamegawanyika katika makundi mawili ambapo, kundi la kwanza ni madeni yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu na kundi la Pili ni madeni yanayopaswa kulipwa na Halmashauri zenyewe.

Kwa upande wa madeni yanayopaswa kulipwa na Serikali kuu, Kamati imefanya uchambuzi wa taarifa kwa Halmashauri 55 zilizofika kwa ajili ya majadiliano na kubaini jumla ya **Shilingi 38,897,981,372.15** ambazo hazijalipwa kwa watumishi. Aidha, majibu ya Maafisa Masuuli kuhusiana na madeni hayo ni kuwa, madeni hayo yameshawasilishwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya uhakiki na ulipwaji. Orodha ya Baadhi ya Halmashauri ambazo Serikali Kuu inadaiwa kiasi kikubwa cha madeni ya watumishi ni jedwali namba 5.

**Jedwali Na. 5** Madeni ya Watumishi yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu

| s/n | Jina la Hamashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam CC | 4,226,962,219.62 |
| 2. | Temeke MC | 2,531,335,775.00 |
| 3. | Chemba DC | 2,140,398,235.00 |
| 4. | Same DC | 2,115,683,931.00 |
| 5. | Bumbuli DC | 1,755,327,798.00 |
| 6. | Mpwapwa DC | 1,570,975,357.00 |
| 7. | Masasi DC | 1,436,108,997.00 |
| 8. | Arusha DC | 1,381,160,358.00 |
| 9. | Kasulu DC | 1,248,455,330.00 |
| 10. | Kilolo DC | 1,049,702,474.00 |
| 11. | Bariadi TC | 1,043,509,808.00 |
| 12. | Busokelo DC | 1,011,521,660.00 |

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi kubwa zinazoendelea za ulipaji wa madeni hayo ambapo, Afisa kutoka Wizara ya Fedha ameieleza Kamati kuhusu taratibu zinazoendelea za ulipaji wa madeni hayo, ni vema Serikali ikaendelea kulipa stahiki hizo za watumishi ili kuongeza ufanisi na morali ya utendaji kazi kwa watumishi wake.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri nyingi nchini zinadaiwa na watumishi wake stahiki mbalimbali ambapo, madeni hayo yanapaswa kulipwa na Halmashauri husika. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kulikuwa na madeni ya watumishi yenye jumla ya **Shilingi 17,132,735,899.22** kwa Halmashauri 55 zilizofanyiwa mahojiano na Kamati. kiasi hicho cha fedha kilichokuwa hakijalipwa kwa watumishi kinahusisha madai ya wastaafu, madai ya likizo, madai ya uhamisho, posho za kujikimu, madai ya matibabu pamoja na stahiki mbalimbali. Mfano wa Halmashauri ambazo zinadaiwa kiasi kikubwa cha fedha na watumishi wake ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 6.

**Jedwali Na. 6:** Madeni ya Watumishi yanayopaswa kulipwa na Halmashauri

| s/n | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Chato DC | 2,987,454,506.00 |
| 2. | Mpwapwa DC | 1,062,962,034.00 |
| 3. | Dar es Salaam CC | 957,638,733.21 |
| 4. | Mtwara DC | 943,443,175.00 |
| 5. | Tunduru DC | 591,846,351.00 |
| 6. | Singida DC | 587,650,929.00 |
| 7. | Sumbawanga DC | 569,679,315.00 |
| 8. | Bariadi TC | 547,670,741.00 |

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa ukaguzi wake, CAG amekuwa akifanya mahojiano na baadhi ya watumishi katika Halmashauri mbalimbali nchini na kuelezwa kuhusu jitihada ndogo zinazochukuliwa na Halmashauri zao katika kuwalipa stahiki zao. Pamoja na Kamati kusisitiza ulipwaji wa madeni hayo, bado kuna haja ya Halmashauri zote kuhakikisha zinakusanya fedha za kutosha na kuwapa kipaumbele watumishi wao kwa kuwalipa madeni yao kwa wakati na kuepuka kulimbikiza madeni mapya.

### 2.3.1.14 Madeni ya Wazabuni (Watoa huduma)

**Mheshimiwa Spika**, watoa huduma mbalimbali wamekuwa wakitoa huduma katika Halmashauri pasipo kulipwa madai yao kwa wakati licha ya Halmashauri kunufaika na huduma zao. Hali hiyo inatishia ukuaji wa uchumi wa watoa huduma hao kutokana na malipo yao kucheleweshwa kwa muda mrefu.

Kama ilivyo katika madeni ya watumishi, madeni ya wazabuni pia yamegawanyika katika makundi mawili ambapo, kuna madeni yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu na ambayo yanapaswa kulipwa na Halmashauri husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa madeni ya Serikali Kuu, Uchambuzi wa Kamati kwa Halmashauri 55 zilizohojiwa umebaini kuwa, Serikali Kuu inadaiwa na wakandarasi na wazabuni jumla ya **Shilingi 14,217,003,907.25.** Baadhi ya Halmashauri ambazo Serikali Kuu inadaiwa na wazabuni ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 7.

**Jedwali Na. 7** Madeni ya wakandarasi na wazabuni yanayopaswa kulipwa na Serikali Kuu

| s/n | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Ubungo MC | 8,532,282,436.92 |
| 2. | Dar es Salaam CC | 1,536,187,978.78 |
| 3. | Chato DC | 1,253,715,329.00 |
| 4. | Kisarawe DC | 996,115,532.00 |
| 5. | Nyang'hwale DC | 530,048,000.00 |
| 6. | Mpwapwa DC | 370,980,835.50 |
| 7. | Biharamulo DC | 350,330,000.00 |
| 8. | Wanging'ombe DC | 325,576,616.00 |

**Mheshimiwa Spika**, wazabuni waliotoa huduma mbalimbali kama chakula, shajala, mafuta pia wanazidai Halmashauri kwa huduma

walizozitoa na ambazo zilipaswa kulipwa na Halmashauri hizo. Licha ya kila mwaka Halmashauri kutenga bajeti ya kugharamia huduma mbalimbali, bado kuna baadhi ya Halmashauri ambazo hazilipi madeni ya wazabuni hao kwa wakati. Kamati imebaini uwepo wa madeni ya wazabuni ambapo jumla ya **Shilingi 29,901,120,085.57** zilikuwa zinadaiwa na Halmashauri 55 zilizofika mbele ya Kamati. Mfano wa Halmashauri zinazodaiwa na wazabuni ni jedwali namba 8.

**Jedwali Na. 8** Madeni ya Wazabuni yanayopaswa kulipwa na Halmashauri

| s/n | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam CC | 9,770,131,055.52 |
| 2. | Ubungo MC | 1,524,848,626.91 |
| 3. | Kasulu DC | 1,521,632,201.00 |
| 4. | Msalala DC | 1,395,961,692.00 |
| 5. | Chalinze DC | 1,324,495,703.00 |
| 6. | Momba DC | 834,300,114.00 |
| 7. | Iringa DC | 787,702,211.00 |
| 8. | Chato DC | 750,000,000.00 |
| 9. | Bariadi TC | 562,312,143.00 |
| 10. | Bukoba MC | 539,749,597.00 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeelezwa na Wakurugenzi juu ya mikakati ya ulipaji wa madeni hayo. Hata hivyo, kiwango kilichoelezwa kutengwa katika bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya ulipaji wa madeni ni kidogo ikilinganishwa ukubwa wa madeni yaliyopo hali itakayosababisha madeni hayo kulipwa kwa miaka mingi zaidi. Endapo madeni hayo hayatalipwa kwa wakati kuna hatari ya kuongezeka kwa gharama ya ulipaji wa madeni hayo kutokana na riba za ucheleweshaji wa malipo.

### 2.3.1.15 Kutorejeshwa kwa mikopo ya programu ya Kupanga, Kupima na Kurasimisha (KKK) Shilingi Bilioni 21.85

**Mheshimiwa Spika**, OR-TAMISEMI, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, zilitoa mikopo ya **Shilingi Bilioni 42.28** kwa Halmashauri 58. Mkopo huo ulitokana na programu ya Kupanga, Kupima na Kurasimisha viwanja (KKK). Uendelevu wa program hiyo kwa kiasi kikubwa unategemea uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kurejesha mikopo kwa Wizara ya Ardhi, nyumba na maendeleo ya Makazi ambapo kasi ya urejeshwaji unategemewa na kasi ya mauzo ya viwanja vilivyopimwa na kulipiwa fidia stahiki.

Kinyume na matarajio ya Serikali, baadhi ya Halmashauri hazikutumia fedha hizo katika lengo lililokusudiwa hivyo kuzifanya Halmashauri hizo kushindwa kurejesha mikopo hiyo Wizarani kwa wakati. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023, kiasi cha mkopo kilichorejeshwa na Halmashauri ni **Shilingi Bilioni 20.42** na kubakiwa na deni la **Shilingi Bilioni 21.85** ambalo Halmashauri 47 kati ya Halmashauri 58 zilishindwa kulipa madeni yake kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mambo mengi, sababu zilizochangia Halmashauri hizo kushindwa kulipa deni hilo ni pamoja na kutumia fedha za programu ya KKK kwa kutekeleza shughuli ambazo haziusiani na miongozo ya programu **Shilingi Milioni 327.82**, kutolipwa kwa fidia ya ardhi **Shilingi Milioni 468** kwa familia zilizoathirika na utwaaji wa ardhi, migogoro ya ardhi katika maeneo ya mradi pamoja na kasi ndogo ya uuzaji wa viwanja vilivyopimwa, hali iliyosababisha mradi kukosa tija na fedha kushindwa kukusanywa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, Mfano wa Halmashauri ambazo bado hazijarejesha kiasi chote cha fedha ni Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze **Shilingi 1,700,000,000.00**, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala **Shilingi 1,165,158,000.00**,

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga **Shilingi 774,531,142**, Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa **Shilingi 200,000,000.00** na Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto **Shilingi 185,639,404.00**.

### 2.3.2 Tathmini ya Rasilimali watu na Mishahara

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mambo mengine, Kamati inaamini kuwa, ufanisi katika utekelezaji wa majukumu kwa watumishi wa Halmashauri unachagizwa na mambo mbalimbali ikiwemo kulipwa stahiki zao kwa wakati, kupandishwa vyeo kwa wakati na uwepo wa mazingira wezeshi ya ufanyaji kazi. Katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zinohusiana na rasilimali watu kama ifuatavyo: -

#### 2.3.2.1 Kutolipwa kwa malimbikizo ya mishahara Shilingi 11,420,214,782

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha watumishi wanapata stahiki zao kwa wakati, Kanuni Na. E.23 ya Mwongozo wa Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 imefafanua kuhusu haki anayotakiwa kupatiwa mtumishi wa Serikali pale anapopandishwa daraja au kuteuliwa katika kiwango cha juu.
Kinyume na matakwa ya Kanuni hiyo, katika mwaka wa fedha 2022/2023, kuna malimbikizo ya mishahara ambayo hayajalipwa kwa watumishi wa Halmashauri kwa zaidi ya miezi 12 yanayofikia **Shilingi 11,420,214,782.** Kutolipwa kwa madeni hayo kwa muda mrefu kunapunguza ufanisi wa utendaji kazi wa watumishi hao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi za Serikali za kulipa madeni hayo ambapo, malimbikizo ya mishahara yamepungua kwa **Asilimia 72.97** kutoka **Shilingi 42,257,173,197** zilizoripotiwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia **Shilingi 11,420,214,782** mwaka 2022/2023. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kuhakikisha madeni hayo yote yanalipwa na madai mapya yote ya watumishi yawe yanalipwa kwa wakati.

### 2.3.2.2 Makato ya Kisheria kutowasilishwa katika Taasisi husika Shilingi Bilioni 36.09

**Mheshimiwa Spika**, mishahara ya watumishi hujumuisha makato mbalimbali ya kisheria na ambayo si ya kisheria. Makato hayo yanayokatwa kutoka katika mishahara ya watumishi hao hupaswa kuwasilishwa kwa taasisi husika kwa wakati na kwa mujibu wa Sheria zilizoanzisha taasisi hizo. Taasisi zinazopaswa kupokea makato hayo ni pamoja na Mifuko wa Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF), Kodi ya mapato na marejesho ya mikopo kwa taasisi za kifedha.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, mchanganuo wa makato ya watumishi ambayo hayakuwasilishwa katika taasisi husika ni pamoja na PSSSF **Shilingi 3,594,289,922.00**, Kodi ya mapato **Shilingi 51,006,301.00**, NHIF **Shilingi 40,550,453.00**, Mfuko ya Hifadhi ya Jamii **Shilingi 54,585,990.00**, Mfuko wa fidia kwa wafanyakazi **Shilingi 204,834,010.00** na Taasisi nyinginezo **Shilingi 68,566,144.00** na kufanya jumla ya makato yote ambayo hayajawasilishwa kufikia **Shilingi 4,013,832,820.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri kushindwa kupeleka makato hayo kwa wakati hasa kwa watumishi wanaolipwa mishahara kwa kutumia mapato ya ndani kuna athari ya moja kwa moja kwa watumishi ambao makato yao hayajawasilishwa licha ya fedha hizo kukatwa katika mishahara yao. Aidha, athari nyingine ni Halmashauri husika kutozwa faini kubwa ya ucheleweshaji wa malipo kwa taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati zimekiri kupata athari kwa kutozwa faini/adhabu ambazo zimekuwa ni kubwa zaidi ya madeni ambayo hayakuwasilishwa kwa muda. katika Halmashauri 46 zilizokaguliwa na CAG, faini/adhabu inayotokana na ucheleweshaji wa malipo ni **Shilingi 32,075,513,149**

na **Shilingi 4,013,832,820** ndiyo michango ambayo haikuwasilishwa na kufanya jumla ya deni lote kuwa ni **Shilingi Bilioni 36.09**.

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga iliijulisha Kamati kuwa, Halmashauri ilipata adhabu na kutakiwa kuilipa PSSSF **Shilingi 45,714,385,154** kutokana na kushindwa kupeleka michango ya watumishi ya **Shilingi 238,405,571.00**. Licha ya kuwa Halmashauri imekwishalipa jumla ya **Shilingi 119,974,320.00** na kubakiwa na deni la **Shilingi 118,431,251.00**, bado kiasi hicho cha riba kinadaiwa na PSSSF.

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri nyingi ambazo hazijawasilisha michango ya watumishi wake katika mfuko wa PSSSF, Kamati imebaini kiasi kikubwa cha riba/adhabu inayotozwa na PSSSF kwa Halmashauri hizo. Kamati inashauri Serikali kuangalia upya utaratibu unaotumiwa na mfuko huo katika kutoza adhabu. Vile vile, Halmashauri zote nchini zinapaswa kuwasilisha michango ya watumishi wake kwa wakati.

### 2.3.2.3 Wakuu wa Idara kukaimu kwa muda mrefu

**Mheshimiwa Spika**, ufanisi wa utendaji kazi wa Maafisa Masuuli pamoja na mambo mengine unategemea ufanisi wa wakuu wa idara ambao wanatekeleza majukumu katika idara zao kwa niaba yake. Changamoto ambayo Kamati imeibaini ni baadhi ya Idara na vitengo katika baadhi ya Halmashauri kutokuwa na wakuu wa idara wenye mamlaka kamili kutokana na sababu mbalimbali.

Sababu mojawapo iliyotajwa na Wakurugenzi waliofika mbele ya Kamati ya kutokuwepo kwa Wakuu wa idara wenye mamlaka kamili ni Mamlaka husika kutopeleka watumishi wanaostahili katika Halmashauri hizo hali iliyosababisha watumishi wasio na sifa zinazotakiwa kisheria kukaimu nafasi hizo kwa muda mrefu. Vile vile, Sababu nyingine ni mchakato unaotumika kuwathibitisha watumishi

wenye sifa ili waweze kuwa na mamlaka kamili kuchukua muda mrefu sana.

**Mheshimiwa Spika**, tathimini ya Kamati imebaini kuwa, wakuu wa idara wengi ambao hawajathibitishwa wamekuwa wakikaimu katika nafasi hizo kuanzia mwaka mmoja na wengine hadi kufikia miaka mitano. Jedwali namba 9 linaonesha orodha ya baadhi ya Halmashauri ambazo zina wakuu wa idara wanaokaimu katika nafasi zao kwa muda mrefu.

**Jedwali Na. 9** Nafasi zilizo wazi za Wakuu wa Idara, Divisheni na Vitengo

| s/n | Jina la Halmashauri | Nafasi zilizo wazi |
|---|---|---|
| 1. | Nanyamba TC | 1. Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari<br>2. Mkuu wa Kitengo cha Mazingira na Usimamizi wa Taka<br>3. Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi<br>4. Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu<br>5. Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria<br>6. Mkuu wa Kitengo cha Tathmini na Ufuatiliaji |
| 2. | Kyela DC | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani |
| 3. | Kisarawe DC | 1. Mkuu wa Idara ya Miundombinu maendeleo ya vijijini na mijini<br>2. Mkuu wa Kitengo cha Hifadhi ya maliasili na mazingira, viwanda, biashara na uwekezaji<br>3. Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti wa Taka na usafi wa mazingira<br>4. Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia na Mawasiliano |
| 4. | Nyang’hwale DC | 1. Mkuu wa Idara ya Afya (Mganga Mkuu |

| | | |
|---|---|---|
| | | wa Wilaya)<br>2. Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria<br>3. Mkuu wa Kitengo cha Ugavi |
| 5. | Sumbawanga DC | 1. Mkuu wa Kitengo cha Mazingira<br>2. Mkuu wa Idara ya Utamaduni (traditional and culture)<br>3. Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani<br>4. Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA (IT)<br>5. Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano |
| 6. | Monduli DC | 1. Mkuu wa Kitengo cha ujenzi<br>2. Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 7. | Magu DC | 1. Mkuu wa Idara ya Miundombinu maendeleo ya vijijini na mijini<br>2. Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano<br>3. Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA<br>4. Mkuu wa Kitengo cha Mazingira na Usimamizi wa taka<br>5. Mkuu wa Idara ya Michezo na Utamaduni<br>6. Mkuu wa Kitengo cha hifadhi ya maliasili na mazingira, viwanda, biashara na uwekezaji |
| 8. | Hai DC | 1. Mkuu wa Divisheni ya Viwanda, biashara na uwekezaji<br>2. Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu na maendeleo ya vijijini na mijini<br>3. Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria<br>4. Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Taka na usafi wa mazingira<br>5. Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Hifadhi ya Mazingira<br>6. Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Takwimu<br>7. Mkuu wa Kitengo cha Michezo, Sanaa na itamaduni |

### 2.3.3 Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na mapungufu katika usimamizi wa Mikataba.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha mianya ya upotevu wa fedha za umma inayotokana na ununuzi wa umma inaondolewa, Mwaka 2023, Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma. Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kiasi kikubwa cha fedha za umma kinachotumika katika eneo la ununuzi wa umma kinakuwa na tija na kunakuwa na thamani ya fedha. Aidha, kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2023, Sheria iliyotumika ni kabla ya Bunge kufanya marekebisho ya Sheria hiyo. Katika kuhakikisha kunakuwa na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni, Kamati iliangalia maeneo yafuatayo: -

#### 2.3.3.1 Kufanya Ununuzi wa Shilingi Bilioni 28.13 nje ya mfumo wa kielekitroniki

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 20 Agosti 2019, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ilitoa tangazo la ununuzi wa Umma kufanyika kwa njia ya mfumo wa kielektroniki. Lengo la Serikali la kuanzisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki ni kuongeza ufanisi, kupunguza muda wa ununuzi, kupunguza vihatarishi, na kuboresha uwazi na haki katika ununuzi wa umma kupitia ununuzi wa kielektroniki.

Utekelezaji wa tangazo hilo umekuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya Maafisa ununuzi kutokuwa na ujuzi wa kutosha na kukosekana kwa usaidizi wa haraka wa matumizi ya mfumo na kutokuwa na wazabuni wa kutosha waliojisajili katika mfumo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto zilizobainishwa na Maafisa Masuuli waliofika mbele ya Kamati, ni lazima Halmashauri zizingatie matakwa ya Kanuni ya 342 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa

Umma za mwaka 2013 kwani kutozingatiwa kwa Kanuni hiyo kunaweza kuzisababishia Halmashauri hizo hasara.

Mfano wa Halmashauri ambazo zilifanya ununuzi nje mfumo wa NeST ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ambayo ilinunua vifaa vya ujenzi vya **Shilingi 531,349,050.00** na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga iliyonunua vifaa vya ujenzi vya **Shilingi 279,840,407.00** nje ya mfumo.

### 2.3.3.2 Ununuzi wa Shilingi Bilioni 4.79 kutoidhinishwa na Bodi za zabuni

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Bodi za zabuni yamewekwa ili kusimamia ubora na thamani ya fedha katika mchakato wa ununuzi pamoja na kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji wa Maafisa Masuuli. Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zinazuiwa kutoa zabuni ambazo hazijaidhinishwa na bodi za zabuni. Katazo hilo limetolewa chini ya Kanuni ya 55 (2), 163 (4) na 185 (1) za Kanuni za Ununuzi za Mwaka 2013.

Katika kuhakikisha kila Halmashauri inazingatia Kanuni hiyo, uchambuzi wa Kamati wa Ripoti ya CAG kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulibaini **Halmashauri 19** sawa na **Asilimia 10.3** ya Halmashauri zote 184 ambazo zilitoa zabuni ambazo hazikuidhinishwa na bodi za zabuni za Halmashauri zao. Kutozingatiwa kwa Kanuni hiyo kunaziweka Halmashauri hizo katika hatari ya kukosa thamani ya fedha ya bidhaa au huduma iliyolipiwa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa Halmashauri ambazo hazikuzingatia matakwa ya Kanuni tajwa hapo juu na kufanya ununuzi bila ya kuidhinishwa na bodi ya zabuni ni Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni **Shilingi 1,458,720,100.00**, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke **Shilingi 773,473,558.00**, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto iliyofanya ununuzi wa **Shilingi 47,538,036.00** na Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli iliyofanya ununuzi wa **Shilingi 238,554,910.00**.

### 2.3.3.3 Kufanya Ununuzi wa Shilingi Bilioni 28.87 nje ya mpango wa ununuzi

**Mheshimiwa Spika**, katika maandalizi ya bajeti ya kila mwaka, kila taasisi huandaa mpango wa matumizi wa fedha zilizotengwa katika bajeti. Katika eneo la ununuzi wa umma, Taasisi nunuzi huandaa mpango wa ununuzi wa mwaka ili utekelezaji wake uendane na bajeti iliyotengwa katika eneo husika.

Kukosekana kwa udhibiti wa ndani kunakopelekea kufanya ununuzi nje ya mpango wa ununuzi uliopangwa katika mwaka husika kunakwamisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Halmashauri husika. Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 imewekwa ili kudhibiti tatizo hilo. Kinyume na maelekezo ya Kanuni hiyo, zimebainika baadhi ya Halmashauri ambazo zilifanya ununuzi nje ya mpango wa mwaka wa ununuzi.

**Mheshimiwa Spika**, kufanya ununuzi nje ya mpango wa ununuzi kunaongeza uwezekano wa kufanyika kwa matumizi yasiyo na tija katika Halmashauri kwa kufanya ununuzi ambao haukupangwa na kukwamisha shughuli zilizopangwa kufanyika katika mwaka husika. Aidha, katika kutoa ufafanuzi wa hoja zilizoibuliwa na wajumbe wa Kamati, baadhi ya Halmashauri zimeeleza kuwa, changamoto hiyo kwa kiasi kikubwa inatokana na kutohuishwa kwa mipango ya ununuzi kwa fedha zinazopokelewa nje ya bajeti. Katika kutoa mfano wa hoja hii, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni **Shilingi 4,638,346,190.00**, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke **Shilingi 2,669,567,475.00** na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala **Shilingi 440,000,000.00** zilizfanya ununuzi nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka wa Halmashauri.

### 2.3.3.4 Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa Mikataba

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uendeshaji wa shughuli mbalimbali, Halmashauri kama zilivyo Taasisi nyingine zimekuwa zikishitaki na

kushitakiwa kutokana na sababu mbalimbali. Hata hivyo, imebainika kuwa, Licha ya uwepo wa wanasheria katika Halmashauri zote nchini, mara nyingi Halmashauri zimekuwa zikipoteza kesi zinazofunguliwa dhidi yake na kutakiwa kulipa kiasi kikubwa cha fedha. Hata kwa kesi zinazofunguliwa mahakamani na Halmashauri dhidi ya wadaiwa mbalimbali, pia Halmashauri zimekuwa zikipoteza kesi hizo.

Kamati imekutana na hoja kadhaa zinazohusiana na Halmashauri kutakiwa kulipa fedha kutokana na kushindwa kesi mbalimbali hali inayosababisha matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma. Mfano wa tatizo hilo limetokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilishindwa kesi na kutakiwa kumlipa mkusanya mapato Adosta Investment Co Ltd jumla ya **Shilingi 268,546,265**. Chimbuko la deni hilo ni kuwa, Halmashauri iliingia mikataba mitatu tofauti na wakala wa ukusanyaji wa mapato Adosta Investment Co. Ltd na alitakiwa kwa kila mkataba kuwasilisha kiasi cha **Shilingi Milioni 75**. Mkataba ulieleza kuwa, kiasi kitakachozidi kutoka **Milioni 75** kitakuwa ni malipo yake.

Wakati wa utekelezaji wa mkataba huo, Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) pia ilikuwa inafanya ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya maeneo ambayo alipewa Adosta kukusanya. Kutokana na hali hiyo, Adosta alionekana kushindwa kuwasilisha kwa Halmashauri **Shilingi Milioni 339**. Hata hivyo, mzabuni aliwasiliana na Mkurugenzi wa Halmashauri kwa maandishi kumjulisha juu ya NFRA kukusanya mapato katika eneo lake la mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, Mkurugenzi alimjibu mzabuni kwa maandishi kuwa asikusanye mapato katika maeneo hayo na badala yake Halmashauri itakusanya na kiasi kitakachozidi kitawasilishwa kwa mzabuni. Baada ya mzabuni kuonekana kutowasilisha mapato ya

**Shilingi Milioni 339**, Halmashauri ilifungua kesi dhidi yake. Hata hivyo, Halmashauri ilishindwa kesi hiyo baada ya mzabuni Adosta kufungua kesi dhidi ya Halmashauri juu ya madai ya fedha ambazo Mkurugenzi wa Halmashauri aliahidi kumlipa mzabuni baada ya kulipwa na NFRA.

Kamati ilitaka kufahamu iwapo NFRA iliwasilisha fedha hizo kwa Halmashauri na chimbuko la deni la **Shilingi Milioni 268** wakati kesi ya awali ilikuwa ni **Shilingi Milioni 339**. Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Ndg. Herbert J. Mbise alijuulisha kamati kuwa,

**Nukuu:-**

***"Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ni kwamba, actually counter claim yake haikuwa Shilingi Milioni 268. Counter claim yake ilikuwa ni Shilingi 120,577,250 ikiwa ni sehemu ambayo kwa mujibu wa makubaliano na ofisi, alionekana yuko deserved kupewa kutokana na makusanyo yaliyofanywa kutoka NFRA, yale ya shilingi milioni mia mbili Hamsini na ngapi nilizozisema kumradhi. Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tofauti hiyo ilipokwenda mahakamani ambayo yeye anaidai kama counter claim, hukumu ya Mahakama ikamwongeza na vitu vingine vinavyoipeleka kwenye shilingi 268. Kwa hiyo, hukumu ya mahakama ikatoa riba ya 25% kwenye zile fedha zilizokusanywa mwaka huo 2015. Decision ya kesi ilikuwa ni mwaka 2018. Kwa hiyo ikatoa 25 percent kwa hicho kipindi, ambayo ilikuja Shilingi 97,969,015.60. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama pia ilitoa madhara ya jumla aliyoyapata kwenye biashara ya figure ambayo ni Shilingi Milioni 50 kamili. Kwa hiyo ukizijumlisha hizi zote ndio unapata ile Shilingi Milioni 268. Naomba kuwasilisha."***

**Mwisho wa Nukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa usimamizi wa mikataba kumeisababishia Halmashauri hasara ya **Shilingi Miloni 268**. Serikali

ihakikishe Wakurugenzi wote wanakuwa na usimamizi madhubuti wa mikataba.

### 2.3.3.5 Kuchelewesha malipo kulikosababisha Riba

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikichukua mikopo kutoka katika Taasisi mbalimbali kwa sababu mbalimbali. Hata hivyo, Halmashauri hizo zimekuwa zikishindwa kurejesha fedha hizo kwa wakati ulioainishwa katika mikataba hali inayosababisha kutozwa adhabu ya ucheleweshaji wa malipo.

Katika eneo hilo, Halmashauri ya Mji Bariadi iliingia Mkataba namba TIB/CBL/CORP/BTC/18/09/06 kwa ajili ya mkopo wa **Shilingi 1,543,775,085.00** (Principal Amount). Mkataba huo uliingiwa tarehe 06 Septemba, 2018 kwa ajili ya kulipa fidia ya ardhi eneo la nyaumata katika vijiji vya sesele na maperani. Kwa mujibu wa Mkataba, hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2020, fedha yote ilitakiwa iwe imekwishalipwa.

**Mheshimiwa Spika**, hadi mkaguzi anakamilisha kazi yake mwezi Novemba, 2023, Halmashauri ilikuwa haijalipa mkopo huo na kusababisha adhabu ya **Shilingi 626,409,678.00** na kusababisha mkopo kufikia **Shilingi 2,170,184,763.00**. Hadi Halmashauri inakutana na Kamati mwezi Agosti, 2024, Mkurugenzi aliieleza Kamati kuwa, jumla ya **Shilingi 979,042,603.00** zimekwishalipwa na kubakiwa na deni la **Shilingi 1,191,142,160.00**.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, endapo Halmashauri haitakuwa na mikakati ya ulipaji wa deni hilo kwa haraka itakuwa katika hatari ya kuchukuliwa hatua za kisheria na TIB ikizingatiwa kuwa, uwezo wa Halmashauri wa kukusanya mapato ni mdogo ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23 Halmashauri iliweza kukusanya **Shilingi Bilioni 3.06**.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto nyingine ya ucheleweshwaji wa malipo kinyume na makubaliano yaliyopo katika mikataba ya utendaji kazi kumeisababishia Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kutakiwa kulipa riba ya **Shilingi 2,229,977,455** kutokana na kuchelewa kumlipa mkandarasi aliyetekeleza mkataba wa ujenzi wa kituo cha mabasi kilichopo Mbezi Luisi madai yake ya **Shilingi 8,915,391,448.**

### 2.3.4 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imetamka kuhusu uwepo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kazi zake zimefafanuliwa katika Ibara ya 146 ya Katiba hiyo. Katika utekelezaji wa jukumu la kuharakisha maendeleo kwa wananchi, Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi katika bajeti yake ya kila mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya maendeleo unafadhiliwa kwa fedha za Serikali Kuu na fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri. Kwa upande wa fedha za mapato ya ndani, tarehe 3 Januari, 2018, OR-TAMISEMI ilitoa barua yenye nambari ya kumbukumbu CBD.421/422/01/43. Katika barua hiyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziligawanywa katika makundi mawili, zikipewa misimbo ya "A" na "B", ambapo, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilitakiwa kutenga 60% na 40% ya mapato yao ya vyanzo vya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo mtawalia.

Kamati imekuwa ikichambua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri ili kubaini iwapo miradi hiyo ina tija na ufanisi na kwamba inakidhi malengo ya uanzishwaji na kuna thamani ya fedha. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zifuatazo:-

### 2.3.4.1 Miradi yenye thamani ya Shilingi Bilioni 2026.89 kutokamilika kwa wakati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikifuatilia kwa karibu juu ya ufanisi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri nchini ili kubaini iwapo kuna thamani ya fedha. Wakati wa ufuatiliaji, Kamati imebaini uwepo wa miradi mingi kutokamilika kwa wakati ambapo, katika mwaka 2022/2023 miradi yenye thamani ya **Shilingi 206,886,504,449** ilikuwa haijakamilika.

Kamati inatambua juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo miradi mingi ya kimkakati imetekelezwa. Aidha, kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, Wakurugenzi wameijulisha Kamati kuwa, baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati hasa kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Serikali Kuu inasababishwa na Serikali kutopeleka fedha hizo za miradi kwa wakati. Aidha, Serikali imekuwa ikipeleka fedha mwishoni mwa mwaka hali inayosababisha hadi mwaka unafungwa fedha hizo zinakuwa hazijatumika kutekeleza miradi iliyopangwa kutokana na kukamilisha taratibu za kisheria kama taratibu za ununuzi.

**Mheshimiwa Spika**, miradi kutokamilika kwa wakati kunaondoa tija ya utekelezwaji wa miradi hiyo kwa kuwa manufaa ambayo yalilengwa kuwafikia wananchi yanakuwa hayawafikii kwa wakati uliopangwa hali inayosababisha kutokuwepo kwa thamani ya fedha ya miradi hiyo.

Miradi mingi ambayo kwa kiasi kikubwa haijakamilika ni maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi, miradi ya ujenzi wa Ofisi za Halmashauri, miradi ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya, miradi ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari na miradi ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.

Katika Halmashauri zilizofika kwa ajili ya mahojiano, Halmashauri ambazo zina miradi ya kimkakati ambayo haijakamilika kwa wakati ni pamoja na mradi wa chumvi Itumbula wenye thamani ya **Shilingi 535,000,000** unaotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Momba na mradi wa kiwanda cha uzalishaji asali wenye thamani ya **Shilingi 540,792,619** unaotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo.

**Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa miradi ya maendeleo kunatarajiwa kuongeza chachu ya maendeleo katika maeneo husika. Hivyo basi, Kamati inaendelea kusisitiza juu ya ukamailishaji wa miradi yote ili kuleta ustawi wa wananchi.

### 2.3.4.2 Miradi iliyokamilika kutoanza kutumika Shilingi Bilioni 11.21

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya fedha nyingi kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, baadhi ya miradi imekuwa ikikamilika na kushindwa kutumika kwa muda mrefu. Katika ukaguzi unaoishia tarehe 30 Juni, 2023, miradi yenye thamani ya **Shilingi 11,206,285,784** ilibainika kutoanza kutumika licha ya miradi hiyo kukamilika. Kutotumika kwa miradi hiyo kunaondoa thamani ya fedha iliyotumika katika miradi hiyo na kuwakosesha wananchi wa maeneo husika fursa za kiuchumi ambazo wangeweza kuzipata kutokana na kutumika kwa miradi hiyo.

Kamati imeelezwa kuwa, Kutotumika kwa miradi husika kunatokana na uhaba wa rasilimali mbalimbali kama ukosefu wa watumishi, ukosefu wa maji na umeme, ukosefu wa samani na ukosefu wa vifaa tiba na vifaa vingine muhimu kwa upande wa vituo vya kutolea huduma za afya.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa kupitia Taarifa za CAG na kufanya mahojiano na Afisa Masuuli, Kamati ilibaini kuwa, Mwaka 2010, Halmashauri ya Wilaya ya Makete ilikabidhiwa Soko la wakulima Ngiu lililojengwa na kwa fedha za mradi wa DADPS na MVIWATA

lenye thamani ya **Shilingi 489,170,100**. Hata hivyo, hadi Halmashauri inafika mbele ya Kamati, Soko hilo halijaanza kutumika.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto nyingi zilizopo katika masoko mengi nchini, ni vema Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya uendeshaji wa masoko yote nchini ili kubaini kama kuna ufanisi na thamani ya fedha katika miradi hiyo pamoja na kuangalia kiasi halisi cha fedha kilichowekezwa ikilinganishwa na faida inayopatikana.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini uwepo wa vituo vya kutolea huduma za afya kutoanza kutumika kutokana na kukosekana kwa wataalamu wa huduma za afya, kukosekana kwa kichomea taka, kukosekana kwa nyumba ya watumishi, kutokamilika kwa vyumba vya upasuaji, kukosekana kwa jokofu na umeme na maji pamoja na vifaa vingine.

#### 2.3.4.3 Fedha za mapato ya ndani kutopelekwa katika miradi ya maendeleo Shilingi Bilioni 17.60

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyofafanuliwa hapo awali kuhusu ulazima wa kila Halmashauri kutenga fedha kutoka katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati imefanya uchambuzi wa mwenendo wa upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pekee, katika Halmashauri 80 zilizokaguliwa hazikupeleka jumla ya **Shilingi Bilioni 17.60**.

Uchambuzi wa Kamati unatokana na matakwa ya Aya ya 83 (iii) na iv) ya mwongozo wa maandalizi ya mipango na bajeti kwa mwaka 2022/23 wa Novemba 2021 ambayo iliwaagiza Maafisa Masuuli ambao mapato yao ya ndani yanazidi **Shilingi Bilioni 5** kutenga 60% ya mapato yao ndani kwa shughuli za maendeleo na Halmashauri ambazo mapato yao ya ndani yako chini ya **Shilingi Bilioni 5** kutenga 40% ya mapato ya ndani kwa shughuli za maendeleo.

Katika uchambuzi huo, imebainika Halmashauri nyingi kutozingatia takwa hilo kwa kutopeleka fedha katika miradi ya maendeleo hali inayosababisha utekelezaji wa miradi hiyo kuchukua muda mrefu sana na kupunguza tija ya uanzishwaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa kiasi kilichopaswa kupelekwa katika miradi ya maendeleo ikilinganishwa na kiasi halisi cha fedha kilichopelekwa na kubaini Halmashauri nyingi kukiuka takwa la kutekeleza miradi kwa kutumia mapato ya ndani. Katika uchambuzi huo zipo Halmashauri ambazo zilipeleka fedha zote za miradi ya maendeleo kama H/W Hai, H/M Ubungo, H/M Temeke, H/M Kinondoni, H/W Biharamulo, H/W Msalala, H/W Singida, H/W Wanging'ombe, H/W Mkuranga, H/W Masasi, H/Mji Newala, H/W Tunduru, H/W Songe ana H/M Mtwara Mikindani.

Aidha, kwa Halmashauri ambazo hazikupeleka kiasi chote cha fedha, Maafisa Masuuli wamekiri kutumia fedha hizo za maendeleo kwa matumizi mengineyo na kuahidi kuzirejesha fedha hizo kutoka katika makusanyo ya mapato ya ndani ili ziweze kukamilisha miradi ambayo haijakamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo (2020/2021 hadi 2022/2023), Halmashauri 55 ambazo zimefika mbele ya Kamati hazikutenga jumla ya **Shilingi 38,866,003,932.43** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mfano wa Halmashauri ambazo hazikupeleka fedha katika miradi ya maendeleo kwa ukamilifu wake kwa kipindi cha miaka mitatu (2020/2021 hadi 2022/2023) ni kama inavyoonekana katika jedwali namba 10.

**Jedwali Na. 10** Halmashauri ambazo hazikupeleka fedha zote za miradi ya maendeleo kutoka katika mapato ya ndani

| Jina la Hamashauri | Kiasi kilichopaswa kupelekwa (3 yrs) | Kiasi kilichopelekwa (3 yrs) | Kiasi ambacho hakikupelekwa (3yrs) |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam CC | 97,984,720,167.00 | 76,190,609,425.00 | 21,794,110,742.00 |
| Singida MC | 4,711,701,895.00 | 2,395,331,065.00 | 2,316,370,831.00 |
| Kigamboni MC | 15,241,787,146.00 | 13,145,699,741.00 | 2,096,087,404.00 |
| Chato DC | 2,178,734,052.00 | 1,112,775,049.00 | 1,065,959,003.00 |
| Kyela DC | 3,066,494,232.00 | 2,079,822,607.00 | 986,671,625.00 |
| Sumbawanga DC | 3,312,709,081.00 | 2,535,663,279.00 | 777,045,802.00 |
| Kigoma Ujiji MC | 2,873,667,865.00 | 2,350,169,863.00 | 523,498,002.00 |
| Kilolo DC | 3,623,505,080.00 | 3,397,878,267.00 | 512,715,540.00 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imewataka Wakurugenzi wote kuhakikisha fedha za miradi ya maendeleo zinapelekwa kwa wakati na kwa fedha ambazo zilizotumika kwa matumizi mengineyo zinarejeshwa na CAG afanye uhakiki wa utekelezaji wa hoja hiyo katika kila robo mwaka.

### 2.3.4.4 Fedha za miradi ya maendeleo kutumika kwenye miradi mingine na matumizi mengineyo Shilingi Bilioni 7.73

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikifanya uchambuzi wa kina wa namna fedha za umma zilivyotumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri. Matokeo ya uchambuzi huo ni kwamba, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikitumia fedha hizo kwa miradi ambayo haikupangwa na kwa shughuli ambazo si za maendeleo ambazo zilipaswa kugharamiwa na fedha za matumizi mengineyo na kuziripotia kama miradi ya maendeleo hali inayozorotesha kasi ya maendeleo ya maeneo husika.

Kifungu Na. 27(4) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kinahitaji rasilimali zilizoidhinishwa kutumika kwa lengo lililokusudiwa na kwa kuzingatia vifungu mbalimbali vilivyobainishwa kwenye makadirio ya taasisi za serikali. Aidha, Kifungu Na.41 cha Sheria ya Bajeti, [Sura ya 439], kinazuia kubadili matumizi ya fedha za maendeleo kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Tofauti na matakwa ya vifungu hivyo, baadhi ya Halmashauri zilitumia fedha za miradi ya maendeleo kutekeleza miradi mingine na matumizi ya kawaida. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, CAG alibaini fedha za miradi jumla ya **Shilingi Bilioni 7.73** kutumika kwenye miradi mingine na matumizi ya kawaida. Utumiaji wa fedha hizo kinyume na malengo ya Serikali kunarudisha nyuma dhumuni la Serikali la kuhakikisha kila Halmashauri inawajibika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu.

Kwa upande wa miradi ambayo inatekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri, Kamati imekuwa ikipitia miradi yote iliyotekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani kama ilivyoainishwa katika Sheria. changamoto iliyobainika katika eneo hili inatokana na kutokuwepo kwa mwongozo wa namna matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo zinavyopaswa kutumika.

Aidha, Ofisi za Sekretarieti za mikoa (RAS) kutokuwa na utaratibu mzuri wa kufuatilia namna fedha hizo zilivyotumika ili kubaini iwapo lengo lililokusudiwa na Serikali limefikiwa, kumesababisha baadhi ya Maafisa Masuuli kufanya matumizi ya fedha za miradi kinyume na matarajio.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu nyingine ambayo imekuwa ikitumia fedha za miradi ya maendeleo zaidi ya kiwango cha kisheria ni fedha za tathimini na ufuatiliaji. Sheria imeweka ukomo wa kiwango cha fedha za tathimini na ufuatiliji kutozidi Asilimia 5 ya fedha za

miradi ya maendeleo. Hata hivyo, baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikitumia zaidi ya Asilimia 5 kinyume na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri juu ya uzingatiaji wa maelekezo yaliyotolewa na OR – TAMISEMI kwenye barua ya tarehe 3 Januari, 2018 pamoja na Aya ya 83 (iii) na (iv) ya mwongozo wa maandalizi ya Mipango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023 wa Novemba, 2021.

### 2.3.5 Changamoto za Uendeshaji wa Mfuko wa Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2018 Bunge lilifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 kwa kuongeza kifungu cha 37A ambacho kimeweka masharti ya utengaji na utoaji wa Mikopo kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Aidha, Kanuni za uendeshaji wa mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu umefafanua kwa kina taratibu zote zinazotakiwa kufuatwa na kila Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, katika hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazoishia tarehe 30 Juni, 2023, thamani ya mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ulikuwa ni **Shilingi 245,310,042,163**. Aidha, Kamati ilipokea na kufanya uchambuzi wa mwenendo wa mfuko huo ili kujiridhisha iwapo Sheria na Kanuni za uendeshaji wa mfuko huo zinafuatwa.

Kamati ilipata nafasi ya kusikia maelezo ya wakurugenzi kuhusu uendeshaji wa mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kubaini changamoto mbalimbali ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi na Serikali ili kuboresha utoaji wa mikopo hiyo. Changamoto zilizobainika ni kama zifuatazo; -

### 2.3.5.1 Shilingi Bilioni 7.27 ya mapato ya ndani kutopelekwa katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

**Mheshimiwa Spika**, Sheria inazitaka Halmashauri zote kuchangia Asilimia 10 ya mapato yake ya ndani ya kila mwaka kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. Lengo ni Halmashauri kuweza kutoa mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Utoaji wa mikopo katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu umelenga katika kuongeza chachu ya ukuaji wa kiuchumi kwa wananchi wa Halmashauri husika. Ili kuhakikisha lengo la uanzishwaji wa mfuko huo linafanikiwa kikamilifu, Kamati imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa karibu wa kiasi cha fedha kinachopaswa kupelekwa katika mfuko pamoja na kiasi halisi cha fedha kilichopelekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa hesabu zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2022/2023, michango ya Halmashauri katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ilikuwa ni **Shilingi 62,698,754,444**. Hata hivyo, jumla ya Halmashauri 62 sawa na **Asilimia 33.7** ya Halmashauri zote hazikuchangia kikamilifu Asilimia 10 ya mapato yake ya ndani katika mfuko huo. Kushindwa kuchangia kikamilifu katika mfuko kunapunguza fursa ya wananchi wengi kunufaika na mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya uwepo wa hoja hii, Kamati inazipongeza baadhi ya Halmashauri ambazo zimekuwa zikipeleka kwa wakati fedha zote za Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama Kanuni inavyotaka. Baadhi ya Halmashauri zilizopeleka fedha zote ni pamoja na H/W Kisarawe, H/M Kibaha, H/W Kasulu, H/W Kyela, H/M Mtwara Mikindani, H/W Songea, H/W Tunduru, H/Mji Newala, H/Mji Nanyamba, H/W Masasi, H/W Wanging'ombe, H/W Makete, H/W Singida, H/W Kongwa, H/W Nyang'hwale, H/M Bukoba na H/W Bumbuli.

Licha ya kuwa baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikizingatia takwa la Kanuni, zipo baadhi ya Halmshauri ambazo hazikupeleka fedha hizo kwa wakati. Kamati ilihoji sababu ya baadhi ya Halmashauri kutochangia kikamilifu katika mfuko na kubaini fedha zilizokusanywa zilielekezwa katika matumizi mengineyo ya Halmashauri badala ya kupelekwa katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kamati pia ilibaini baadhi ya Halmashauri kutochangia kikamilifu katika mfuko kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo (2020/2021 hadi 2022/2023) ambapo, kwa Halmashauri 55 zilizohojiwa na Kamati, Jumla ya **Shilingi 2,627,649,131.65** zilikuwa hazijapelekwa katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mfano wa Halmashauri ambazo hazikuweza kuchangia kiasi chote cha fedha katika mfuko ni jedwali namba 11 la Taarifa hii.

**Jedwali Na. 11**: Halmashauri ambazo hazikuchangia kikamilifu katika Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa miaka mitatu (2020/2021 hadi 2022/2023)

| Jina la Halmshauri | Kiasi kilichopaswa kuchangiwa (3yrs) | Kiasi halisi kilichochangiwa (3yrs) | Pungufu (3yrs) |
|---|---|---|---|
| Kigoma/Ujiji MC | 718,416,966 | 369,349,133 | 349,067,832 |
| Chato DC | 544,683,513 | 269,029,004 | 275,654,509 |
| Chalinze DC | 2,740,434,695 | 2,556,788,889 | 183,645,806 |
| Bariadi TC | 665,121,071 | 523,776,599 | 141,344,472 |
| Chemba DC | 410,808,565 | 286,700,000 | 124,108,565 |
| Sumbawanga DC | 828,176,664 | 708,944,110 | 119,233,159 |

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha wananchi wote wanaostahili kupata mikopo kupitia utaratibu wa Mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wananufaika na fursa hiyo, Kamati imeendelea kusisitiza juu ya uzingatiaji wa Sheria katika kuchangia

Asilimia 10 ya mapato ya ndani katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

### 2.3.5.2 Shilingi Bilioni 38.81 za mikopo kutolewa bila ya kuzingatia uwiano wa 4:4:2

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu imefafanua mgawanyo wa fedha unaostahili kutolewa kwa makundi yote ambayo ni Asilimia 40 kwa wanawake, Asilimia 40 kwa vijana na Asilimia 20 kwa watu wenye ulemavu.

Licha ya maelekezo ya kina yaliyotolewa katika Kanuni, Halmashauri 94 zilitoa mikopo ya jumla ya **Shilingi Bilioni 38.81** bila ya kuzingatia uwiano sahihi wa 4:4:2 wa utoaji wa mikopo hiyo. Baadhi ya Wakurugenzi wameeleza kuwa, sababu za mikopo hiyo kutototolewa kwa uwiano sawa ni baadhi ya makundi hasa kundi la watu wenye ulemavu kutojitokeza kwa ajili ya uchukuaji wa mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ya utoaji wa mikopo kwa uwiano sahihi itamalizika endapo Halmashauri zote zitaweka msisitizo kwenye utoaji elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kutumia fursa ya mikopo inayopatikana katika Halmashauri zao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa, endapo Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii watatekeleza majukumu yao kikamilifu katika eneo la kupata vikundi vyote kwa mujibu wa mgawanyo wa kisheria. Hatua za makusudi zichukuliwe na Maafisa Masuuli ili kuhakikisha wananchi wote wanapata elimu na kufahamu fursa za kiuchumi zinazopatikana kwa kuchukua mikopo hiyo.

### 2.3.5.3 Mikopo iliyotolewa kwa vikundi ya Shilingi Bilioni 79.76 kutorejeshwa

**Mheshimiwa Spika**, mikopo inayotolewa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inapaswa kurejeshwa kwa wakati ulioainishwa katika mkataba wa makubaliano baina ya Halmashauri na vikundi ili vikundi vingine viweze kunufaika na mikopo hiyo. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Halmashauri zilitoa mikopo ya jumla ya **Shilingi 73,411,018,877**. Hata hivyo, kutokana na ufuatiliji mdogo wa ukusanyaji wa mikopo hiyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023, Halmashauri zilishindwa kukusanya **Shilingi Bilioni 79.76**.

Kutorejeshwa kwa mikopo ya vikundi kwa wakati kunapunguza kasi ya utoaji wa mikopo hiyo kwa wahitaji hali inayoondoa azma ya Serikali ya kusaidia wananchi. Jitihada za makusudi zinatakiwa kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa vikundi vilivyopewa mikopo na kuchukua hatua za kisheria kwa vikundi vitakavyokiuka matakwa ya mikataba yao. Kwa Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati, jedwali namba 12 linaonesha Halmashauri ambazo hazijakusanya mikopo hiyo kwa kiasi kikubwa.

**Jedwali Na. 12**: Halmashauri ambazo hazijakusanya mikopo iliyotolewa katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

| s/n | Jina la Halmashauri | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Kinondoni MC | 6,173,215,764.00 |
| 2. | Temeke MC | 5,301,079,463.00 |
| 3. | Ubungo MC | 4,873,474,532.00 |
| 4. | Dar es Salaam CC | 3,139,588,131.00 |
| 5. | Kibaha TC | 1,762,824,323.00 |
| 6. | Kigamboni MC | 1,753,900,490.00 |
| 7. | Chalinze DC | 1,488,352,540.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Mkuranga DC | 1,404,313,570.00 |
| 9. | Tandahimba DC | 606,506,942.00 |
| 10. | Bukoba MC | 577,948,096.00 |
| 11. | Wanging'ombe DC | 463,734,744.00 |

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri kushindwa kukusanya kiasi hicho kikubwa cha fedha, kunapunguza uwezo wa mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuhudumia wananchi wengi zaidi kama ambavyo Serikali imedhamiria. Aidha katika Halmashauri 55 zilizofika mbele ya Kamati, fedha za mikopo jumla ya **Shilingi 36,581,519,694.00** zilikuwa hazijakusanywa kutoka katika vikundi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na changamoto mbalimbali zilizobainika katika uendeshaji wa mfuko huo, Mwezi Aprili, 2023, Serikali ilisitisha shughuli zote za utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na ulemavu ili kufanya maboresho ya mfumo wa utoaji wa mikopo hiyo. Aidha, Tarehe 16 Aprili, 2024, wakati akiwasilisha bajeti ya OR – TAMISEMI, Waziri alitangaza mikopo kuanza kutolewa kuanzia mwezi Julai, 2024 ambapo, iliyotarajiwa kutolewa ni Shilingi Bilioni 227.96. Mchanganuo wa fedha hizo ni Bilioni 63.67 marejesho, Bilioni 63.24 fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili yam waka 2023/2024 na Bilioni 101.05 fedha zilizotengwa kwa ajili yam waka 2023/2024.

Kamati inatambua kuwa fedha hizo hazijaanza kutolewa kwa vikundi kutokana na maboresho yanayofanyika. Hata hivyo, Katika kutaka kujiridhisha juu ya hatua zinazochukuliwa na Serikali katika maboresho ya mfumo huo, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Kamati ya Bajeti zilikutana na OR – TAMISEMI kwa ajili ya kupitishwa katika utaratibu mpya ulioandaliwa wa utoaji wa mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano ya kina kuhusu mfumo mpya wa utoaji wa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye

ulemavu, Kamati zote tatu ziliona bado kuna changamoto ambazo zinahitaji kuondolewa ili mapungufu yaliopo yasiweze kujirudia. Serikali inatakiwa ikazifanyie kazi changamoto hizo ili kuboresha zaidi utoaji wa mikopo hiyo na wananchi wengi waweze kunufaika kama ambavyo Serikali imedhamiria.

Changamoto zilizobainika ni pamoja na kuruhusu fedha za kundi moja kuweza kukopeshwa na kundi lingine, kutowekwa wazi kwa utaratibu wa utolewaji wa mikopo kwa kutumia mifumo ya benki, uwepo wa sharti la lazima la matumizi ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) licha ya changamoto zilizopo za upatikanaji wa vitambulisho hivyo, kutozingatia upatikanaji wa mtandao katika maeneo ya vijijini, kiasi kikubwa cha fedha za ufuatiliaji wa mikopo hiyo kitakachopunguza uwezo wa mfuko kukopesha pamoja na uwepo wa adhabu kutolewa kwa wakopaji pekee. Kutokana na changamoto hizo zilizobainika, Kamati inaishauri Serikali kuondoa changamoto zilizobainishwa na wajumbe pamoja na kuanza na Halmashauri chache za mfano (pilot study) ili kubaini ufanisi wa utoaji wa mikopo hiyo kabla ya kufungua dirisha la utoaji wa mikopo kwa Halmashauri zote Nchini.

### 2.3.6 Changamoto katika usimamizi wa Mifumo ya Kielektroniki

**Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbalimbali, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa shughuli za Serikali umehamishiwa katika mifumo mbalimbali ya kielektroniki. Matumizi ya mifumo hiyo inalenga katika kuziwezesha OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati ili kuongeza kasi ya uwajibikaji na kutoa huduma haraka kwa wananchi.

Kumekuwa na mifumo kadhaa inayotumika katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini. OR-TAMISEMI wanasimamia jumla ya mifumo **Ishirini na Mbili (22)** inayotumika katika sekta mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo, katika sekta ya Elimu, kuna

mifumo minne inayotumika ambayo ni pamoja na Mfumo wa sensa ya elimu ngazi ya shule – (Annual School Census - ASC), Mfumo wa usimamizi wa shule na utunzaji wa taarifa zake (School Information System – SIS), Mfumo wa kuwasilisha madai yasiyokuwa ya mshahara kwa watumishi (Madeni MIS) na Mfumo wa uchaguzi na upangaji wa wanafunzi (Selform & Selection - MIS).

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa sekta ya Afya kuna mifumo mitatu inayotumika ambayo ni Mfumo wa uratibu na usimamizi wa shughuli za Afya Tanzania (Government of Tanzania Health Operations Management Information System – GoTHOMIS), Mfumo wa bima kwa wote - ngazi ya jamii (Community Health Fund - iCHF-IMIS) na 25. Mfumo wa usafiri wa dharura kwa wajawazito na vichanga (M-MAMA).
Aidha, kuna jumla ya mifumo Saba (7) inayotumika katika eneo la fedha ambayo ni Mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa - TAUSI, Mfumo wa LGRCIS, Mfumo wa uhasibu na utoaji taarifa za fedha katika vituo vya kutolea huduma (Facility Financial Accounting and Reporting System - FFARS), Mfumo wa ukaguzi na ufuatiliaji wa taarifa za fedha (Inspection and Financial Tracking Management Information System - IFT MIS), Mfumo wa uwezeshaji wa maombi ya mkopo wa asilimia 10 (Wezesha Portal), Mfumo wa Mipango na Bajeti (Planning and Reporting System – PlanRep) na Mfumo wa Maegesho wa TARURA (TARURA eRevenue MIS – TeRMIS -Parking)

Eneo la ufuatiliaji na tathmini lina mifumo mitatu ambayo ni Mfumo jumuishi wa tathimini na usimamizi (Integrated Monitoring and Evaluation System - iMES), *Dashboard* na Mfumo wa kuhifadhi taarifa za wadau wa maendeleo na matokeo ya tafiti (WadauPortal). Vile vile, eneo la uongozi (governance) linatumia jumla ya mifumo minne inayojumuisha *Biometric/E-attendance*, GWF, Mfumo wa Mawasiliano ya Umma (Contact Center) na Mfumo wa kuratibu na kuwezesha usajili na kutunza taarifa za maeneo ya utawala ya

Mamlaka za Serikali za Mitaa (Administrative Area Registry - AReS). Aidha, kwa upande wa rasilimali watu kuna mfumo mmoja wa ajira.

Pamoja na uwepo wa mifumo hiyo mingi, Kamati imebaini changamoto kadhaa zilizopo katika matumizi ya mifumo hiyo ambazo ni pamoja na kutosomana kwa mifumo hiyo, kukosekana kwa wataalamu wa IT wa kuendesha na kusimamia mifumo hiyo, kutokuwepo kwa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumiaji wa mifumo, kukosekana kwa miundombinu muhimu katika baadhi ya maeneo kama umeme na mtandao.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikiboresha utendaji wa mifumo iliyopo hali iliyopelekea changamoto ya kuhamisha matumizi ya mifumo kutoka mfumo mmoja kwenda mwingine katika kipindi cha muda mfupi. Kamati imejulishwa kuwa, kuhamisha matumizi ya mifumo kunatokana na ukweli kwamba, baadhi yao imetengenezwa na kusimamiwa na wazabuni kutoka nje ya nchi (vendors) hali iliyosababisha Serikali kuingia katika gharama kubwa za kulipia mifumo hiyo kila mwezi ikiwa ni pamoja na kuhatarisha usalama wa taarifa zinazowekwa katika mifumo hiyo. Kwa muktadha huo, kwa sasa Serikali inatumia wataalamu wake wa ndani katika kuunda na kusimamia mifumo mbalimbali.

Kamati inatambua nia njema ya Serikali ya kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma. Hata hivyo, kuhamisha matumizi ya mfumo mmoja kwenda mwingine mara kwa mara kuna madhara mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupotea kwa fedha zilizotumika kujenga mfumo wa awali, gharama za kuzimamia mfumo huo na kupotea kwa fedha zilizotumika kufundisha watumiaji wa mfumo huo wa awali.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha kunakuwa na thamani ya fedha kwa mifumo ambayo imetengenezwa na wataalamu wa ndani, Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna bora ya kuboresha mifumo iliyopo kwa kuongeza udhibiti na kuongeza moduli

zitakazoimarisha udhibiti badala ya kuachana kabisa na mifumo hiyo na kuingia gharama kubwa za uundaji wa mifumo mingine.

Kwa upande wa Halmashauri zilizojadiliwa na Kamati, Changamoto zilizobainika katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki ni Halmashauri nyingi kutofunga mfumo wa GOT – HOMIS katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

**Mheshimiwa Spika**, ili kudhibiti mapato, Mwongozo Na. CEB.151/297/02/"N"/61 uliotolewa na OR – TAMISEMI tarehe 17 Oktoba, 2016 ulizitaka Hospitali zote za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati kufunga na kutumia mfumo wa kielektroniki wa GOT – HOMIS (Government of Tanzania Health Operations Management Information System).

Mfumo huu ulianzishwa kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya ili iweze kusaidia na kurahisisha shughuli za vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kusimamia uzalishaji na uhifadhi wa taarifa na takwimu za wagonjwa, mapato na dawa.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha Halmashauri zinakuwa na uwajibikaji na upatikanaji wa taarifa kwa haraka, Kamati imekuwa ikihoji juu ya vituo vyote vya kutolea huduma kufungwa mfumo wa GOT-HOMIS. Hata hivyo, Halmashauri nyingi nchini zimeshindwa kufunga mfumo huo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya kwa kutoa sababu kuwa, mapato ya Halmashauri yamekuwa hayatoshelezi kufunga mfumo huo katika vituo vyote kwa wakati mmoja.

Kushindwa kufunga mfumo huu kunapunguza mapato ya vituo hivyo, uwajibikaji pamoja na taarifa muhimu kutopatikana kwa haraka. Aidha, Halmashauri zilizobainika kutozingatia matakwa ya kanuni tajwa hapo juu kwa kiasi kikubwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Momba ambayo, kati ya **Vituo 45**, ni vituo **vitatu tu** ndivyo

vilivyofungwa mfumo wa GOT-HOMIS na **vituo 42** havijafungwa mfumo huo. Vile vile, katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, katika ya vituo 58, vituo vilivyofungwa mfumo wa GOT-HOMIS ni **16** pekee na kusaliwa na **vituo 42** ambavyo havijafungwa mfumo huo.

**2.3.7 Tathmini ya Uwekezaji wa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam katika Benki ya kibiashara ya DCB**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuchochea ukuaji wa mapato ya ndani, Halmashauri zimekuwa zikifanya uwekezaji katika maeneo ya kimkakati kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa Uchumi, kuboresha utoaji wa huduma na kusaidia maendeleo ya jamii. Katika kutekeleza hilo, mwaka 2001, Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam zilikubaliana kuanzisha Benki ya Jamii ya Dar es Salaam ambayo ilianza kazi zake mwaka 2002.

Halmashauri zilizohusika na uanzishwaji wa benki hiyo ni pamoja na Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ambazo kwa ujumla wake ziliwekeza jumla ya **Shilingi Bilioni 26.89** katika hisa **31,923,990**.

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam ni sehemu tu ya wanahisa wa benki hiyo. Mchanganuo wa umiliki wa Hisa katika benki ya DCB unaonekana katika jedwali namba 13 hapa chini

**Jedwali Na. 13:** Mchanganuo wa umiliki wa Hisa katika Benki ya DCB

| s/n | Jina la Mwanahisa | Idadi ya Hisa | Umiliki kwa % |
|---|---|---|---|
| 1. | Umoja Unit Trust Scheme | 13,529,856 | 14.43% |
| 2. | Dar es Salaam City Council | 10,228,320 | 10.47% |
| 3. | Ilala Municipal Council | 7,866,859 | 8.06% |
| 4. | UTT – Asset Management & Investor's Services Plc | 7,028,838 | 7.20% |
| 5. | National Health Insurance Fund | 6,000,000 | 6.14% |
| 6. | Kinondoni Municipal Council | 5,625,019 | 5.76% |
| 7. | Temeke Municipal Council | 3,422,252 | 3.50% |
| 8. | Ubungo Municipal Council | 2,877,367 | 2.95% |
| 9. | Kigamboni Municipal Council | 2,281,502 | 2.34% |
| 10. | Regular Income Unit Trust Scheme | 1,588,497 | 1.63% |
| 11. | Children's Career Plan Unit Trust Scheme | 402,847 | 0.41% |
| 12. | UTT – Projects & Infrastructure Development Plc | 100,000 | 0.10% |
| 13. | Others | 36,134,115 | 37.00% |
| **TOTAL** | | **97,646,913** | **100%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kulingana na jedwali hapo juu, Halmashauri za Dar es Salaam kwa pamoja zinamiliki **Asilimia 33** ya mtaji wote wa Benki hiyo ambapo, Pamoja na Mashirika mengine, Serikali ina umiliki wa ujumla kwa **Asilimia 63** ya mtaji wote. Hii ina maana kwamba, Serikali kupitia vyombo na mamlaka zake ina udhibiti wa maslahi katika uendeshaji wa benki hiyo kwa kuwa, vyombo hivyo vinamilikiwa na Serikali Kupitia Msajili wa Hazina.

Kwa muktadha huo, DCB inamilikiwa na Serikali kupitia Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam, UTT na NHIF. Hata hivyo, Benki hii hapo awali ilianzishwa kama benki binafsi iliyosajiliwa chini ya Sheria ya

Makampuni na kwa hivyo, hakuna Sheria ya Bunge ya kuanzishwa kwake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu hiyo, benki hii haimo kwenye orodha ya Mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina na hivyo, haijawahi kuwasilisha Taarifa zake za fedha kwa CAG kwa ajili ya ukaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na Kifungu cha 9(a) iii & iv cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008. Huu ni ukiukwaji wa Kifungu cha 30(b) na (e) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 ambacho, kinazitaka Taasisi zote ambazo Serikali imewekeza fedha zake na zile ambazo Serikali ndio mwanahisa mkubwa kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kukutana na uongozi wa DCB pamoja na wakurugenzi wote wa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam ili kufahamu juu ya nafasi ya Serikali katika uendeshaji wa benki hiyo na sababu ya hesabu za benki hiyo kutokaguliwa na CAG. Hata hivyo, Uongozi wa Benki hii uliieleza Kamati kuwa, Serikali haina umiliki mkubwa wa Hisa kwakuwa, Hisa za UTT zinatokana na uwekezaji wa mwananchi mmoja mmoja hivyo si mali ya Serikali.

Hoja iliyotolewa na DCB haina mashiko kwakuwa, UTT ipo chini ya Msajili wa Hazina na hesabu zake zinakaguliwa na CAG. Kwa muktadha huo, hata benki ya DCB inapaswa kuwa chini ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, uwekezaji uliofanywa na Halmashauri hizo katika Benki ya DCB kiujumla hauna tija na kuzisababishia hasara Halmashauri zilizowekeza (H/Jiji Dar es Salaam, H/M Temeke, H/M Kinondoni, H/M Kigamboni na H/M Ubungo) kwakuwa, tangu kuanzishwa kwa benki hiyo, Halmashauri zote hazijawahi kupata gawio. Vile vile, thamani ya hisa za DCB imeendelea kushuka kwa **Shilingi 50** kutoka **Shilingi 190** hadi **Shilingi**

**140** ambapo, wakati wa uanzishwaji wa benki hiyo, hisa moja ilikuwa ni **Shilingi 1000**.

Kuendelea kupungua kwa thamani ya hisa, kunasababisha Halmashauri kuendelea kupata hasara ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023, H/M Temeke ilipata hasara ya **Shilingi 2,943,136,720.00**, H/M Kinondoni ilipata hasara ya **Shilingi 3,431,261,840.00**, H/Jiji Dar es Salaam ilipata hasara ya **Shilingi 6,249,188,940.00**, H/M Kigamboni ilipata hasara ya **Shilingi 1,962,091,720.00** na H/M Ubungo ilipata hasara ya **Shilingi 2,150,007,740.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iangalie namna bora ya uendeshaji wa DCB ili Halmashauri hizo zisiendelee kupata hasara kwa kuwa, uwekezaji uliopo sasa hauna tija kwa wanahisa na ni upotevu wa fedha za umma.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO
### 3.1 Melezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa jicho la Bunge katika kuisimamia Serikali katika matumizi ya fedha za umma katika eneo la Mamlaka za Serikali za Mitaa ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Kamati ina maoni ya jumla yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya Halmashauri zimekosa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kushindwa kuandaa mikakati madhubuti ya ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato vyenye uhakika na kutegemea ruzuku ya Serikali Kuu kwa kiasi kikubwa. Changamoto hiyo pia imesababisha Halmashauri nyingi kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, Katika eneo hili la mapato, Kamati ina maoni ya jumla kuwa, Halmashauri zote nchini ziangalie fursa za biashara zinazopatikana katika maeneo yao ya usimamizi, kuhuisha kanzi data za wafanyabiashara waliopo katika maeneo yao, kufahamu kiasi halisi cha mauzo ghafi ya wafanyabiashara na kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma ili Halmashauri zote ziweze kujiendesha na kupunguza utegemezi wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo la uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya Serikali, Kamati ina maoni kuwa, Halmashauri zote zitekeleze majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni kama utengaji wa mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, upelekaji wa fedha katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na ulipaji wa madeni ya watumishi na wazabuni ili wananchi waweze kunufaika na uwepo wa Halmashauri hizo na lengo la utungwaji wa Sheria na Kanuni hizo liweze kufikiwa.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuhakikisha mapendekezo ya Kamati yanafanyiwa kazi kikamilifu. Jambo hilo limedhihirika wakati wa uchambuzi hesabu za Halmashauri zilizofika mbele ya Kamati ambapo, hoja nyingi zimekuwa zikipungua.

**Mheshimiwa Spika**, utoaji wa mapendekezo ya Kamati umezingatia hoja iliyopo, athari ya hoja hiyo pamoja na hatua zinazopaswa

kuchukuliwa na Serikali ili kuondoa hoja hizo. Ili kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya CAG, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa Maazimio yote yaliyotolewa na Bunge tarehe 02 Novemba, 2023.

Kwa muktadha wa uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023, Mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

### 3.3.1 Kukosekana kwa mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa Mapato ya ndani

**KWA KUWA**, kwa kiasi kikubwa uendeshaji wa shughuli za Halmashauri zimekuwa zikitegemea ruzuku ya Serikali hali iliyosababishwa na kukosekana kwa mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya ndani;

**NA KWA KUWA**, hali hiyo imesababisha baadhi ya Halmashauri kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, upotevu wa fedha za Umma na kuongeza mzigo kwa Serikali;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe kuwa, mapato ya **Shilingi 61,151,832,760** yanayotokana na vyanzo muhimu yanakusanywa na Halmashauri zinazohusika;

b) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinahuisha kanzi data ya walipa kodi ili kupata taarifa sahihi na idadi kamili ya wafanyabiashara wanaostahili kulipa ushuru wa huduma na kuwasilisha kwa CAG kabla ya tarehe 30 Machi, 2025;

c) Serikali ihakikishe Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inakuwa na takwimu sahihi za mauzo ghafi ili Halmashauri ziweze kukusanya kiwango sahihi cha ushuru wa huduma;

d) Serikali ihakikishe Halmashauri zinakusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.65** kutoka kwa mawakala wa ukusanyaji mapato;

e) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinafanya usuluhishi wa madai yote katika mfumo wa LGRCIS yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 45.02** ili kujua wadaiwa halali wa Halmashauri na wadaiwa wasio halali ili waweze kuondolewa katika mfumo kabla ya tarehe 30 Machi, 2025; na

f) OR – TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi za RAS katika mikoa yote zifuatilie na kubainisha mashauri yote yaliyopo TAKUKURU yanayohusishwa na fedha zilizokusanywa kwa kutumia mashine za POS ambazo hazikuwasilishwa benki na kuhakikisha kiasi cha **Shilingi Bilioni 6.17** kilichokusanywa kwa POS kinawasilishwa benki kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

### 3.3.2 Usimamizi Usioridhisha katika Matumizi ya Fedha za Umma pamoja na Akaunti ya Amana

**KWA KUWA**, kumebainika kuwepo kwa ukiukwaji Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali katika matumizi ya fedha za umma kama Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438, Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 pamoja na Mwongozo wa uhasibu wa mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019;

**NA KWA KUWA**, ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo hiyo kumesababisha matumizi yasiyofaa ya fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa na upotevu wa fedha za umma;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe Halmashauri zote hazifanyi Malipo yasiyo na stakabadhi za kielektroniki kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438 [iliyorekebishwa mwaka 2019];

b) Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo zilitumia jumla ya **Shilingi Bilioni 5.16** kwa shughuli ambazo hazikukusudiwa zirejeshe fedha hizo katika Akaunti ya Amana kabla ya tarehe 30 Juni, 2025; na

c) Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo zilitumia **Shilingi Bilioni 1.95** zaidi ya kiasi kilichowekwa katika Akaunti za Amana kurejesha kiasi hicho cha fedha kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

### 3.3.3 Madeni (Payables) ya Halmashauri kutolipwa kwa wakati

**KWA KUWA**, kumekuwepo kwa madeni makubwa ya watumishi na wazabuni katika Halmashauri nyingi nchini;

**NA KWA KUWA**, uwepo wa madeni hayo unapunguza morali na ufanisi katika utendaji kazi wa watumishi katika Halmashauri, kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi hasa kwa wazabuni wazawa, pamoja na kuziweka Halmashauri katika hatari ya kufunguliwa kesi za madai na ulipaji wa riba unaotokana na ucheleweshaji wa malipo;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali (Wizara ya Fedha) ilipe madeni yote ya watumishi na wazabuni yaliyohojiwa na CAG kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2023; na

b) Serikali ihakikishe Halmashauri 47 ambazo zinadaiwa kiasi cha **Shilingi Bilioni 21.85** kinachotokana na mikopo ya

programu ya Kupanga, Kupima na Kurasimisha (KKK) zinarejesha fedha hizo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

### 3.3.4 Tathmini ya Rasilimali watu na Mishahara

**KWA KUWA**, Ripoti ya CAG imebainisha changamoto zinazowakuta watumishi katika utendaji wao wa kila siku ikiwa ni pamoja na kutolipwa malimbikizo ya mishahara na kutothibitishwa katika nafasi walizonazo kwa muda mrefu;

**NA KWA KUWA**, kuchelewa kulipwa kwa malimbikizo ya mishahara ni kinyume na Mwongozo wa Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ilipe malimbikizo ya mishahara ya watumishi yenye jumla ya **Shilingi 11,420,214,782**;

b) Serikali iwasilishe katika Taasisi za PSSSF, NHIF, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa fidia kwa wafanyakazi na Taasisi nyinginezo jumla ya madeni ya **Shilingi 4,013,832,820**. Vile vile, Serikali iangalie upya utaratibu unaotumiwa na mfuko wa PSSSF katika kutoza adhabu za ucheleweshaji pamoja na kufuata taratibu za kisheria ili kushughulikia hoja ya **Shilingi 32,075,513,149.00** inayotokana na faini/adhabu ya kutowasilisha michango kwa wakati; na

c) Serikali ihakikishe Halmashauri zote zina wakuu wa Idara, vitengo na Divisheni wenye sifa na vigezo vinavyotakiwa kisheria ili waweze kuwa na mamlaka kamili katika nafasi zao.

### 3.3.5 Ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 na mapungufu katika usimamizi wa Mikataba

**KWA KUWA**, kumekuwepo na changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 kwa Baadhi ya Halmashauri nchini;

**NA KWA KUWA**, changamoto hiyo imesababisha kutokuwepo kwa thamani ya fedha katika ununuzi wa umma pamoja na upotevu wa fedha za Umma;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe Halmashauri zote nchini zinazingatia kikamilifu matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 410 pamoja na Kanuni zake.

### 3.3.6 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo

**KWA KUWA**, kukosekana kwa usimamizi wa karibu katika Halmashauri nyingi kumesababisha miradi kutokamilika kwa wakati, fedha za mapato ya ndani kutotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, fedha za miradi ya maendeleo kutumika kwa matumizi mengine na miradi iliyokamilika kutoanza kutumika;

**NA KWA KUWA**, uwepo wa changamoto hizo kumesababisha kukosekana kwa tija ya uanzishwaji wa miradi hiyo pamoja na kuwakosesha wananchi manufaa ambayo yangepatikana iwapo miradi hiyo ingetumika kama ilivyokusudiwa;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha ili miradi ambayo haijakamilika yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 206.89** inakamilika ili thamani ya fedha ya miradi hiyo iweze kupatikana;

b) Serikali iondoe dosari zote zilizobainishwa na CAG kwa miradi ambayo imekamilika lakini haijaanza kutumika ili miradi hiyo ianze kutumika kwa maslahi mapana ya wananchi; na

c) Serikali ihakikishe Halmashauri zote nchini zinazingatia matakwa ya maelekezo yaliyotolewa na OR – TAMISEMI kwenye barua ya tarehe 3 Januari, 2018 pamoja na Aya ya 83 (iii) na (iv) ya mwongozo wa maandalizi ya Mipango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023 wa Novemba, 2021 kuhusu upelekaji wa fedha za mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo na kuchukua hatua za kiutendaji kwa watakaokiuka maelekezo ya Serikali.

### 3.3.7 Changamoto za Uendeshaji wa Mfuko wa Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

**KWA KUWA**, utaratibu wa uendeshaji wa mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu umekuwa na changamoto mbalimbali hali iliyosababisha kusitishwa kwa utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;

**NA KWA KUWA**, kutoondolewa kwa changamoto hizo kwa haraka kabla ya kufungua dirisha la ukopeshaji wa fedha hizo kutawakosesha wananchi wengi fursa ya kunufaika na mikopo hiyo;

**KWA HIYO BASI**, Bunge liaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe Halmashauri zote ambazo hazikuchangia Asilimia 10 ya mapato yake ya ndani katika mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanapeleka fedha hizo katika mfuko kabla ya kufikia mwezi Juni, 2026;

b) Kabla ya kufikia tarehe 30 Juni, 2026, Serikali ihakikishe mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambayo haijarejeshwa yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 79.76** iwe imekusanywa; na

c) Serikali iendelee kufanya maboresho ya Kanuni mpya za utoaji wa mikopo katika vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Vile vile, Serikali ianze kutoa mikopo hiyo kwa Halmashauri chache (pilot study) ili kupima ufanisi wa mchakato huo.

### 3.3.8 Changamoto katika usimamizi wa Mifumo ya Kielektroniki

**KWA KUWA**, kumekuwa na matumizi ya mifumo mingi ya kielektroniki katika ngazi ya Halmashauri ambayo utumiaji wake umekuwa na changamoto mbalimbali kama wananchi na wataalamu kukosa elimu ya matumizi sahihi ya mifumo hiyo, mifumo iliyopo kutosomana, kukosekana kwa wataalamu wa IT na kukosekana kwa baadhi ya moduli katika baadhi ya mifumo;

**NA KWA KUWA**, kutofanyiwa kazi kwa changamoto zilizopo kutaondoa maana ya uanzishwaji wa mifumo hiyo na kusababisha upotevu wa fedha za umma;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe Halmashauri zote nchini zinakuwa na wataalamu wa kutosha wa ICT wenye weledi, kuhakikisha mifumo yote inayotumika katika ngazi ya Halmashauri inasomana na kunakuwa na maboresho ya mara kwa mara ya mifumo ili kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma;

b) Serikali ihakikishe Halmashauri zinatenga bajeti ya kutosha ili vituo vyote vya kutolea huduma za afya vifungwe mfumo wa GOT-HOMIS; na

c) Serikali (OR – TAMISEMI) itenge bajeti ya kutosha ya usimamizi wa mifumo ya kielektroniki inayotumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 3.3.9 Tathmini ya Uwekezaji wa Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam katika Benki ya kibiashara ya DCB

**KWA KUWA**, utendaji wa Benki ya Jamii ya Dar es Salaam (DCB) umekuwa ukishuka kila mwaka hadi kusababisha thamani ya hisa moja kufikia **Shilingi 140** kutoka **Shilingi 1000** wakati wa uanzishaji wa benki;

**NA KWA KUWA**, kuporomoka kwa thamani ya hisa na utendaji usioridhisha wa DCB umesababisha wanahisa zikiwemo Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo zimewekeza **Shilingi Bilioni 26.89** kupata hasara inayofikia **Shilingi 16,735,686960.00**;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba:

a) Serikali ihakikishe mabadiliko ya Sheria yanafanyika ili Benki ya Jamii ya Dar es Salaam (DCB) iondoke kutoka benki binafsi na iweze kuwa katika orodha ya Mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina kwakuwa, Serikali kupitia Taasisi zake ina umiliki wa Hisa kwa **Asilimia 63** ya mtaji wote;

b) Serikali ihakikishe Taarifa za hesabu za Benki ya Jamii ya Dar es Salaam (DCB) ziwe zinawasilishwa kwa CAG kwa ajili ya ukaguzi kwakuwa Serikali ni mwanahisa mkubwa katika benki hiyo; na

c) Serikali ifanye tathmini ya kina juu ya ufanisi na utendaji wa Benki ya Jamii ya Dar es Salaam (DCB) na kuona iwapo kuna tija ya Taasisi zake kuendelea kuwekeza katika benki hii.

### 3.3.10 Utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyotolewa katika taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali za Mitaa

**KWA KUWA**, bado kuna hoja ambazo zimesababisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwa Halmashauri zote nchini kutofanyika kikamilifu;

**NA KWA KUWA**, kutokamilika kwa utekelezaji wa mapendekeo ya CAG kunaashiria uendelevu wa matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri zote;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake kikamilifu na bila ya vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo muhimu kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kuwa

wavumilivu na kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1) Mhe. Halima James Mdee, Mb. – Mwenyekiti
2) Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb. - M/Mwenyekiti
3) Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb. – Mjumbe
4) Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb. – Mjumbe
5) Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb. – Mjumbe
6) Mhe. Issa Ally Mchungahela, Mb. – Mjumbe
7) Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi, Mb. – Mjumbe
8) Mhe. Jesca J. Msambatavangu, Mb. – Mjumbe
9) Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb. – Mjumbe
10) Mhe. Lemburis Saputu Mollel, Mb. – Mjumbe
11) Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb. – Mjumbe
12) Mhe. Ally Juma Makoa, Mb. – Mjumbe
13) Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb. – Mjumbe
14) Mhe. Michael C. Mwakamo, Mb. – Mjumbe
15) Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb. – Mjumbe
16) Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar, Mb. – Mjumbe
17) Mhe. Abdul Yusuf Maalim, Mb. – Mjumbe
18) Mhe. Mussa Omar Salim, Mb. - Mjumbe
19) Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangala, Mb. - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka I. Leonard kwa ushauri wake kwa Kamati pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kusomwa kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho japo siyo kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles

Kichere. Aidha, napenda kuishukuru OR – TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha kwa ushirikiano walioutoa katika Kamati kwa kutoa ufafanuzi kila ilipohitajika kufanya hivyo.

**4.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa** Spika, Naomba kutoa Hoja

Halima James Mdee, Mb.
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**

29 Oktoba, 2024

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono japo kuna Wabunge naona wamekaa, sijawaelewa vizuri lakini hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)*. Mheshimiwa Augustino Holle Vuma naona anasindikizwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobas Katambi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. VUMA A. HOLLE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA *(PIC)*:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya Kamati naomba uniruhusu angalau kwa nusu dakika, nikupongeze wewe binafsi kwa namna ambavyo

umeliheshimisha Bunge siku siyo nyingi zilizopita kwenye Mkutano wa *IPU* wa 149 uliofanyika Jijini Geneva Uswiswi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye kikao kile tulikuwa tunafuatilia, kulitokea vurugu kubwa na hoja nzito zikatoka, lakini ulivyozipangua kwa ujasiri mkubwa na umahiri wa hali ya juu, kimsingi ilitupatia heshima kama Bunge na kama Taifa, lakini zaidi ulimheshimisha Mheshimiwa Rais mwenyewe ambaye alikuwa ni kiongozi wa kampeni zako wakati unagombea Urais wa *IPU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai wa kuweza kufika siku hii ya leo. Kutokana na ufinyu wa mudam naomba taarifa hii yote kama inavyosomeka katika Kitabu cha Kamati iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu uwekezaji wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kuliomba Bunge likubali kuipokea na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inalenga kuliarifu Bunge lako Tukufu juu ya mwenendo wa uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na Serikali, ili kuliwezesha kujadili na kutoa maazimio yanayoendana na utekelezaji wa jukumu lake la kusimamia na kuishauri Serikali ili kuboresha ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni; sehemu ya utangulizi, sehemu ya ufafanuzi wa shughuli za ufuatiliaji wa mitaji ya umma, sehemu ya maoni na mapendekezo na sehemu ya hitimisho. Aidha, njia zilizotumiwa

katika kutekeleza majukumu ya Kamati ni kama ilivyoainishwa katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufafanuzi wa shughuli za Kamati kufuatilia mitaji ya umma, Bunge limepewa nafasi muhimu ya usimamizi wa shughuli za umma ikiwemo uwekezaji wa mitaji ya umma. Ili Bunge lichukue nafasi yake ya usimamizi unaostahili Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, hufuatilia mwendeno na masuala ya mitaji ya umma kwa lengo la kutoa taarifa na mapendekezo kwa Bunge. Kwa msingi huu sehemu hii inaripoti shughuli zilizofanyika katika kufuatilia ufanisi na uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya jumla ya uwezekazi wa mitaji ya umma, hali ya jumla ya uwekezaji wa mitaji ya umma katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 inaonesha kuwa, thamani ya mitaji ya umma katika mashirika, taasisi za umma na kampuni mbalimbali ni shilingi trilioni 75.79. Uongezaji huu ni sawa na ongezeko la asilimia tatu ikilinganishwa na kiwango cha shilingi trilioni 73.36 kwa mwaka fedha 2021/2022. Kiasi hicho cha mtaji kimewekezwa kwenye maeneo makuu mawili; eneo ambalo Serikali ina hisa 51% au zaidi na ambalo Serikali ina hisa chache, 50% na pungufu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma, tathmini ya ufanisi ilifanyika kwa kuzingatia vigezo maalum wakati wa kufuatilia uwekezaji. Vigezo hivyo ni pamoja na kiasi cha gawio, kiasi cha michango ya 75% ghafi, kiasi cha michango kutokana na makusanyo ya ziada na michango mingine na vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina. Vigezo hivyo ni viashiria vinavyosaidia kubaini iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma unafanyika kwa ufanisi na kwa kuwa umezingatia miongozo mujarabu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya ujumla wa makusanyo; Mapato ya Serikali kutokana na uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ni trilioni 1.008. Kiasi hiki ni jumla ya

mapato kutoka katika mitaji kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa kubwa na ambazo Serikali ina hisa chache. Mchanganuo wa makusanyo hayo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 01 la taarifa hii. Uchambuzi wa ujumla unaonesha kuwa:

(i) Kwa ujumla wa mapato yasiyo ya kikodi kwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kwa 29% ikilinganishwa na mwaka 2021/2022. Katika ongezeko hilo, ziada na michango mingineyo imeongezeka kwa kiwango cha 179%;

(ii) Kiasi cha michango iliyopokelewa kutokana na 15% ya mapato ghafi ya taasisi zinazostahili kuchangia pamoja na wasilisho la *TTMS* kila kimoja kimeongezeka kwa asilimia saba;

(iii) Mapato ya gawio kwa mwaka 2022/2023 yamepungua kwa asilimia nane kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Gawio lilichukua sehemu kubwa ya mapato yasiyo ya kikodi kwa kufikia 42%. Katika mwaka 2022/2023 mchango wa gawio katika mapato ulipungua kwa 33% ya mapato yasiyokuwa ya kikodi yaliyokusanywa;

(iv) Mwaka wa fedha 2021/2022 ziada ya michango mingineyo ilichangia mapato yasiyo ya kikodi kutokana na mitaji ya umma kwa 12% tu, na kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mchango wake uliongezeka na kufikia 34% ya mapato yasiyo ya kikodi kutokana na mitaji ya umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliainisha uwekezaji wa Serikali katika taasisi ambako ina hisa chache na uwekezaji katika taasisi ambako ina hisa nyingi kama ifuatavyo:

(a) Uwekezaji wa kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa chache.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uwekezaji inaonesha kuwa thamani ya hisa katika taasisi ambazo Serikali ina hisa chache ilitofautiana kwa miaka miwili. Aidha, idadi ya kampuni au taasisi ilitofautiana kati ya mwaka 2022/2023 na 2021/2022. Wakati mwaka 2021/2022 Serikali ilikuwa na hisa chache kwenye taasisi 51. Mwaka 2022/2023 Serikali ilikuwa na hisa chache kwenye taasisi 56. Ongezeko hilo la taasisi ni 12%.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kiasi cha gawio kilichopokelewa na Serikali ulionesha kuwa, kuna tofauti kati ya mwaka 2022/2023 na mwaka 2021/2022. Mwaka 2022/2023 Serikali ilipokea gawio la kiasi cha shilingi bilioni 131.2 kutoka katika taasisi 15 kati ya 56; na mwaka 2021/2022 Serikali ilipokea kiasi cha gawio kuanzia shilingi bilioni 204.37 kutoka katika taasisi 14 kati ya 50. Mchanganuo bayana unaonekana katika jedwali Na. 01, ambapo idadi ya taasisi ambazo Serikali ina hisa chache iliongezeka kwa 12% ikilinganishwa na mwaka 2022/2023; thamani ya hisa kwenye taasisi au kampuni ambayo Serikali ina hisa chache, imeongezeka kwa asilimia tisa ikilinganishwa na mwaka 2021; na Kiasi cha Dola kilichopokelewa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kiliongezeka kwa 13%.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinatoa maelezo ya ufanisi wa mitaji ya Umma kwa namna tofauti. Kwanza, inaonyesha kuwa, juhudi za Serikali kuwekeza katika kampuni zinalipa na faida inaongezeka. Ushahidi huu ni ongezeko la idadi ya taasisi ambazo Serikali imewekeza na ongezeko la thamani ya hisa za Serikali ikilinganishwa na mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kwenye ulinganisho kati ya ongezeko la thamani ya hisa na ongezeko la kiwango cha gawio. Wakati thamani ya hisa imeongezeka kwa asilimia tisa, kiasi cha

gawio kilichoongezeka ni 13%. Kwa maneno mengine, ongezeko dogo kwenye thamani ya hisa imesababisha ongezeko kubwa la gawio.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji kwenye taasisi na mashirika ya Umma ambayo Serikali ina hisa nyingi; ufanisi wa mtaji wa Umma kwenye mashirika, kampuni na taasisi ambazo Serikali ina hisa nyingi unaweza kupimwa kwa kuangalia mapato yasiyo ya kikodi yanayojumuisha gawio, michango ya 15% ya mapato ghafi na ziada na michango mingineyo.

Mheshimiwa Spika, upimaji huu unafanyika kwa kulinganisha michango ya taasisi hizo katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa miaka miwili tofauti ya uwekezaji. Kwa urahisi wa ufafanuzi, Jedwali Na. 3 linaonyesha taswira ya ufanisi ambapo Serikali imeongeza idadi ya mashirika, kampuni na taasisi ambazo ina hisa nyingi, kutoka 248 mwaka 2021/2022 hadi 250 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, namba tatu; thamani ya hisa kwenye maeneo ya uwekezaji ambayo Serikali ina hisa nyingi imeongezeka kutoka shilingi trilioni 70.8 kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, hadi shilingi trilioni 72.97 kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, gawio; Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, kiasi cha gawio kilichokusanywa kutoka katika Mashirika ya Umma ambayo Serikali inamiliki hisa nyingi, kilikuwa ni shilingi bilioni 109. Kiasi hiki ni pungufu kwa 47% ukilinganisha na kiasi cha gawio kilichokusanywa kutoka katika taasisi hizi, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo gawio lilikuwa shilingi bilioni 207.2.

Mheshimiwa Spika, aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kiasi cha gawio kilichokusanywa katika mashirika yanayojiendesha kibiashara kilichangiwa na mashirika tisa kati ya 31 yanayopaswa kuchangia, sawa na 27.3% ya mashirika yaliyotoa gawio kupitia kipengele hiki.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali iimarishe mikakati ya kusimamia mashirika haya ili kuhakikisha yanajiendesha kwa ufanisi na kupata faida ili yaweze kutoa gawio. Aidha, Serikali iweke mfumo wa uwajibishaji kwa ambao hawatekelezi agizo hilo. Hapa maana yake mashirika ambayo tuna hisa nyingi yanasuasua, yale ambayo tuna hisa kidogo ndiyo yanafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namba mbili, michango ya 15% ya Mapato Ghafi; michango ya 15% ya Mapato Ghafi imeonyesha ufanisi wa mitaji ya Umma kwa taasisi stahiki. Kwa mwaka 2020/2021, makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 202.2. Mwaka 2021/2022 yalikuwa shilingi bilioni 324, na mwaka 2022/2023 yalikuwa ni shilingi bilioni 346. Mwenendo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Na.4. Maana yake hapo kuna mabadiliko makubwa sana; yanafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinaonyesha kuwa, ufanisi wa ukusanyajii wa michango ya 15% ya Mapato Ghafi umekuwa ukiongezeka, ambapo kwa mwaka 2021/2022 uliongezeka zaidi ya 37.5% na mwaka 2022/2023 uliongezeka kwa 6.4%. Hivyo, kwa ujumla wake ufanisi umeongezeka.

Mheshimiwa Spika, aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini pia, pamoja na ufanisi wa michango hii kuongezeka kwa mwaka 2022/2023, lakini idadi ya taasisi zilizochangia zilipungua kutoka taasisi 25 mwaka 2021/2022, hadi taasisi 23 mwaka 2022/2023, katika taasisi 28 zinazopaswa kuchangia chini ya kipengele hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine ni kwamba, kipengele hiki bado hatujakitumia kwa ukamilifu. Kama kitasimamiwa kikamilifu na taasisi na mashirika yote yakachangia kwa mujibu wa sheria, Serikali itapata mapato mengi zaidi kupitia kifungu hiki.

Mheshimiwa Spika, namba tatu, ziada na michango mingine; kipengele cha ziada na michango mingine kinajumuisha 70% ya ziada ya mapato yanayotokana na shughuli kwa taasisi zinazotoa huduma, michango ya hiyari na mapato yatokanayo na shughuli za ufuatiliaji zinazofanywa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/2023, kipengele hiki kimekuwa na ufanisi ambapo jumla ya shilingi bilioni 287.2 zilikusanywa, kiasi ambacho ni ongezeko la 63.4% ukilinganisha na shilingi bilioni 105 kilichokusanywa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mwaka 2021/2022 kiasi cha michango na michango mingineyo kiliongezeka kwa 64%, ambacho ni kiasi kikubwa. Aidha, idadi ya tasisi zilizochangia kwa mwaka 2023 imepungua kwa 25%, ingawa mchango umeongezeka.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, taasisi na mashirika ya umma yakisimamiwa kikamilifu na kuongeza ufanisi wake, yanaweza kuongeza mchango wake katika Mfuko wa Serikali na tija ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kuweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, mambo ya jumla kuhusu uendeshaji wa mitaji ya Umma; Kifungu cha 11(1)(b) cha Kanuni zetu za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kinaipa Kamati jukumu la kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilibaini mambo mbalimbali ya kiutendaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini; moja ya kigezo cha utendaji ambacho taasisi na mashirika ya Umma wamewekewa na Msajili wa Hazina, ni kuhakikisha utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini unapungua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2022/2023, utegemezi wa ruzuku umeongezeka, ambapo kwa miaka mitatu mfululizo umekua kwa 21.2%, kutoka shilingi bilioni 13.234 mwaka wa fedha 2021/2022, hadi kufikia shilingi bilioni 17.456 mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kuna mashirika 63 ambayo kutokana na uendeshaji wa shughuli zake yanapata mapato makubwa kuliko ruzuku wanayopokea kutoka Serikalini, lakini bado yanapokea ruzuku kutoka Serikalini. Ni vyema mashirika haya yakasimamiwa kikamilifu kuhakikisha yanatekeleza majukumu yake kikamilifu na yanakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato na yanadhibiti matumizi yake, kisha wapewe mpango wa kujiondoa kwenye utegemezi wa ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, uchambuzi wa Kamati ulibaini, katika mashirika 35 yanayojiendesha kibiashara, mashirika 17 yanapokea ruzuku kutoka Serikalini. Mashirika haya yanapaswa kuongeza ufanisi kutumia fursa zilizopo sokoni ili kuongeza mapato yake na hatimaye kujitoa katika utegemezi wa ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilibaini, utegemezi wa ruzuku ya matumizi mengineyo pamoja na mishahara, umeongezeka pia, ambapo kwa mujibu wa Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, imeeleza kuwa, kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, utegemezi wa matumizi mengineyo ya mishahara umeongezeka kutoka shilingi bilioni 793.58 mwaka 2021/2022, hadi shilingi trilioni 1.33 mwaka 2022/2023. Ongezeko hili ni sawa na 40%, ambapo ni ongezeko kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mategemeo ya Serikali kuanzisha taasisi na mashirika ya umma ni pamoja na yajiendeshe kwa ufanisi, yatoe huduma stahiki kwa wadau wake ili yaweze kutengeneza faida na hatimaye kuweza kujitegemea katika uendeshaji wake kwa lengo la

kuipunguzia Serikali mzigo. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali iyasimamie kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utendaji wa taasisi na mashirika ya umma; katika kutekeleza jukumu la kuhakikisha mitaji katika mashirika na taasisi za umma inasimamiwa ili kuleta tija, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kuna baadhi ya taasisi na mashirika na Wakala wa Serikali utendaji wake unasuasua, jambo ambalo linaathiri tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma. Mambo yaliyobainika katika uchambuzi wa Kamati ni kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mashirika ya Umma yamepata hasara na nakisi kwa miaka mitatu mfululizo. Baadhi ya mashirika ya Umma yamepata hasara au nakisi katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Hali hiyo inatokana na bodi na menejimenti za taasisi hizo kuwa na usimamizi usioridhisha na hivyo kusababisha kukosekana kwa ufanisi ikiwemo kutokuwa na ubunifu katika kuendeleza vyanzo vilivyopo vya mapato na vilevile, kushindwa kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuhakikisha utendaji wa taasisi unakuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa taasisi hizo ni pamoja na Kampuni ya Uwekezaji ya *TANOIL*, *TTCL*, Bodi ya Mkonge, Shirika la Masoko ya Kariakoo *(KMC)*, Mamlaka ya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya kupata hasara mfululizo inaleta mashaka katika uendelevu wa taasisi na inaweza kusababisha malengo ya kuanzishwa kwa taasisi hizi kutofikiwa. Hivyo, kuna umuhimu wa utendaji wa taasisi hizi kutathminiwa upya kwa lengo la kuboresha utendaji ili kuleta tija ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbili, hali mbaya ya ukwasi katika taasisi na mashirika ya umma; uchambuzi wa Kamati umebaini baadhi ya mashirika umma kutokuwa na ukwasi wa kutosha, hali ambayo imesababisha mashirika mengi kujiendesha kwa madeni kutokana

na kutumia huduma za wazabuni bila kulipa. Mfano, mashirika ya umma ambayo kwa miaka mitatu yamekuwa yakizalisha madeni ni pamoja na *TTCL*, Shirika la Posta, Kampuni ya Ranchi za Taifa, *TFRA*, Bodi ya Mkonge na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, baadhi ya mashirika ya umma kushindwa kutumia fursa walizonazo; uchambuzi umebainisha kwamba, baadhi ya mashirika ya umma pamoja na uwepo wa ushindani na Sekta Binafsi, bado yana fursa kwenye ushindani kutokana na majukumu yao, lakini hayajaweza kutumia fursa hiyo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mashirika hayo ni pamoja na *TTCL* kwenye soko la mawasiliano, ambapo kuna fursa kupitia mradi wake mkubwa wa *Fiber* Mlangoni, lakini Ranchi ya *NARCO* kwenye Soko la Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake, *CPB* kwenye Soko la Nafaka, na Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* kwenye masuala ya uvuvi kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mashirika haya ni yale yanayojiendesha kibiashara. Ni vyema Serikali ikatathmini uendeshaji wa mashirika haya na kuyawezesha kwa maeneo ambayo ni kikwazo kwayo ili yaweze kujiendesha kikamilifu na kuweza kushindana katika soko, na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mashirika ya umma yana mapungufu ya mtaji wa uendeshaji. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, kuna baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mtaji wa uendeshaji, jambo ambalo linaathiri utendaji wa mashirika husika. Changamoto hii imepelekea taasisi na mashirika hayo ya umma kujiendesha kwa kutumia mtaji mdogo, au hasi kabisa, jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Mfano wa taasisi hizo ni *TTCL*, Bohari ya Dawa *(MSD)*, Benki ya Maendeleo *(TIB)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mapato ya Serikali ukilinganisha na mahitaji ya fedha, ni vyema taasisi na mashirika ya umma yaliyo na fursa ya kuwekeza yaelekezwe kutumia njia mbadala za upatikanaji wa fedha, kama vile kushirikisha Sekta Binafsi *(Public Private Partnership)*, mikopo kutoka taasisi ya fedha, na vilevile kutumia fursa ya upatikanaji wa fedha kupitia Soko la Hisa, ambapo mashirika yanaweza kuuza hisa au kuuza Hati Fungani katika soko kwa lengo la kupata mitaji ya utekelezaji wa shughuli zao, hatimaye kuweza kuweza kupunguza utegemezi wa ruzuku. Hapa *Tanga UWASA* wameupiga mwingi kwenye ile *bill bond*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi ya uwekezaji kuanza kabla ya kukamilika kwa maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi; uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, baadhi ya miradi ya maendeleo imekuwa ikianzishwa kabla ya kukamilishwa maandalizi yote ya msingi ikiwemo kufanya upekuzi wa kina kwa wakandarasi na kufanya maandalizi ya fedha, jambo ambalo limekwamisha miradi mingi ya uwekezaji kuweza kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa baadhi ya miradi, taasisi na mashirika ya umma yamekuwa yakisaini mikataba na wakandarasi kabla ya kukamilisha maandalizi ya fedha. Hivyo, kupelekea miradi kuchelewa kuanza, hivyo kusababisha kuzalishwa kwa riba za ucheleweshaji na hivyo kuongeza gharama za utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya miradi imeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na wakandarasi waliokabidhiwa miradi kutokuwa na sifa za kutosha. Mfano wa Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi vya Manyoni na Nyakanazi unaotekelezwa na Wizara na kusimamiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)*, kupitia fedha za ufadhili takribani *Euro* milioni 19.21, ambapo ufadhili huu ulitoka nchi za Umoja wa Ulaya, na malipo yalifanyika kwa kuzingatia hatua za utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi alikabidhiwa mkandarasi *M/S Impressa* ambaye alifilisika miaka miwili baada ya kukabidhiwa mradi. Mkandarasi huyu alitekeleza mradi huu kwa 60% Manyoni na 50% Nyakanazi. Tafsiri ya jambo hili ni kuwa, mkandarasi huyu hakufanyiwa upekuzi wa kina ili kubaini uwezo wake halisi, hususan kipengele cha uwezo wa kifedha. Matokeo yake ni mkandarasi kushindwa kukamilisha kazi yake kwa wakati na pia kufilisika. Hivyo, hataweza kukamilisha kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, jambo hili limesababisha msaada uliokuwa umepatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi hii kukoma (kusitishwa) kwa kuwa malipo *(disbursement of fund)* yalitegemea hatua za utekelezaji wa mradi. Kwa hiyo, kufilisika kwake kumepelekea kusitishwa kwa msaada, na hivyo mradi umesimama kwa takribani miaka sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, taasisi zinazotekeleza miradi ya uwekezaji ni vyema zifanye maandalizi ya awali, ikiwemo kujiridhisha juu ya upatikanaji wa fedha, upekuzi wa wakandarasi na uzingatiaji wa mikataba ya utekelezaji wa miradi kwa lengo la kuhakikisha miradi wanayoitekeleza inakamilika kwa wakati na kuiepushia Serikali mzigo wa gharama zisizo za msingi zinazotokana na riba.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijiji-miji; Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa ya uwekezaji ya Wakala wa Nishati Vijijini. Uchambuzi wa Kamati ulibaini tija ya uwekezaji katika Miradi ya *REA*, katika maeneo yenye mwonekano wa vijiji-miji ni ndogo kwani, kasi ya uwekezaji uliofanywa wa kusambaza huduma katika maeneo hayo imekuwa ni kubwa ukilinganisha na kasi ya uunganishaji wa wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hii ni kutokana na uwezo mdogo wa vipato vya jamii ya maeneo hayo ambao wanatozwa gharama sawa na

maeneo ya hadhi ya miji na majiji. Hivyo, wananchi wa maeneo hayo kushindwa kuunganisha umeme na hivyo kushusha ufanisi na tija ya uwekezaji unaofanywa na Serikali katika sekta hiyo, kwani ni watu wachache sana waliojiunga katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia jambo hili, Kamati ilielezwa kuwa, Serikali inaendelea na mchakato wa kutathmini bei halisi na stahiki zinazopaswa kutozwa katika maeneo yenye sifa hizo, ili kuwezesha walengwa kuanza kujiunga na huduma ya umeme kulingana na uwezo wao halisi wa kipato cha kiuchumi (ile shilingi 27,000).

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yaliyotolewa na Serikali, uchambuzi wa Kamati hii umebaini kuwa mchakato huo umechukua muda mrefu mno. Jambo hili linaendelea kuathiri ufanisi wa mtaji na kushusha tija ya uwekezaji inayofanywa na Serikali katika miradi ya *REA* kwa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto katika uendeshaji wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA)*, pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)*; jukumu la Mamlaka za Hifadhi ni kuendeleza uhifadhi wa Maliasili na Malikale pamoja na kuendeleza utalii. Utekelezaji wa majukumu hayo ni moja ya sababu iliyopelekea kuchochea ukuaji wa Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, katika kutekeleza majukumu yake, mamlaka hizi zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kufuatia janga la UVIKO 19, taasisi ya *NCAA* na *TANAPA* ziliathirika ikiwa ni matokeo ya athari za janga hilo na hivyo Serikali katika kunusuru uendeshaji wa taasisi hizo ilifanya marejeo ya ukusanyaji wa mapato na kuanza kuzipa ruzuku taasisi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi ambacho Sekta ya Utalii ilikuwa imeathirika, aidha kutokana na kurejea kwa Utalii kwa nguvu zilizowekwa na Serikali ikiongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, idadi ya watalii imeongezeka, hivyo taasisi hizi sasa kwa mapato ambayo yanakusanywa zinaweza kuchelewa kujiendesha, lakini bado utaratibu wa makusanyo yao yanakusanywa na *TRA* na wao kupokea ruzuku kwa ajili ya kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, awali Taasisi ya *NCAA* na *TANAPA* waliweza kukusanya mapato yao na kuyatumia kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mamlaka ikiwemo; kuboresha miundombinu kwa wakati kipindi inapohitajika na kufanikisha utekelezaji wa jukumu zima la Utalii na kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, aidha, mabadiliko yaliyofanywa kutokana na athari za UVIKO 19, mamlaka hizi zinalazimika kusubiri mgao wa ruzuku kutoka Serikalini jambo ambalo kiasi kikubwa linakwamisha utendaji wa mamlaka, kwani fedha hizi zimekuwa haziendi kwa wakati stahiki, kwani msimu wa Utalii huanzia mwezi Julai hadi Septemba lakini pia bajeti wanazotengewa zimekuwa kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya mamlaka, jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu yake hususani miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufinyu wa bajeti, ufinyu wa bajeti pamoja na ucheleweshwaji wa fedha kwa taasisi hizi umeathiri pia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo upande wa *NCAA* athari za ucheleweshwaji wa fedha za miradi zimesababisha mkandarasi kudai riba ya ucheleweshaji wa miradi miwili; ambao ni ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mamlaka pamoja na ujenzi wa barabara ya *view point* kiasi cha shilingi milioni 219, hii ni hasara tunapata.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kuwa mapato halisi yanayotokana na shughuli za Utalii katika hifadhi hizi ni makubwa, lakini bajeti inayoidhinishwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za hifadhi ni ndogo. Haiakisi mahitaji halisi ya mamlaka hilo jambo linaloathiri utendaji kazi wa hifadhi hizi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imebaini kuwa changamoto ya miundombinu ya barabara pamoja na vyoo imekuwa vikwazo kwa watalii hususani watalii kutoka nje ya nchi, jambo linalopunguza idadi ya watalii hususani wale *returning visitors* akija harudi tena, hivyo kuathiri mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya *NCAA* na *TANAPA* ni kati ya taasisi ambazo zilikuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa katika mfuko Mkuu wa Serikali kabla ya kuathiriwa na janga la UVIKO 19. Juhudi kubwa za Serikali zimefanyika na hatimaye taasisi zimeweza kurudi katika hali ya awali ya uzalishaji wa mapato licha ya kukabiliwa na changamoto zilizobainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa, Serikali kutafakari ufumbuzi wa jambo hili na taasisi za kimkakati kuruhusiwa kukusanya mapato yake ili ziweze kuwa na ukwasi muda wote na kuwezesha kutekeleza majukumu yake hususani jukumu la ujenzi na ukarabati wa miundombinu za mamlaka ili kuwezesha kuwa na ufanisi na kuweza kuhudumia watalii kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati; mapendekezo, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni tegemeo la Bunge katika kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na Serikali kwa lengo la kuliwezesha Bunge lako Tukufu kusimamia na kuishauri Serikali kuhusu uwekezaji unaofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi na ufuatiliaji uliofanywa na Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati ambayo kwa maoni ya Kamati, iwapo Bunge litaridhia, yanakusudia

kutatua changamoto zilizopo katika uwekezaji wa mitaji ya umma na hatimaye kuongeza ufanisi wa uwekezaji mkubwa uliofanywa na unaoendelea kufanywa na Serikali.

(i) Kuhusu uchangiaji katika Mfuko Mkuu wa Serikali, Bunge linaazimia kwamba;

(a) Serikali iweke utaratibu wa kuziwajibisha bodi na menejimenti za taasisi na mashirika ya umma yanayoshindwa kutekeleza kigezo hiki cha kisheria cha kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(b) Serikali kupitia Msajili wa Hazina iongeze usimamizi kwa taasisi na mashirika ya umma kuhakikisha yanaimarisha utendaji wake kwa lengo la kuongeza mapato yake na kuongeza mchango wake katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

(ii) Kuhusu utegemezi wa ruzuku Serikalini, Bunge linaazimia kwamba; Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) kufanya upembuzi yakinifu wa mashirika yanayotegemea ruzuku na kuyawekea mipango ya kupunguza utegemezi hususani katika kipengele cha mishahara na matumizi mengineyo yaani *OC*.

(b) kusimamia taasisi na mashirika ya umma yanayotegemea ruzuku kuhakikisha yanatafuta njia mbadala zakupata rasilimali ikiwemo kutumia mikopo nafuu na kushirikisha sekta binafsi yaani *public private partnership* katika kutekeleza miradi ya uwekezaji ya kibiashara na vilevile kutumia fursa ya upatikanaji wa fedha katika soko la hisa kwa kuuza hisa au hati fungani kwa lengo

la kupata mitaji na kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamikia miradi hiyo.

(iii) Kuhusu tathimini ya utendaji wa taasisi katika mashirika ya umma, Bunge linaazimia kwamba; Serikali kupitia Msajili wa Hazina kufanya mapitio ya taasisi na mashirika ya umma kwa lengo la kubainisha changamoto wanazokabiliana nazo na kuweka mpango mahususi wa kutatua changamoto hizo ili taasisi husika ziweze kuongeza ufanisi wake na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana;

(iv) Kuhusu upungufu wa mtaji katika Benki ya *TIB*, Bunge linaazimia kwamba; Serikali kuiongezea mtaji Benki ya Maendeleo *TIB* ili kukidhi matakwa ya kisheria ya Benki Kuu *BOT* na kumudu ushindani katika soko kwani ni muhimu benki hii ikiendelea kuwepo ili kutekeleza malengo ya uanzishwaji wake;

(v) Kuhusu ucheleweshwaji wa malipo ya wakandarasi, Bunge linaazimia kwamba; Serikali kupitia Msajili wa Hazina kusimamia kikamilifu taasisi na mashirika ya umma kuhakikisha wanakamilisha maandalizi yote ya awali kabla ya kuingia mikataba ya utekelezaji wa miradi husika kwa lengo la kuepusha kuongeza Serikali mzigo utokanao na ulipaji wa riba za ucheleweshwaji.

(vi) Kuhusu wakandarasi wasiokuwa na vigezo kupewa kazi za utekelezaji wa miradi. Naomba kufanya maboresho kwenye pendekezo hili badala linavyosomeka katika taarifa iliyokuwa mezani leo asubuhi naomba lisomeke kama ifuatavyo; Bunge linaazimia kwamba Serikali isimamie kikamilifu taasisi na mashirika ya umma yanayotekeleza miradi ya uwekezaji ili kuhakikisha yanafanya upembuzi wa kina na kujiridhisha juu ya

uwezo wa wakandarasi wanaokabidhiwa miradi hiyo kwa lengo la kujiepusha na changamoto katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo changamoto ya miradi kutokamilika kwa wakati;

(vii) Kuhusu gharama za kuunganisha umeme vijiji miji; Bunge linaazimia kwamba Serikali kupitia Wizara ya Nishati na mamlaka zake zinazohusika ihakikishe inaharakisha kukamilisha tathimini ya gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya namna hiyo na kubainisha majina ya maeneo na gharama ndani ya miezi sita ili kuongeza ufanisi wa mtaji unaowekezwa katika miradi hii. Jambo hili litasababisha kukamilisha azma ya Serikali yakupeleka nishati ya gharama nafuu vijijini kwa lengo la kukuza uchumi na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wa vijijini; *(Makofi)*

(viii) Kuhusu kuzingatia vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina;

(a) Bunge linaazimia kwamba Msajili wa Hazina afanye marejeo ya vigezo vya utendaji na kuvipanga kwa taasisi kulingana na uhalisia na majukumu ya taasisi au shirika husika.

(b) kuzisimamia taasisi na mashirika ya umma kuhakikisha zinajiendesha ndani ya vigezo vya utendaji ilivyopatiwa kwa lengo la kuleta ufanisi na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

(c) kuweka utaratibu wa kuwachukulia hatua stahiki bodi na menejimenti za taasisi zinazoshindwa kutekeleza vigezo vya utendaji walivyopatiwa.

(ix) Kuhusu changamoto katika uwendeshaji wa Mamlaka za Hifadhi Ngorongoro pamoja na Shirika la Hifadhi *TANAPA*; Bunge linaazimia kwamba Serikali irejeshe utaratibu wa zamani wa Taasisi za *NCAA* na *TANAPA* kukusanya mapato yake kwa lengo la kuwawezesha kuwa na ukwasi muda wote ili waweze kufanya maendeleo ya maeneo wanayoyasimamia kwa wakati na kuongeza ufanisi kwa taasisi hizi muhimu katika tasnia ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ujenzi na Uendeshaji wa Stendi ya Msamvu; Bunge linaazimia kwamba Serikali irudishe uendeshaji wa Stendi ya Msamvu kwa Mfuko wa *PSSF* ili mradi utumike kurejesha gharama za uwekezaji na baada ya Mfuko kurudisha gharama za uwekezaji stendi itarejea kuwa mali ya Manispaa ya Morogoro. Jambo hili litaipunguzia Serikali mzigo wa kulipa gharama za uwekezaji zilizotolewa na Mfuko wa *PSSF*.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti Wabunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo, ushauri na miongozo ya Kiti chako kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika taasisi na mashirika ya umma kwa madhumuni ya kupata tija ya uwekezaji na kuboresha ustawi wa jamii kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wangu wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya

Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa mno. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima yakuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua wajumbe hao majina yao ni kama yalivyooneshwa kwenye taarifa ya Kamati, kutokana na changamoto ya muda naomba nisiyasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuishukuru Ofisi ya Msajili wa Hazina inayoongozwa na Ndugu Nehemiah Mchechu, kwa ushirikiano wa dhati mlioutoa kwa Kamati na kushauri namna bora ya kuwezesha taasisi na mashirika ya umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija kwa Taifa na kupata chumo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa ushirikiano wa hali ya juu walioutoa ikiwa ni pamoja na kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati mpaka sasa ninapowasilisha taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, hoja, taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma unaofanywa na taasisi na mashirika ya umma. Maoni na mapendekezo yanatokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati yanalenga kuishauri Serikali katika eneo la uwekezaji na mitaji ya umma ili uwekezaji huo uwe wa ufanisi na ulete tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likubali kupokea taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa

mitaji ya umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kuijadili ili kuamua na kuiwezesha Serikali kufanyanyia kazi Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Kicheko)*

## TAARIFA YA KAMATI YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KUHUSU UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutujaalia uhai kuweza kufika siku ya leo. Kutokana na ufinyu wa muda naomba taarifa hii yote kama inavyosomeka katika kitabu cha Kamati iingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamatiya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (*PIC*) kuhusu Uwekezaji wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kuliomba Bunge likubali kuipokea na kuijadili.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inalenga kuliarifu Bunge lako Tukufu juu ya Mwenendo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Serikali ili kuliwezesha kujadili na kutoa maazimio yanayoendana na utekelezaji jukumu lake la kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuboresha ustawi wa jamii.

**Mhesimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu **nne** ambazo ni Sehemu ya Utangulizi, sehemu ya ufafanuzi wa shughuli za ufuatiliaji wa mitaji ya umma, sehemu ya maoni na mapendekezo na Sehemu ya hitimisho. Aidha, njia zilizotumiwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati ni kama zilivyobainishwa katika taarifa ya Kamati.

## UFAFANUZI WA SHUGHULI ZA KAMATI KUFUATILIA MITAJI YA UMMA

**Mheshimiwa Spika**, Bunge limepewa nafasi muhimu ya usimamizi wa shughuli za umma ikiwemo uwekezaji wa mitaji ya umma. Ili Bunge lichukue nafasi yake ya usimamizi unaostahili, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, hufuatilia mwenendo na masuala ya mitaji ya umma kwa lengo la kutoa taarifa na mapendekezo kwa Bunge. Kwa msingi huu, sehemu hii inaripoti shughuli zilizofanyika katika kufuatilia ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma.

## HALI YA JUMLA YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** hali ya jumla ya uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inaonesha kuwa thamani ya mitaji ya umma katika mashirika, taasisi za umma na kampuni mbalimbali ni **shilingi trilioni 75.79**. Uwekezaji huu ni sawa na ongezeko la asilimia 3 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **trilioni 73.36** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kiasi hicho cha mtaji kimewekezwa kwenye maeneo makuu mawili, eneo ambalo Serikali ina hisa asilimia 51 au zaidi na ambalo Serikali ina hisa chache (asilimia 50 au pungufu).

## TATHMINI YA UFANISI WA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** tathmini ya ufanisi ilifanyika kwa kuzingatia vigezo maalum wakati wa kufuatilia uwekezaji. Vigezo hivyo ni pamoja na Kiasi cha gawio; Kiasi cha michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi; Kiasi cha michango kutokana na makusanyo ya ziada na michango mingine; na Vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina. Vigezo hivyo ni viashiria vinavyosaidia kubaini, iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma unafanyika kwa ufanisi na kuwa umezingatia miongozo mujarabu.

## HALI YA JUMLA YA MAKUSANYO

**Mheshimiwa Spika,** mapato ya Serikali kutokana na uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni shilingi **trilioni 1.008**. Kiasi hiki ni jumla ya mapato kutokana na mitaji kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa kubwa na ambazo Serikali ina hisa chache. Mchanganuo wa makusanyo haya ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 01 la Taarifa hii. Uchambuzi wa jumla unaonesha kuwa:

i) Kwa ujumla mapato yasiyo ya kikodi kwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia 19 ikilinganishwa na mwaka 2021/2022. Katika ongezeko hilo ziada na michango mingineyo imeongezeka kwa kiwango cha asilia 173.

ii) Kiasi cha michango iliyopokelewa kutokana na asilimia 15 ya mapato ghafi ya taasisi zilizostahili kuchangia pamoja na wasilisho la TTMS, kila kimoja kiliongezeka kwa asilima 7;

iii) Mapato ya gawio kwa mwaka 2022/2023 yamepungua kwa asilimia asilimia 8, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, gawio lilichukua sehemu kubwa ya mapato yasiyo ya kikodi kwa kufikia asilimia 42. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 mchango wa gawio katika mapato ulipungua kufikia asilimia 33 ya mapato yasiyoya kikodi yaliyokusanywa.

iv) Mwaka wa fedha 2021/2022 ziada na michango mingineyo ilichangia mapato yasiyo ya kikodi kutokana na mitaji ya umma kwa asilimia 12 tu. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mchango wake uliongezeka na kufikia 34 ya mapato yasiyo ya kikodi kutokana na mitaji wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliainisha uwekezaji wa Serikali katika taasisi ambako ina hisa chache na uwekezaji katika taasisi ambako ina hisa nyingi kama ifuatavyo:-

**a) Uwekezaji kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa chache**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za uwekezaji zilionesha kuwa thamani ya hisa za Serikali katika taasisi ambazo Serikali ina hisa chache ilitofautiana kwa miaka miwili. Aidha, idadi ya kampuni au taasisi ilitofautiana kwa mwaka 2022/2023 na 2021/2022. Wakati kwa mwaka 2021/2022 Serikali ilikuwa na hisa chache kwenye taasisi 50, mwaka 2022/2023 Serikali ilikuwa na hisa chache kwenye taasisi 56 Ongezeko hilo la taasisi ni asilimia 12.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa kiasi cha gawio kilichopokelewa na Serikali ulionesha kuwa kuna tofauti kati ya mwaka 2022/2023 na mwaka 2021/2022. Kwa mwaka 2022/2023, Serikali ilipokea gawio la kiasi cha shilingi Bilioni 231.2 kutoka taasisi 15 kati ya 56 na mwaka 2021/2022 Serikali ilipokea kiasi cha Shilingi Bilioni 204.37 kutoka taasisi 14 kati ya 50.

Mchanganuo bayana unaonekana katika Jedwali Na. 01. Ambapo;

i) Idadi ya Taasisi ambazo Serikali ina hisa chache iliongezeka kwa asilimia 12 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023;

ii) Thamani ya hisa za Serikali kwenye Taasisi au Kampuni ambapo Serikali ina hisa chache iliongezeka kwa asilimia 9 ikilinganishwa na mwaka 2021/2022; na

iii) Kiasi cha gawio kilichopokelewa na Serikali kwa mwaka 2022/2023 kiliongezeka kwa asilimia 13.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo zinatoa maelezo ya ufanisi wa mitaji ya umma kwa namna tofauti. Kwanza, inaonesha kuwa juhudi za Serikali kuwekeza katika kampuni zinazolipa faida zinaongezeka. Ushahidi wa hili ni ongezeko la idadi ya taasisi ambazo Serikali inawekeza na ongezeko la thamani ya hisa za Serikali ikilinganishwa na mwaka 2021/2022. Eneo lingine ni kwenye ulinganisho kati ya ongezeko la thamani ya hisa na ongezeko la kiasi cha gawio. Wakati thamani ya hisa imeongezeka kwa asilimia 9, kiasi cha gawio kimeongezeka kwa asilimia 13. Kwa maneno mengine ongezeko dogo kwenye thamani ya hisa limesababisha ongeko kubwa la gawio.

**b) Uwekezaji kwenye taasisi na Mashirika ambazo Serikali ina hisa nyingi**

**Mheshimiwa Spika,** ufanisi wa mtaji wa umma kwenye mashirika, kampuni au taasisi ambazo Serikali ina hisa nyingi unaweza kupimwa kwa kuangalia mapato yasiyo ya kikodi yanayojumuisha gawio, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi na ziada na michango mingineyo. Upimaji huo unafanyika kwa kulinganisha mchango wa taasisi hizo katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa miaka miwili tofauti ya uwekezaji. Kwa urahisi wa ufafanuzi, Jedwali Na. 03 linaonesha taswira ya ufanisi. Ambapo,

i) Serikali imeongeza idadi ya Mashirika, Kampuni na Taasisi ambazo ina hisa nyingi kutoka 248 mwaka 2021/2022 hadi 250 mwaka 2022/2023; na

ii) Thamani ya hisa kwenye maeneo ya uwekezaji ambayo Serikali ina hisa nyingi imeongezeka kutoka shilingi trioni 70.8 mwaka 2021/2021 hadi shilingi trilioni 72.97 mwaka 2022/2023.

## i) Gawio

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/23 kiasi cha gawio kilichokusanywa kutoka katika mashirika ya umma ambayo Serikali inaumiliki wa hisa nyingi kilikuwa **shilingi bilioni 109**, kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia 47.4 ulilinganisha na kiasi cha gawio kilichokusanywa kutoka katika taasisi hizi kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambapo gawio lilikuwa **shilingi bilioni 207.2**. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kiasi cha gawio kilichokusanywa kutoka katika mashirika yanayojiendesha kibiashara kilichangiwa na mashirika 9 kati ya 33 yanayopaswa kuchangia, sawa na asilimia 27.3 ya Mashirika yaliyotoa gawio kupitia kipengele hiki. Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali iimarishe mikakati ya kuyasimamia mashirika haya ili kuhakikisha yanajiendesha kwa ufanisi na kupata faida ili yaweze kutoa gawio. Aidha, Serikali iweke mifumo ya uwajibishaji kwa ambao hawatekelezi agizo hili la kisheria.

## ii) Michango ya Asilimia 15 ya Mapato ghafi

**Mheshimiwa Spika**, Michango ya Asilimia 15 ya mapato ghafi imeonesha ufanisi wa mitaji ya umma kwenye taasisi stahiki. Kwa mwaka 2020/2021 makusanyo yalikuwa ni Sh. Bilioni 202.2, mwaka 2021/2022 yalikuwa shilingi Bilioni 324 na mwaka 2022/2023 yalikuwa ni shilingi Bilioni 346.3. Mwenendo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Na. 04.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu hizo zinaonesha kuwa, ufanisi wa ukusanyaji wa michango ya 15% ya mapato ghafi umekuwa ukiongezeka ambapo kwa mwaka 2021/22 uliongezeka zaidi kwa asilimia 37.5 na mwaka 2022/2023 uliongezeka kwa asilimia 6.4. Hivyo, kwa ujumla wake ufanisi umeongezeka. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini pia, pamoja na ufanisi wa michango hii kuongezeka mwaka 2022/23 lakini idadi ya taasisi zilizochangia zilipungua kutoka taasisi 25 mwaka 2021/22 hadi taasisi 23 mwaka 2022/23 kati ya taasisi 28 zinazopaswa kuchangia chini ya kipengele

hiki. Kwa maneno mengine ni kwamba kipengele hiki bado hatujakitumia kwa ukikamilifu, kama kitasimamiwa kikamilifu na taasisi na mashirika yote yakachangia kwa mujibu wa sheria, Serikali itapata mapato mengi zaidi kupitia kifungu hiki.

### iii) Ziada na Michango mingineyo

**Mheshimiwa Spika**, kipengele cha ziada na michango mingineyo kinajumuisha asilimia 70 ya ziada ya mapato inayotokana na shughuli kwa taasisi zinazotoa huduma, michango ya hiyari na mapato yanayotokana na shughuli za ufuatiliaji zinazofanywa na Msajili wa Hazina. Kwa mwaka wa fedha 2022/23 kipengele hiki kimekuwa na ufanisi ambapo jumla ya **shilingi bilioni 287.2** zilikusanywa kiasi ambachi ni ongezeko la aslimia 63.4 ukilinganisha na kiasi cha **shilingi bilioni 105** kilichokusanywa mwaka 2021/22.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umabaini kuwa, Mwaka 2021/2022 kiasi cha michango ya ziada na michango mingineyo kiliongezeka kwa asilimia 63.4 ambacho ni kiasi kikubwa. Aidha, idadi ya taasisi zilizochangia kwa kwaka 2022/23 zimepungua kwa asilimia 25.8 ingawa mchango umeongezeka. Ni dhahiri kwamba taasisi na mashirika ya umma yakisimamiwa kikamilifu na kuongeza ufanisi wake yanaweza kuongeza mchango wake katika mfuko wa Serikali na tija hasa ya uwekezaji mkubwa uliofanya na Serikali ikaweza kupatikana.

## MAMBO YA JUMLA KUHUSU UENDESHAJI WA MITAJI YA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu 11(1)(b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2023 kinaipa Kamati jukumu la kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilibaini mambo mbalimbali ya kiutendaji kama ifuatavyo:-

### 1.1.1 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini

**Mheshimiwa Spika,** moja ya kigezo cha utendaji ambacho taasisi na mashirika ya umma wamewekewa na Msajili wa Hazina ni kuhakikisha utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini unapungua mwaka hadi mwaka. Kwa mujibu wa taarifa ya utendaji wa Msajili wa hazina kwa Mwaka wa fedha 2022/2023 utegemezi wa Ruzuku umeongezeka ambapo kwa miaka mitatu mfululizo umekua kwa asilimia 21.2 kutoka **shilingi bilioni 13.234 m**waka 2021/2022 hadi kufikia **shilingi Bilioni 17.456** mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna mashirika Sitini na Tatu (63) ambayo kutokana na uendeshaji wa shughuli zake yanapata mapato makubwa kuliko ruzuku wanayopokea kutoka Serikalini lakini bado yanapokea Ruzuku kutoka Serikalini. Ni vema Mashirika haya yakasimamiwa kikamilifu kuhakikisha yanatekeleza majukumu yake kikamilifu, yanakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato na yanadhibiti matumizi yake kisha yapewa mpango wa kujiondoa kwenye utegemezi wa ruzuku.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini pia katika ya mashirika Thelethini na Tano (35) yanayojiendesha kibiashara, mashirika Kumi na Saba (17) yanapokea ruzuku kutoka Serikalini. Mashirika haya yanapaswa kuongeza ufanisi, kutumia fursa zilizopo sokoni ili kuongeza mapato yake na hatimaye kujitoa katika utegemezi wa ruzuku.

Aidha, Kamati ilibaini utegemezi wa Ruzuku ya matumizi mengineyo pamoja na mishahara umeongezeka pia, ambapo kwa mujibu wa taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2022/23 imeeleza kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo utegemezi wa matumizi mengineyo na mishahara umeongezeka kutoka **shilingi bilioni 793.58** mwaka 2021/22 hadi **shilingi trilioni 1.33**

Mwaka 2022/23, ongezeko hili ni sawa na **asilimia 40.64** ambalo ni ongezeko kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, mategemeo ya Serikali kuanzisha taasisi na mashirika ya umma ni pamoja na yajiendeshe kwa ufanisi, yatoe huduma stahiki kwa wadau wake ili yaweze kutengeneza faida na hatimaye kuweza kujitegemea katika uendeshaji wake kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iyasimamie kikamilifu na kuyawekea mpango muda mfupi na wakati wa kujitoa kwenye utegemezi wa ruzuku ili kuipunguzia Serikali mzigo.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina inahitajika kuongeza juhudi katika kufanya marekebisho/maboresho katika taasisi husika. Maboresho haya yahusishe kuimarisha vyanzo vya mapato pamoja na mifumo ya ukusanyaji wa mapato; na kurekebisha gharama za uendeshaji ili kuhakikisha mapato, matumizi na ufanisi wa taasisi vinaendana; na kuboresha mbinu na mikakati ya biashara kwa mashirika yanayojiendesha kibiashara ili yaweze kushindana katika soko na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

### 1.1.2 Tathimini ya Utendaji wa taasisi na Mashirika ya umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha mitaji katika mashirika na taasisi za umma inasimamiwa ili kuleta tija. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna baadhi ya taasisi na mashirika na wakala za Serikali utendaji wake unasuasua, jambo ambalo linaathiri tija ya uwekezaji wa mtaji wa umma. Mambo yaliyobainika katika uchambuzi wa Kamati ni kama ifuatavyo:-

**i) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yamepata hasara au nakisi kwa miaka mitatu mfululizo**

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yamepata hasara /nakisi katika kipindi cha miaka miwili mfululizo. Hali hii inatokana na Bodi na menejimenti za taasisi hizo kuwa na usimamizi usioridhisha na hivyo kusababisha kukosekana kwa ufanisi, ikiwemo kutokuwa na ubunifu katika kuendeleza vyanzo vilivyopo vya mapato na vilevile kushindwa kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuhakikisha utendaji wa taasisi unakuwa na tija. Mfano wa taasisi hizo ni pamoja na Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL, (TTCL), Bodi ya Mkonge (TSB), Shirika la Masoko ya Kariakoo (KMC), Mamlaka ya Elimu ya Juu n.k Hali ya kupata hasara mfululizo inaleta mashaka katika uendelevu wa taasisi na inaweza kusababisha malengo ya uanzishwaji wa taasisi hizi kutofikiwa. Hivyo, kuna umuhimu wa utendaji wa taasisi hizi ukatathiminiwa upya kwa lengo la kuboresha utendaji ili kuleta tija ya uwekezaji.

**ii) Hali mbaya ya Ukwasi kwa baadhi ya taasisi na mashirika ya Umma.**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini baadhi ya taasisi na mashirika ya umma kutokuwa na ukwasi wa kutosha hali ambayo umesababisha mashirika mengi kujiendesha kwa madeni kutokana na kutumia huduma za wazabuni bila kulipia. Mfano wa mashirika ya umma ambayo kwa miaka mitatu mfululizo yamekuwa yakizalisha madeni ni pamoja na (TTCL), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), (TFRA), Bodi ya Mkonge Tanzania n.k.

**iii) Baadhi ya taasisi na Mashirika ya umma kushindwa kutumia fursa walizo nazo**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi pia umebainisha kwamba, baadhi ya mashirika ya umma pamoja na uwepo wa ushindani na sekta

binafsi bado yana fursa kwenye ushindani kutokana na majukumu yao lakini hayajaweza kutumia fursa hizo kikamilifu. Mashirika hayo ni pamoja na TTCL kwenye soko la mawasiliano ambapo kuna fursa kupitia mradi wake mkubwa wa fibre mlangoni. Ranchi ya NARCO kwenye soko la uzalishaji wa mifugo na mazao yake; CPB kwenye soko la nafaka; na Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) kwenye masuala ya uvuvi kibiashara. Mashirika haya ni yale yanayojiendesha kibiashara, ni vema Serikali ikatathimini uendeshaji wa mashirika haya na kuyawezesha kwa maeneo ambayo ni kikwazo kwayo ili yaweze kujiendesha kiukamilifu na kuweza kushindana katika soko na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

**iv) Baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yana Upungufu wa mtaji wa uendeshaji**

**Mheshimiwa Spika,** uchambazi wa Kamati ulibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mtaji wa uendeshaji jambo linaloathiri utendaji wa shirika husika. Changamoto hii imepelekea taasisi na mashirika ya umma hayo kujiendesha kwa kutumia mtaji kidogo au hasi kabisa jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi, mfano wa taasisi hizo ni pamoja na (TTCL), Bohari ya Dawa (MSD), Benki ya Maendeleo TIB.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia mapato ya Serikali ukilinganisha na mahitaji ya fedha ni vema taasisi na Mashirika ya umma yaliyo na fursa za kuwekezaji yaelekezwe kutumia njia mbadala za upatikanaji wa fedha kama vile kushirikisha Sekta Binafsi (Public Private Partnership - PPP), Mikopo kutoka taasisi za fedha, na vilevile kutumia fursa ya upatikanaji wa fedha kupitia soko la hisa ambapo mashirika yanaweza kuuza hisa au kuuza hati fungani (bond) kwenye soko kwa lengo la kupata mitaji ya utekelezaji wa shughuli zao na hatimaye kuweza kupunguza utegemezi wa Ruzuku.

### 1.1.3 Baadhi ya Miradi ya Uwekezaji kuanza kabla ya kukamilika kwa maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, baadhi ya miradi ya maendeleo imekuwa ikianzishwa kabla ya kukamilisha maandalizi yote ya msingi ikwemo kufanya upekuzi wa kina wa wakandarasi na kufanya maandalizi ya fedha jambo ambalo limekwamisha miradi hii ya uwekezaji kuweza kukamilika kwa wakati. Aidha, kwa baadhi ya miradi, taasisi na mashirika ya umma yamekuwa yakisaini mikataba ya utekelezaji na Wakandarasi kabla ya kukamilisha maandalizi ya fedha hivyo kupelekea miradi kuchelewa kuanza na hivyo kunasababisha kuzalishwa kwa riba za ucheleweshaji na hivyo kuongeza gharama za utekelezaji wa mradi.

Vile vile, Kamati ilibaini, kuna baadhi ya miradi imeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na wakandarasi waliokabidhiwa miradi kutokuwa na sifa za kutosha. Mfano ni Mradi wa ujenzi wa vituo vya pamoja vya vya ukaguzi vya Manyoni na Nyakanazi unaotekelezwa na Wizara ya Fedha na kusimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kupitia fedha za ufadhili takribani EURO milioni 19.21 ambapo ufadhili huu ulitoka Nchi za Umoja wa Ulaya na malipo yalifanyika kwa kuzingatia hatua za utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika**, mradi alikabidhiwa mkandarasi M/S Impresa ambaye alifilisika miaka miwili (2) mara baada ya kukabidhiwa mradi. Mkandarasi huyu alitekeleza mradi huu kwa asilimia 60 (Manyoni) na asilimia 50 (Nyakanazi). Tafsiri ya jambo hili ni kuwa mkandarasi huyu hakufanyiwa upekuzi wa kina ili kubaini uwezo wake halisi hususani kipengele cha uwezo wa kifedha. Matokeo yake ni mkandarasi kushindwa kukamilisha kazi yake kwa wakati na pia kufilisika hivyo hataweza kukamilisha kazi yake. Aidha, jambo hili limesababisha msaada uliokuwa umepatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi hii kukoma (kusitishwa) kwa kuwa malipo

(disbusment of fund) yalitegemea hatua za utekelezaji wa mradi, kwa hiyo kufilisika kwake kumepelekea kusitishwa kwa msaada na hivyo miradi hii imesimama kwa takribani miaka sita sasa.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kuwa kwa taasisi zinazotekeleza miradi ya uwekezaji ni vema zifanye maandalizi yote ya awali ikiwemo kujiridhisha juu ya upatikanaji wa fedha, upekuzi wa wakandarasi na uzingatiaji wa mikataba ya utekelezaji wa miradi kwa lengo la kuhakikisha miradi wanayotekeleza inakamilika kwa wakati na kuiepusha Serikali na mizigo ya gharama zisizo za msingi zinazotokana na riba.

### 1.1.4 Gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijiji-miji

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa ya uwekezaji ya Wakala wa Nishati vijijini, uchambuzi wa Kamati uliibaini kuwa tija ya uwekezaji katika miradi ya REA katika maeneo yenye mwonekano wa vijiji-miji ni ndogo, kwani kasi ya uwekezaji uliofanywa wa kusambaza huduma katika maeneo hayo imekuwa kubwa ikilinganishwa na kasi ya uunganishaji wa wananchi katika maeneo hayo. Hii ni kutokana na uwezo mdogo wa vipato vya jamii ya maeneo hayo ambao nao wanatozwa gharama sawa na maeneo yenye hadhi za miji au majiji hivyo wanachi wa maeneo hayo wanashindwa kuunganisha umeme na hivyo kushusha ufanisi na tija ya uwekezaji unaofanywa na Serikali katika sekta kwani ni watu wachache sana wanaojiunga katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia jambo hili Kamati ilielezwa kuwa, Serikali inaendelea na mchakato wa kutathmini bei halisi na stahiki zinazopaswa kutozwa katika maeneo yenye sifa hizo ili kuwezesha walengwa kuweza kujiunga na huduma ya umeme kulingana na uwezo wao halisi wa kipato na kiuchumi. Pamoja na maelezo yaliyotolewa Serikali, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mchakato huo umechukua muda mrefu jambo linaloendelea

kuathiri ufanisi wa mtaji na kushusha tija ya uwekezaji iliyofanywa na Serikali kwenye miradi ya REA kwa maeneo hayo.

### 1.1.5 Changamoto katika utendaji wa Mamlaka za Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

**Mheshimiwa Spika**, Jukumu la mamlaka za hifadhi ni Kuendeleza uhifadhi wa maliasili na malikale pamoja na kuendeleza utalii. Utekelezaji wa majukumu haya ni moja ya sababu inayopelekea kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii nchini. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa katika kutekeleza majukumu yake Mamlaka hizi zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya utekelelazaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia janga la UVIKO-19, Taasisi za NCAA na TANAPA ziliathirika ikiwa ni matokeo ya athari za janga hilo, na hivyo Serikali katika kunusuru uendeshaji wa Taasisi hizo ilifanya marejeo ya ukusanyaji mapato na kuanza kuzipa ruzuku Taasisi hizi katika kipindi ambacho sekta ya utalii ilikuwa imeathirika. Aidha, kutokana na kurejea kwa utalii kwa nguvu zilizowekwa na Serikali ikiongozwa na Rais wa JMT, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, idadi ya watalii imeongezeka na hivyo, Taasisi hizi sasa kwa mapato ambayo yanakusanywa zinaweza kujitegemea kujiendesha lakini bado utaratibu wa makusanyo yao kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wao kupokea ruzuku kwa ajili ya kujiendesha unaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, awali taasisi ya NCAA na TANAPA waliweza kukusanya mapato yao na kuyatumia kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mamlaka ikiwemo kuboresha miundombinu kwa wakati pindi inapohitajika na kufanikisha utekelezaji wa jukumu zima la utalii na kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria. Kutokana na mabadiliko yaliyofanywa kutokana na athari za UVICO-19 Mamlaka hizi zinalazimika kusubiri mgao wa

ruzuku kutoka Serikalini jambo ambalo kwa kiasi kikubwa linakwamisha utendaji wa Mamlaka kwani fedha hizi zimekuwa haziendi kwa wakati stahiki kwani misimu ya utalii huanzia mwezi Julai hadi Septemba. Lakini pia bajeti wanazotengewa zimekuwa ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya mamlaka jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu yake hususani miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** ufinyu huu wa bajeti pamoja na ucheleweshaji wa fedha kwa taasisi hizi umeathiri pia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwa upande wa NCAA athari za ucheleweshaji wa fedha za miradi zimepelekea wakandarasi kudai riba za ucheleweshaji kwa miradi miwili (ujenzi wa jengo la Makao makuu ya Mamlaka pamoja na ujenzi wa Barabara ya View Point) kiasi cha jumla ya shilingi milioni 219.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini kuwa mapato halisi yatokanayo na shughuli za utalii katika hifadhi hizi ni makubwa lakini bajeti inayoidhinishwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za hifadhi hizi ni ndogo haiakisi mahitaji halisi ya malmaka hizi jambo linaloathiri utendaji kazi wa hifadhi hizi. Aidha, Kamati imebaini kuwa changamoto ya miundombinu ya Barabara pamoja na vyoo imekuwa kikwazo kwa watalii hususani watalii kutoka nje ya nchi jambo linalopunguza idadi ya watalii hususani returning visitors hivyo kuathiri mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, taasisi za NCAA na TANAPA ni kati ya taasisi ambazo zilikuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa katika mfuko Mkuu wa Serikali kabla ya kuathiriwa na janga la UVICO -19, Juhudi kubwa za Serikali zimefanyika na hatimaye taasisi hizi zimeweza kurudi katika hali ya awali ya uzalishaji wa mapato licha ya kukabiliwa na changamoto zilizobainishwa hapo juu. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali kutafakari ufumbuzi wa jambo hili na taasisi hizi za kimkakati kuruhusiwa kukusanya mapato yake ili ziweze kuwa na ukwasi muda wote na kuwawezesha kutekeleza majukumu yake hususani jukumu

la ujenzi na ukarabati wa miundombinu za mamlaka ili kuziwezesha kuwa na ufanisi na kuweza kuhudumia watalii kwa ufanisi zaidi.

## MAONI NA MAPENDEKEZO

## MAPENDEKEZO

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni tegemeo la Bunge katika kufuatilia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Serikali kwa lengo la kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuisimamia na Kuishauri Serikali kuhusu uwekezaji inaoufanya na Serikali. Kutokana na uchambuzi na ufuatiliaji uliofanywa na Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati ambayo kwa maoni ya Kamati, iwapo Bunge litaridhia yanakusudia kutatua changamoto zilizopo katika uwekezaji wa mitaji ya Umma na hatimaye kuongeza ufanisi wa Uwekezaji mkubwa uliofanya na unaoendelea kufanywa na Serikali.

### 1. Kuhusu Uchangiaji katika Mfuko Mkuu wa Serikali

Bunge linaazimia kwamba:

i) Serikali iweke utaratibu wa kuziwajibisha Bodi na Menejimenti za Taasisi na Mashirika ya Umma yanayoshindwa kutekeleza kigezo hiki cha kisheria cha kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali; na

ii) Serikali kupitia Msajili wa Hazina iongeze usimamizi kwa Taasisi na Mashirika ya umma kuhakikisha yanaimarisha utendaji wake kwa lengo la kuongeza mapato yake na kuongeza mchango wake katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**2. Kuhusu Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini**

Bunge linaazimia kwamba, Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

i) kufanya upembuzi wa Mashirika yanayotegemea ruzuku na kuyawekea mipango ya kupunguza utegemezi hususani katika kipengele cha mishahara na matumizi mengineyo (OC); na

ii) Kusimamia Taasisi na Mashirika ya umma yanayotegemea ruzuku kuhakikisha yanatafuta njia mbadala za kupata rasilimali ikiwemo kutumia mikopo nafuu na kushirikisha sekta binafsi (Public Private Partnership-PPP) katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ya kibiashara na vilevile kutumia fursa ya upatikanaji wa fedha kupitia soko la hisa kwa kuuza hisa na hati fungani kwa lengo la kupata mitaji ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi hiyo.

**3. Kuhusu Tathimini ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma**

Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina kufanya mapitio ya Taaasisi na Mashirika ya umma kwa lengo la kubainisha changamoto wanazokabiliana nazo na kuweka mpango mahususi wa kutatua changamoto hizo ili taasisi husika ziweze kuongeza ufanisi wake na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

**4. Kuhusu Upungufu wa Mtaji kwa Benki ya Maendeleo TIB**

Bunge linaazimia kwamba, Serikali kuongeza mtaji kwa benki ya maendeleo TIB ili kukidhi matakwa ya sheria ya Benki Kuu (BOT) na kumudu ushindani kwenye soko kwani ni muhimu benki hii ikaendelea kuwepo ili itekeleze malengo ya uanzishwaji wake.

**5. Kuhusu Ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi**

Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina kusimamia kikamilifu taaasisi na mashirika ya umma kuhakikisha wanakamilisha maandalizi yote ya awali kabla ya kuingia mikataba ya utekelezaji wa miradi husika kwa lengo la kuepusha kuiongezea Serikali mzigo utokanao na ulipaji wa riba za ucheleweshaji.

**6. Kuhusu Wakandarasi wasiokuwa na vigezo kupewa kazi za utekelezaji wa miradi. (Mheshimiwa Spika, naomba kufanya maboresho kwenye pendekezo hili, badala ya linavyosomeka kwenye taarifa iliyowekwa mezani leo asubuhi naomba lisomeke kama ifuatavyo)**

Bunge linaazimia kwamba, Serikali isimamie kikamilifu taasisi na mashirika ya umma yanayotekeleza miradi ya uwekezaji ili kuhakikisha yanafanya upekuzi wa kina na kujiridhisha juu ya uwezo wa wakandarasi wanaokabidhiwa miradi hiyo kwa lengo la kujiepusha na changamoto katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo changamoto ya miradi kutokamilika kwa wakati.

**7. Kuhusu Gharama za kuunganisha umeme kwa maeneo ya vijiji – miji**

Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Mamlaka zake zinazohusika ihakikishe inaharakisha kukamilisha tathmini za gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya namna hiyo na kubainisha majina ya maeneo na gharama ndani ya miezi sita ili kuongeza ufanisi wa mtaji uliowekezwa katika miradi hii. Jambo hili litapelekea kukamilisha azma ya Serikali ya kupeleka nishati ya gharama nafuu vijijini kwa lengo la kukuza Uchumi na kuboredha hali ya maisha ya wanachi wa vijijini.

**8. Kuhusu Uzingatiaji wa vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina**

Bunge linaazimia kwamba,

i) Msajili wa Hazina afanye marejeo ya vigezo vya utendaji na kuvipanga kwa Taasisi kwa kulingana na uhalisia wa majukumu ya Taasisi au Shirika husika;

ii) Kuzisimamia Taasisi na Mashirika ya umma kuhakikisha zinajiendesha ndani ya vigezo vya utendaji ilivyopatiwa kwa lengo la kuleta ufanisi na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana; na

iii) Kuweka utaratibu wa kuwachukulia hatua stahiki Bodi na Menejimenti za Taasisi zinazoshindwa kutekeleza vigezo vya utendaji walivyopatiwa.

**9. Kuhusu Changamoto katika utendaji wa Mamlaka za Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)**

Bunge linaazima kwamba, Serikali irejeshe utaratibu wa zamani wa taasisi ya NCAA na TANAPA kukusanya mapato yake kwa lengo la kuwawezesha kuwa na ukwazi muda wote ili waweze kufanya maendeleo ya maeneo wanayosimamia kwa wakati na kuongeza ufanisi wa Taasisi hizi muhimu katika Tasnia ya Maliasili na Utalii.

**10. Kuhusu Ujenzi na uendeshaji wa Stendi ya Msamvu**

Bunge linaazimia kwamba, Serikali irudishe uendeshaji wa stendi ya Msamvu kwa Mfuko wa PSSSF ili mradi husika utumike kurejesha gharama za uwekezaji na baada ya Mfuko kurudisha gharama za uwekezaji stendi itarejea kuwa mali ya Manispaa ya Morogoro. Jambo hili pia litaipunguzia Serikali mzigo wa kulipa gharama za uwekezaji zilizotolewa na Mfuko wa PSSSF.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo, ushauri na miongozo ya kiti chako kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee napenda kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma kwa madhumuni ya kupata tija ya uwekezaji na kuboresha ustawi wa jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao, majina yao ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati, kutokana na changamoto ya Muda naomba nisiyasome.

**Mheshimiwa Spika**, Vilevile, napenda kuishukuru Ofisi ya Msajili wa Hazina inayoongozwa na Ndugu Nehemia Mchechu kwa ushirikiano wa dhati mlioutoa kwa Kamati na kushauri namna bora ya kuwezesha Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija kwa Taifa na kupata chumo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Baraka

Ildephonce Leonard kwa ushirikiano wa hali ya juu walioutoa ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati mpaka sasa ninapowasilisha taarifa hii ya Kamati.

**Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati yanalenga kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo uwe wa ufanisi na ulete tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likubali kupokea Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kuijadili ili kuamua na kuiwezesha Serikali kuyafanyia kazi maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa wasilisho hilo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wetu ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia, lakini kwa kuangalia muda wetu huenda atafanikiwa Mbunge mmoja ama wawili. Tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, ikiwa muda utatutosha atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kabla sijaanza mchango wangu naomba kusema mambo machache. Nakupongeza kwa dhati kwa namna unavyotekeleza wajibu wako katika Umoja wa Mabunge Duniani; moja ya sifa ya kiongozi mahiri ni kusema ukweli wa mambo magumu kwa ujasiri, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtaalam wa uchumi wa Marekani Profesa Rostain, aliwahi kusema linalotofautisha nchi zilizoendelea na zinazoendelea ni jambo moja tu, udhibiti na matumizi sahihi ya fedha za umma katika kuleta maendeleo ya wananchi. Nimeona nianze na jambo hili kutokana na umuhimu wa hoja iliyopo mbele yetu katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, unaposikiliza kwa makini taarifa za wenyeviti kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, utabaini kwamba kuna matumizi yasiyo sahihi katika fedha za umma. Kwa bahati mbaya matatizo tunayoyajadili leo yamekuwa yakijirudia kila mwaka. Kwa maoni yangu makosa haya hayatokani na ukosefu wa uweledi na ujuzi wa masuala ya kihasibu bali linatokana na udhaifu wa usimamizi na kutokufuatwa kwa maadili ya kazi.

Mheshimiwa Spika, mtaalam mmoja wa uongozi bwana Maxwell, aliwahi kusema maneno yafuatayo: "*Everything rises and falls on leadership*" kila kitu kinategemea uongozi, kwa hiyo mafanikio na udhaifu wa taasisi unatokana na uongozi. Ili kuondoa kasoro hizo nilizozibainisha hapo juu naomba nipendekeze mambo sita yafanyiwe kazi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, Serikali inapofanya uteuzi wake wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika yote na Taasisi zote za Umma izingatie taaluma, ujuzi, uweledi, uzoefu na tabia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, watendaji Wakuu wa Mashirika yote ya Umma wateuliwe kwa kuzingatia tabia zao, umahiri wao, uzoefu wao, elimu zao na mitazamo yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, Serikali iwapeleke Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi katika mafunzo ya kikazi nje ya nchi hasa katika mashirika makubwa sana ya kihasibu kwa mfano *Deloitte*, *KPMG*, *PricewaterhouseCoopers* na *Ernst & Young* ili wajifunze namna ya kuongoza mashirika na utamaduni wa kuendesha makampuni na mashirika ya umma ili yajiendeshe kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, hivi sasa tunayo Taasisi ya Uongozi Serikalini, ambayo ipo chini ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Kwa bahati mbaya taasisi hii haina majengo ya kudumu, haina wahadhiri wa kudumu, haina wataalam wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwa Serikali taasisi hii ihamishiwe Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili ipate kuwa na sehemu ya kufanyia kazi, wahadhiri wenye uwezo ili watoe mafunzo katika masuala mbalimbali, kwa mfano maendeleo ya uongozi na nitaeleza faida chache sana za taaluma ya maendeleo ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuelewa kufanya mipango, kuteua wafanyakazi na wataalam wenye uwezo, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo ya Taifa. Mtakumbuka chuo cha zamani cha Mzumbe kilikuwa kinafanya kazi nzuri sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tano, naiomba Serikali iimarishe mifumo yake hasa katika kutathmini utendaji wa mashirika, najua kazi hii imeshaanza kufanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, naomba kazi hii iendelee.

Mheshimiwa Spika, pendekezo langu la mwisho, Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa kuimarisha, wa kutekeleza agizo la kuimarisha matumizi ya mifumo ya kisasa katika shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ya bajeti imependekeza sio mara moja sio mara mbili, kwanza mifumo ya *TRA*, *TPA* pamoja na halmashauri za wilaya ziunganishwe pamoja na ziowane ili kudhibiti udanganyifu Serikalini na la pili, tumependekeza siyo mara moja, siyo mara mbili, Serikali ianzishe utaratibu wa matumizi ya mifumo ya kidijitali ili malipo ya Serikali yafanyike bila ya kutumia fedha tasilimu.

Mheshimiwa Spika, bila shaka utakubaliana na mimi kama mambo haya sita niliyoyataja yatasimamiwa, yatatekelezwa ipasavyo bila shaka tutapiga hatua kuliko hapa tulipo sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana! Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na uchangiaji mchana tutakaporejea, kwa hivyo wale wote waliomba kuchangia wajiandae kuchangia hiyo jioni. Tunaye Mheshimiwa George Natany Malima, yupo Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Aida Khenani na wengine kadri watakavyojitokeza.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu Zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023;**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2023; na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Alishatamkwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatia Mheshimiwa George Malima na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, ajiandae.

Mheshimiwa George Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, nianze na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uwekezaji mkubwa. Ameruhusu fedha nyingi

sana kwa ajili ya uwekezaji kwenye Mashirika na Taasisi mbalimbali za Serikali. Kwa hesabu za Mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali imewekeza zaidi ya shilingi trilioni 75.79 kwenye Mashirika mbalimbali ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* na katika uchambuzi wa Kamati yetu tumeangalia sana mashirika mbalimbali ambayo Serikali imewekeza mitaji, lakini tumeona baadhi ya mashirika utendaji wake wa kazi au uendeshaji wa mashirika hayo umekuwa ukisuasua sana. Jambo ambalo limeondoa kabisa tija ambayo tulikuwa tumeitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kutoa mfano wa mashirika hayo machache, yapo mengi lakini machache, mojawapo ni: Shirika la *TANOIL* hii ni Kampuni Tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC);* Shirika lingine ni *TTCL;* na lingine ni Bodi ya Mkonge. Haya ni mashirika ambayo uendeshaji wake umekuwa wa kusuasua sana. Kwa miaka mitatu mfululizo Mashirika haya yamekuwa yakitengeneza hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mashirika ya namna hii hayatufikishi kule ambako tulikuwa tunatarajia. Hayana uwezo wa kutoa mchango katika kuinua uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina iweke usimamizi wa karibu sana kwa mashirika kama haya ili lile lengo tulilokusudia, lengo ambalo Serikali na lengo ambalo Mheshimiwa Rais angetarajia la kuongeza uchumi wa Taifa letu liweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumeliona ni hali ya tegemezi wa ruzuku ya Serikali, Mashirika mengi bado yanategemea ruzuku hayawezi kujiendesha yenyewe. Hii inatokana na ukweli kwamba hayaendeshwi vizuri. Kuna udhaifu kwenye *management,* kuna udhaifu kwenye Bodi za Mashirika haya. Kwa

hiyo, mashirika haya yameendelea kutegemea Serikali bila ruzuku ya Serikali hayawezi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika hayo ambayo nimeyataja ni kati ya hayo ambayo yanaendelea kutegemea ruzuku ya Serikali. Ukiangalia Ripoti ya Msajili wa Hazina ya mwaka 2022/2023 inasema kwamba utegemezi wa mashirika mbalimbali umeongezeka ambapo kwa miaka mitatu mfululizo umekuwa kwa 21.2% kutoka shilingi bilioni13.2 mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi bilioni 17.4 kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali kuwekeza kwenye mashirika kama haya lilikuwa ni kwamba yaendeshwe vizuri ili ule utegemezi wa ruzuku uendelee kupungua kila mwaka. Sasa jambo hili limeshindikana baadhi ya mashirika yameshindwa kabisa kutekeleza utaratibu huu. Kwa hiyo, yameenda yanaendelea kupokea ruzuku na kusababisha mzigo kwa Serikali. Fedha ambazo zingeenda kufanya majukumu mengine zinaendelea kupelekwa kwenye mashirika kama haya ambayo kimsingi hayafanyi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza ningeshauri Serikali iangalie mashirika kama haya kama hayawezi kujirekebisha, kama hayawezi kufanya vizuri basi hakuna sababu ya kuendelea kuyapa ruzuku. Fedha hizi ambazo zinatolewa kwenye mashirika haya ziweze kufanya kazi nyingine za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa niaba ya Serikali isimamie kwa karibu mashirika haya ikiwezekana baada ya muda mfupi yajikwamue yaweze kujiendesha yenyewe bila kutegemea ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida nyingine ambayo tumeiona ni upungufu wa mitaji ya uendeshaji, yapo mashirika ambayo hayana fedha kabisa ya kujiendesha yanaendesha mashirika yao kwa madeni. Wanashindwa kabisa kulipa hata fedha za watoa huduma,

fedha za wakandarasi wao ni kwa sababu hawana mitaji na ningeweza kushauri ikiwezekana watafute njia mbadala. Zipo Taasisi za kifedha ambazo zinatoa mikopo, lipo soko la hisa, wanaweza kutumia utaratibu wa *PPP* wakaweza kupata mitaji ili waweze kujiendesha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika kama hayo ambayo nimesema hayana pesa kabisa yanaendeshwa kwa shida na kwa madeni ni pamoja na *TTCL, MSD* (Bohari ya Dawa), Benki ya maendeleo *(TIB)* na kuendelea. Mashirika haya hayana fedha yanaendeshwa kwa madeni, matokeo yake hatuwezi kupata ile tija ya uwekezaji ambayo ilikuwa imekusudiwa. Kwa hiyo, tunashauri wazingatie sana ikiwezekana watafute fedha katika vyanzo ambavyo nimevitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hali mbaya ya ukwasi kwa baadhi ya Taasisi hizi, hazina fedha kabisa. Taasisi kama hizi kama Serikali haiwezi kuwasaidia basi tujue kabisa haziwezi kuendelea. Ukiangalia hesabu zao wana mizigo ya madeni, wao wenyewe wapo hoi. Kwa hiyo, nadhani tusiendelee kuweka fedha nyingi kwenye mashirika kama haya ama tubadilishe *management* yake, tuweke watu wengine ambao wanaweza kuwa na uwezo wa kuendesha mashirika haya vizuri badala ya kuendelea kuwatumia wale wale ambao hawafanyi vizuri hilo ni jambo muhimu sana. Kupitia Ofisi ya *TR,* Serikali itafute *management* yenye uwezo, bodi zenye uwezo ili kusimamia mashirika haya ili yajiendeshe kwa faida na ile tija tunayo kusudia tuweze kuiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mashirika mengi ambayo yanaonekana kama yana mitaji mikubwa sana kwenye hesabu zao. Ukienda kuangalia hesabu kama ya *TTCL* utakuta ina mtaji mkubwa lakini kinazalishwa kutokana na hiyo mitaji ni kidogo sana. Unakuta ama wana majengo ambayo hayapangishwi, wana ardhi ambayo haijaendelezwa, wengine wana mitambo ambayo imepitwa na wakati kwa sababu ya mabadiliko ya teknolojia lakini

imeendelea kuonekana kwenye hesabu zao kwamba hawa watu wana mtaji mkubwa, lakini mitaji hiyo haizalishi kile ambacho kilitarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo wanaingia gharama ya uendeshaji, gharama ya kutunza hayo majengo, gharama ya kutunza viwanja kulipia kodi, gharama ya kutunza mitambo ambayo haiwezi kuzalisha tena. Kwa hiyo, ninashauri hatua zichukuliwe na mashirika haya ikiwezekana watunze au watumie mitaji ambayo inazalisha badala ya kuendelea kuingia hasara ya uendeshaji wa mitaji ambayo haifanyi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri sana jambo hili Serikali iliangalie kwa karibu kupitia Msajili wa Hazina, yale mashirika ambayo yana mitaji mikubwa haizalishi chochote ile mitaji ama iuzwe ili tusiendelee kuingia gharama ya kutunza majengo ambayo hayawezi kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa George Natany Malima.

Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatia Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hizi Kamati zetu zote tatu. Wakati Wenyeviti wa Kamati wanasoma taarifa zao hakuna Kamati hata moja haijazungumzia suala la madeni iwe kwenye taasisi, iwe kwenye halmashauri na Wabunge wanajua siku zote kwenye Bajeti za Wizara mbalimbali tumekuwa tukizungumzia suala la madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huu ni mwaka wangu wa 14 nikiwa humu Bungeni, haya mambo yamezungumzwa sana bado hatujaona jitihada za dhati za kukomesha madeni. Nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa aliyesoma kwenye Kamati ya *PAC* amezungumzia suala la deni la *TANESCO* tumelisema sana hili na tukasema hili Shirika mwisho wa siku linakuja kuwa muflisi na hiyo ni *TPDC* bilioni 713 bado madeni mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaenda kwenye Bajeti ya Wizara ya Maji tumezungumzia Serikali namna inavyodaiwa na mamlaka zake za maji na mimi nilichangia na tukasema hizi mamlaka zitashindwa kujiendesha. Leo kwenye taarifa hapa imesema, Mwenyekiti wa *PIC* amezungumzia hapa madeni mbalimbali na akatolea mfano, *TTCL,* POSTA, *NFRA* na maeneo mengine. Lazima tuwe na mipango madhubuti ya kuhakikisha tunashughulikia changamoto mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa upande wa Kamati ya *LAAC* madeni kwenye halmashauri ni bilioni 887, madeni ya wazabuni ni bilioni 38.233. Wazabuni wa nchi hii wamekuwa wakitembea kulalamika wanatakiwa walipwe. Wazabuni wa nchi hii ni wananchi wetu wanaotupa huduma. Sasa mtu anakuja kukuhudumia ubwabwa, anakuja kukujengea barabara unakaa zaidi ya miaka mitatu humlipi huyu mtu amekopa benki, umeenda kuweka mafuta *petrol station* humlipi zaidi ya miaka mitatu. Hebu sisi tuvae viatu vyao, siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni nani hapa atafanya biashara mtu aje amkope akae zaidi ya miaka mitatu asilipe? Kuna akina mamantilie, watu wanakopa benki wafanye kazi na halmashauri zao, wafanye kazi na Serikali yao, wachangie uchumi wa nchi yao tuwalipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye madeni ya watumishi yasiyo ya mshahara maana madeni ya malimbikizo ya

mishahara kwenye halmashauri ni takribani bilioni 11, marupurupu mengine ya watumishi bilioni 44 kwenye halmashauri. Hawa watumishi ndio tunatarajia tukipeleka pesa kwenye halmashauri zetu za miradi ya maendeleo ndiyo wasimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watumishi hawawezi kugoma wanagomea mioyoni. Ogopa sana mtu anafanya kazi kwa *stress* anadai mshahara mdogo halipwi kwa wakati. Halafu unamshushia trilioni ya shilingi, kwa nini tusitengeneze mazingira ya watu kuchukua rushwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunazungumzia Serikali ilipe madeni, halmashauri hizi zisimamiwe zilipe madeni ya watumishi. Sisi Kamati yetu wakija pale tunajua wana uwezo wa kudai ji-*commit* hapa ndani ya miaka miwili lipa madeni *and then* halmashauri kusanya, endelea kufanya kazi za maendeleo. Hivi vitu si vizuri, havileti picha nzuri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na suala la madeni tulishakubaliana kuhakikisha pesa zinazotengwa kwenye halmashauri za maendeleo ziende kwenye maendeleo. Kuna halmashauri ambazo zinapeleka 20% kutokana na uwezo wake, nyingine 60%, nyingine 40% na nyingine 70%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia halmashauri 55 tulizokutana nazo kati ya 184 hazijapeleka fedha za maendeleo bilioni 38.836. Waheshimiwa Wabunge, tupo hapa kuhakikisha wananchi wetu wanapata maendeleo, tunapitisha bajeti hapa kuna matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Ndio maana mkienda Majimboni mnalalamikiwa hamtimizi ahadi. Watendaji wa Serikali hii wanakula pesa za miradi ya maendeleo. Wanatumia pesa zao za *OC,* wanatumia pesa za miradi ya maendeleo bilioni 38, tujiulize zingejenga shule ngapi? Tujiulize zingejenga hospitali ngapi? Hizi nazo wanatumia zao na bado pesa

za miradi za maendeleo wanaenda kuzitumia kwa ajili ya kununua bagia, sambusa na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri tu za Jiji la Dar es Salaam; Jiji la Dar es Salaam kwa miaka mitatu haijapeleka fedha za maendeleo bilioni 21, Singida haijapeleka fedha za maendeleo bilioni mbili, Kigamboni bilioni mbili, Chato bilioni moja. Sasa hawa wananchi watapataje maendeleo na wakurugenzi wapo na wamekuja kwenye kikao wanakiri kwamba tulitumia kwenye matumizi mengine. Serikali inapeleka ruzuku na bado wanakusanya pesa zao za matumizi ya kawaida wanakula na wanakula fedha za wananchi, pesa zao za miradi ya maendeleo zinazotokana na kodi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mambo kama wawakilishi wa wananchi tupo hapa kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo, haya mambo siyo ya kuyafumbia macho. Unakuta Mkurugenzi anafanya kosa hili anahamishwa anapelekwa kwenye halmashauri nyingine. Sasa unajiuliza analindwa na nani? Nani anakula naye? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye fedha za asilimia kumi. Mwaka jana tulizungumza, leo pesa ambazo hazijakusanywa (chechefu) shilingi bilioni 79 na *CAG* alikuwa anatuambia ameamua kwa Mkoa wa Dar es Salaam afanye ukaguzi maalum, wakati anaenda kuhakiki zaidi ya vikundi 49 vilikuwa vikundi hewa. Shilingi bilioni 79 za Watanzania, kuna baadhi wameunda vikundi hewa, hawa Maafisa Maendeleo wa Jamii hawa, hii kamati ya kutoa mikopo; na tunasikia sasa hivi Serikali inataka kufungua dirisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuweke kanuni na hawa wanaotoa ndiyo chanzo cha tatizo, wanaunda vikundi vyao na ninyi wenyewe Wabunge hamjui. Ukienda Kinondoni tu kuna shilingi bilioni sita zipo nje, Temeke shilingi bilioni tano, Ubungo shilingi bilioni

4.8, Kibaha shilingi bilioni moja, Kigoma shilingi bilioni moja na hizi ni chechefu. Kwa mfano, kwa Jiji la Ilala tu mbali ya hizi chechefu kuna shilingi bilioni 19 zipo nje. Kama hizi zimeshindwa kukusanywa, hizo zilizo ndani ya muda zitakusanywa? Je, huo mpango wa kuhakikisha mnataka kutoa mabilioni mengine ya shilingi bila kutibu tatizo hili na hawa watu wapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulienda kutembelea kikundi kimoja, wale vijana wakasema hata hapa tulipo ni kwa mama maendeleo. Alituambia tujikusanye, tumepata shilingi milioni 35; ndani ya miaka mitatu wamerudisha shilingi laki tano. Tukaambiwa pale wanatengeneza mradi wa kutengeneza chaki, hakuna hata maboksi 100, shilingi milioni 35 haionekani na huyo mtu bado yupo kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya mambo hatuwezi kuyafumbia macho. Hata kama hela ya Serikali haiumi, jamani hii ni Tanzania yetu, hii ni Tanzania yetu. Hizi pesa tumepewa tuzilinde, tuzikusanye, ili tusonge mbele, sio kila siku tung'ang'anie kuzungumzia jambo moja. Hapa Mwenyekiti wakati anasoma, mtu kabisa hapeleki michango ya *PSSF*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hitimisha Mheshimiwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu hapeleki michango ya *PSSF* halafu *penalty* inakuwa kubwa. Nilikuwa naangalia karibia shilingi bilioni tatu haijaenda kwenye Mifuko. Wastaafu wanatembea na bahasha, maskini wanachangisha wakope wakalipe zile hela za haki zao, ili waweze kupata mikopo. *It is not fair,* sio sawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili tayari Mheshimiwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bulaya. Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, atafuata Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia na nitaanzia pale ambapo mjumbe mwenzangu alipoishia ili niendelee. Katika hizi hotuba ambazo zimesomwa hapa, suala la madeni na kikubwa mimi nitaenda kwenye madeni madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi tujiulize kwa sababu, upo utaratibu mzuri ambao Serikali imeshauweka kwamba, Halmashauri yoyote ikikusanya mapato yake ina *percent* ya kutumia na ya kupeleka kwenye miradi ya maendeleo, 40% kwa 60%. Zipo Halmashauri nyingine zinapewa %30 kutokana na ukubwa wa mapato yake, nyingine zinapewa mpaka 80%, lakini bado Serikali kuu inaongeza ruzuku kwenye matumizi ya kawaida, shilingi milioni 79 kwa mwaka huu uliofanyiwa ukaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ukiangalia sisi Kamati yetu ya *LAAC* tukapita, Halmashauri 55 bado zinadaiwa na wale wazabuni wadogo wadogo, hawa wanao-*supply stationaries*, chakula na wanaowapa mafuta. Halmashauri zile zinadaiwa shilingi bilioni 29, sasa *total* ya madai yote inakuwa shilingi bilioni 87, lakini kwa zile 55 tulizoangalia ni shilingi bilioni 29. Sasa unajiuliza, hawa wana ile 60% ya kwao ya kuendeshea shughuli zao, ikiwa ni pamoja na kulipia chakula, kulipa mafuta na *stationary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye miradi ya maendeleo inaeleza kabisa fedha ya ufuatiliaji isizidi asilimia tano ya ile fedha nzima ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa. Kwa hiyo,

kule kwenye miradi ya maendeleo kumeshaji-*set* kwenyewe, kwamba, atakwenda kuangalia kituo cha afya, shule inavyojengwa kwa kutumia zile fedha, asitumie zile fedha zaidi ya asilimia tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta Halmashauri ile imetumia zile asilimia tano, imetumia ruzuku iliyoletewa na Serikali kati ya hii 79, imetumia ile 60% waliyokusanya wenyewe na bado imewakopa mama ntilie chakula, haijawalipa. Hizi hela za *OC* zinakwenda wapi? Yaani hiki ndiyo tunachoiomba Serikali irudi kule chini, itupe mchanganuo, hizi hela za *OC* huwa zinakwenda wapi kwenye halmashauri zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Halmashauri moja katika Mkoa wa Iringa, siyo Manispaa ya Iringa, mama ntilie anadai zaidi ya shilingi milioni 150 amelisha chakula kwa mwaka huu wa fedha, nafikiri anaitwa *Turumba Food and Catering*. Shilingi milioni 150 wamekula chakula kwenye vikao vyao, mama yule anadai shilingi milioni 150, sasa wamemwacha wamehamia tena kumfilisi mwingine na hii ndiyo *trend* kwenye Halmashauri nyingi. Tunawauliza hao wanaowadai bado wanawahudumia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hapana. Sasa ina maana sisi tunapeleka hizi fedha au Serikali inapeleka hizi fedha ikachechemue ule uchumi wa watu wetu wa chini, kumbe zinaishia hapa juu kwenye Halmashauri, watu wetu hawapati na ndiyo maana malalamiko ya hali ngumu. Watu mifukoni hatuna kitu, yanakuwa makubwa. Kwa hiyo sasa tunaomba hii ikaangaliwe, *OC* zinatumika vipi, ile inayopeleka Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna *issue* ya *ceiling*. Kuna Halmashauri nyingine ukiangalia *CAG* anasema zinatakiwa zikusanye shilingi bilioni 911, zimekusanya shilingi bilioni 912, lakini Kigamboni wamekuja tumewahoji kwenye Kamati yetu, Kigamboni wamewekewa *ceiling* ya shilingi bilioni 11, lakini wao wamekusanya

shilingi bilioni 13, wana-*exceed* shilingi bilioni mbili. Kwa hiyo, Halmashauri nyingine zina uwezo wa kujitanua, zikatanua yale mapato yake, lakini zinabanwa na *ceiling* ambayo Serikali sijui, Wizara ya Fedha sijui, ni Sheria za Umoja wa Mataifa au *whatever, IMF* wanatubana kwa hiyo, wale wanashidwa kuongeza *effort* kwenye kukusanya mapato. *If that is the case,* basi tuangalie namna, tutatumia akili gani, ili kuona zile halmashauri zikusanye mapato zinavyoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya *NHIF*. Kwanza *NHIF* yenyewe inajiendesha kwa hasara sasa hivi. Nilipata mtu mmoja aka-*calculate* akasema, tukitaka *NHIF* ijiendeshe labda kila anayechangia sasa aongeze asilimia 2.2 ya mchango wake ndiyo itafika kwenye *balance* ya kwamba, inazalisha faida kwa hiyo, maana yake ni ipo chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *NHIF* inadai kila Halmashauri wanawakata hela; mmeshindwa kujaza fomu, mmekosea kujaza fomu, nimesikia hapa nimeambiwa na Benjamin kumbe wanakosea kujaza fomu mpaka wanadaiwa *penalty* ya shilingi bilioni tatu. Sasa mimi najiuliza na ukiangalia makosa yenyewe, kosa lenyewe tumeliona juzi pale; *NHIF* wanasema dawa au huduma iliyotolewa kwenye kituo cha afya haikutakiwa kutolewa kwenye kituo cha afya, kwa hiyo, hiyo huduma tunawakata hela. Vifaa tiba kwenye nchi hii vinapelekwa na Serikali. Mnapelekaje dawa mnayojua haitakiwi kutumika kwenye vituo vya afya ili *NHIF* wazikate halmashauri? Kwa hiyo, wanadumaza huduma za afya kule chini. Sasa hivi tunajua vituo vya afya vimejengwa, vya kisasa, lakini wenzetu wa *NHIF* waende kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kutibiwa siku moja, daktari kani-*diagnose* akaniambia nataka nikutibu, nikufanyie *operation* hii. Wao wakasema haiwezekani, sisi kwenye mikataba yetu hatuna *operation* ya hivyo, labda ufanye *operation* ya *analogy*. Sasa, yaani kule kuna madaktari, sisi tukiwa *diagnosed* na madaktari wetu,

madaktari bingwa wenye huduma za kisasa wao hawataki wanataka kuturudisha kwenye huduma *according* to wao wanavyotaka na ndivyo wanavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi *NHIF* hawajui kwamba, leo hii katika vituo vya afya tunafanya *operation* za akinamama wajawazito? Halafu unamshtaki nesi kwa kutoa matibabu ambayo hayakutakiwa kutibiwa kwenye kituo cha afya, ilitakiwa kuwa hospitali ya wilaya, hawajui leo tuna Madaktari Bingwa kwenye hospitali za wilaya? Kwa hiyo, halmashauri nyingi zimepigwa *penalty* ya kukataliwa zile fedha, sio kweli. Tunataka Wizara ya Afya wakakae na *NHIF* warudishe fedha za watu, waache uporaji. Halafu hii Serikali ni yetu, watu tunataka tuwahudumie wananchi wetu, sio suala la *penalty*. Wenyewe zikirudi huko juu wanafanya nini? Ziende zikatibu wananchi kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja kwenye suala lingine. Pamoja na mambo haya niliyoyaongea, *CAG* safari hii amefanya kazi kubwa sana. Amefanya ukaguzi wa ufanisi kwenye masuala ya afya ya akili kwenye nchi hii. Sasa wote mtakuwa mmesoma fedha, mmesoma kampuni, mmesoma nini, hamjasoma afya ya akili. Tatizo kubwa ni afya ya akili. *CAG* amesema kabisa, mtu yeyote mwenye afya nzuri ya akili anaweza ku-*contribute* vizuri kwenye nchi yake, kutoa mchango sahihi kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna watendaji ambao hawatoi michango sahihi kwa sababu, huduma za afya ya akili hazijawekewa msingi kwenye nchi hii. Leo hii tumekwenda kukagua shule moja Chaduru huko, watu wamejenga msingi, kozi ya msingi wa jengo inakwenda kozi 18. Fedha yote imeishia kwenye msingi, huyo mtu ana afya nzuri ya akili? Anatoa mchango gani kwenye hii nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajua kabisa thamani yangu. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini, mwanamke, unalazimisha

nikatibiwe kwenye *analogy,* ili nife? Halafu utanipata wapi mtu kama mimi kwenye nchi hii? Sasa hawa wenzetu nao wana afya nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani afya ya akili hata humu ndani tukisema watu wanafikiria ni mambo ya uchizi. Sio mtu amekuwa kichaa, lile ni tatizo tayari. Afya ya akili ni ustawi tu wa akili zetu na *CAG* kasema kumbe kuna Sheria ya Afya ya Akili ya Mwaka 2008, Kipengele cha 31(1)(b), kinataka Wizara iunde Baraza la Afya ya Akili Nchini, ili kutoa huduma za kisaikolojia na huduma saidizi. *CAG* kasema kama hatutoliangalia hili watu watazidi kupata matatizo mengi, watashidwa ku-*perform* katika ile *standard* tunayotaka wa-*perform,* vijana wetu watazidi kulewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unashangaa humu ndani leo hii watu wamekwenda kutoa huduma za afya ya akili wamewaangalia wazee, wamewaangalia watoto wale waliopata mimba za utotoni, watoto wa mazingira magumu na wamewaangalia watu wenye ulemavu. Tuulizane humu ndani, kati ya wazee wetu wa zamani waliokuwa wanachukuwa majembe wanakwenda kuchimba barabara, wanajitolea na sisi leo tunajengewa barabara za lami, tunamwaga takataka, tunataka Serikali ituzindulie, nani ana afya mbaya ya akili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini ukawaangalie wazee badala ya uanze kutuangalia sisi kwanza afya zetu zikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala ni sheria. Tunataka Baraza la Afya ya Akili Nchini hii liundwe. Sheria inaelekeza tangu Mwaka 2008, ili vijana wetu wapate *support* ya ushauri. Tunasema si kwamba, mambo hayaendi kule chini, mambo yanakwenda, mikopo inakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, wenzangu wameongelea hiyo 4:4:2 inakwenda kwenye vikundi, lakini vikundi vile vikipewa mikopo

tumeshaambiwa mikopo ile hairudi. *CAG* anasema, ili mtu aweze kurudisha mkopo lazima akili yake iweze ku-*perform,* yaani a-*produce productively* siyo tu suala la kwenda kazini, anakwenda kazini anazalisha kwa tija?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakwenda Milembe, dawa ya afya ya akili iliyopo Milembe ni moja tu, ya aina moja, wakati ubongo una sehemu tatu na sehemu zote zikiathirika zinahitaji matibabu tofauti. Tunaomba suala hili lichukuliwe kwa uzito, tutapunguza matatizo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawacheka wenzetu si ndiyo? Tunaona wenzetu sijui vijana wao wamefanyaje, wameingia humu wanaleta vituko, wanaleta maandamano na sisi tusipohangaika na kuwaweka vizuri vijana kwenye akili tuna changamoto kubwa; *CAG* amesema suala hili limesababisha tukakosa ushauri wa kisaikolojia na vijana wengi wameingia kwenye ulevi uliokithiri, ni nani hapa sio shahidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unachukua kabisa kijana, umepanda bodaboda unaona kabisa huyu tukifika ni kudra za Mwenyezi Mungu. Watoto wadogo, leo tuna viongozi ambao sasa hivi ukienda kwenye mitaa ya mijini kote kuna *casino* zimewekwa kila mahali. Wanaotoa vibali ni wasomi wa nchi hii ambao wanajifanya wana afya ya nzuri ya akili, kutuletea *casino* kwenye makazi ya watu, watoto wanashinda wanakimbia humo, wanakunywa, wanavuta bangi, hawana akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema suala la afya ya akili tuanze kufundishwa sisi tulioko juu. Huku ghorofani kukishakuwa kumechanganyikiwa hata tufanyaje, ndiyo maana leo watu wanatafuta, kila zikipelekwa fedha za madarasa hazitoshi, tumeongeza wanasema hazitoshi. Kituo cha afya mara ya kwanza tumepeleka shilingi milioni 470 hazitoshi, tumepeleka shilingi milioni 580 hazitoshi, tunataka shilingi milioni 640. Tunapeleka shilingi milioni

640 hazitoshi. Mtu anajenga nyumba, anajenga shule mahali penye mwinuko, anatafuta *level* ya mlima kuanzia kule chini mpaka apate *level* ya pale juu, halafu ndiyo ajenge darasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani kama huyu mtu ana akili timamu kwa nini asijenge kwa *leveling?* Waheshimiwa, si tulikuwa Rwanda hapa? Si tuliona zile nyumba zao zilivyo juu ya milima, hivyo? Sasa wangekuwa wanatafuta *level* wale, mpaka wakakutane kule juu, hela yote shilingi milioni 600 si inaishia huko? Huku juu Wizara, wenzetu TAMISEMI, kule kwenye wasomi tunawashukuru, hivi hawajui nchi hii kama kuna *Southern Highlands of Tanzania?* Tuna ukanda wa ziwa, tuna ukanda wa kati, hawajui? Wametoa ramani zote za *flat rate,* afya zao zikoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Afya jambo hili siyo la kulifanyia mzaha. Kampeni zenyewe, Marekani wameanza kampeni za afya ya akili tangu Mwaka 1958 na unakuta wale ma-*first ladies* kama akina nani, ndiyo wanakuwa ma-*organizer* wa zile kampeni. Sisi hatufanyi kampeni, tunasubiri siku ya kujinyonga duniani ndiyo tunafanya kampeni ya afya ya akili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka hizi kampeni ziwe *intensive,* watu wajue. Humu ndani mimi nakutana na watu, siwezi kuwataja ninyi jamaa zangu, Waheshimiwa wenzangu, muda wenyewe tuliopo sio mzuri tutalipuana vichwa, lakini wengi wao humu na ninyi pia, hamuelewi. Mkiniona mimi mnaniambia balozi wa afya ya akili, mnafikiri balozi wa machizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio maana yake. Nawaambia kila siku suala la afya ya akili ni ustawi wa akili ya mtu kichwani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuja ukichaa, tayari ni tatizo. Niombe sana, *CAG* ametusaidia, ametoa mapendekezo ya namna ambavyo tunaweza tukashughulika na suala la afya ya akili, kutojibu hoja za *CAG* ni kukosa afya ya akili. Wajibu hoja za *CAG*, anawasaidia wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jesca. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatia Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niungane na wachangiaji waliotangulia katika kutoa mchango wangu kwenye kujadili Kamati zote zilizowasilisha hoja. Pamoja na kwamba, hoja hizi zimekuwa zikijirudia kila wakati, lakini bado tunaona kuna jitihada za Serikali kwenye baadhi ya maeneo tunaona yanaboreshwa na lazima tu-*acknowledge* kwa baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sekta ambazo zinafanya vizuri na ni muhimu sasa nikazitaja. Mathalani, sekta ya nishati inafanya vizuri, Sekta ya Maji inafanya vizuri, vilevile Sekta ya Afya inafanya vizuri pamoja na Sekta ya Ujenzi, changamoto tu ni rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na eneo la kukosekana kwa mipango madhubuti ya Halmashauri zetu katika kukusanya mapato ya ndani. Tumeambiwa hapa na Kamati kwamba, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2023, Serikali kuu imepeleka fedha takribani shilingi trilioni 7.6 kwenye halmashauri zetu nchini, shilingi trilioni 2.4 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi trilioni 5.2 ni fedha za matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kueleza hapa kwamba, bado tuna changamoto kubwa kama Taifa kwenye halmashauri zetu. Bado halmashauri zetu zimekuwa zikitegemea kwa 90% Serikali Kuu na hii inakwenda kinyume na Sera yenyewe ya Ugatuzi wa Mamlaka au Madaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Nchi za Afrika Mashariki, nitazitaja, kama Kenya, Uganda, Rwanda na nyinginezo, Serikali za Mitaa zinajitegemea zenyewe kwa mapato ya ndani. Changamoto ipo wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kupeleka fedha kwenye halmashauri zetu siyo jambo baya, ni jambo jema, lakini yapo maeneo Serikali Kuu haina sababu ya kupeleka fedha. Ukipeleka fedha maana yake unakwenda kuzifanya halmashauri hizi zikose kuwa na fikra mbadala au kuwa na ubunifu wa vyanzo vingine vya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa Jiji la Ilala, Jiji la Ilala linakusanya bilioni 130, lakini bado linapelekewa fedha za matumizi mengineyo na mishahara ya watumishi na bado linapelekewa fedha za maendeleo, sikatai kwenye sekta ya maendeleo, zinaweza kupelekewa, lakini siyo kwa maana zifanane na Halmashauri zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali Kuu imepata mzigo mkubwa wa utegemezi kutoka Serikali za Mitaa? Ni kwa sababu tuna changamoto kubwa ya Halmashauri zetu kuwa wabunifu katika kukusanya mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kushauri, kwa changamoto hii ili tuweze kuzijengea uwezo Halmashauri zetu ziwe na uwezo wa kukusanya mapato ya ndani na wakati mwingine ziweze kujitegemea kwa sehemu fulani na siyo 90% kwa Serikali Kuu,

nashauri jambo la kwanza ni kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani ili Wakurugenzi na Menejimenti wanavyopeleka mapendekezo yao ya vyanzo vingine kuhusu mikakati mbalimbali ya kukusanya mapato ya ndani waweze kuwaelewa na wawaunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo kimsingi lingefanywa ni lazima sasa Serikali iwape Wakurugenzi wote wa Halmashauri vigezo mahsusi vya utendaji kazi *KPI – Key Performance Indicators* na wapimwe kila baada ya kipindi cha miezi sita. Hii itasaidia Wakurugenzi wa Halmashauri kuwa wabunifu. Watakuwa wabunifu kwa sababu wanaamini baada ya miezi sita atapimwa kwa *KPI* aliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto ambayo tunayo na ninadhani hili ni jambo ambayo kimsingi linatekelezeka. Wakipewa na wapimwe kwa maana ya namna gani wanaweza wakawa wabunifu wa vyanzo vya mapato, kukusanya mapato, lakini pia na matumizi yao yawe yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze hapa bayana, kwa nini tumekuwa na changamoto mara kwa mara kwenye taasisi zetu za umma? Ninaamini kwamba ukiona taasisi yoyote haifanyi vizuri, changamoto siyo watumishi wa kada ya chini, mara nyingi tunakosea sana, yaani tunamwacha Mkurugenzi wa taasisi hapa juu halafu tuna-*deal* na wale anaowasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utamaduni wa utawala wowote ule kuna kitu kinaitwa utamaduni wa utawala. Maana yake, utamaduni wa utawala unajengwa na kiongozi wa taasisi. Kwa hiyo, ukiona taasisi yoyote inatuhumiwa kwa rushwa, maana yake anayekula rushwa ni Mkuu wa Taasisi. Wale wasaidizi wanafuata *boss* alivyo. Kwa hiyo, sioni sababu ya ku-*deal* na watu wa chini halafu tunawaacha Wakurugenzi wa taasisi pale wanatamalaki. Kwa hiyo, ushauri wangu ni muhimu sasa badala ya kumwajibisha

mtumishi wa kawaida, wawajibishwe wakuu wa taasisi, hii itasaidia kwa sababu mkuu wa taasisi ndiyo anayejenga utamaduni wa taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze kwenye eneo moja ambalo linahusu Halmashauri zetu kudaiwa. Tumeambiwa na Kamati hapa, baadhi ya Halmashauri zinadaiwa kiasi cha fedha takribani bilioni 21.85. Kuna fedha ambazo Wizara ya Ardhi ilipeleka kwenye Halmashauri kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha, madeni wanayodaiwa mpaka sasa ambayo fedha hazijarejeshwa ni bilioni 21.85.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nishauri hapa kwa Halmashauri hizi ambazo zina changamoto hii. Wakati huo huo Halmashauri hizo zinadai fedha 42,536,221,960, fedha ambazo hazijalipwa kutokana na mauzo ya viwanja. Sasa, mimi sioni kwa nini wanashindwa kulipwa hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwa hawa wakurugenzi wenye hii kadhia, kimsingi ushauri wangu hapa, wana viwanja vipo. Kwa sababu wangeweza kushusha bei ya hivyo viwanja, vingenunulika. Mfano, kiwanja kinachouzwa 1,000,000 ukimwambia leo mtu ambaye ameshindwa kulipa 1,000,000 akulipe 500,000 na ukampa *notice* ya mwezi mmoja analipa. Tena atakimbia atakopa fedha, atalipa haraka sana kwa sababu anajua hiyo umempa fursa ya yeye kupata kiwanja chake. Ni hesabu ndogo sana. Kwa hiyo, nawashauri wakurugenzi wote wenye viwanja ambao kimsingi wana kadhia ya kutorejesha fedha hizi bilioni 21, washushe bei, hivyo viwanja vitakimbiliwa na hiyo fedha itapatikana na wataweza kulipa mkopo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la makusanyo kwa kutumia *POS (Point of Sales)*. Labda nieleze changamoto za makusanyo au kukusanya tozo kwa kutumia *POS*. Kwanza, *POS* inaruhusu mjadala kati ya mtoza ushuru na anayetoa ushuru. Wana-

*compromise*, kwa sababu kama mtu alitakiwa alipe laki sita tozo anamwambia nipe 200,000 nakusamehe. Sasa nadhani kwa sasa umepitwa na wakati. Tunaweza kuutumia kwa maeneo ambayo hayana fursa au hayana mtandao kwa maana ya *internet* hasa kule vijijini, lakini hadi Dodoma, Arusha Mjini na Dar es Salaam hadi Ilala Jiji bado *POS* zinatumika kwa ajili ya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mfumo mzuri ni wa kutumia *control number*. Hakuna nafasi ya watu ku-*compromise* na hakuna mazingira ya kujadiliana alipe kiasi gani, lakini *POS* bado zinatoa nafasi ya mtoza ushuru na mtoa ushuru ili wakubaliane apate kidogo, Serikali ikose kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), nadhani wapo hapa watusaidie. *POS* siyo kwamba ziache kutumika, ila zitumike kwa maeneo ambayo hawana *access* ya *internet* na *TRA* wanafanya hivyo nchi nzima. Kwa sababu *control number* inamlazimisha mtu alipe kiasi anachopaswa kulipa na huu ndiyo mfumo utakaotusaidia kudhibiti mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye eneo lingine la riba zinazotokana na ucheleweshwaji wa madai au malipo kwa wakandarasi. Jambo hili linaweza kuepukika. Waswahili wanasema, heri kinga kuliko tiba.  Tunafahamu zipo changamoto kadhaa kwenye kuwalipa wakandarasi lakini zipo ambazo zinaweza kuepukika mathalani, miradi ya ujenzi wa barabara. Karibu miradi mingi ina changamoto hii ya kulipwa malipo kwa wakandarasi. Mtakumbuka ripoti ya *CAG* iliyopita Wizara ya Ujenzi, *TANROADS* walikuwa wanadaiwa bilioni 700. Hizo ni riba tu. Sasa tunaweza kuepuka hii hasara ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaepukaje? Ni lazima sasa tuwe na vipaumbele, kupanga ni kuchagua, kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha, tuchague. Kwa mfano, barabara ina mahitaji

makubwa kwa Taifa letu. Ukitoka hapo sekta ya maji ina mahitaji makubwa kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, kuna baadhi ya sekta kimsingi tunaweza kuziacha kidogo, lakini sekta hizi muhumu ambazo kimsingi ndiyo uchumi wa Taifa letu zikawekewa mkazo mathalani leo pale Jimboni kwangu kuna barabara ambayo kimsingi namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Mheshimiwa Rais kuridhia. Hii barabara sasa inakwenda kuwa na hadhi ya *trunk road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ninayoizungumza ni inayounganisha Mikoa ya Pwani na Nyanda za Juu Kusini, lakini mpaka leo ninavyozungumza, barabara hii imepata kandarasi na hapo namshukuru sana Mheshimiwa Rais. Pamoja na mapenzi mema ya Mheshimiwa Rais na mapenzi mema ya Serikali katika kuunganisha Mikoa hii ya Pwani na Nyanda za Juu Kusini, ujenzi wa barabara hii bado unasuasua. Hivyo basi, rai yangu ni kwamba ili tuepukane na kadhia ya riba zinazosababishwa na kucheleweshwa kwa malipo ya wakandarasi, ni muhimu mradi huu nao ukalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mkandarasi amesaini mkataba mwaka jana mwezi wa Novemba mpaka leo amepeleka mitambo *site*, yuko *site* hajalipwa fedha na anadai bilioni tisa tu malipo ya awali. Kwa hiyo, huyu kesho atakuja kudai riba, sasa ni hasara ambazo zinaepukika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naishauri Serikali kwamba, hasara za namna hii ambazo zinaepukika, kwanza tuwe na vipaumbele kwenye mikataba yetu. Hatuna sababu ya kuwa na mikataba mingi ambayo hatuwezi kukidhi kulingana na rasilimali fedha. Ni muhimu sana tukafanya tathmini ya kina, tuwe na mikataba ambayo kimsingi Serikali inaweza ku-*afford* kulipa kandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kwenye mradi huu ameweza kuruhusu barabara hii ijengwe kwa kiwango

cha lami kilometa 100. Kutoka kipande cha kutoka Ifakara mpaka Mbingo pale Mialeijima, kilometa 62.5 mradi wa bilioni 97, mkandarasi anadai bilioni tisa tu *advance payment* mpaka sasa hajalipwa toka Novemba mwaka jana. Kesho huyu atakuja kudai riba atakwenda kwenye mpango ule ule wa riba ambazo kimsingi tunaweza kuziepuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi wa pili naye amesaini mkataba kipande cha kilometa 37.5 kutoka Mbingo pale Miale kwa maana ya Ijima Miale mpaka kwenda Chita, Kambi ya Jeshi pale Makutano, sasa jambo hili linawezekana. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba ni muhimu kwa Serikali ifanye tathmini ya kina kwenye miradi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie, kwa sababu kwenye uchumi tunasema *opportunity cost, you fore gone for the best alternative*. Rasilimali fedha ni ndogo kulinganisha na mahitaji. Kwa hiyo, tukiwa na mipango ambayo inaendana na rasilimali fedha kwa uwezo wa Serikali, itatusaidia kama Taifa kuepukana na malipo ya riba ambazo zinasababishwa na kutolipa wakandarasi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ahsante sana na Mungu atubariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kunambi. Atafuatia Mheshimiwa Mwakamo. Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, wajiandae.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*. Ninampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu kwa namna alivyowasilisha mawazo yetu kwa sababu taarifa aliyoiwasilisha ni taarifa iliyotufanya tukeshe muda mwingine mpaka saa sita usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wetu kwa kutupongeza Wajumbe wako wakati unachangia kwa ile kazi ulivyoiona ngumu na ninaamini baada ya kutoa pongezi kwetu basi kutakuwa na namna ya kuitazama Kamati kwa kazi kubwa inayofanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Serikali kwa namna ambavyo inatekeleza majukumu yake na pongezi zangu nitaenda nazo sawasawa na namna ambavyo tumeipitia taarifa yetu, wakati huohuo nitatoa ushauri na maoni mengine kwenye michango ambayo wenzangu wametoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunapitia taarifa na namna Mheshimiwa Mwenyekiti alivyoiwasilisha na amelieleza Bunge kwamba CAG amefanya ukaguzi kwenye Halmashauri 184, lakini kwenye Halmashauri 184, halmashauri 181 zimepata hati zinazoridhisha na Halmashauri tatu zimepata hati zenye shaka lakini hakuna hati mbaya ambayo imepatikana kwa hesabu hizi ambazo zimekaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa sababu ukiangalia taarifa iliyopita ya 2022/2023, tulikuwa na hati zisizoridhisha 170. Kwa hiyo, utaona Halmashauri zimeongezeka. Pia, tulikuwa na hati zenye shaka 13, sasa ziko tatu, utaona ni namna gani hatua zimechukuliwa. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa namna ambavyo mmeweza kusimamia kutoka taarifa ile mpaka taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ya kujiuliza, pamoja na kwamba zipo taarifa za kuongezeka kubadilika kwa hati, tulichokigundua kama Wajumbe wa Kamati, hati ni jambo moja na hali halisi ya utekelezaji wa masuala yake ni jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa yetu ya Kamati, imeonesha mapato yasiyokusanywa yenye thamani ya bilioni 61.15.

Sasa ukiitazama taarifa unapozungumzia mapato yasiyokusanywa, katika hali ya kawaida hizi ni fedha ambazo zingekusanywa zingesaidia Serikali kutatua changamoto mbalimbali za wananchi wake. Kwa hiyo, rai yangu ni kuiomba Serikali ijaribu kutupia macho kwenye maeneo ambayo *CAG* ameyabainisha kwamba kuna vyanzo vya mapato havijabadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo kazi ambayo ninaamini Serikali iliamua kuwa na *CAG* kufanya kazi zake na ndiyo maana *CAG* akaonekana ni jicho la Bunge ili atuoneshe kitu gani kimepungua katika maeneo gani. Ingekuwa ni taarifa za kisomi kwa maana ya watu wanafanya wanazuoni, basi tungesema *CAG* anatufanyia *research* ya kutuonesha changamoto zilipo ili kutatua changamoto zilizopo. Kwa hiyo, naomba Serikali iitumie taarifa ya CAG, siyo kwa kutafuta kuhukumu tu, ni kwa kutafuta kutatua changamoto za kuyaongeza mapato ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote kama Waheshimiwa Wabunge tunajua, kwenye Majimbo yetu miradi mbalimbali ya maendeleo imetekelezwa na wananchi wanajua utekelezaji wa miradi ile umesimamiwa vizuri na Serikali ya Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, asingeweza kufikia malengo ya kukusanya basi asingekuwa na uwezo wa kutekeleza miradi mbalimbali ambayo leo inatusaidia wananchi kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye eneo hili la makusanyo na kwenye makusanyo ambayo hayajakusanywa, ukitazama unakuta ni kwenye vyanzo ambavyo vinakusanyika. Unakwenda kwenye Halmashauri wanashindwa kukusanya fremu zao zilizopo stendi na kwenye masoko. Wamepangisha wenyewe, watu wamewapa kwa mikataba halafu unaambiwa wanashindwa kukusanya. Sasa unajiuliza, hivi Mkurugenzi na timu yake kwenye halmashauri hiyo, kama wanashindwa kukusanya kitu ambacho kinaonekana kwa macho kwamba asubuhi ukiamka unamkuta

mfanyabiashara uliyempangisha yuko pale, unashindwa kukusanya mapato yake, utaweza kazi gani sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali hasa TAMISEMI, iwasimamie vizuri Wakurugenzi wafanye makusanyo haya ili yaweze kusaidia kurekebisha hesabu zetu na kuweza kupata vyanzo vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta wanashindwa kukusanya leseni za biashara, yaani mtu ameamua kufanya biashara, Mtanzania ameamua kufanya biashara, ameweka duka lake pale anafanya biashara na Serikali wanajua, kumpitia kukusanya tu inashindwa, matokeo yake tuna bilioni 61.15 hazijakusanywa. Kiasi ambacho pesa hizi zingekusanywa Waheshimiwa Wabunge na wananchi zingetusaidia kwenye miradi, tunajua kila kinachokusanywa na halmashauri kinatoa 10% ambayo inakwenda kwenye mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, ni imani yetu kwamba hii mikopo ambayo tunaitegemea wengi isiyo na riba, maana yake mapato haya yangekusanywa na kule kingeongezeka kitu, maana yake wakopaji wangekuwa wengi na uchumi wa wananchi hao ungeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri sana Serikali hasa TAMISEMI, itupie jicho iitizame taarifa ya *CAG* kwenye hili eneo la makusanyo yasiyokusanywa yenye thamani ya shilingi bilioni 61 yakusanywe na yaweze kwenda kutumika kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza juu ya madeni, tuna madeni kwenye halmashauri yanayotokana na posho za kisheria, uhamisho, kukaimu nafasi za kimadaraka na madeni ya wazabuni na vyanzo vingine vinavyosababisha madeni, tuna madeni takribani bilioni 87.32 haya yanaitwa madeni, uanzishwaji wa madeni haya, mengine yanazuilika na tunaposema madeni

maana yake sasa Serikali inalazimika kwenda kutafuta hela za kulipa madeni ambayo mengine yangezuilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe umeitisha kikao cha halmashauri, huna pesa ya chakula unamkopa mzabuni, unashindwa kumlipa, unakaa miaka mitatu halafu unakuja kumlipa pesa ile ile ambayo wewe uliikopa baada ya miaka mitatu, lakini yeye benki kule alikoenda kuchukua mpaka akakuhudumia, analipa na riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri Serikali katika kulisaidia Taifa hili na hasa kuwasaidia Watanzania ambao ni wahangaikaji wanaotafuta uchumi kwa ajili ya kuendesha maisha yao, hebu tutazame namna ya kuhakikisha madeni haya yanalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa Serikali ingetoa mwongozo kwa Wakurugenzi, anayesababisha deni kuna kitu kitamkuta sidhani kama madeni haya yangezalishwa, lakini yapo madeni ambayo Wakurugenzi wanayazalisha wakiamini kwamba kwani kesho si nitahama! Sasa akihama anamwachia mwenzie, inakuwa taabu kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekutana na madeni mengine ni vichekesho, wanakiri vifaa wanapokea, wanasema kabisa kweli ulileta *stationary* au wanasema kabisa kwamba, ni kweli ulituhudumia chakula kwenye Baraza la Madiwani lakini wanasema, tunashindwa kukulipa kwa sababu nyaraka hazijakamilika. Sasa nyaraka hizo za nani, wewe uliyetoa *order* hukumbuki uliagiza kitu gani? Kwa nini usilipe kulingana na ulichokiagiza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, kwa kuwasaidia Watanzania hawa, hebu tutoe maelekezo mazuri kwa Wakurugenzi, ikifika sehemu Wakurugenzi wanaozalisha madeni yasiyo ya lazima, basi kuwe na hatua zinazochukuliwa kwao. Ikiwa hivyo ninaamini

kabisa yapo madeni ya Watanzania wenzetu ambao wanatoa huduma kwenye halmashauri zetu yasingeweza kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna makato ya kisheria ambayo yanakatwa na yanatakiwa yapelekwe kwenye taasisi. Tuna Wakurugenzi kwa maana ya Halmashauri, wanadaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mifuko ya Fidia kwa Wafanyakazi, sasa unajiuliza, hela ya mtumishi umekata na alipaswa aipate kwenye mshahara wake, umeichukua, nini kinakufanya usiipeleke kunako stahili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali hili linajibika kwa majibu rahisi sana, ni kwa sababu yule anayesimamia jukumu hili, halisimamii kwa moyo wa upendo, anajisahau kama yeye ni mtumishi kwamba makato yale yanatakiwa baada ya mtu kustaafu yamrejee. Sasa watumishi wengi wanateseka, amestaafu amemaliza muda wake wa kazi anashindwa kupata mafao yake, mifuko inamwambia, mwajiri wako hakuleta pesa! Hili ni jambo la hatari na kwa kufanya hivyo inazua maswali mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati tulipokuwa tunapitia taarifa hii tunapata tabu sana. Unakuta kwa mfano, *PSSSF* wao wanadai deni la bilioni nne, lakini kwa sababu madeni haya yanakaa muda mrefu yanakwenda yanazalisha riba mpaka bilioni 32! Sasa unajiuliza, yaani ni kama kuna mazungumzo kwamba, hebu tukae muda mrefu ili tukilipa labda tugawane, maana hata hatuelewi inakuwaje! Inawezekanaje wewe ushindwe kulipa deni dogo halafu uje kubaki uwe na deni kubwa, utalilipa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninafikiri madeni ya namna hii, kwa sababu Mifuko hii ni ya Serikali, inasimamiwa kwa maslahi makubwa ya watumishi; mimi ningeishauri Serikali irudi ikae na Mifuko hii ili wapate naona bora ya kuondoa haya kwa sababu imekuwa mizigo kwa halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri nyingi zinashindwa kutekeleza kwa sababu wanapiga hesabu anachodaiwa ni kidogo, lakini riba aliyowekewa ni kubwa. Sasa labda turudi tukae na taasisi hizi, tuzungumze nazo, tufike sehemu ikiwezekana ziondolewe hizi riba ili yalipwe haya madeni ya kawaida. Tuziondoe hoja za *CAG* kwa sababu hoja za *CAG* sasa zinashindwa kufungwa kwa sababu kila mwaka *CAG* anapoleta taarifa ile hoja ipo, kwamba inaonekana halmashauri fulani haijapeleka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijiuliza ni kwa nini haijapeleka, kwa sababu kuna riba kubwa, hivyo ameshindwa. Sasa kwa sababu ile ni taasisi yetu kwa nini tusikae chini yazungumzwe ili tuziondoe hizi hoja? Kwa sababu kila tunapokagua hizi halmashauri unakuta kwamba hoja zilizopita za miaka kadhaa ya nyuma unakuta hoja 18 hazijapatiwa majibu, ukizitazama hakika hazitajibika, kwa sababu hawatakuwa na uwezo wa kuyatekeleza hayo waliyoagizwa hao wakurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawana uwezo kwa sababu gani, aliyezalisha taizo hilo amekwishahamishwa takribani halmashauri tatu hadi nne, kwa hiyo huyu aliyekuwepo leo hana nafasi ya kuona kama hili jambo lina msingi wa kulishughulikia. Kwa hiyo, ningeiomba sana Serikali yangu, Serikali ambayo ninaamini kabisa inatekeleza kazi kwa upendo wa wananchi wake ikae chini kutafuta namna ya kushughulikia mambo haya ili hizi hoja za *CAG* ziweze kufutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, wenzangu wamezungumza hapa; halmashauri au nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa sheria na hakuna kiongozi aliyepata bahati au Mtanzania aliyepata bahati kupewa mamlaka kwenye nchi hii asiyejua taratibu za kutumia sheria na miongozo mbalimbali. Sasa, sisi wanakamati tunakutana na maswali mengi. Unaposikia Mkurugenzi wa halmashauri fulani ametumia mapato yasiyostahili; ameambiwa kabisa kwamba endapo utasimamia miradi ambayo unaitekeleza kwa vyanzo vya

mapato tumia asilimia tano, kwa mfano, ya mapato hayo kama sehemu ya usimamizi wa miradi, lakini anatumia 40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anakuja kwenye Kamati anawaambia naomba radhi. Sasa Kamati unaiomba radhi wewe hukuwa unajua kama ukifanya hivi ni kinyume na utaratibu? Niiombe TAMISEMI, makosa kama haya, kama Wakurugenzi hawa, Maafisa Masuhuli hawa kama hawatakuwa na kitu watakachokiogopa kwamba wakifanya hivyo watakuwa wamefanya kinyume na utaratibu kila siku, kila mwaka wataendelea kufanya makosa haya wakiamini wakija kwenye Kamati wataomba radhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalisema hili kwa sababu bahati nzuri kwenye zile Kamati hatukai Waheshimiwa Wabunge peke yetu kwa maana ya sisi kama wawakilishi tu wa wananchi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hitimisha tafadhali.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nisisitize na niiombe Serikali Taarifa yetu ya Kamati namna ambavyo Mheshimiwa Mwenyekiti wetu amewasilisha ingekuwa vyema sana kama baada ya kuwasilishwa mkaifanyia kazi kwa uhakika kwa sababu tumetoa maoni ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, ahsante sana. Anafuatia Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ya kuchangia hoja zilizopo mezani. Nikiri kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)*. Kwanza ninampongeza CAG kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye halmashauri zetu ya kukaguza Hesabu za Serikali za Mitaa na kuangalia changamoto inayozikumba Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo. Kwanza tuzishukuru Serikali zote mbili za Awamu ya Tano na Awamu ya Sita, Serikali hizi mbili zimepeleka fedha nyingi sana kwenye halmashauri zetu. Katika fedha hizo kuna miradi ya kuanzia mwaka 2018 bado haijakamilika mpaka hesabu hizi zinavyoongelewa leo. Kuna miradi ya 2021/2022 haijakamilika mpaka leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli katika miradi hiyo jumla ya bilioni 206 zimetumika lakini miradi hiyo bado haijakamilika mpaka leo. Kwa kweli hili linakatisha tamaa hasa kwenye nia ya kusimamia na kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Fedha zimekwenda lakini miradi haijakamilika na hii inatokana na sababu tofauti tofauti. Wenzangu wameelezea, jengo moja la shule ya msingi lilikuwa linapewa takriban nchi nzima kwa milioni 20; miradi hii mingi haikuweza kukamilika. Vituo vya afya vilipewa milioni 500 katika maeneo yote, lakini miradi hii haikukamilika bila kuangalia uhalisia wa eneo ambalo mradi unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine wamejenga milimani, maeneo mengine wamejenga kwenye maji. Haya yote wakurugenzi walikuwa wanatueleza tulipokuwa tunawahoji ni kwa nini hawajakamilisha miradi yao hadi hivi leo. Mpaka sasa hivi kuna miradi ya bilioni 11.6 imekamilika lakini haitumiki. Haya yote ni changamoto ambazo Serikali inatakiwa iende ikaziangalie ili kuhakikisha kwamba miradi hii inayotolewa na fedha za Serikali Kuu inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea kwenye miradi hii utaona kwamba miradi mingi sana ambayo haijatekelezwa ni miradi ya elimu, miradi ya afya ambayo inagusa mwananchi wa kawaida kule vijijini. Tunaomba Serikali ifanye jitihada ili miradi hii ambayo imelalia kwa muda mrefu, zaidi ya miaka mitatu ikiwa imetolewa fedha na Serikali Kuu na bado haijakamilika, basi Serikali itoe fedha kwenda kukamilisha miradi hiyo ili wananchi waweze kunufaika kutokana na malengo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika ukaguzi imeonesha kwamba kuna halmashauri nyingi zina maboma yamejengwa na wananchi wengi sana, lakini nayo bado haijakamilika mpaka leo. Tulikuwa tunawahamasisha wajenge maboma na Serikali itatoa vifaa vya madukani. Wengi wamefanya hivyo, lakini maboma yale bado hayajakamilika mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itafute namna ya kupeleka fedha kwenda kukamilisha yale maboma yaliyojengwa na wananchi ili nao waendelee kujitolea kwa ajili ya kutatua matatizo ya maboma ambayo yapo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la tatizo la matumizi mabaya ya fedha kwenye manunuzi. Mkaguzi *(CAG)* ameeleza matatizo kadha wa kadha ambayo yametokana na kutokufuata Sheria ya Manunuzi. Wengi wanafanya manunuzi bila kutoa risiti, wengi wanafanya manunuzi kwa *cash* na wengi hawatumii mitandao kutafuta wazabuni. Yote haya ni kukiuka Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti yetu tumeonesha malipo yasiyokuwa na stakabadhi yenye jumla ya bilioni 7.42 imeonekana na *CAG* kufanyika katika halmashauri zetu. Vilevile malipo ya fedha ya taslimu, wametoa fedha taslimu kwa wazabuni yenye thamani ya bilioni 1.440 nayo yametolewa taslimu bila kufuata utaratibu wa manunuzi. Bado kuna miradi mingine fedha imetolewa taslimu

yamelipwa bila kufuata Sheria ya Manunuzi pamoja na kuwa na mikataba ambayo haijapitiwa kwenye Bodi ya Zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali isimamie matumizi mazuri ya Sheria ya Manunuzi kwenye halmashauri zetu. Wakati mwingine hata matumizi ya *force account* imekuwa ni tatizo; kwa maana ya kwamba wananchi tulisema *force account* mpaka kufikia milioni 100 iendelee *force account,* lakini unakuta sasa *force account* ya mradi wa milioni tatu unaenda kwenye mtandao bei inakuwa kubwa kuliko hali ya uhalisia wa soko. Jambo hili linaleta mchanganyiko na linaleta dharama kubwa ya ujenzi katika majengo yetu ambayo yanajengwa na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ambalo nilipenda sana nilizungumzie na ambalo wenzangu wamelizungumza kwa haraka haraka ni suala na makusanyo. Makusanyo kwenye halmashauri zetu kuna wengine wanakusanya zaidi, wengine wanakusanya kidogo hali inayowafanya washindwe kukamilisha miradi ambayo wameipanga kwenye bajeti kutokana na makusanyo madogo. Hata wale waliokusanya makusanyo makubwa nao wanashindwa kukamilisha miradi yao kwa kukosa kupeleka fedha kwenye miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali isimamie hili, Serikali itafute namna ya kufanya ili halmashauri zetu zitimize wajibu wake wa kujenga miradi ya maendeleo vijijini kama sheria inavyosema, kwamba kutoka na mapato ya halmashauri yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwangu yalikuwa ni hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpakate, ahsante sana. Anayefuata ni Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na niwapongeze Kamati zote tatu kwa taarifa ambazo zimewasilishwa hapa. Nitagusa Kamati mbili, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ambayo mimi ndiyo Mjumbe pamoja na *LAAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa namna ambavyo amewasilisha taarifa ambayo Wajumbe kwa kweli tulitumia muda wetu mwingi, tukatimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo malengo ya Kamati yetu ni kutamani tunavyomaliza Bunge kipindi hiki, basi kuwe na mabadiliko makubwa kwenye taasisi hizi. Bado changamoto ni nyingi sana, naomba nianze na taasisi ambazo bado zinategemea ruzuku kutoka Serikalini. Taasisi hizi zote si kwamba hazijui kwamba Serikali inapowekeza wanatakiwa waanze kupunguza utegemezi mwaka hadi mwaka. Nitatolea mfano wa taasisi hizo ambazo bado zimekuwa zikitegemea ruzuku ya Serikalini; *TIB, TTCL, CPB* na *UDART*, hizo ni chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya miaka mitatu mfululizo kumekuwa na ongezeko la utegemezi. Yaani badala ya wao sasa tuseme wamekuwa ili na watu wengine waendelee kuwezeshwa, lakini miaka mitatu mfululizo utegemezi umeendelea kuongezeka. Hiyo miaka mitatu kutoka bilioni 13.234 imeongezeka mpaka bilioni 17.456. Nini kitatokea, kuna shida ya *management* pamoja na bodi zilizopo huko. Kama shida ni *management* ni lazima tuanze kufikiri upya namna ya kupata watu hawa wanavyoweza kuleta mapinduzi kwenye taasisi hizi. Tofauti na hapo tutarudi kule kule tu. Jambo la kwanza ambalo lazima tulifanye lazima Msajili wa Hazina aongezewe nguvu ili waweze kuwajibika watu hawa kwa sababu shida ni uwajibikaji kwenye hizi taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kuna utegemezi mkubwa lakini kuna mashirika 63 ambayo yanapata mapato

makubwa kutokana na shughuli ambazo wanazifanya ambazo ni zaidi ya ruzuku wanazozipata Serikalini lakini bado wanahitaji ruzuku kutoka Serikalini. Sasa hili jambo halikubaliki. Kwa hiyo kuna haja sasa ya kupitia upya usimamizi wa hizi taasisi. Kama kuna shida kwenye bodi angalau mfumo ubadilike wa kuwapata wasimamizi wa hizi bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mashirika 35 ambayo yanajiendesha kibishara, mashirika 17 bado yanapokea ruzuku kutoka Serikalini, halafu tunasema ni mashirika ambayo yanajiendesha kibiashara, sasa ambayo hayajiendeshi kibiashara itakuwaje? Ni changamoto. Pamoja na changamoto hiyo bado kuna ongezeko la mishahara na matumizi kwa miaka mitatu mfululizo kwenye mashirika hayo, kutoka bilioni 793.58 hadi trilioni 1.33. Badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma na sababu ni kwamba kuna shida kwenye mfumo na upatikanaji wa *management* ya hizi taasisi. Kama ongezeko hilo la 40.64% kusipokuwa na mabadiliko ya kimfumo hatutasonga mbele, tutabaki hapa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, kuna haja ya kupitia upya menejimenti ya taasisi hizi pamoja na bodi zenyewe ndipo tutapata mabadiliko kwenye hizi taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mashirika ya umma yamepata hasara kwa miaka mitatu mfululuzo; *TANOIL, TPDC, TTCL, TCB* na Shirika la Masoko la Kariakoo. Sasa yaani ukiangalia dude kama la *TTCL*, ukiangalia fedha ambazo zimewekezwa pale? Kwa nini wanapata hasara, ni kwa sababu kuna shida ya uendeshaji, kuna shida ya menejimenti. Kwa hiyo ni lazima kuwe na mabadiliko makubwa kwenye hizi taasisi tofauti na hapo hatuwezi kufika popote tutacheza hapo hapo siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna hiyo changamoto, pia kumekuwa na shida hata mikataba ambayo wao wanaingia; na

jambo hili tumekuwa tunalizungumza mara kadhaa kwenye hizi taasisi. Nini kinatokea kama wanajua kabisa kwamba taasisi hizi tunahitaji kuwekeza ili tupate matokeo chanya. Shida inapokuwa kwenye menejimenti ni lazima hata katika mikataba mtaingia mikataba ya hovyo na mwisho wa siku mtasababisha hasara kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inapelekea, kwa sababu kuna shida ya menejimenti na kwenye bodi kunakuwa na changamoto ya ufanisi wa hizi taasisi na ufanisi hauwezi kuwepo kama shida ni mfumo. Nchi hii shida siyo sheria, shida siyo kanuni, kuna shida kwenye mfumo wenyewe, kwanza upatikanaji wa hizi taasisi zenyewe, vilevile na kwenye menejimenti zinazokwenda kuendesha hizi taasisi. Hatuwezi kufika popote kama hatutafanya mabadiliko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na mazingira ambayo yamejitokeza, Kamati tumeshauri mambo kadhaa. Jambo la kwanza, ni vizuri Serikali ipitie upya na kutoa elimu kwa taasisi hizi wajue majukumu yao, vilevile waendelee kupimwa na wawekewe malengo ili wale ambao hawajafikia malengo waweze kuondolewa waingie watu wengine wenye sifa; na inawezekana hata wanaoingia sifa zao pia zina changamoto. Kwa hiyo ni vizuri kubadilisha mfumo wa upatikanaji wa hao watu ambao wanaweza wakasimamia taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwa sababu nimezungumzia hiyo changamoto ya menejimenti, kunakuwa na shida, hata vyanzo vilivyopo kuvisimamia kikamilifu ni changamoto na vilevile wanakosa ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato na ndiyo maana watakuwa tegemezi miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nirudi kwenye miradi ambayo haikamiliki kwa wakati, changamoto ni ile ile, ya mfumo pamoja na usimamizi uliopo. Nchi hii ukiangalia uwekezaji ambao

umefanywa na Serikali na *return* ambayo inapatikana ni vitu viwili tofauti. Ni kwa nini? Ni kwa sababu kuna shida hiyo ambayo ninaizungumza ya mfumo. Kuna miradi ambayo imefanyika kwenye taasisi hizi nilizozitaja hapo. Miaka sita miradi haijakamilika, mkandarasi anapata kazi ndani ya mwaka mmoja amefanya kazi kidogo eti anasema amefilisika; ni kwa nini, ni namna ya upatikanaji wa hao wakandarasi, hakuna uadilifu, hatimaye Serikali inapata hasara, tunapata kazi ya kumwambia CAG sijui ukafanye ukaguzi, shida ni mfumo wa nchi hii, lazima tubadilishe upatikanaji wa menejimenti kwenye hizi taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida nyingine ni vipaumbele, ni lazima tuwe na vipaumbele, yaani kama hatuna vipaumbele, ni vigumu sana kufikia malengo. Leo utaamka na hili, kesho utaamka na lile, mwisho wa siku huwezi kufikia malengo ambayo mmejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niguse kidogo suala la 10%. Niwapongeze sana Kamati, wamefanya uchambuzi mkubwa sana na si mara ya kwanza jambo hili linazungumzwa hapa. Kuna haja ya kuwa na ufuatiliaji maalum juu ya maagizo lakini na yale ambayo Bunge linaazimia kwa sababu hatuwezi kuwa tunarudia haya mambo kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata taarifa kwamba wanapokwenda kurudisha hiyo 10% wanataka kuwepo na kamati sijui wilayani, mkoani. Hivi ni nani alisema kwamba shida ya 10% ilikuwa ni kamati? Tunataka tunaporudi kwenye hiyo 10% tuangalie tulikosea wapi, turekebishe ili tujue tunatokaje hapa tulipo. Halafu unapeleka huko mkoani na wilayani, Mheshimiwa Mbunge hajui, diwani hayupo, mnawapelekea watu gani wakasimamie hivi vitu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kwenye hii mikopo inayotolewa kuna makundi ambayo yanatajwa kwenye kata fulani kwa mfano Kata ya Namanyele, Kijiji cha Mkangale, Diwani tu wa

Kata hiyo hakijui hicho kikundi, unafikiri nani anakitengeneza? Shida siyo kamati shida hapa ni uadilifu na usimamizi wa hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapa leo asubuhi kwenye swali la msingi. Leo kama halmashauri zinajua sheria inawataka wapeleke kiasi gani kwenye mapato ya ndani kwa nini wasianze kuwajibishwa ambao wanashindwa kusimamia hiyo sheria kwa sababu shida ni usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza, kuna haja ya kufuatilia kwa kina, tulikosea wapi tujue tunabadilisha nini ili tunapokwenda kwenye mabadiliko, tusiende kwenye mabadiliko ya nadharia twende kwenye mabadiliko ambayo tunajua tumefanya tafiti za kina na tunakwenda kuboresha makosa yetu tuliyoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madeni amelizungumza sana Dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya hapa na siyo mara moja. Yaani madeni yanaanzia kule kwa watoto wenu kwenye halmashauri kule mpaka huku juu. Hivi leo mamalishe aliyekopa fedha benki, amepeleka chakula halmashauri, kule benki kila mwezi asiporejesha kuna riba. Halmashauri imekaa na fedha ya mamalishe kwa zaidi ya miaka mitano, kwa nini na wao wasilipe kwa riba kama ambavyo yeye anatakiwa akalipe kule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo limekuwa na mazoea kwa sababu wanaoonewa ni watu wetu wa chini. Sisi kazi yetu kama Bunge lazima tusimamie hili jambo. Wanapoingia na tutawashauri wananchi wetu, kwenye makubaliano yoyote yale iwe ni kwa maandishi na kuwe na riba kama watakosa kulipa kama walivyokubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunawalaumu wakandarasi, hivi huyu mkandarasi anafanyaje kazi kwa uadilifu? Yaani madai anadai Serikali mpaka unashangaa halafu mwisho wa siku mnasema,

wakandarasi wa ndani siyo waaminifu, siyo waaminifu vipi wakati fedha hamuwapatii, mnataka wafanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida Khenani. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatia Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo kwenye taarifa zetu za Kamati ya *PIC*, *PAC* na *LAAC*. Kwa ujumla niwashukuru Wenyeviti wetu wa Kamati zote tatu kwa kuweza kusoma taarifa zetu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa mjumbe wa Kamati ya *PIC*, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, najikita moja kwa moja kwenye taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Augustine Vuma wa Kamati ya *PIC* kwenye maeneo mawili. Eneo la kwanza ni kwenye ukurasa wa 29 hadi 31 wa taarifa yetu ambayo imezungumzia kuhusu gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijiji-miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajenga hoja kwenye hilo eneo, nitangulie kusema ninaishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa kutekeleza kwa ufanisi kwenye Miradi yetu ya *REA*. Hivi juzi tu tuliambatana na Mkurugenzi Mkuu wa *REA* kwenda katika Kijiji cha Zinga-Kibaoni ambapo tuliweza kuzindua umeme. Sasa utekelezaji wa miradi ya umeme awamu ya tatu, mzunguko wa pili imefikia 99% ya utekelezaji katika jimbo la Kilwa Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishukuru Serikali, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri inayoendelea. Wananchi wangu walipata

*bonus* kubwa sana ya kugawiwa majiko ya gesi 231 katika mpango wa Serikali unaoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Samia Hassan, Rais wetu wa kupambana na nishati isiyokuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninapozungumza, hata jana tayari Kijiji cha Ngarambilihenga umeme umewaka na kesho tunatarajia vijiji viwili vya mwisho umeme utawashwa; Kijiji cha Liyomanga na Nambondo katika Kata ya Mingumbi na Kata ya Namayuni. Naipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii changamoto imekuwa kubwa na mara kadhaa tuliifahamisha Serikali. Nakumbuka katika Bunge la mwaka juzi la Bajeti, Mheshimiwa Waziri wa Nishati wa wakati ule, Mheshimiwa Januari Makamba wakati anahitimisha hotuba yake ya bajeti aliipokea hoja hii ya gharama kubwa za uunganishaji wa umeme katika vijiji-miji. Mwaka huu Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko naye alipokea na akaahidi kwamba itafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani katika Bunge lililopita la mwezi Agosti na Septemba, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii Dada yangu Mheshimiwa Judith Kapinga naye aliipokea akaahidi kwamba itatekelezwa. Mheshimiwa Mwenyekiti ameeleza vizuri katika taarifa ya Kamati yetu. Hili jambo bado linaendelea kusumbua wananchi wetu, na kwa kuwa wananchi wetu wanaishi katika vijiji-miji ambavyo *either* viko katika majiji yetu, *either* katika manispaa zetu, *either* katika halmashauri zetu za miji, au halmashauri zetu za wilaya ambavyo bado ni vijiji vimekuwa *registered* kama vijiji vina hali ya ukijiji. Kwa hiyo, vipato vya wananchi wetu vimekuwa vidogo, lakini bado wanalazimika kulipishwa shilingi 320,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, ufanisi wa miradi hii ya *REA,* tija imekuwa ndogo sana kwa sababu wananchi hawana kipato cha kuweza kutosheleza kulipa gharama hizo. Kwa hiyo, naungana

na Kamati yangu ya *PIC* kuiomba Serikali iweze kuboresha eneo hili. Kwa mfano Kilwa tu, pale Somanga Kaskazini na Somanga Kusini katika Kata ya Somanga ni vijiji ambavyo vipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, haviko hata ndani ya Mamlaka ya Miji Midogo, ni vijiji kabisa. Ukienda Hoteli Tatu *the same* wanalazimishwa walipe shilingi 320,000. Kwa hiyo ni watu wachache ambao wamechangamkia hii fursa ambayo kama wangeweza kuunganishiwa mapema wangeweza kupata manufaa makubwa kimaendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, niombe Serikali yetu ya Awamu ya Sita iliangalie kwa haraka hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati tumesema tumeipa Serikali *time frame* ya miezi sita, lakini kwa sababu tayari Serikali iliahidi kulishughulikia jambo hili tangu mwaka juzi mwaka jana na mwaka huu ninaona pengine inaweza ikalishughulikia jambo hili mapema zaidi. Kwa hiyo, kama itaweza hata ndani ya miezi mitatu hili jambo walishughulikie likamilike ili tunapokwenda kwenye mambo ya uchaguzi na mambo mengine mambo yawe yamekaa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia suala la Bodi ya Mkonge na ufanisi wake, Bodi yetu ya *TSB Tanzania Sisal Board*. Kwanza niishukuru Serikali na kuipongeza kwa juhudi kubwa ambazo imefanya ya kufufua zao hili. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi kubwa sana kuanzia Mwaka wa Fedha 2019/2020 ya kufufua zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya zao hili inaonesha mwaka 1964 Tanzania iliongoza duniani kwa kuzalisha zao la mkonge. Tulizalisha tani 230,000. Kwa hiyo, ndiyo tulikuwa wa kwanza duniani katika *ranking* za uzalishaji na zao la mkonge lilichangia 65% kutuingizia fedha za kigeni. Kwa hiyo, ndiyo zao pekee ambalo lilikuwa limeingiza fedha nyingi kuliko mazao mengine yoyote. Kwa hiyo, kwa umuhimu huu, naiomba Serikali iongeze juhudi za kuwekeza mtaji mkubwa, kuwekeza fedha nyingi katika zao hili ili

taasisi hii au Bodi hii ya zao la mkonge Tanzania iweze kujiimarisha na kuweza kuzalisha ili turudi kule tulikotoka kwa sababu viwango vya uzalishaji hapa katikati vilishuka sana vikawa chini ya tani 50,000. Sasa hivi imepanda baada ya juhudi ambazo Serikali imefanywa, sasa hivi tunazalisha wastani wa tani 80,000 ingawa malengo kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni tani 120,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tufikie huko na turudi enzi zile za miaka ya 1960, tunahitaji kuiwezesha kifedha hii Bodi ya Mkonge Tanzania. Ninao ushauri au mapendekezo katika eneo hilo kwa sababu hili zao linahitajika sana na lina soko sana katika Nchi za China, Morocco, Saudi Arabia, Misri na nchi zaidi ya 26 hapa duniani. Kwa hiyo, naomba Serikali iongeze mtaji, iongeze fedha kwa Bodi ya Mkonge Tanzania ili hii Bodi iweze kutafuta mitambo, iweze kulima, iweze kununua mitambo ya *corona* na hatimaye kuzalisha zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi pia, waweze kufikia hata yale maeneo ambayo yalikuwa na uzalishaji mkubwa. Kwa mfano, vijiji vinavyozunguka Mkoa wa Lindi wote, kuanzia Kilwa mpaka Lindi Vijijini, kule Kitumbikwela, mpaka kule Kikwetu, Somanga na vijiji vyote vya Mkoa wa Lindi vinalima sana mkonge lakini kutokana na mtaji kuwa mdogo, Bodi imeshindwa kuvifikia vijiji hivyo na hatimaye imeshindwa kuhamasisha na tumejikuta bado tuna *mark time* lile ongezeko la uzalishaji limekuwa dogo. Kwa hiyo naomba Serikali iangalie. Vilevile, iwaongezee fedha kwa ajili ya kuanzisha ile *block farming* ambao ndiyo utaratibu wa kisasa ambao unatumika maeneo mengi duniani na ambao sisi Tanzania tumeanza kuutumia katika mazao mbalimbali ili kuboresha uchumi wetu kupitia mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kwa kuboresha zao la mkonge, kwa kuipatia mahitaji hii bodi, kwa kuipatia mtaji basi tutasonga mbele na tutarudi katika enzi mpya za mafanikio na kuweza kukuza uchumi wetu kwa kasi kubwa na hatimaye kufikia

malengo ambayo tumejiwekea katika Serikali yetu na hatimaye kupata maendeleo katika nyanja zote kiuchumi pamoja na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndulane. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, atafuatia Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba nzuri kabisa ambazo zimewasilishwa na wenyeviti wetu wa hizi Kamati za *LAAC*, *PIC* na *PAC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanzia alikoishia wajina wangu, Mheshimiwa Francis Ndulane, ambaye amegusia jambo ambalo nilitaka niliseme, lakini kwa sababu nilishajipanga nalo nani muhimu tukilisema mara nyingi na wengi nina uhakika Serikali itaona kwamba sasa umefika wakati wa jambo hili kuweza kulifanyia kazi kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *connection fee* ya umeme, mara baada ya *REA* kupeleka umeme kwenye vijiji vyetu na kumaliza kuweka umeme, sasa wale wanaobaki wanatakiwa wajiendeleze kuchukua umeme wanakutana na shida ya *connection fee*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilimsikiliza Mheshimiwa Naibu Waziri vizuri akijibu swali, suala la *connection fee* kwenye vijiji. Hili suala limekuwa gumu kidogo, kwa mfano, katika Jimbo langu la Iramba Mashariki, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, kipo Kijiji cha Iguguno, ni Kijiji lakini kwa sababu kuna vijumba vya bati vya zamani vimekuwa vingi, ukiangalia kwa haraka haraka unaweza ukadhani ni mji. Leo wanaambiwa wa-*connect* umeme kwa shilingi 320,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumelisema hapa mara nyingi, lakini *TANESCO* wamekuwa wagumu sana kutekeleza jambo hili, kila wakati ukiwafuatilia wenyewe wanasema michakato inaendelea, tathmini inaendelea nchi nzima kuangalia wapi ni miji. Leo nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba mji mdogo ni ule ambao upo kwa mujibu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtinga, nakuomba radhi kidogo, naomba uketi.

Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi kidogo, nimefuatilia hotuba za Wabunge, najua tuna changamoto mbalimbali kwenye maeneo yetu, lakini madhumuni ya siku hizi mbili ni kujadili taarifa tatu ambazo zimekuja Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mtinga, nakupa nafasi lakini naomba niwaelekeze Waheshimiwa Wabunge waliobaki, tujielekeze kwa sababu Serikali iko hapa ili iweze kuchukua ushauri mahususi kwenye haya maeneo matatu ambayo yamesomewa taarifa zake leo asubuhi na nimefanya *consultation* na Sekretarieti hapa kuna hiyo changamoto. Kwa hiyo, tafadhali tujielekeze huko ili ku-*focus* michango yetu na kuiwezesha Serikali kutekeleza kazi yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunachangia Kamati lakini tunatoa mifano hai ili hoja zikae vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ku-*connect* umeme kwa shilingi 320,000 kwenye vijiji ambavyo hata TAMISEMI haitambui kwamba ni mji mdogo, lakini wananchi wanaambiwa watoe shilingi 320,000 linafubaza maendeleo na ninashukuru Kamati ya *PIC* wameongelea hili jambo.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Wapi taarifa? Mheshimiwa Mwenyekiti wa *PIC,* tafadhali, Mheshimiwa Vuma.

**TAARIFA**

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Francis kuhusu hoja yake ya gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijiji-miji, kwamba ni suala ambalo liko *valid* na kwenye taarifa yangu ya leo ukurasa wa 14 nimelitaja. Kwa hiyo, ni jambo ambalo liko *valid* kabisa, endelea kushindilia vizuri ili Serikali iweze kutoa tathmini. Tumependekeza maazimio kwamba tuwape miezi sita ili waweze kukamilisha hiyo tathmini na tuweze kutoka kwenye hiyo sintofahamu ambayo tunayo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa, unapokea taarifa?

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili na niombe Kamati wametoa miezi sita lakini jambo hili tumeliongelea muda mrefu sana. Hili ni suala la kutoa tamko tu kwa sababu kama ni miji midogo inajulikana TAMISEMI, kama ni vijiji vinajulikana TAMISEMI. Kwa hiyo, hili suala wala siyo la miezi sita, mimi ningeliomba Bunge lako Kamati ifupishe zaidi katika maazimio, ni tamko tu litolewe kwamba vile ambavyo ni vijiji ambavyo havijawa miji waendelee na *connection fee* ya shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiombe *TANESCO*, hii bei ya shilingi 27,000 hata mjini bado inafaa kutumika kwa sababu ukienda kwenye miji mingine nguzo moja inaweza ikahudumia zaidi ya nyumba saba mpaka nane, lakini wanashindwa kuunganisha kwa sababu ya shilingi 320,000. Kama *TANESCO* wataziunganishia hizo nyumba umeme watapata ile fedha ya malipo ya mtu anatumia

umeme, biashara itakuwa kubwa zaidi. Tunapoelekea niombe *TANESCO* inabidi tufike mahali tugawe nguzo kwa wananchi ili wakitumia umeme walipe ile *connection fee* hata kama itabidi kulipa kidogo kidogo kwenye *bills* lakini nguzo zije.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo vijijini umeme umeshaenda, mwananchi anauona kwa jirani lakini anashindwa kupata kwa sababu hakuna nguzo. Kwa hiyo, ningeomba hii *TANESCO* hata ikibidi lizalishwe shirika lingine ndani yake yawe mawili ili lingine lishughulikie tu kugawa nguzo huko vijijini na lingine lishughulikie mambo mengine kwa sababu ni shirika kubwa ambalo wananchi wanahitaji sana huduma yake, lakini nadhani limelemewa kwa sababu ya ukubwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri na hivi ndiye Naibu Waziri Mkuu waliangalie hili suala la *TANESCO* kuweza hata kugawanywa yawe mashirika mawili ili ufanisi uwe mkubwa zaidi na ubunifu uongezeke kwa sababu zitakuwepo bodi mbili na menejimenti mbili zaidi. Kwa hiyo mambo mengine makubwa zaidi yanaweza yakafanyika na wananchi wakapata huduma hii ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, naomba niseme suala la halmashauri kulipa madeni kwa wazabuni wadogo wadogo. Kuna watu wanaumia sana, yaani mtu amejenga madarasa, mtu kajenga bweni halafu mtaji wenyewe alikopa shilingi milioni 40, milioni 30 hawajalipwa zaidi ya miaka 10. Ukienda kule wanakwambia kwa sababu wewe ni Mbunge hebu chukua hata hii barua, nenda kaniangalizie madeni yangu, nenda kamwone Mheshimiwa Waziri, nenda kamwone nani, watu wanalia wanasikitika wakati majengo waliyojenga wanayaona na yanatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe hili suala Serikali iliangalie, ilipe watu wetu wa ndani madeni yao. Mbona haya makampuni

makubwa yanayojenga ambayo kuna riba ndani yake mbona hela zinaenda? Mbona madaraja ya Busisi yanaenda, huko kwenye umeme mkubwa unaenda kwa sababu kuna riba kubwa ndani yake, lakini hawa wa kwetu wadogo wadogo hizo shilingi milioni 30, milioni 40 ndiyo mitaji yao na sisi ndiyo maisha yetu kule kijijini yanaenda kwa sababu uchumi unazunguka kwa hizo fedha. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali, halmashauri ziangaliwe na haya mashirika mengine *SUWASA*, GUWASA na mengine ambayo wamehudumiwa hebu walipe hizi fedha. Serikali iangalie fedha ilipwe ili uchumi uendelee kuzunguka kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wetu wanateseka, wanalia sana, wanatuangalia kwa macho ya huruma, mtu anakulilia mpaka unasema hivi wewe nenda huko ukamwambie Waziri, unamwambia kuna taratibu, ukimuuliza *document* anakwambia walishasema madeni yamehakikiwa kila kitu imebaki kulipwa tu. Hebu tuombe hili suala liangaliwe kwa umakini ili wananchi wetu wapate fedha ambazo zinazunguka huko chini na ndiyo tunazozitegemea fedha hizi katika mzunguko wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kugusia uendeshaji wa mwendokasi. Nchi yetu inatumia fedha nyingi sana kujenga mwendokasi. Mpaka sasa barabara zinajengwa kila kona pale Dar es Salaam, lakini uendeshaji wake, mtu unaenda kwenye kituo unakaa muda mrefu na hii labda kwa sababu ni kampuni moja. Tuiombe Serikali ziwekwe kampuni kadhaa pale, ziwaze kushindana. Yawepo mabasi ya *blue* pale, mabasi ya njano, mtu unakuwa unaangalia nikisimama hapa likija basi la njano haraka unajua hili basi linafaa nitakata tiketi kwa sababu hawachelewi kufika. Hii kuwa na mtu mmoja tunatumia fedha nyingi kujenga miundombinu mizuri ya kisasa lakini bado huduma zinakuwa mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe hili suala liangaliwe kwa umakini ili haya mashirika yetu yaweze kutoa huduma ambayo

wananchi, nchi yetu ni ya kisasa ina *SGR* ina kila kitu na hii mwendokasi iende vizuri ili tuendelee kutamba katika Afrika Mashariki na kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Isack Mtinga kwa mchango wako. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana! Nami nitoe shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu wa maoni kwenye hizi Taarifa tatu za Kamati ya *PAC, PIC* na *LAAC* ambazo zimewasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwanza kwa kuomba radhi Bunge kutokana na tukio la leo asubuhi la kukatiza Siwa. Halijawahi kutokea hilo tukio tangu niingie Bungeni mwaka 2015, ila limetokea leo kwa sababu nilikuwa nimetegesha wakati wa swali namba 20 ndiyo ningezunguka kule nyuma halafu nije nisogee pale kwenye *podium*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lilipoahirishwa hilo swali na kutolewa, ghafla Mheshimiwa Spika, alisimama nami ikabidi niendelee kukaa hapahapa. Kwa hiyo, nilipoitwa nikakosa muda wa haraka wa kukimbia na ndiyo maana nikakatiza, naomba radhi sana kwa kosa hilo na halitojirudia tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nizungumzie maeneo machache; nianze na suala la madeni, taasisi za umma ambazo ni taasisi za Serikali zinadaiana. Kwa mfano, unakuta *TPDC* inaidai *TANESCO, TANESCO* inadai Mamlaka za Maji, Taasisi za Serikali zinadaiwa na Mamlaka za Maji, hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu

na madeni ni makubwa ambapo kwa haraka haraka ukisema uyalipe yote kwa mara moja, inaweza ikawa ni shida kwa hizi taasisi za Serikali vilevile. Kwa hiyo, naomba kuwe na *central commitment* kama ambavyo tumependekeza. Hata hivyo, hii *central commitment* itokee kwenye ngazi za juu kabisa, hasa kwenye Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nafahamu kwamba ziko ankara ambazo zinabishaniwa, basi hizi ankara ambazo zinabishaniwa, taasisi zikae kwa pamoja zifanye *reconciliation*, wakubaliane ni madeni gani ambayo ni halali, halafu wapate jumla. Ikiwezekana, hii mipango ya malipo inayoitwa *payment schedules* iandaliwe kwa taasisi zote. Kwa kweli hata kama utakuwa na *payment schedules* nzuri za namna gani, taasisi moja moja kulipa haya madeni itakuwa ni vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2002, nilikuwa Afisa wa Serikali, wakati Baraza la Mawaziri lilipitisha uamuzi ambao naamini hata sasa hivi unaweza ukachukuliwa. Nilikuwa Afisa, Mheshimiwa Lukuvi, akiwa Mbunge anakumbuka; walipitisha maamuzi mahususi kwamba, madeni yote ambayo Taasisi za Serikali wanadaiana, yote yajumlishwe na yalipwe *centrally* na Wizara ya Fedha kupitia *central budget*, halafu baada ya hapo kama kutakuwa na madeni mapya, basi madeni hayo yawe yanaingizwa kwenye bajeti za kila taasisi na kila Wizara kwa kila mwaka ili madeni yawe yanalipwa *internally,* badala ya kulimbikiza madeni ambayo baadaye yanakuja kuisumbua Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uamuzi ule ulifanyiwa kazi na mwaka 2003 nadhani ililipwa hundi ya karibu shilingi bilioni 68 na baada ya hapo madeni mapya hayakuibuka tena, mpaka baada ya mwaka 2007 ndiyo yakaanza kuibuka tena madeni ya taasisi za Serikali kudaiana. Kwa hiyo, nafikiri kwamba ule uamuzi wa mwaka 2002 wa Serikali kupitia Baraza la Mawaziri, ungerejewa ili kusudi madeni haya makubwa yaliyopo sasa hivi yaratibiwe na Wizara ya

Fedha na yalipwe yote, ili madeni mapya sasa yawe yanaingizwa kwenye bajeti za kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nami ningependa kulizungumzia, ni mifumo ya kielektroniki; *observation* hizi hata Mheshimiwa Rais ameshazitoa kuhusu mifumo ya kielektroniki inayosomana hasa hasa *across government* na taasisi zake kama *TRA* na taasisi nyingine. Kwa kweli mapendekezo kwenye eneo hili yako mengi na yameshatolewa sana, kwa mfano kwenye Kitambulisho cha *NIDA*. Naishukuru Serikali sana iko kwenye mpango wa kuunganisha *NIDA* na *RITA*, hiyo ni hatua muhimu sana ya kuboresha eneo hili la utambuzi. Nami nategemea kwamba, tuwe na utambuzi kama uliopo Marekani, Mmarekani ambaye ana *personal identification number*, taarifa zake zote za kuzaliwa, kazi, biashara na kila kitu anachokifanya, ziko kwenye *personal identification number*.

Mheshimiwa Spika, hapa Tanzania kama tutafaulu kuweka taarifa zote za Mtanzania kwenye *personal identification number* ambayo ndiyo inabeba Kitambulisho cha *NIDA*, basi inawezekana tukafaulu kutatua matatizo mengi sana yakiwemo matatizo ya kodi na matatizo mengine mengi sana. Kwa hiyo, haya mapendekezo ambayo yako kwenye taarifa zetu, naomba yafanyiwe kazi kwa kina. Siyo kusoma tu pendekezo kama lilivyo, hapana, Serikali iende kwa kina ifanye mapitio ya kina ili kuboresha kila maeneo ambayo yamependekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeona linahitaji kuangaliwa kwa kina, ni haya madai ya hospitali ambayo yanakwama kule *NHIF*. Nadhani napo kinachohitajika ni *checklist* tu, *checklist* ya vigezo na masharti kama itaandaliwa vizuri na ikakubalika kwenye mkutano wa wataalam wa hospitali pamoja na Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF),* inawezekana hiyo ika-*solve* matatizo mengi sana, kwa sababu kila hospitali itakuwa na *checklist*

inayofahamika kwamba, kuna moja, mbili, tatu, nne tano na vigezo na masharti ni moja, mbili, tatu, nne, tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yule anayeandaa pale hospitalini atazingatia hiyo *checklist* na yule anayepelekewa pale *NHIF* na yeye ataangalia ile *checklist*. Kwa hiyo, itapunguza matatizo ya kukataliwa kwa maombi ya malipo ya hospitali mbalimbali. Kwa kweli mengine mengi yaliyopendekezwa ni mazuri, ninaomba Bunge lako Tukufu lizingatie mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati hizi tatu ili kuboresha utendaji wetu na mifumo yetu ya uendeshaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph George Kakunda. Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, ajiandae.

**MHE. DKT. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya jioni hii ya kuchangia katika Taarifa za Kamati ya *PAC, LAAC* pamoja na *PIC*. Kabla ya yote nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa utashi mwema wa kuweka mazingira mazuri ya Ofisi ya *CAG* ikafanya kazi vizuri kwa mujibu wa taratibu na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana pia Mheshimiwa *CAG* pamoja na wataalam wake ambao kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi kwa weledi na utashi kwa maslahi mapana ya nchi yetu, ndiyo maana tunapata taarifa kama hizi mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisiposhukuru na kupongeza Kamati ya *LAAC* chini ya Mwenyekiti

Halima Mdee na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Stanslaus Mabula, pamoja na wajumbe wa Kamati. Tuko *floor* moja, wamekuwa wakifanya kazi mpaka usiku ili kuhakikisha kwamba, hizo halmashauri 55 ambazo wameziita mbele ya Kamati, wamepitia kwa ufasaha na kujiridhisha na utendaji kazi na ndio maana tunaona taarifa kama hizi. Mwisho na kwa umuhimu, napongeza Bunge lako Tukufu kwa kutoa mazingira mazuri kwa Kamati hizo zote ili kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nina machache, lakini mengi itakuwa ni kuishauri Serikali, *CAG* amepewa hadidu za rejea, Sheria na Katiba ya Nchi imwongoze katika utumishi wa kufanya kazi na ndiyo maana anafanya kazi nzuri. Hata hivyo, kuna baadhi ya mazingira ambayo Serikali inatakiwa iangalie kwa jicho la pekee ili sisi wenyewe tusifanye vitabu vyetu vya Serikali yetu kila siku kuwa na mapungufu ambayo yangeweza kuzuilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikupe mfano, nimesoma ukurasa wa 15 Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe haijakusanya fedha takribani bilioni sita kutoka kwa *Yapi Merkezi*. Nitoe ushuhuda wa eneo hili, nami nilikuwa Mkurugenzi, eneo hili nimelifuatilia kwa kina nikiwa Wilaya ya Kisarawe, Wilaya ya Kibaha, Mvomero ambayo nilikuwa naisimamia, nikiwa Kilosa ambapo wote tulikuwa tunafuatilia fedha ambazo ni za ushuru wa huduma waliokuwa wanatakiwa kulipa Yapi Merkezi na tulifanya vikao vikubwa. Hapa, Mheshimiwa Chamriho alikuwa Katibu Mkuu Ujenzi, akaja akawa Katibu Mkuu wa Madini, tukaenda Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, lakini yote ambayo tulifanya kama wakurugenzi enzi hizo, kwa kweli yote yaliishia njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hizi halmashauri wamesema wamechukua *sample*, lakini wakienda katika wilaya hizo watakuta madai mengine hayo hayo ya *Yapi Merkezi* ambapo baadaye yalitolewa maelekezo kwamba, "hatuwezi kutoa fedha mfuko huu tukarudisha huku." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni nini? Sasa hii taarifa ikiwa kwenye vitabu vya CAG inaendelea kuonesha kwamba, bado kuna madeni makubwa ambayo kimsingi hayatekelezeki. Ninaomba kutoa ushauri wangu kwa Serikali, niiombe kunapokuwa na miradi mizuri kama hii ya kimkakati ambayo ni faida kwa Taifa letu, basi Serikali inapoona mazingira ambayo hizi sheria zetu tulizozitunga haziwezi kutekelezwa, ni kiasi cha kutoa utaratibu ambao utafuatwa ili isiendelee kuonekana katika vitabu vyetu na kuchafua au kuweka taswira inayoonekana kwamba Serikali haifanyi kazi vizuri au halmashauri haifanyi kazi kwa niaba ya Serikali. Hili likitibiwa naamini tutakaa vizuri na vitabu vitakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine ambalo sheria ni ngumu kidogo, ni Sheria ya Madeni ya Mifuko. Najiuliza, adhabu ya faini ya 1000% ya kutoza halmashauri au taasisi ambayo haijapeleka makusanyo ya mtumishi kwa muda, inatoka wapi? Nani ambaye aliitunga? Unaona hapa makusanyo ya Mifuko ya bilioni nne, adhabu yake ni bilioni 32. Hii ni Sheria ambayo kwa kweli Serikali inatakiwa kukaa na kuiangalia kwa kina na kuitafakari. Kwa sababu unapokuwa unajikatisha tamaa, au unapokuwa unadai madai ndani ya Serikali hiyo hiyo, kwamba halmashauri ipigwe faini ya bilioni nne, zije bilioni 32, siamini kama tunakuwa tunajenga, sana sana hapa tutakuwa tunatishana na mwisho wa siku haya madeni yatashindikana kulipwa, mwisho wa siku yanabaki kwenye vitabu vyetu, inaonekana vitabu siyo visafi. Kwa hiyo, niiombe Serikali yetu iangalie maeneo mengine ambayo inaweza kuyaboresha ili isionekane kila dakika kwamba tuna mahesabu kwenye vitabu ambayo hayaendi sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, kama Hazina inalipa mishahara kwa watumishi wetu, kwa nini isije na mkakati wa kutoa haya mafao ya watumishi wote yakawa yanapelekwa moja kwa moja kwenye hii Mifuko na tukaondoa hili ombwe ambalo hela zikija huku hazipelekwi kwa wakati, halmashauri inaanza kuchafuka na

madeni yanakuwa hayalipwi? Ni ngumu sana kuisemea halmashauri, lakini sisi sote ni mashuhuda, kule chini wakati mwingine halmashauri wanajitoa kwa moyo ili kuhakikisha kwamba shughuli za halmashauri zinakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata maeneo mengine sisi wote humu ni mashuhuda, Serikali imepeleka fedha nyingi za miradi, leo tunapiga makofi na kupongeza kwa kazi nzima ya Mheshimiwa Rais na sisi wasimamizi, kazi imefanywa na halmashauri hizo hizo. Leo tukiulizana, hivi unaweza ukajenga darasa kwa shilingi 12,500,000 na madawati ndani yake? Unaweza ukajenga tundu la choo kwa shilingi 1,100,000 ukaweka na vifaa vyote mle ndani? Kwa hiyo, kuna wakati mwingine wakurugenzi wanajifunga mikanda ili kuhakikisha kwamba kazi za Serikali zinakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatutetei kwamba wakurugenzi hawafanyi baadhi ya maeneo na kuna mapungufu, hapana. Hata hivyo, kuna maeneo mengine lazima tuyaangalie kwa kina na tufanye tathmini ya kweli ili tukipeleka fedha kule, zisaidie kuendesha miradi na ziwe zinatosha na hawa watu watashindwa kuchafuka kwa sababu pesa zitakuwa zinatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo lingine ambalo nataka nishauri kulingana na Taarifa ya *LAAC, page 12*. Tumeona kuna halmashauri ambazo zimekusanya mapato chini ya malengo. Serikali imeendelea kufanya kazi nzuri ya kuzilea halmashauri zetu, nakumbuka miaka mitatu nyuma, Halmashauri ya Kakonko ilikuwa ni halmashauri ambayo mapato yake ilikuwa ni milioni 200 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini halmashauri hiyo *structure* yake ni sawa na halmashauri nyingine zote nchini. Kwa hiyo, hata uendeshaji wa halmashauri hiyo ilikuwa ni changamoto. Hata hivyo, baadaye kwa uwekezaji wa Serikali na kuendelea kuiwezesha kiuchumi, kuwekeza kwa miradi ya kimkakati, Halmashauri ya

Kakonko ikatoka kwenye milioni 200, ikaja milioni 700 na leo tunaongelea bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri nyingine ilikuwa ni Halmashauri ya Gairo ambayo ilikuwa haiwezi kukusanya zaidi ya milioni 400, lakini leo tunaiona Gairo imekwenda na mpaka sasa hivi ina bajeti ya kukusanya bilioni 1.7 kwa sababu ya uwekezaji wa miradi ya kimkakati ndani ya halmashauri hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu hapa ni kuishauri Serikali, tulikuwa na jambo zuri la miradi ya kimkakati na hasa katika zile halmashauri ambazo kwa kweli vyanzo vya mapato ni adimu kulingana na jiografia ilipowekwa halmashauri. Kwa hiyo, nami niendelee kuiomba Serikali, zile halmashauri ambazo tunaona kwamba makusanyo hayakwenda vizuri, tusiende kuwahukumu, ila, tuangalie kwa undani kwamba, sababu ya msingi ni ipi ambayo imefanya halmashauri hiyo isifanye vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni suala la ubadhirifu, basi hatua zichukuliwe, lakini kama ni sababu ya jiografia na maeneo ambayo hayawezi *ku-favor* halmashauri kukusanya, basi turudi kwenye ule utaratibu wetu uliokuwepo, tuweze kuwekeza katika miradi ya kimkakati ili kuinua mapato ya halmashauri hizo. Naamini baada ya muda, hizo halmashauri zote zitakusanya fedha kulingana na kiwango ambacho kinatakiwa. La sivyo, kwa sasa halmashauri zitaogopa kuji-*stretch* kuweka bajeti kubwa ya kukusanya ili kuogopa kutofikia malengo, suala ambalo litakuwa siyo zuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine wa mwisho ni ushuru wa huduma, tunaona katika Taarifa yetu ukurasa wa 15, imeonekana kwamba ushuru wa huduma unakusanywa kwa shida kidogo na sheria yetu inaruhusu halmashauri zikusanye 0.3% ya mauzo ghafi baada ya kupunguza *VAT* na ushuru wa bidhaa, lakini makusanyo hayo yasipopelekwa kwa wakati, maana yake 1.5%

ndio *penalty* ya zile fedha, ambazo ni kama wamekwenda zaidi ya 500% ya ile Sheria ya 0.3 *percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niiombe Serikali yetu Tukufu, katika maeneo kama haya unapokusanya ushuru wa huduma wa halmashauri wa mapato ghafi, yaani kwa kweli kwa wafanyabiashara ni kazi ambayo ni ngumu kidogo. Hii kwa kweli imeleta shida sana kwa sababu huyo huyo mfanyabiashara analipa *corporate tax* ya *TRA*, yeye ni *agent* wa kukusanya *VAT*, atalipa *OSHA*, leseni, *fire* na atalipa fedha za kukusanya taka. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili tuliangalie, kwa kweli hili limekuwa ni suala ambalo utekelezaji wake kwa wafanyabiashara hata ukienda kwenye majiji yote, nenda pale Jamhuri, nenda Kariakoo kuna ugumu. Kukusanya 0.3% kutoka kwenye mapato ghafi ya *service levy* kwa kweli bado ni kitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niiombe Serikali, kwa sababu inawapenda wafanyabiashara wake na inataka iwakuze kimtaji ili waweze kukua, iliiangalie suala hili kwa undani zaidi. Ni bora kutathmini na kuweka malengo, kukadiria kiasi ambacho mfanyabiashara anaweza kulipa, lakini ukipigia kwenye *percentage* ya malipo ghafi, kidogo inakuwa inamuumiza mfanyabiashara na ninaamini inakuwa ni ngumu sana katika kutekeleza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi hoja zinaweza zikaendelea kuonekana kwenye vitabu vyetu kwa sababu tunahitaji kuangalia kwa kina, kufanya tathmini na kuangalia namna gani ya kuboresha na kuweka mazingira mazuri ya wafanyabiashara wetu ili waweze kulipa bila kusita kokote, lakini na Serikali yetu iendelee kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niiombe sana Serikali, halmashauri zetu zinafanya kazi vizuri na ukitaka kuujua utamu wa ngoma uingie ucheze. Bahati mbaya, halmashauri zimekuwa

zikionekana kwamba hazifanyi kazi vizuri hasa katika haya makusanyo na taarifa za *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, kwa usimamizi mzuri wa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia, Ofisi yetu ya Rais, TAMISEMI, niombe kuwe na utaratibu wa kwenda kufanya tathmini ndani ya halmashauri zetu, jinsi gani ya kuboresha upatikanaji wa mapato, lakini na yale yanayowasibu wao na kuwawekea mazingira mazuri ya kufanya, baada ya kufanya hivyo, tutawapa mazingira mazuri ya kufanya kazi, makusanyo yatakuwepo, lakini na hizi hoja za Serikali kama siyo kwisha, basi zitaweza kupungua kwa kiasi kikubwa kuliko sasa hivi. Maana yake kila halmashauri inaonekana kuna wizi, kuna ukwapuaji, lakini mazingira ni magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mfano, tunapopeleka shilingi 12,500,000 darasa limaliziwe, lakini unakuta kinachotakiwa pale ni milioni 17 au 18. Hakuna *room* ambayo mkurugenzi atarudi kwa mleta fedha kumwambia kwamba, zimepungua naomba uniongezee. Haya, niambie hizo fedha nyingine alizitoa wapi? Lazima ajifunge mkanda ili kuhakikisha mradi huo umekamilika na watoto wetu wameingia darasani. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kwa nia njema, iendelee kuboresha mazingira mazuri, halmashauri zetu zinafanya kazi vizuri na sisi sote ni mashuhuda, miradi imetekelezwa vizuri, ili sasa *CAG* akienda kule akute mambo yako sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja na nashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent ninakushukuru sana kwa mchango wako.

Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji ndiye atakayekuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa heshima hii. Nitaomba nichangie kwa kifupi sana kwenye mada zote tatu, lakini kila mmoja atachukua la kwake halafu tutaelewana mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya Serikali ni *chain of command* na Serikali inatekeleza majukumu yake baada ya kuidhinishwa na Bunge kwa kufuata Sheria na Kanuni za Fedha na kiongozi anayestahili kulisimamia hili ni Bunge hili, kwamba Serikali tunairuhusu iende ikafanye matumizi baada ya kupitisha bajeti lakini baadaye tunakuja kuangalia nini kimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku nyuma niliwahi kusema kwamba huwa tunakutana muda mrefu hapa tunachagua, tunaamua halafu tuna wapa wenzetu wakatekeleze ila kwa bahati nzuri au kwa bahati mbaya sana inaonekana tunalo tatizo kwenye *chain of command*. Maana yake ni kwamba Serikali inatoa maelekezo, lakini watendaji nadhani hawaelewi au wanafanya kwa makusudi kutokusikiliza maelekezo ambayo yanatolewa na Serikali ili kuhakikisha kwamba sheria zinafanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe mfano hapa na nitaomba ninukuu ili nikae kwenye mstari. Liko tatizo la fedha ambazo hazitakiwi kubaki mwisho wa matumizi au mwisho wa mwaka. Sasa kwenye Waraka Namba moja wa Mwaka 2021/2022 tarehe 7 Juni, 2022 ulitolewa Waraka Namba Moja na Mhasibu Mkuu wa Serikali ambao unaandaa taarifa za mwaka ukiwakumbusha Maafisa Masuuli kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali na kuhakikisha kuwa *account* ya masurufu haina bakaa mwishoni mwa mwaka wa fedha yaani tarehe 30 Juni, 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nini kilichobainika? Kilichobainika ni kwamba Taasisi saba zilikuwa na bakaa ya shilingi bilioni 2.45, nini maana yake? Maana yake Serikali inatoa maelekezo, lakini watekelezaji wanaopanga na kuruhusiwa kufanya

wanafanya yaleyale kinyume kabisa na maelekezo, maana yake nini? Maana yake huu ni uvunjaji wa Sheria za Fedha na kanuni kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taasisi nyingi hapa nitaomba nitaje chache, kwa mfano Wizara ya Mambo ya Ndani ilibakiza milioni 195, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya milioni 72, Hospitali ya Rufaa ya Sekou-Toure milioni 276 na nyingine. Ukifanya majumuisho unapata bilioni 2.45 zimekaa hazina maelekezo. Kwa maana hiyohiyo tunakwenda kwenye taasisi zilizofanya ununuzi nje ya mipango, lakini wakati huohuo ziko taasisi ambazo zimekusanya fedha, kwa mfano halmashauri zetu lakini zimekusanya fedha hazikuwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizifanyia hesabu kuna mambo matatu yanafanyika kwa wakati mmoja. Wako wanaokusanya fedha, lakini hawapeleki kwenye Mfuko Mkuu, lakini wako wanaokaa na fedha kwa muda mrefu, lakini wako wanaokaa na fedha ambazo zinatumika nje ya utaratibu. Sasa maana yake ni nini? Maana yake ukiangalia kwa haraka haraka ni mambo mawili au matatu: la kwanza, hawa wanaopewa maelekezo kwa mujibu wa sheria inawezekana sheria hizi kwa sababu wanazifahamu, lakini wanajua udhaifu wake wameamua kwa makusudi kukiuka maelekezo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenye hili, lazima Serikali iwe na meno makali, Serikali iache kuchekacheka na kuwachekea hawa kwa sababu wanatuweka kwenye kipindi kigumu, bahati mbaya sana tunaelekea kwenye eneo ambalo tutakwenda kuulizwa. Niliwaambia wenzangu mwaka 2021 tutakwenda kuulizwa na wapigakura na Chama chetu tumefanya nini? Sasa kwa stahili hii maana yake lazima tujipange upya na lazima meno yetu yawe makali kuhakikisha kwamba kila maelekezo tunayoyatoa kwa watendaji wetu lazima wayafuate siyo kwa hiari. Kwa hiyo, mimi

ombi langu Serikali iongeze meno, ing'ate na sisi tuone kwamba imeng'ata, isiwachekee hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa ujumla fedha ambazo ziliachwa bila ya kutumika kwa harakaharaka tu ni shilingi milioni 409, lakini kule nyuma nimesema ni shilingi bilioni 1.8 zimeachwa tu bila ya kazi, lakini hizohizo zinakwenda kutumika huko bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda hautoshi, ninaomba nichangie kidogo tena kwenye hoja ya ongezeko la deni linalotokana na kupanda kwa viwango vya kubadilisha fedha. Ziko taasisi zetu kwa mfano, mimi natokea kwenye Kamati moja ya NUU (Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama) kwenye Kamati hii kuna chombo chetu sisi tunakiita Jeshi la Polisi. Kwa mwaka ule wa 2023 Jeshi letu lilikuwa linadaiwa shilingi bilioni 6.621, deni hili limekaa mpaka tunatakiwa kulipa shilingi bilioni 244.51.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Ni kwa sababu tu tumechelewa kulipa na ni kwa sababu ni fedha za kigeni, kwa hiyo kutoka 114 tunakiwa kulipa 244, nini maana yake? Maana yake ni kwamba tumeongeza zaidi ya mara mbili ya fedha hizi ambazo ni kwa sababu tu mmoja anafanya maamuzi mwingine anatekeleza, lakini hapa katikati hakuna kiungo, kwa hiyo mmoja anaamua lini alipe na nani amlipe. Jambo hili halijakaa sawa kwa sababu hii ni fedha nyingi ya wananchi ambayo tungeweza kuilipa kwa wakati deni hili lisingeweza kutoka 114 mpaka kufika 244 maana yake ni zaidi ya 50%. Sasa hili halikubaliki na halitujengei heshima kama Bunge kwa sababu sisi tunatakiwa tuongeze ukali kuishauri Serikali kwa kuwa mambo haya yanawaumiza sana wananchi na kwa kweli yanatuweka kwenye wakati mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kifupi kabisa niongelee kwenye kutumia fedha nje ya mfumo wa *electronic*. Sisi tunapofanya bajeti na tukaiidhinisha Serikali ikatumie na Serikali

inaweka mifumo maana yake lazima watendaji wetu watekeleze kwa mujibu wa utaratibu. Inakuwaje Serikali inaelekeza, lakini watalaam hawatekelezi na siku zinavyokwenda haya yanaongezeka, linatuweka kwenye kipindi kigumu kama Wabunge, lakini kama Wabunge kutoka kwenye Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona aibu hata kutaja hapa, lakini niruhusu nitaje kwa heshima kabisa ili wenzetu hawa wajifunze. Ukifanya hesabu ya harakaharaka hizi ni bilioni 149 nje ya mfumo wa *electronic,* hivi hii *guts* wanatoa wapi hawa? Ninaomba nirudie kusema bado huu ni mwaka wa nne ninasema bado Bunge letu halijafanya kazi ya kung'ata. Bunge letu lipo halijafanya kazi ya kung'ata ili kila mtu ajue kwamba Bunge lina jukumu la kusimamia na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe mfano, Taasisi ya Wakala wa Barabara inazo 82, Shirika la Magereza 6,551, Wizara ya Elimu 51.24, halafu Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Musoma 591. Ukiyataja haya unapata kichefuchefu hivi hawa watu hii nguvu wameitoa wapi? Hii Serikali ambayo tumeipa dhamana na sisi kama Bunge tunaisimamia na yenyewe ina sheria za kufanya kazi, hawa watu wamepata wapi *guts* hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwamba Bunge lako hili lazima lioneshe kwa nguvu zote kwamba hatukubaliani na mchezo huu. Kila siku tunaendelea kuilazimisha Serikali itafute hela, Serikali inatafuta, lakini wanaotekeleza kule wanafanya wanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ili tuweze kufanya kazi kama Bunge, ili tuweze kufanya kazi kama Wabunge, ili kila mmoja akae kwenye mstari wake, ninaona aibu kuyasoma haya maana yake hayanipi raha. Ninaomba sana nishauri haya na haya sikuyashauri leo niliyashauri mwaka 2021: la kwanza, tuhakikishe kwamba sisi kama Bunge na Kamati zetu zote zinazohusika na

mambo ya fedha kwa ujumla zifanye kazi ya kuziita taasisi zote. Wenzetu hapa wamesema wamekagua kwa mfano kwenye halmashauri 30% au 31% ya halmashauri bado. Tulisema kila aliyepewa pesa ya Serikali lazima ziwe *accounted for,* hilo la kwanza; *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninaomba nirudie wito wangu nilioutoa mwaka 2021 kwamba Bunge linatakiwa kufanya kazi sambamba na Serikali. Bunge hili kazi yake ni kuisimamia na kuishauri Serikali, sasa kama sisi tumefanya kazi ya kushauri lakini hatuisimamii Serikali maana yake sisi wenyewe hatufanyi kazi ya kutekeleza sheria ambazo tumezitunga wenyewe. Ombi langu, Bunge lichukue nafasi yake ya kuisimamia Serikali na kuishauri Serikali kwa sababu sisi tunaunda Mhimili mwingine ambao ndiyo Mhimili pekee unaoweza kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zahor mchangiaji wetu wa mwisho wa leo.

Waheshimiwa Wabunge nitumie fursa hii kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati zetu zote tatu ambao walipata fursa ya kuwasilisha maoni ya Kamati zetu za Kudumu za Bunge. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao tulipata fursa kwa niaba ya Wabunge wengine na kwa niaba ya wananchi kuchangia na kuishauri Serikali. Ninawashukuru sana Serikali mmekuwa makini tangu asubuhi mpaka sasa kuendelea kupokea maoni na ushauri wa Wabunge na Kamati. Shughuli hii itaendelea kesho.

Baada ya kusema haya, ninaomba sasa niahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 30 Oktoba, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*